**6 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 6 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. MUSSA R. SIMA K. n. y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA– KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Daktari Pius Stephen Chaya Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 531

**Ujenzi wa Jengo la *OPD* - Kituo cha Afya Kintinku**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Jengo la *OPD* katika Kituo cha Afya cha Kintinku ambacho kimeanza kutumika bila kuwa na jengo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali ilitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi na

ukarabati wa Kituo cha Afya Kintinku. Aidha, majengo matano yalijengwa ikiwa ni pamoja na jengo la Wazazi, jengo la Upasuaji, jengo la Kufulia, jengo la kuhifadhia maiti na nyumba ya mtumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imetenga shilingi milioni 20 katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la *OPD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu msingi katika vituo vya afya kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya Kintiku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Pius Chaya swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwanza nitumie fursa hii kuipongeza Serikali na kuishukuru wametupatia bilioni moja kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana ya Mkoa. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Kintiku kinahudumia takribani Halmashauri tatu, Halmashauri ya Bahi, Halmashauri ya Chemba na baadhi ya vijiji vya Halmashauri ya Manyoni. Kituo hiki kipo kwenye *high way* ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza. Je, lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa *(ambulance)* ili iweze kusaidia kwenye kituo hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili katika Kata ya Nkonko kuna kituo cha afya ambacho kilijengwa, vilevile walijenga jengo la *x-ray* ambalo bado halijakamilika. Je, lini Serikali itakamilisha jengo hilo la *x-ray* katika Kituo cha Afya cha Nkonko ili kiweze kuanza kutoa huduma? ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, kwanza kuhusu hichi Kituo cha Afya cha

Kintiku. Ni kweli ninakiri kwamba kituo hiki cha afya ni muhimu sana kwa sababu kipo barabarani na kama alivyosema Mheshimiwa Chaya ni kituo kinachohudumia Wilaya ya Chemba, kinachohudumia wakazi wa Wilaya ya Bahi na Wilaya ya Manyoni yenyewe na kipo kilometa takribani kama 26 ama 27 kutoka mpakani mwa Dodoma na Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hivi sasa imetenge bilioni 93 kwa ajili ya ununuzi wa magari 316 ya wagonjwa nchi nzima na kwa kuanzia kila Halmashauri itapata walau magari mawili ya wagonjwa. Tayari magari 117 yameshanunuliwa mpaka kufika mwezi Mei mwaka huu na tutahakikisha tunaweka kipaumbele kwenye vituo vya afya vya maeneo ya kimkakati kama Kituo cha Afya cha Kintiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la Kituo cha Afya Kata ya Nkonko ambacho kinahitaji jengo la *x-ray*. Tutaangalia katika mwaka wa fedha 2023/2024 kuona ni namna gani Serikali Kuu itaongeza nguvu kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuweza kukamilisha ujenzi wa jengo hili la *x-ray* katika Kituo cha Afya cha Nkonko ili wananchi wa maeneo haya waweze kuanza kupata huduma za *x-ray*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kituo cha Afya Kiloleni Wilaya ya Busega hakina wodi za kulaza wagonjwa kabisa. Je, lini Serikali itajenga wodi hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ujenzi wa wodi ni katika vipaumbele vya Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Daktari Samia Suluhu Hassan, ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa, ujenzi wa vyumba vya upasuaji, ujenzi wa mochwari na kadhalika katika vituo vya afya na tutaangalia ni namna gani katika kituo cha afya alichokijata

Mheshimiwa Midimu kinaweza kipata fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi hizi kule Wilayani Busega.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kata ya Lahoda, Kata ya Jangalo na Kata ya Kinyamshindo zote zipo mpakani mwa Singida pia na Manyara. Je, ni lini mkakati wa Serikali wa kujenga vituo vya afya katika Kata hizo? ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hii ya Lahoda, Jangalo na nyinginezo zilizokuwepo pembezoni katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Serikali itaweka kipaumbele kuhakikisha kwamba tunaanza ujenzi wa majengo ambayo yanahitajika kwenye vituo hivi vya afya na tutaangalia katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ili tuweze kupeleka fedha hizi kuanza ujenzi wa vituo hivi vya afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Wananchi walihamasika sana katika ujenzi wa vituo vya afya pamoja na zahanati. Je, Serikali hamuoni kwamba kuna haja ya kumaliza yale maboma yote nchi nzima kabla hamjaanza ujenzi mpya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimfahamishe Mheshimiwa Bulaya kwamba Serikali hii

ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan ilianza ujenzi wa vituo vya afya 234 nchi nzima ambavyo vimekamilika na ilitumika gharama ya bilioni 117. Sasa tunaangalia kutafuta fedha kwa ajili ya ku-*support* jitihada za wananchi katika maeneo mbalimbali nchini, kwa ajili ya umaliziaji wa vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kuna shilingi milioni 50 ambazo zilipelekwa katika kila Halmashauri kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa zahanati za maeneo ambayo wananchi walianza ujenzi wenyewe. Hii inaonesha ni namna gani Serikali hii ya Daktari Samia Suluhu Hassan ipo *committed* katika ku-*support* jitihada za wananchi ambazo wameanza kujipelekea maendeleo.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi Mbunge wa Lushoto sasa aulize swali lake.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kabla ya kuuliza swali kuna marekebisho pale wameandika Kata ya Makaya badala ya Kata ya Makanya, baada ya marekebisho hayo sasa naomba swali Namba 532 liweze kupata majibu ya Serikali.

Na. 532

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Kata ya Kwai na Makanya – Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya katika Kata ya Kwai na Makanya Lushoto?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali ilitenga shilingi bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya 234 kwenye Kata za kimkakati ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ambayo iliyotengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Lunguza HC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu ngazi ya Afya ya Msingi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya afya kwenye Kata za kimkakati kote nchini zikiwemo Kata za Kwai na Makanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa Kituo cha Afya Mlola hakina gari la wagonjwa na hii imepelekea hasa kwa wagonjwa mahtuti kupelekwa na bodaboda katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto. Je, Serikali lini itapeleka gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Mlola ili kuokoa maisha ya wananchi wetu?

Swali la pili, nimeongea kwa muda mrefu sana kuhusu kupeleka fedha katika Kituo cha Afya Gare lakini mpaka sasa hivi hakuna mafanikio yoyote, kama waswahili wanavyosema kuona ni kuamini. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kuongozana na mimi kwenda kuona nguvu za wananchi wale wa Gare kwa ajili ya ku-*support* Kituo kile cha Afya Gare?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Shekilindi kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekua akifuatilia sana suala hili la magari katika Kituo cha Afya Mlola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kumjibu maswali yake mawili ya nyongeza hili la magari Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Daktari Samia Suluhu Hassan imetenga fedha shilingi bilioni 93 kwa ajili ya ununuzi wa magari 316 ambayo kila Halmashauri ya Wilaya itapata walau magari mawili ya kubebea wagonjwa. Vilevile kuna bilioni 61 ambayo Serikali hii ya Daktari Samia Suluhu Hassan imetenga kwa ajili ya ununuzi wa magari mengine ambayo kila Halmashauri itapata gari moja walau la *supervision* katika Halmashauri za Wilaya ili wataalam wetu wa afya waweze kutembelea zahanati zetu na vituo vyetu vya afya. Hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi kwamba tutahakikisha vilevile katika magari haya mgao huo basi Mlola nayo inapewa kipaumbele kupata gari hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la Kituo cha Afya cha Gere kule Wilayani Lushoto nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge niko tayari kuongozana naye Mheshimiwa Shekilindi, kuelekea Wilayani Lushoto kwa ajili ya kuweza kukagua jitihada hizi za wananchi na kuona ni namna gani Serikali kuu inaweza ika-*support* juhudi hizi za wananchi wa eneo la Gere.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Florence Samizi swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Mulungu Jimboni Muhambwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Daktari Samizi la lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kujenga kituo cha afya. Tutaangalia ahadi hii na nitakaa na Mheshimiwa Samizi kuona ni namna gani tunaweza

tukakaa na wataalam wetu kuona tunapataje fedha za kutekeleza ahadi hii katika mwaka wa fedha wa 2023/2024. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Anton Albert Mwantona swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Masache Kasaka.

Na. 533

**Ukarabati wa Shule ya Sekondari Kayuki – Rungwe**

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, lini Shule ya Sekondari Kayuki itafanyiwa ukarabati kama alivyoagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kutekeleza agizo lililotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu la kukarabati Shule ya Sekondari Kayuki zinaendelea ambapo Halmashauri imekamilisha *BOQ* kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari Kayuki na imebainika kuwa shilingi milioni 776 zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupata fedha kwa ajili ya kukarabati shule hiyo unaendelea ambapo ukarabati mdogo kwenye hosteli na jengo la utawala umefanyika kwa shilingi milioni 17.4. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukarabati shule hii kama alivyoelekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasaka swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa Mkoa wa Mbeya kuna shule nyingi kongwe ambazo zimechakaa sana zinahitaji ukarabati mkubwa. Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule hizi ndani ya Mkoa wa Mbeya lakini na kwa Tanzania kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ndani ya Wilaya ya Chunya tuna shule kongwe ambazo zipo toka enzi za mkoloni lakini Serikali ilisema itatoa fedha na mpaka sasa hivi haijatoa fedha kwa ajili ukarabati.

Je, lini Serikali itatoa fedha hizo ili ukarabati uweze kufanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasaka, kwanza kuhusu shule kongwe lini Serikali itakarabati shule hizi Mkoani Mbeya. Niseme tu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitafuta fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati wa shule kongwe na tayari shule kongwe 84 hapa nchini zimekwisha karabatiwa ikiwemo nyingine zilizo katika Mkoa wa Mbeya. Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa shule hizi kongwe hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maelezo yanaenda pia kwenye swali lake la pili la shule kongwe kule Wilayani Chunya, tutaangalia katika awamu inayofuata ya ukarabati wa shule kongwe tuweze kuweka kipaumbele vilevile katika shule kongwe ambazo zilijengwa na mkoloni kule Wilayani Chunya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Sima swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kulitokea changamoto katika shule yetu ya sekondari ya Utemini

ambapo ilipelekea sasa kuwahamisha wanafunzi wale wote kuwapeleka kwenye shule zingine Utemini sekondari Mheshimiwa Waziri. Miundombinu haikuwa rafiki katika ufundishaji na Serikali ikawa imeahidi kuleta fedha za kujenga shule ya Utemini sekondari, nataka kujua tu ni lini fedha hiyo itakuja kuhakikisha shule hiyo inajengwa? ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sima, Serikali kwa sasa imetenga shilingi bilioni 63 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari katika kila Halmashauri hapa nchini. Muda si mrefu Waheshimiwa Wabunge wataona katika Halmashauri zao shilingi milioni 570 ndiyo *minimum* ambayo itapelekwa kwa sababu tumeangalia na uwiano wa maeneo na gharama za ujenzi, lakini *minimum* inakwenda shilingi milioni 570 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule za sekondari mpya ikiwemo hizi za katika Manispaa ya Singida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Tarafa ya Hagati ina shule ya Sekondari ya Hagati ni shule kongwe.

Je ni lini Serikali itatenga fedha na kuikarabati shule hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimeshasema kwenye maelezo yangu ya awali. Serikali hii ya Awamu ya Sita ilikuwa imeshatenga fedha ya kukarabati shule kongwe 89 kote nchini na hiyo ilikuwa ni katika awamu ya kwanza na bado Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule zingine kongwe ikiwemo hii Shule ya Hagati iliyopo kule Jimboni kwa Mheshimiwa Kapinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 534

**Ujenzi wa Barabara ya Ikana – Chitete**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Ikana – Chitete pamoja na kujenga kwa kiwango cha lami barabara za milimani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali imetoa shilingi bilioni 1.03 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo ambapo miamba ilipasuliwa kwenye kipande chenye urefu wa kilometa mbili ambacho kilikuwa na mwinuko mkali uliokuwa unafanya magari yashindwe kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali kupitia *TARURA* imetenga shilingi milioni 460 kwa ajili ya kuweka tabaka la zege la mita 200, ujenzi wa mifereji na kuongeza upana wa barabara kwa kujaza kifusi kwenye eneo la kona kali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nilitaka tu kusema kwamba, pamoja na kuchimba miamba hiyo, barabara hiyo bado magari hayawezi kupanda. Kwa hiyo, pamoja na kufanya

jitihada zote hizo wanapaswa kufanya kazi ya ziada kuhakikisha magari yanapanda katika ule mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali yangu mawili ya nyongeza ambayo nilitaka Mheshimiwa Waziri aweze kunijibu. Kuna Barabara ya Kanga – Ifwekenya haijalimwa muda mrefu. Nilitaka kufahamu ni lini Serikali itailima barabara hii na kuiweka kuwa kwenye kiwango cha kokoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Mlowo – *NAFCO* – Magamba ambayo inaunganisha Wilaya ya Songwe na Makao Makuu ya Mkoa. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha barabara hii inaweza kupitika muda wote na kutengenezwa kiwango cha lami ili iweze kuunganisha Mkoa wa Songwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwandabila, la kwanza juu ya hii Barabara ya Kanga hadi Ifwekenya. Barabara hii ina urefu wa kilometa 20.4 na tayari Serikali kutoka mwaka wa fedha 2021/2022 ilianza kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa maeneo korofi ya barabara hii. Mwaka wa fedha huo nilioutaja, Serikali ilitenga Shilingi milioni 250 kwa ajili ya ukarabati na hivi sasa kuna fedha nyingine katika mwaka wa fedha tunaomaliza, ilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa kilometa saba kwa barabara hii ya Kanga kwenda Ifwekenya. Mwaka wa fedha tunaoenda kuanza Julai mosi 2023/2025 kuna Shilingi milioni 60 ambayo imetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii. Serikali itaendelea kukarabati barabara hii kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha kuhakikisha kwamba huduma kwa wananchi zinapatikana muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili kuhusu barabara hii ya Mlowo – *NAFCO,* nikiri kwamba ni barabara muhimu sana ambayo inaunganisha Wilaya ya Songwe na Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe pale Mlowo. Barabara hii imetengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili

ya matengenezo ya kawaida. Kwa sababu barabara hii pia na yenyewe haipo katika kiwango cha changarawe, kwa hiyo, katika mwaka wa fedha unaoanza wataanza ukarabati katika maeneo korofi kuweka changarawe badala tu ya kuwa wameilima na greda, wataanza kuweka kifusi katika maeneo korofi na tutaendelea kuitengea fedha kadiri ya miaka ya fedha inavyokwenda na upatikanaji wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Ni kweli tulitengewa fedha, Shilingi bilioni moja kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amejibu kwenye maswali yangu ya msingi. Barabara hii ya Ikana – Chitete ni barabara ambayo inaunganisha Tarafa ya Ndalambo pamoja na Tarafa ya Msangano ambapo Tarafa ya Ndalambo ndiyo kuna soko la kimataifa. Shilingi milioni 400 ambazo tumetenga kwa sasa haziwezi kushusha ule mlima; je, Serikali haioni kupitia Wizara ya TAMISEMI angalau mtuongezee shilingi milioni 600 nyingine ili tuweze kushusha ule mlima kikamilifu kama ambavyo Mlima wa Jimbo la Kwela unapitika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, jiografia ya kule na kuna mito mingi kwa ajili ya kueleka katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya hii ya Momba kule Chitete na inaunganisha pia tarafa hizi mbili ya Ndalambo na Msangano. Kama nilivyokuwa nimeshasema kwenye majibu yangu ya msingi, tayari Serikali ilikuwa imeanza ukarabati wa njia hii katika yale maeneo ambayo yalikuwa ni korofi sana. Tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuona ni namna gani tunaweza tukaongeza nguvu kwa ajili ya kuongeza ukarabati wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna maeneo ambayo mto unapita ukitoka juu kwa sababu tunapozungumzia ni chini na

unatakiwa upite kwenda kupanda mlima mrefu sana na kukutana na barabara ya Zambia. Tayari Serikali ilikuwa imeshaanza ukarabati wa vivuko vile katika maeneo ambayo maji pia yanapita. Kwa hiyo, tutakaa na Mheshimiwa Condester kuweza kuona ni namna gani tunaendelea na ukarabati huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad Mbunge wa Chaani, sasa aulize swali lake.

Na. 535

**Kutangaza bidhaa zinazotokana na Mwani**

**MHE. JUMA USONGE HAMAD** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzitangaza ndani na nje ya nchi bidhaa zinazotokana na Zao la Mwani?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Usonge Hamad Juma, Mbunge wa Jimbo la Chaani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitangaza bidhaa za zao la mwani nchini kupitia maonyesho, warsha na matamasha mbalimbali ikiweno Sherehe za Wakulima Nane Nane, Maonesho ya Biashara za Kimataifa Saba Saba, Sherehe za Siku ya Mvuvi Duniani na Siku ya Chakula Duniani. Pia bidhaa za mwani zinatangazwa katika vyombo vya habari mbalimbali ikiwemo runinga, redio, magazeti na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Korea

Kusini imeandaa Tamasha la Uvuvi Korea na Afrika *(Korea African Fisheries Forum)* litakalofanyika Zanzibar kuanzia tarehe 14 hadi 15 Juni, 2023 litakalojumuisha wadau kutoka Korea Kusini na Senegal. Tamasha hili linalenga kutangaza shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji za Afrika ikiwemo zao la mwani na bidhaa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inaandaa mpango wa kutangaza bidhaa za mwani nje ya nchi kwa kutumia Balozi zetu zilizopo katika nchi mbalimbali kupitia matamasha, vikao na warsha zitakazofanyika katika nchi hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yenye kutia matumaini hususan kwenye Balozi zetu. Ila tukumbuke kwamba tuna takribani zaidi ya miaka 30 sasa tokea mwani huu uletwe hapa kwetu Tanzania ambayo ni nchi ya tatu duniani kwa kuzalisha mwani mwingi, lakini bado hatujaona jitihada kubwa za kuhakikisha mwani utambulika nchini na kuwa na thamani kwa wakulima wetu: Je, ni upi mpango wa Serikali sasa wa kushirikiana na taasisi ya sayansi na teknolojia iliyokuwepo Dar es Salaam pamoja na ile taasisi ya Zanzibar ambayo inashughulika na masuala ya mwani ili kuhakikisha mwani unakuwa na thamani nzuri na unatambulika? Hilo swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wizara imejipangaje sasa ili kutoa elimu kwa wakulima wetu ili wafahamu faida zinazopatikana kwenye huo mwani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa ukaribu zao la mwani. Zao la mwani ni moja ya mazao ya kimakakati katika Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi ambayo yanatokana na mazao ya bahari. Kwa hiyo, mpango wa Serikali ni pamoja na kuzitumia hizi taasisi ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge hapa kwa maana ya *COSTECH*

pamoja na *ZSF* iliyoko upande wa Zanzibar. Malengo haya tutaendelea kuyasisitiza kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha sasa huu mwani unakuwa maarufu siyo kwa Tanzania peke yake, ni mpaka nchi za pembezoni ili kuongeza biashara kubwa na pato la Taifa kwa ujumla kwa pande zote mbili; Tanzania Bara pamoja na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, hilo ndiyo mpango wetu wa sasa kuhakikisha kwamba tunaongeza *engagement* ya watu katika zao hili la mwani ikiwemo vijana, akina mama pamoja na wanaume ambao watahitaji kuingia katika zao hili. Kwa hiyo, tutatoa elimu na tutaongeza wataalam kwa ajili ya kusaidia zao la mwani. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwani ni zao ambalo likisanifiwa linaweza likatoa bidhaa nyingi ambazo zinatoa faida kwa wakulima: Je, ni lini Serikali itawapelekea viwanda vidogo vidogo katika yale maeneo ambayo yanazalisha mwani Zanzibar na Tanzania kwa ujumla? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Moja ya mpango wa Serikali ni pamoja na kuwawezesha wakulima wa mwani na ndiyo maana ukifuatilia katika Hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambayo aliitoa hapa Bungeni, moja ya mikakati tuliyonayo ni pamoja na kuwanunulia vifaa vya kisasa na kuongeza tija katika zao la mwani ikiwemo kuwapatia viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuzalisha kama sabuni, mafuta yanayotokana na mwani. Kwa hiyo, hayo ni sehemu ya mpango ambao Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina swali dogo tu la nyongeza. Tunafahamu kwamba mwani ni muhimu sana na unaleta fedha za kigeni lakini mwani unalimwa sana na wanawake na hata kule Jimboni kwangu Mchinga, wanawake wanalima mwani, lakini bei yake ni ndogo ndogo sana. Serikali ina mpango gani juu ya hili jambo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nampongeza Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Mchinga kwa kuwa Halmashauri yake ya Mchinga hapa nchini ni moja ya halmashauri ambazo zinaongoza kwa uzalishaji wa zao la mwani. Kwa hiyo, hilo linafahamika, na ni kweli zao la mwani wakulima wakubwa ni akina mama. Sisi kama Serikali tunakiri kwamba bado changamoto ya bei ipo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati yetu tuliyonayo ni pamoja na majibu ya swali la msingi kama tulivyojibu kwamba, ni kutangaza zao la mwani, kutafuta masoko nje ya nchi hususan katika nchi ya China ambapo ndipo wanunuzi wakubwa wa zao hili ili kuhakikisha kwamba sasa tunaongeza bei kwa wakulima wetu wa ndani ili kupata tija na kuongeza pato la Taifa kwa nchi nzima. Kwa hiyo, hilo liko ndani ya mipango yetu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 536

**Fedha kwa ajili ya utelekezaji wa miradi ya maji – Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maji katika maeneo ya Mkunda Kaengesa, *Kaoze Group* na Ilemba Kwela?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI,** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa miradi ya maji ya *Mkunda Group, Kaoze Group* na Ilemba. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2023/2024 na kunufaisha wananchi wa vijiji vya Mkunda, Kaengesa A, Kaengesa B, Kianda, Ilemba A, Ilemba B, Kaswepa na Kaoze.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Clement Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Serikali ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Mradi wa *Kalole Group* utakaohudumia Kijiji cha Skaungu, Kazi, Katonto na Kalole: Je, ni lini Serikali itaanza kujenga mradi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Serikali iliahidi kupitia Mradi wa *MAU* kuchimba visima kwenye mji mdogo wa Laela na Mpui ambapo kuna changamoto kubwa ya maji. Nataka kujua, hivyo visima vya dharura mtaanza kuchimba lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deus Sangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mradi wa Kaole sisi kama Wizara tumeshajipanga kwa mwaka ujao wa fedha tutakwenda kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, maeneo haya mawili ya Laela na Mpui, Mradi wa *MAU* unaendelea kufanya kazi kwa maana taratibu zinaendelea kukamilishwa na tayari kwa pale Laela utaratibu umekamilika na mwezi huu wa Juni mwishoni tutaanza kuutekeleza kwa kuchimba kile kisima. Pale Mpui mkandarasi ambaye ataenda kufanya usanifu ameshapatikana na mwezi huu Juni anakwenda kufanya kazi. Mara baada ya kumaliza usanifu, tutachimba visima hivi tulivyoahidi kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuanza kutekeleza miradi ya Vijiji vya Mkongokieyendo, Minyinga pamoja na Sakaa, lakini kwa masikitiko makubwa, mpaka sasa miradi ile imesimama na inasemekana mkandarasi hajalipwa fedha: Ni lini sasa Serikali italipa fedha ili mkandarasi amalizie miradi ile ambayo ina faida kubwa kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtaturu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi vyote alivyovitaja Mheshimiwa ni kweli miradi inaendelea na sisi kama Wizara tumeshaanza kulipa wakandarasi. Hapo katikati kidogo fedha hatukuwanayo, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ametupatia fedha tayari na tunaanza kulipa wakandarasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuahidi kupeleka mradi mkubwa wa Shilingi bilioni 42 kwa ajili ya wananchi wa Kinazi A na B na maeneo ya Msingo ambao hawana kabisa majisafi na salama. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais. Shilingi bilioni 42 ni mradi mkubwa. Mheshimiwa Mbunge hongera pia kwa kuendelea kufuatilia miradi hii mikubwa ya kimkakati na mradi huu tunaanza kuutekeleza mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi wa Kata za Kimuli, Businde na Bugara hupata changamoto sana ya maji hasa tunapoelekea wakati huu wa kiangazi, lakini ni eneo ambalo lina mvua za kutosha: Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kujenga matanki makubwa ili wakati wa mvua tuwe tunavuna maji na wakati wa kiangazi kama hiki tunachokiendea wananchi wanaweza kupata maji ili kuondoa adha wanayopitia kuchota maji ambayo ni tope? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kata hizi alizozitaja zina changamoto ya maji na sisi kama Wizara tunafahamu. Ushauri wa kujenga matanki makubwa tunauchukua, lakini vile vile tumejipanga kuhakikisha maeneo haya yote tunakwenda kuyapatia majisafi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Je, ni lini wananchi wa Kata ya Ng'ang'ange katika Wilaya ya Kilolo watapatiwa fedha ya mradi wa maji au kuchimibwa visima ili waweze kupata majisafi na salama kwa sababu sasa hivi wanatumia maji ya mito? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza Mheshimiwa Dkt. Ritta, hata juzi nimekuona ukiwa na Mheshimiwa Waziri Aweso kuhakikisha changamoto ya maji inakwenda kutatuliwa ukiongozana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo. Vile vile katika kata hii uliyoitaja ya Ng'ang'ange sisi kama Wizara tunafahamu na tunakwenda kupeleka utatuzi kwa kuchimba visima na unafahamu gari tumeshaifikisha, umeiona wewe mwenyewe. Kwa hiyo, kisima hiki kitachimbwa ndani ya mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo Mbunge wa Baraza la Wawakilisi sasa aulize swali lake.

Na. 537

**Hitaji la nyumba za askari – Kengeja**

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawajengea nyumba za kuishi Askari wa Jeshi la Polisi waliopo Kengeja?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**, alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mahitaji ya nyumba za kuishi Askari Polisi katika eneo la Kengeja Mkoa wa Kusini Pemba. Tathmini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili za makazi ya kuishi familia nne za Askari Polisi imefanyika, ambapo kiasi cha fedha Shilingi 368,412,200/= zinahitajika. Fedha hizo zimetengwa katika Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa fedha hizi tayari zimeshatengwa:-

(a) Je, ujenzi huu utaanza mwezi gani?

(b) Je, uko tayari tufuatane kwa pamoja ili kwenda kujiridhisha hali halisi ilivyo kwa nyumba zile? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, fedha hizi zimetengwa katika Bajeti ijayo 2023/2024. Kwa hiyo, wakati wowote baada ya mwezi Julai fedha zitakapotoka na ujenzi ukaanza, niko tayari kuongozana na Mbunge ili kwenda kushuhudia maendeleo ya ujenzi huo, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati nyumba za Polisi zilizopo Madungu Wilaya ya Chake Chake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea eneo la Chake Chake na kubaini mbali ya uchakavu wa Kituo cha Polisi cha ngazi ya Wilaya, vile vile nyumba za Askari zimechakaa sana. Hata hivyo, Serikali imeanza kujenga hanga moja ambalo litachukua Askari lakini tutaendelea kuzikarabati nyumba hizo kadiri tunavyopata fedha ili Askari wote waweze kukaa kwenye makazi yenye hadhi stahiki, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia Shomar, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, ni lini ujenzi wa nyumba ya Kamishna wa Zanzibar itajengwa kwa vile hivi sasa anakaa uraiani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kutokuwepo kwa nyumba yenye hadhi anakaa Kamishna wa Polisi ZanzIbar na katika bajeti hii inayoendelea tumeweza karabati ofisi ya kamishna. Hatua

itakayofuata katika bajeti ijayo ni kuhakikisha kwamba nyumba ya Kamishna wa Polisi Zanzibar inajengwa na kukamilishwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza ulizwa swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante napenda kuuliza swali. Nyumba za askari polisi Wilayani Maswa ni za siku nyingi sana zimejengwa na mkoloni je, ni lini Serikali itajenga nyumba hizo upya ili ziwe na hadhi ya kuishi askari polisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu, Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwa upande wa Maswa si nyumba tu ambazo zimejengwa wakati wa mkoloni. Hata kituo cha polisi ngazi ya wilaya hakipo chenye hadhi stahiki. Katika bajeti ijayo tutaanza utaratibu wa kuweka fedha kwa ajili ya ujenzi wa hizo nyumba, lakini na kuanza kujenga kituo cha polisi chenye hadhi wilaya kama ambavyo imewahi kuulizwa na Mbunge wa Jimbo husika na tukamjibu hapa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA. KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante je, ni lini Serikali itawajengea nyumba za kuishi Jeshi la Polisi Wilaya ya Micheweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri ambavyo tutapata fedha tutaendelea kuimarisha na kujenga Vituo vya Polisi na Makazi ya Askari. Kwa hiyo, Micheweni ni moja ya eneo litakalozingatiwa katika ujenzi wa nyumba za askari, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuwa Kituo cha Polisi Chimala ni duni na makazi ya askari wale ni duni je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo hicho pamoja na makazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua jinsi ambavyo Chimala kunaendelea kwa kasi kule Mbarali na niwapongeze wananchi wa Chimala pamoja na uongozi wao akiwemo Mbunge na *DC* kuanza Ujenzi wa Kituo cha Polisi Chimala na hatua itayofuata ni kuingia ujenzi wa nyumba za makazi ya askari. Serikali itawaunga mkono pamoja na wadau kama ambavyo *RPC* ameanza kufanya ili kuhakikisha kwamba Chimala wanapata nyumba bora za kuishi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu kule Makete hamna Nyumba za Jeshi la Polisi, ukienda Dodoma hapa nyumba za askari polisi hapa hazifai, ukienda *Oster Bay* Dar es Salaam hazifai ni upi mkakati mahususi wa Serikali wa kujenga nyumba za polisi nchini kama ambavyo JWTZ imefanya kwa ajili ya maaskari wao? Kwa hiyo tunaomba majibu ya Serikali kwa kushirikiana na *National Housing.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la mkakati zaidi. Niliwahi kueleza hapa katika moja ya maswali kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi inao mpango wa miaka kumi wa ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Polisi na Makazi kwa ajili ya Askari. Kwa hiyo, mpango tunao kazi tuliyonayo ni kutafuta fedha kadri tunavyoendelea utekelezaji tunapata fedha kutoka kwenye tozo lakini tutapata fedha kutoka kwenye bajeti ya maendeleo kwa madhumuni ya kujenga vituo na nyumba hizo. Kwa hiyo, maeneo yote yatafikiwa kadri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Nishati Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 538

**Bei ya kuunganisha umeme Kijiji cha Lwamgasa kuwa tofauti na vijiji vingine – Busanda**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini bei ya kuunganisha umeme katika Kijiji cha Lwamgasa ni shilingi 321,000 tofauti na vijiji vingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Byabato majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa kutoka TAMISEMI, eneo la Lwamgasa linatambuliwa kama Mji Mdogo na hivyo malipo ya gharama ya kuunganisha umeme iliwekwa 320,960 kwa vile panakidhi mwonekano wa mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepokea maombi mengi kutoka kwa wakazi wa maeneo ya vijiji miji wanaotozwa shilingi 320,960 kama gharama za kuunganisha umeme ndani ya mita 30 iwe 27,000. Kijiji cha Lwamgasa ni miongoni mwa vijiji miji hivi. Kwa sasa, uchambuzi bado unaendelea ili kubaini uhalisia wa maeneo hayo. Uchambuzi ukikamilika gharama halisi stahiki zitatolewa, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza kwa vile taarifa za TAMISEMI hazikuwa sahihi je, Serikali iko tayari kuwarejeshea wananchi pesa ambazo zimezidi kutoka shilingi 27,000 hadi 321,000 baada ya taarifa yetu kujulikana kwamba siyo sahihi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, zoezi la kubaini vijiji mji ambavyo vimetajwa hapa kwenye swali la msingi litakamilika lini ili wananchi wenye uwezo mdogo kwenye vijiji vyetu waweze kupata umeme ikiwemo Kaduda, Chibingo, Ibondo na vingine vingi? Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Tumaini Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niweke taarifa sahihi kwamba tunaamini kabisa taarifa za TAMISEMI zilikuwa sawa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji. Isipokuwa kinachogomba ni ile hali ya kwamba watu wanatambuliwa kuwa wako mjini lakini wao wanajiona hawako Mjini na kwa sababu tumelibaini hilo tumeona ni vema sasa sisi Wizara ya Nishati twende *site* na kubaini hata kama eneo ni la mji, lakini je, uhalisia wa maisha ya wakazi wa maeneo yale ni wa namna gani? kwa sababu Sheria ya Mipango Miji imeweka maeneo na mazingira ya masharti kama kuna maduka, kama kuna vituo vya afya, kama kuna barabara za lami na nini hayo ndiyo maeneo ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu taarifa ya TAMISEMI kwa mujibu wa sheria ilikuwa sawa. Lakini maeneo hayo yanawakazi wenye vipato tofauti na hivyo sisi tunafanya utafiti na upembuzi yakinifu kuona ni kiasi gani kilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo niseme kwamba anaposema turudishwe kwa wananchi namuomba asielekee huko. Kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita inaweka ruzuku kwenye gharama za kuunganisha umeme kwa kulingana na

maeneo mbalimbali yalivyo. Kwa hiyo Serikali iliweka ruzuku hata hii 320,000 bado ni ruzuku imewekwa ili wananchi waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shughuli ikikamilika ambayo ameuliza kwenye eneo la pili ni lini? Tunaendele, tunafanya kazi hii ni kubwa tulimaliza awamu ya kwanza tukaona kuna maeneo hatukufika tumerudi. Tunaomba yeye na Waheshimiwa Wabunge wawe wavumilivu ili zoezi litakapokamilika tuweze kuja kutoa taarifa sahihi na kuweza kutangaza gharama sahihi kila eneo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Nollo swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Nataka tu nijue Serikali inatumia kigezo gani? tofauti ya 27,000 na shilingi 300,000 ni kubwa mno je, Serikali haioni hebu ije na mkakati wa kuona kiwango fulani ambacho kitakuwa kina *rationale* nzuri kwa wote wanaokaa mjini na wale wa vijijini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kuliwahi kuwa na viwango tofauti tofauti vya kuunganisha umeme. Sasa kwa maneno machache niseme tulipata kipindi fulani mradi wa kupeleka umeme vijijini na ulikuwa unafanyika bure kwa watanzania wote waliyokuwa wanakidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ule mradi ulikuwa wa mfadhili na mfadhili akasema hawezi kutoa bure, kwa hiyo, tutakubaliana kwamba basi mwananchi alipie *VAT* ambayo kipindi hicho *VAT* ilikuwa ni shilingi 27,000 ndiyo *genesis* ya shilingi 27,000 ilipoanzia. Kwa hiyo, tumekwenda nayo kwa utaratibu huo mpaka sasa na Serikali sasa ndiyo inafanya mchakato na upembuzi mpana zaidi ili kuona kama tunaweza tukawa tuna viwango tofauti tofauti kwa misingi tofauti tofauti kama hii 27,000 ilikotokea kipindi hicho ilikuwa kuunganisha, ilikuwa 150,000 nadhani sasa asilimia 18 au 20 nadhani *VAT* ilikuwa asilimia 20 ikawa ni shilingi 27,000 ndiyo *genesis* ya shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama halisi ni shilingi laki saba, laki sita mpaka laki saba. Kwa hiyo, inapungua kwenda laki tatu kulingana na ruzuku ambayo inayotolewa na Serikali kwenye maeneo ya mijini na maeneo ya vijijini au kwenda shilingi 27,000. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Kijiji cha Luganga na Kijiji cha Kilolo ndipo yalipo Makao Makuu ya Wilaya lakini hivi ni vijiji vilivyosajili. Je, Serikali ipo pia tayari kuangalia hivi vijiji kwa sababu wamepewa kulipa zaidi ya shilingi 300,000 ambayo ni tofauti na 27,000 kwenye vijiji vingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuhakikishie Mheshimiwa Nyamoga kwamba maeneo yote yatafikiwa na upembuzi huu unafanyika nchi nzima kwenye maeneo yote ili kuweza kubaini uhalisia wa kila eneo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama navyofahamu wafugaji hawaishi mjini sasa vijiji vya Kisimani na Kilimani pale Himo viliingizwa kwenye Mji mdogo wa Himo na hivyo kukosa fursa ya kufurahia umeme wa *REA*. Je, mnatoa kauli gani kuhusu hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Kimei kwamba azma na nia ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha kila Mtanzania popote alipo anapelekewa huduma ya umeme na tayari tumeshaanza kufikisha kwa kila kijiji. Lakini hatua kubwa inayofuata ni ya kupeleka kwenye vitongoji ambavyo hata juzi kwenye bajeti tumevisema na tunatarajia pesa kubwa tutaipata kwenye mwaka

wa fedha ule mwingine unaofuata ili vitongoji vyote maana yake wananchi wote waweze kupata huduma ya umeme popote walipo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Afya, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani Mbunge wa Nkasi Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 539

**Malalamiko katika huduma za Bima ya Afya**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza: -

Je, ni kwa nini Wananchi wanaotumia Bima ya Afya wanalalamika kuhusu huduma wanazopatiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Mheshimiwa Dkt. Molel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* umekuwa ni nguzo muhimu katika uboreshaji wa huduma za Afya Nchini ambapo Taasisi Binafsi za Afya pamoja na Vituo vya Huduma za Afya vya Serikali vimeonekana kutoweza kujiendesha bila uwepo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutokana na Watanzania wenye uwezo wa kulipa fedha taslimu kuwa wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 70 ya mapato ya vituo vya huduma za Afya vya Serikali pamoja na binafsi vinategemea Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri hayo kumekuwepo na changamoto za kimiongozo ambapo dawa chache zilikuwa zinatolewa katika zahanati na vituo vya Afya. Serikali imefanya maboresho kwa kuongeza idadi ya dawa, vitendanishi na vifaa tiba ambapo kwa ngazi ya zahanati imeongeza kutoka aina 254 hadi 451 na kwa ngazi ya vituo vya Afya toka aina 414 hadi 828.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana na nashukuru pia majibu ya Serikali nimeyasikia. Lakini wananchi wapokata Bima ya Afya wanajua wameweka akiba kwa ajili ya matibabu pale wanapoumwa kumekuwa na utofauti wanapokwenda hospitalini kupata huduma wanaambiwa bima yako daraja lake huwezi kupata dawa hizi, huwezi kupata huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuwapa elimu mapema kabla hawajakata bima ili kujua kwamba bima yake anaweza kupata matibabu gani kwenye eneo lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa *NHIF* na Serikali mmekili kwamba bado kuna changamoto na changamoto hizo na *CAG* naye amezungumza usimamizi mbovu pamoja na taarifa za uongo zinapotolewa. Ni upi mkakati wa Serikali wa kumaliza changamoto hizi ili kurudisha dhana ile kwa Serikali kuliko hivi sasa wananchi wanaamini hatuna maana tena ya kuwa na Bima ya Afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri lakini naomba tu nimwambie kwamba kwenye eneo la *NHIF* hakuna madaraja labda akiwa amechanganya kati ya *NHIF* na *CHF*. Kwenye *CHF* ndiyo kuna madaraja kwa maana kuna kutibiwa

kwenye kunafikia *level* fulani hutibiwi *level* fulani na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tulikuja na mkakati wakati wa kuja na Muswada wa Bima ya Afya kwa watu wote tulikuja na mkakati thabiti wa kuboresha eneo la *CHF* pamoja kwamba tunayo Bima ya Afya kwa wote. Lakini tuone kwa uwezo pili hicho kwa sababu hatufuti *CHF* lakini tukaja na makakati wa kuboresha ili kuondoa madaraja ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nataka kukuhakikishia kwamba matatizo watu wako wa Nkasi wanayoyapata kutokana na hayo mambo tukikubaliana pamoja kwamba baada ya muda tutakuja na Muswada wa Bima ya Afya kwa wote tutaweza kutoa hilo tatizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru hivi karibuni kumekuwa na utata sana katika hii Bima ya *CHF* nini tamko la Serikali hii bima imefutwa au inaendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tulikuwa tumesahau swali lake la pili lakini siku-*concentrate* sana kwa hiyo naomba alirudie swali lake.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua hivi karibuni kumekuwa na utata sana wa Bima ya Afya *CHF* kwa wananchi wa vijijini. Hii bima imefutwa au ipo? Nini tamko la Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bima hii haijafutwa na tunashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ambao ndiyo wanasimamia eneo hili la *CHF* ili kuona katika kipindi hiki cha mpito ambacho kuna haya matatizo ambayo Wabunge

mnayazungumzia tunaboreshaje pamoja sisi na TAMISEMI tuone ni namna gani tunaiboresha ili kuondoa matatizo yayosemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo kuna wenzetu ambao wanafadhili eneo hili kuna Taasisi inafadhili eneo hili wanasaidia kwenye matangazo wanasaidia kwenye kuhamasisha, tunataka tukae nao pamoja tuone namna gani badala ya kufanya matangazo, kufanya warsha na tamasha warudishe hizo fedha waende kuboresha kwenye eneo la kitita ili wananchi kuweza kuondokana na tatizo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHILEWESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Hospitali ya Wilaya Biharamulo tulianza kutoa huduma tarehe 13 Januari, tukapata usajili tarehe 20 Februari. Lakini mpaka sasa tangu tume-*apply* maombi kwa ajili ya kutoa Huduma za *NHIF* kwenye hospitali yetu hatujapata kibali wala hatujapata majibu kutoka *NHIF*. Ni nini kauli ya Serikali juu ya wakazi wa Biharamulo wanaotumia hospitali ile kwa sababu wamekosa haki yao ili hali wanazo kadi na wana kila kitu kinachohusu *NHIF*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimeanza kumjua Mheshimiwa Mbunge kwa yeye kupigania hii hospitali yake. Kwa hiyo, kwa kweli sisi kama Serikali hatutakubali kazi uliyofanya kwa nguvu kubwa kwa miaka miwili wananchi wasiweze kupata huduma. Kwa hiyo, namwagiza Mkurugenzi wa *NHIF* Taifa nampa siku tatu Hospitali yako ya Biharamulo ipate Mfuko wa *NHIF*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna swali la pili la Mheshimiwa Mheshimiwa Aida. Naomba Mheshimiwa Aida, swali la pili lirudie aweze kulijibu. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana niliuliza kwamba kwa kuwa na nyinyi Serikali mmekiri kwamba kuna changamoto kwenye aina ya Bima hiyo ya *CHF* kwamba mkakati wa Serikali ni upi wakumaliza changamoto hizo ili kuondoa hii dhana ambayo wananchi wanayo sasa kuona hakuna haja ya kuwa na Bima ya Afya wanapoenda kwenye huduma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Aida nimekwenda pamoja na yeye kwenye jimbo lake nimeona hilo tatizo na wananchi wamekuwa lalamika. Kwanza nikupongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ulivyo karibu na nilivyopita kule nilikuwa nashangaa ulishindaje kule kwa ile *structure?* Nikajua hapo sasa hivi kwa kweli wewe ni mwanamke wa shoka kwa ushindi uliyopata pale Nkasi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba, tumesema hapa moja nimeeleza kwa swali alilosema mwenzetu Mbunge pale kwamba kwakweli kwa sasa tunashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ambao wanasimamia eneo hilo kwamba tuone kwa kipindi hiki cha mpito ambao bado Muswada wa Bima ya Afya kwa wote haujaja tunakaaje tuweze kuboresha eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kwa sababu kuna taasisi ambayo ina *support* eneo hili na Waziri wa Afya ameishawaita tuone tunakaaje waweze kukaa. Fedha wanazotumia kwenye warsha, matangazo na nini wanaweza kuboresha hicho kitita wakati tunangojea Muswada wa Bima ya Afya kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi mwenyewe eneo hilo la *CHF* sithubutu kulipigania kule jimboni kwangu. Kwa sababu ukipigania halitoi matokeo unayotegemea lakini naamini kwa ushirikiano wetu na TAMISEMI tumeweka mkakati mzuri sana ambao tutaboresha eneo hilo baada ya muda siyo mrefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi Mbunge wa Malinyi sasa aulize swali lake.

Na. 540

**Mpango wa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa la Chakula**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza: -

Je, mpango wa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa la chakula umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo Mheshimiwa Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kutekeleza mpango wa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa imeendelea na jitihada za kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ambapo mkoa una jumla ya skimu 233. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 zaidi ya shilingi bilioni 15 zilitengwa kwa ajili ya kuendeleza skimu za umwagiliaji ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mkandarasi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu wa Bonde la Kilombero na Ifakara amekwishapatikana ili kupitia taarifa hiyo ya miradi mipya ya umwagiliaji iweze kuanzishwa na kuongeza uzalishaji. Sambamba na hilo, Serikali inaendelea kuboresha huduma za ugani, upatikanaji wa pembejeo sahihi ikiwemo mbegu bora na mbolea na uimarishaji wa miundombinu ya uhifadhi wa mazao baada ya mavuno.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri kwa majibu yake. Sasa swali la kwanza, sehemu kubwa ya bonde la Kilombero imechukuliwa kama hifadhi, maeneo ambayo wakulima walikuwa ndio wanalima kupata chakula.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka miradi ya umwagiliaji ya kutosha ili chakula kisipungue?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kuwa na ghala moja la chakula naona kama ni *risk*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ghala jingine la chakula hasa kuliweka katika mikoa ile inayozalisha sana ikiwemo Mkoa wa Ruvuma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Katika swali lake la kwanza, katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Morogoro kupitia bajeti yetu tulitangaza hapa ndani Bungeni kwenye kiambatisho namba tano cha bajeti yetu. Tumelezea vizuri kabisa kwamba Serikali inakwenda kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde ya kimkakati 22, na mabonde matatu yatatoka ndani ya Mkoa wa Morogoro, yaani kwa maana ya bonde la Kilombero ambalo lina hekta 53,340. Tuna bonde la Usangule ambalo linakwenda kuhudumia mpaka Malinyi ambalo lina hekta 2,500 na tuna bonde la Ifakara - Idete ambalo linagusa Wilaya yote ya Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika eneo lake la Malinyi tunao mradi ambao unaendelea mradi wa Itete

wa *scheme* ya umwagiliaji ambao pia utasaidia kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, Serikali inayo dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha ile mikoa mitano ambayo ndio Ghala la Taifa la Chakula kuendelea kuimarisha huduma mbalimbali, hasa katika upatikanaji wa huduma za ugani lakini vile vile na upataikanaji wa pembejeo za mbolea ili wakulima wetu waweze kulima na kuongeza tija, ikiwemo Mkoa wa Ruvuma ambao ni kati ya Mkoa unaofanya vizuri sana kwenye kilimo cha mazao ya chakula.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliongeza zao la parachichi kama zao la kimkakati na katika kutimiza ajenda hiyo, iliamua kuanza ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuchakata parachichi kilichopo Nyololo Mufindi ili isaidie mikoa yote ya Nyanda za juu Kusini. Hata hivyo mpaka sasa hivi ujenzi haujaanza.

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya mradi huu muhimu sana kwa wananchi wa Mufindi na …kwa ujumla?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI W KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika bajeti yetu ya mwaka 2022, 2023 tuliweka mpango wa kujenga *common use facilities* mbili. Moja itajenga Wilaya ya Hai Mkoa wa Kilimanjaro na moja inajengwa nyololo Jimboni kwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa njema Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekamilisha taratibu zote za awali na muda si mrefu mkandarasi atapatikana na kazi ya ujenzi wa *common use facilities* itaanza. Kazi hii ikianza itawapa nafasi wakulima wote wa parachichi kukusanya maparachichi yao

sehemu moja, tukafanya *collection,* tukafanya *grading* na *sorting* na baadaye *packaging* ili maparachichi yetu ya Tanzania ionekane duniani kwamba ni *produce of* Tanzania kuliko hivi sasa ambapo maparachichi mengi yanakwenda katika nchi za jirani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stansalaus Nyongo sawali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kwamba maghala mengi yamejengwa maeneo ambayo mikoa inazalisha chakula, tunakubaliana nayo. Lakini pale kuna mikoa mingine uzalishaji wa chakjula ni kidogo sana na mvua ni za shida. Inapotokea shida ya chakula kunakuwa tena kuna gharama ya kusafirisha; gharama ya fedha na gharama ya muda kutoka maeneo yanayozalisha chakula kwenda kwenye maeneo yasiyozalisha chakula.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka maghala vile vile katika maeneo ambayo mikoa inazalisha kidogo chakula kama Mkoa wa Simiyu na hasa maeneo amabayo yana shida ya chakula? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu ambayo inamalizikia tumetenga shilingi 25 kwa ajili ya ujenzi wa maghala na tumeangalia maeneo yote. Kwa mfano katika Mkoa wa Simiyu hivi sasa kupitia mradi wa *TANIPAC* wa sumu kuvu tumebadilisha matumizi ya ghala lile ili ibaki kuwa sehemu ya ghala kuhudumia Mkoa wa Simiyu na mikoa Jirani ambao uzalishaji wake si mkubwa sawa na mazao ya chaklula ili inapotokea changamoto ya chakula cha msaada basi tuweze kukipeleka kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumezingatia pia jiografia hiyo na uzalishaji katika maeneo husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa sasa aulize swali lake.

Na. 541

**Mikopo kwa wakulima wa kahawa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwakopesha fedha wakulima wa kahawa ili kuondokana na biashara ya butura?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kwa kushirikiana na taasisi za kifedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB),* imeendelea kuwaunganisha wakulima kupitia Vyama vya Ushirika na kuwapatia mikopo na masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imeendelea kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani, Soko la Bidhaa Tanzania pamoja na wadau wengine kuweka mfumo rasmi wa masoko na uuzaji wa kahawa za wakulima Mkoani Kagera ili kuwezesha wakulima wa kahawa kupata masoko ya mazao yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba wakulima wanapata soko la uhakika. Lakini inapofika kipindi cha mavuno ya kahawa kumekuwepo na vitendo vya kuwakamata wakulima wanaotoka kata *A* kwenda kata *B* kuvuna kahawa kwa kuwanyang'anya kahawa na kutaifisha ile kahawa;

Je, ni nini tamko la Serikali juu ya vitendo hivi ambavyo havifai?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mibuni mingi mkoani Kagera imekauka kwa sababu ya ugonjwa wa mnyauko. Tumeangalia kwenye bajeti tumetengewa mibuni (miche ya kahawa) michache;

Je, Serikali iko tayari kuongeza miche mingine ya kahawai li kukidhi mahitaji ya wakulima wa Mkoa wa Kagera?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikubaliki na hairuhusiwi kumkamata mkulima mwenye mazao yake anayoyatoa sehemu moja Kwenda sehemu nyingine ndani ya Wilaya husika, isipokuwa kama mkulima anayatoa shambani kupeleka kwenye *AMCOS* kwa ajili ya Kwenda kufanya *aggregation* hapo ni makosa kumkamata. Vile vile kama kuna mfanyabiashara ambaye pia na yeye anatoa mazao hayo kutoka kwenye *AMCOS* kupeleka kwenye viwanda lazima tuhakikishe awe ana nyaraka ambayo inamruhusu ili kuondokana na usumbufu. Lakini katika ujumla wake Serikali haiwezi kuwa sehemu ya kuzuia maendeleo ya mkulima; na ninatoa maelekezo katika uongozi wa maeneo husika kuhakikisha kwamba wanawalinda wakulima na wasiwanyanyase wakulima katika mazao ambayo wanayalima wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuhusu mibuni. Ni kweli mibuni mingi hivi sasa imeshatimiza zaidi ya miaka 25 na kimsingi imezeeka na inapunguza sana uzalishaji. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa maana ya *TaCRI* pamoja na Bodi ya Kahawa tunaendelea na uzalishaji wa miche ya kahawa. Mwaka huu tumeendelea kuzalisha miche 20,000,000. Vilevile tutaongeza uzalishaji wa kahawa kupitia teknolojia ya chupa ili kuongeza

wigo mpana zaidi na wakulima waweze kupata miche mingi na kwa uharaka zaidi ili kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Mwaka jana Jimbo la Mbulu Vijijini na Jimbo la Babati na Mbulu Mji wakulima waliahidiwa kukopeshwa kulima vitunguu, mahindi katika eneo hilo. Kwa bahati mbaya hawakukopeshwa mpaka msimu umeanza mpka leo.

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilichukue jambo hili la Mheshimiwa Mbunge niende kulifanyia kazi na kufahamu nini ilikuwa ni changamoto ili tuweze kulitatua na changamoto hiyo isijirudie tena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Zao la mkonge ndiyo dhahabu yetu ya Mkoa wa Tanga kwa sasa. Zao la mkonge linachukua miaka mitatu toka kulihudumia mpaka kuanza kuvuna. Wakulima wengi wadogo wadogo wanaoanza wanashindwa pale mwanzo kwa sabbau ya kusubiria miaka mitatu kabla ya kuvuna;

Je, Wizara haioni haja sasa ya kuja na mkakati wa kuwawezesha wakulima wadogo wadogo ili kuedelea kuleta hamasa kwenye zao hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye zao la mkonge Serikali imefanya yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, tumeendelea kuongeza uzalishaji wa miche ya kutosha kupitia *TARI* Mlingano pale Mkoa wa Tanga, na hivi sasa tunajenga maabara ya *tissue culture* kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa miche hii ya mkonge ili wakulima wengi zaidi waweze kuhamasika. Pili; tunahakikisha ya kwamba katika mwaka huu wa fedha tunanunua *decorticators* mbili, ile *corona,* kwa ajili ya uchakataji wa mkonge ili mkonge mwingi zaidi uweze kuchakatwa na kuongeza hamasa ya wakulima kulima zaidi; na la tatu, tunaendelea kuunganisha wakulima wetu na taasisi mbalimbali za kifedha ili waweze kukopesheka na kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la mkonge. Na la mwisho, kwa sababu katika ulimaji wa mkonge kuna *spacing* tumekuwa pia tukiwahamasisha pale katikati kulima mazao mengine ya haraka ili yawasaidie kuiongeza tija na kuongeza kipato katika aina ya zao ambalo wanalilima.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 542

**Ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa hadi Manda na Mkiu – Liganga hadi Madaba**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara za Itoni – Ludewa – Manda na Mkiu – Liganga – Madaba kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda yenye urefu wa kilometa 211.42 inajengwa kwa kiwango cha zege kwa awamu. Hadi sasa, Serikali imekamilisha Sehemu ya Lusitu – Mawengi kilomita 50. Kwa sehemu ya Itoni – Lusitu kilomita 50 kazi za ujenzi kwa kiwango cha zege zinaendelea. Kwa sehemu iliyobaki ya kutoka Mawengi – Manda kilomita 98.1, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara ya Mkiu – Liganga – Madaba yenye urefu wa kilomita 112 inayounganisha barabara ya Itoni – Ludewa hadi Manda na barabara kuu ya Makambako – Songea katika maeneo ya Mkiu na Madaba Mtawalia, tayari imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikihusisha sehemu ya Liganga Nkomangómbe kilomita 70 na Nkomangómbe – *Coal Power* kilomita 4.14. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani nyingi kwa Serikali kwa kukamilisha kipande cha Lusitu - Mawengi na kuanza kipande cha Itoni – Lusitu ambapo kipande kile cha mwanzo kilitumia bilioni 179 cha pili bilioni 90 bado ninaomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, pale Mawengi wakati wanajenga ile barabara kuna wananchi wachache ambao hawakulipwa fidia wamekuwa wakihangaika sana;

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wale ili waache kuhangaika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ningepena kufahamu Serikali imejenga barabara nyingi Ludewa lakini haijaweka taa za barabarani;

Je, ni lini Serikali itakwenda kuweka taa za barabarani hasa maeneo yenye miji ambayo yana wananchi, ili mji wetu uweze kuonekana wa kisasa zaidi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kamonga Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia; wananchi hawa ni kweli walikuwa hawajalipwa na ni kwa sababu zoezi wakati la ulipaji linaendelea hawa wananchi hawakuwepo. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi hao waweze kumuona Meneja wa Mkoa wa Njombe ili aweze kuwapa taratibu zitakazofanyika namna ya kuwalipa wananchi hawa ambao walipisha ujenzi wakati wa mradi huu, hawa wananchi wa Mawengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu taa za barabarani. Kama tulivyosema sehemu zote za wilayani na kwenye miji ama *center* kubwa ni mpango sasa wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaweka taa za barabarani. Na katika mwaka wa fedha ujao nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge moja ya eneo ambalo litafaidika kuwekewa taa ni pamoja na mji wa Ludewa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Ndakidemi swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha barabara ya Kibosho *Shine* hadi kwa Rafael kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Prof. Ndakidemi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ya Kibosho *Shine* kwenda kwa Rafael ina hudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania lakini kuna kipande ambacho pia kinahudumiwa na wenzetu wa *TARURA*. Kwa upande wa barabara ambayo kwa sasa inahudumiwa na *TANROADS* ni mpango wetu kuhakikisha kwamba tunaijenga yote kwa kiwangio cha lami, na hadi sasa mkandarasi yuko *site*. Na katika mwaka unaokuja pia tumetenga fedha kuendelea na ujenzi kwa awamu kwa kiwango cha lami ili kuikamilisha barabara yote hiyo kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza;

Je, lini Serikali itakamilisha barabara ya kutoka Mji Mwema mpaka Pemba Mnazi ni ya muda mrefu sana?

Je, lini sasa itakamilisha kipande cha kutoka Gomvu mpaka Pemba Mnazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Mbunge hasa lile eneo la mwisho sijamsikia vizuri.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Je, Serikali lini itakamilisha kipande cha Gomvu mpaka Pemba Mnazi katika Wilaya ya Kigamboni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nataka kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishafanya taratibu na tuko kwenye hatua za manunuzi kwa maana ya kujenga barabara ya kilometa 41 kwa kiwango cha lami. Barabara ambayo ametaja kilometa 41.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 543

**Ujenzi wa barabara ya Tarime – Mugumu**

**MHE. MWITA W. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa barabara ya Tarime – Mugumu utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa Barabara ya Tarime – Mugumu kilomita 87.14 kwa kiwango cha lami kwa awamu. Ujenzi kwa kiwango cha lami awamu ya kwanza sehemu ya Mogabiri – Nyamongo kilomita 25 unaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 15. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za manunuzi za kumpata Mkandaraasi atakayetekeleza ujenzi wa sehemu ya pili ya kutoka Tarime Mjini – Mogabiri na Nyamongo hadi Mugumu zenye jumla ya kilometa 62.14.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA W. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara inaunganisha Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Serengeti na ndiyo barabara ya kwanza ya lami katika Jimbo la Tarime Vijijini. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kupeleka fedha hapa kujenga barabara hii. Lakini kwa majibu ya Serikali barabara hii imefika asilimia 15, na tumeambiwa Tarehe 24 Mwezi wa Januari Mwaka kesho tunakabidhiwa barabara ya lami. Lakini mkandarasi alipeleka *certificate* Serikalini Oktoba 2022 akidai milioni 874, hajalipwa. Akapeleka *certificate* ya pili Machi 2023 akidai milioni 841, hajalipwa. *Certificate* ya tatu ni Mwezi wa tatu mwaka huu ambayo ni bilioni 1.6.

Je, ni lini, Serikali italipa fedha hizi ili tupate barabara ile Januari mwakani kutengeneza kura za Chama Cha Mapinduzi katika jimbo langu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Barabara hii ina *center* ya Mogabiri, *center* ya Nyamwigora, *center* ya Kimakolele, *center* ya Nyarero, *center* ya Kiwanja, *center* ya Gena na kule Nyamongo;

Je, maeneo haya tutawekewa taa za barabarani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema katika barabara hii ya Tarime – Nyamwaga – Nyamongo hadi Mugumu, tumeainisha maeneo sita ambayo yatawekwa taa. Yale maeneo yote, vijiji vyote vile vikubwa, maeneo sita yatawekewa taa na Mheshimiwa Mbunge pengine baada ya hapa anaweza kuja nimwoneshe vijiji ambavyo vitawekewa taa katika hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi unaoendelea, mkandarasi bado yupo *site* anaendelea kujenga na tuna hakika changamoto iliyokuwepo kubwa ya barabara hii ni mvua kubwa inayoendelea kunyesha. Sasa Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba, kasi ya ujenzi itaendelea na hasa kwa kuwa Serikali sasa tumeshajipanga kuhakikisha kwamba, changamoto zilizokuwepo za malipo yote tunakamilisha na mkandarasi ataendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kipande kilichobaki tunategemea ikiwezekana kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha tutakuwa tumesaini mkataba kwa ajili ya barabara nzima hiyo ya Tarime – Nyamwaga hadi Mugumu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nawaona, ila muda wetu umeisha. Mheshimiwa Askofi Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Barabara ya Tegeta – Basihaya – Bunju mpaka Bagamoyo katika Jimbo la Kawe imejengwa bila mitaro ya maji. Kwa sababu hiyo, husababisha mafuriko makubwa sana kwenye maeneo ya Nyaishozi, Tegeta, Nyamachabes. Sasa, ni lini Serikali itajenga mitaro ya maji kuepusha hatari kwa wananci kwa sababu ya mvua zinazoendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Askofu Gwajima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua katika kipindi hiki mvua imeendelea kubwa sana kwa Jiji la Dar-es-Salaam na eneo alilolitaja kwa kweli limeathirika kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo aliyoyataja yote ya Basihaya, Msikitini, *DAWASA* na Nyaishozi yalikuwa yamefanyiwa *design* yaanze kujengwa kabla, lakini kwa kuwa tuna Mradi

mkubwa wa *BRT IV* maeneo haya yatakuwa ni sehemu ya ujenzi wa Mradi huo wa *BRT IV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Jimbo la Kawe, tulichokifanya, tutawahusisha na tumehusisha pia *TARURA* ili wakati wa kujenga pia hiyo mitaro na wenzetu wa *TARURA* tusije tukajenga halafu kuwe na changamoto kwenye barabara zetu, kwa hiyo nao watahusika. Mkataba uko tayari kusainiwa. Kwa hiyo, muda wowote kazi ya ujenzi kwa *BRT IV* itaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini? Inawezekana hata ikawa Juni tukasaini huo mkataba. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Maswali na Majibu asubuhi hii…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo machache, kuna matangazo; kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni viongozi kutoka *ALMA*; kwanza ni Ndugu Joy Phumaphi ambaye ni *ALMA Executive Secretary;* Dkt. Abraham Mnzava ambaye ni *Senior Malaria Advisor and Director of ALMA* Tanzania*;* yupo pia Ndugu Diego Duque ambaye ni *ALMA Senior Program Officer* na yupo Dkt. Adiel Mushi ambaye ni *Coordinator Tanzania End Malaria Council,* ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ambao ni viongozi kutoka *Chocolate Princess Limited (The Mboni Show)* ambao ni Ndugu Mboni Ally Masimba ambaye ni Mkurugenzi wa *Chocolate Princess Limited* na *Host* wa *The Mboni Show. (Makofi)*

Yupo Ndugu Hassan Hussein Farouq ambaye ni Meneja wa *Chocolate Princess Limited;* yupo Ndugu Ally Salum Mtama *(Mc Mtama)* ambaye ni Meneja Msaidizi wa *Chocolate Princess Limited;* yupo Ndugu Edwin Mwimike Luvanda *(MC Luvanda)* ambaye ni Mratibu wa *Chocolate Princess Limited* na yupo Ndugu Joseph Meshack Chitinka ambaye ni Mratibu pia wa *Chocolate Princess Limited,* ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana ambaye ni Mbunge na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo; kwanza ni Ndugu Saidi Yakubu ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, karibu sana, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Nicholas Mkapa ambaye ni Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Jacqueline Woiso ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Bodi ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania na Afisa Mtendaji Mkuu wa *DSTV;* yupo Ndugu Consolata Mushi ambaye ni Katibu Mtendaji BAKITA na yupo Ndugu Dorin Sinare ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa *COSOTA,* ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Neema Msitha ambaye ni Katubu Mtendaji BMT, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Richard Mganga ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Nyakaho Mahema ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania na yupo Ndugu Michael Kadebe ambaye ni Rais wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Jonathan Bitababaje ambaye ni Mwakilishi Mkurugenzi Mtendaji wa *NBC. (Makofi)*

Yupo Ndugu Stephen Munguto ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa *TFF. (Makofi)*

Yupo Ndugu Wilfred Kidao, Katibu Mkuu *TFF;* yupo Ndugu Mwasiti Badi ambaye ni Mwakilishi Mkurugenzi wa Mkuu *Azam Media* na yupo Ndugu Jacob Steven (JB) Mjumbe wa Bodi ya Filamu Tanzania, ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge naomba kurudia; yupo Ndugu Jacob Steven (JB) ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Filamu Tanzania, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Ali Tembele ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Emmanuel Ishengoma ambaye ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa na yupo Ndugu Emma Lyimo ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Chifu Makomelo Ernest; yupo Ndugu Aron Mikomangwa ambaye ni Katibu wa Machifu Tanzania na yupo Ndugu Chifu Mazengo ambaye ni Chifu Mkuu Kanda ya Kati Dodoma. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Zuhura Soud (Zuchu) ambaye ni Mshindi wa Tuzo za Muziki za BASATA, 2022. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mrisho Mpoto (Mjomba) ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu *Mjomba Music Band. (Makofi)*

Yupo Ndugu Emmanuel Mgaya (Masanja) ambaye ni Mchekeshaji wa *Original Comedy. (Makofi)*

Yupo Ndugu Lucas Mhavile (Joti) ambaye pia ni mchekeshaji. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Conrad Kennedy (Coy Mzungu) ambaye ni mchekeshaji pia. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Vicent Kigosi (Ray) ambaye ni muigizaji. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Yvonne Cherri (Monalisa) ambaye pia ni muigizaji na yupo Ndugu Salim Ahmed (Gabo) ambaye pia ni muigizaji, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Doris Mzirai ambaye ni Meneja wa Msanii Zuchu, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana ambaye ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambao ni kwanza ni Watendaji, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Wapo pia Wawakilishi wa Wanufaika wa Mikopo inayotolewa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Wapo pia Wajumbe wa Chama cha Maafisa Utamaduni na Sanaa na wapo pia Wajumbe wa Shirikisho la Sanaa za Maonesho, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Wajumbe wa Chama cha Waigizaji Tanzania, wapo Wajumbe wa Chama cha Watafuta Mandhari Tanzania; wapo viongozi wa Chama cha Wahariri wa Filamu Tanzania na wapo pia Wajumbe wa *Adorable Wedding Trade Fair,* ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 49 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Maji ambao ni familia yake, Wachungaji na Wanakwaya wa Kanisa la Moraviani Magharibi, Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa David Kihenzile ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bunge, Ndugu Oscar Petro maarufu kama Oscar Nyerere, Msanii pekee aliyevaa kofia ya kuigiza sauti ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa kwangu kutoka Babati ambao ni wapigakura wangu, ahsante na karibuni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga, Ndugu Emanuel Mathias ambaye ni *MC Pilipili* na Ambwene Mwasongwe kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda ni walimu kutoka Jimbo la Newala Vijijini, ahsante. *(Makofi)*

Wapo wageni saba wa Waheshimiwa Wabunge wote kutoka Mkoa wa Manyara ambao ni viongozi wa UVCCM, Mkoa wa Manyara. Mimi pia ni wageni wangu hao, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambao ni wafanyakazi wa *Daniel Company* kutoka Jijini Dodoma, ahsante sana, karibuni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze kutoka Nguruka, Mkoa wa Kigoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 63 wa Mheshimiwa Agnes Marwa ambao ni wanafunzi na walimu 24 kutoka Shule ya Msingi *Kingdom* ya Kinondoni, Jijini Dar es Salaam, ahsante sana na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye Jukwaa la Spika yupo pia Ndugu Murtaza Mangungu ambaye ni Mwenyekiti wa *Simba Sports Club,* karibu sana. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, inatosha. Nashukuru sana. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwenye Jukwaa la Spika pia yupo Ndugu Leodgar Tenga ambaye ni Rais wa BMT, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Charles Kajege ambaye ni Binti yake anayeitwa Erica Charles Kajege, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni wa Mheshimiwa Taletale ambao ni mabondia; kwanza ni Ndugu Twaha Kassim,

Ndugu Ibrahim Nyange, Ndugu Karim Ngwelo, Ndugu *Power* Ilanda na Ndugu Jackson Busanda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge liko tangazo kutoka Kamati ya Maandalizi ya Bunge Bonanza; Kamati inawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Siku ya Jumamosi, tarehe 24 Juni, 2023 kutafanyika Tamasha la Pili la Michezo na Burudani lijulikanalo kama *Bunge Grand Bonanza* lenye kauli mbiu Tupende Michezo Tujenge Taifa Letu.

Aidha, bonanza hilo litahusisha michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa wavu, mpira wa meza, kutembea kwa haraka, kurusha vishale, kuvuta kamba, kurusha tufe, riadha, kukimbia na gunia, mchezo wa bao, mchezo wa karata na kufukuza kuku.

Lengo la bonanza hili ni kuhamasisha Wabunge na watumishi wa Bunge kufanya mazoezi kwa ajili ya kujenga mwili, kuimarisha afya, kutoa burudani, kuimarisha na kuendeleza ushirikiano kama taasisi, hivyo kuongeza tija katika kazi. Bonanza hilo ambalo linadhaminiwa na Benki ya CRDB litafanyika katika Shule ya Sekondari ya John Merlin, Miyuji, Jijini Dodoma na kufuatiwa na tafrija jioni katika viwanja vya Bunge ambako pia kutakuwa na burudani kama vile kucheza dansi, uimbaji, ngoma za jadi na utamaduni, ushairi na utenzi, kuimba taarab, muziki wa kufoka *(rap music),* maonesho ya mavazi na ucheshi.

Kwa tangazo hili Waheshimiwa Wabunge na watumishi ambao hawajajiandikisha katika michezo mbalimbali wanaombwa wajiandikishe na kuendelea kujiandaa na bonanza hilo kwa kushiriki kikamilifu katika mazoezi kabla ya siku hiyo, ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali. Kwamba, Bunge sasa…

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Kiti. Mheshimiwa Waitara.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba Mwongozo wa Kiti kwa mujibu wa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati anajibu swali Namba 538 kuhusu bei ya umeme shilingi 27,000 na bei ya umeme katika maeneo hayo hayo shilingi 321,000, alitoa maelezo hapa ambapo pia jana maelezo hayo aliyatoa kwamba wanasubiri kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kuweza kujua ni nani alipe shilingi 27,000 ya umeme na nani alipe shilingi 321,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maelezo ya Serikali ni maelezo ambayo yanaumiza watu kwenye maeneo yetu ambayo tunayawakilisha Wabunge hapa. Maeneo haya yanafahamika vizuri, nimeshasema kwa mfano pale Nyamwaga ni kijijini, Kilindi ni kijijini, Nyangutu ni kijijini, Kiwanja ni kijijini na vigezo vilivyotumika sio sawasawa, yaani kuna eneo lilikuwa labda umepeleka Kituo cha Polisi, eti hicho kinakuwa kigezo cha kupandisha bei ya umeme iwe shilingi 321,000. Kuna mahali tumepeleka kituo cha afya.

Sasa miradi ya kijamii ambayo Serikali imeipeleka kwenye maeneo yetu, haiwezi kugeuzwa kuwa adhabu tena ya watu kunyimwa huduma ya umeme eti kwa sababu, kuna huduma hizo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili Kiti chako kitupe Mwongozo kwa sababu huu uchambuzi ambao unafanyika na usanifu wa kina maana yake ni kwamba, wananchi wetu wanaendelea kunyimwa umeme mpaka mchakato ukamilike. Kama Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitoa maelezo kama vigezo itakuwa imetuonea sana watu wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kiti chako kwa sababu, jambo hili watu hawapati umeme na watu wanalalamika.

Umeme unapita nyumbani kwa mtu jirani kabisa halafu mwenzake mwenye uwezo ameweka wale maskini hawana huduma ya umeme. Mpango wa Serikali ni kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote na vijiji vyote bila kubagua watu. Hii ilikuwa ni ahadi ya Serikali, umeme utapelekwa vijijini kwa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili ulipe uzito ili Waheshimiwa Wabunge wenzangu wasirudie tena kuuliza maswali haya. Serikali ijibu *once and for all* ili watu waweze kupata umeme, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi pia nasimama kwa Kanuni ya 76, Mwongozo ni kwenye swali Namba 541. Wakati Naibu Waziri akijibu swali kuhusu kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo au ufafanuzi ninaotaka niupate kwako ni kwamba, wananchi wa Wilaya ya Kyerwa na ukifika wakati huu ambao ni wa mavuno ya kahawa imekuwa siyo tena wakati wa neema, umekuwa ni wakati wa kunyanyaswa na kupigwa kwa kisingizio kwamba moja, wananunua magendo; mbili, wanavusha kahawa; tatu, wananunua ndiyo huo butura tunasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tukio la kushangaza juzi, kama siku tatu zilizopita, wananchi wa Kata ya Murongo, Kijiji cha Masheshe, kuna mwananchi mmoja alikuwa anatoa kahawa shambani analeta nyumbani akavamiwa nyumbani kwake, akapigwa na Wanajeshi, akapigwa na Askari, eti sababu anavusha kahawa, anataka kupeleka kahawa Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala halijatokea Masheshe tu, halijatokea Murongo tu ni suala ambalo linafanyika kila siku Bugomora, ni suala ambalo linafanyika Kibale na Kata nyingine ambazo zinazunguka mpaka wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue, hata kama alikuwa na wazo lolote la kufanya kitu ambacho hakiko sahihi, kwamba anavusha kahawa, ambacho najua siyo kweli. Je, mwongozo wako unasemaje, ni sahihi kwa wanajeshi kuendelea kujichukua hatua na kuwapiga wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaweza tukawa humu ndani tunaendelea kujadili wakati kuwa Watanzania wanaonewa, wanasingiziwa, wanavunjwa mikono na kunyang'anywa kahawa yao na hasa hivi tunapoenda kwenye msimu wa kahawa. Ninataka mwongozo wako katika namna sahihi ya ku-*deal* na hizo *issues,* lakini pia usalama wa mwananchi kutoa kahawa yake shambani na kuikausha nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako katika hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wamesimama Wabunge wawili, amesimama Mheshimiwa Mwita Waitara, kwa mujibu wa Kanuni ya 76 akiomba Mwongozo wa Kiti kama jambo lililotokea mapema leo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 76.

Sasa kwa sababu jambo hili linahusu swali Na. 538 ambalo liliulizwa kwa Wizara ya Nishati, basi namwelekeza Mheshimiwa Waitara alete swali hilo kama swali la Msingi ili lipate majibu sahihi ya Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia amesimama Mheshimiwa Anatropia akizungumzia swali Namba 541 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kwenye Wizara hii ya Kilimo, naomba pia Mheshimiwa Anatropia kwa sababu umezungumza jambo hili kwa uchungu, basi ulilete kama swali la Msingi ili Serikali ilete majibu sahihi. Ahsante sana na huo ndiyo Mwongozo wangu. *(Makofi)*

Katibu.

**6 JUNI, 2023**

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ili awasilishe hoja yake ya Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2023/24, Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu 96 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama tulivyowasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini, kuniteua kuwa Waziri wa Wizara hii muhimu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, hasa kipindi hiki ambapo masuala ya utamaduni na sanaa yanakwenda vizuri kabisa, lakini pia timu zetu nchini zinafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana katika nchi yetu, ni Wizara ambayo kwa maneno mengine naweza kusema ni Wizara yenye nguvu shawishi *(soft power)* ya nchi, kwa maana ya kuwa inawaleta wananchi wenye itikadi tofauti pamoja, inaimarisha mshikamano na ushirikiano, inaleta furaha miongoni mwa wananchi, inadumisha amani, kujenga na kuimarisha afya za wananchi. Pia, inatoa ajira nyingi kupitia

michezo na Sanaa, na leo hii tumeshuhudia wadau mbalimbali wakitambulishwa hapa kwenye Bunge lako tukufu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, chambilecho wahenga, chanda chema huvikwa pete, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa maendeleo ya nchi yetu. Pia, nimpongeze kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka miwili ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta zetu ambayo yametokana na uongozi wake ulio mahiri, wenye weledi, umakini na upeo mkubwa unaoendelea kuliimarisha Taifa letu ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi na wadau wetu wote wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo tunamuahidi Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuendelea kumpa ushirikiano, kuchapa kazi kwa bidii na kwa weledi ili kuendana na fikra, maono, na falsafa yake ya "Kazi Iendelee". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa namna alivyo mstari wa mbele kwa kuwa kichocheo cha ukuaji wa Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo hivi karibuni tumeshuhudia akiridhia Kocha wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kulipwa mshahara na Serikali. Aidha, ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wake katika michezo, Mheshimiwa Rais alinunua tiketi 2,000 wakati wa mchezo wa Timu ya Taifa dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda *(The Cranes)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, amehamasisha Timu zetu za Yanga na Simba ambazo zimeshiriki mashindano ya Kimataifa ngazi ya Afrika kwa kuwazawadia kila goli lililofungwa katika mashindano hayo shilingi milioni tano katika hatua ya makundi. Hamasa hiyo iliendelea kwa timu hizo zilipofika hatua ya robo na nusu fainali kwa kutoa zawadi ya shilingi milioni kumi kwa kila goli lililofungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua ya fainali tumeshuhudia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongeza dau kwa kuzawadia kila goli shilingi milioni ishirini. Aidha, ameweza kununua

tiketi 5,000 zenye thamani ya shilingi milioni ishirini na tano kwa ajili ya mashabiki kuingia kuishangilia timu ya Yanga katika mchezo uliofanyika tarehe 28 Mei, 2023 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya *USM Algiers. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ametoa usafiri wa ndege ya kuipeleka Timu ya Yanga na baadhi ya mashabiki wake Nchini Algeria. Waliporudi waliandaliwa chakula malumu, sote tumeshuhudia jana usiku katika hafla maalumu ya kuwapongeza wachezaji wa timu hiyo na uongozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hiyo tu, katika hafla hiyo pia walialikwa wadau wa michezo mbalimbali, tumeona Timu ya Simba iko pale, Azam iko pale, timu mbalimbali zilikuwepo. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuleta Watanzania wote pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Mheshimiwa Rais ndiyo chachu ya mafanikio ya timu za Simba na Yanga katika mashindano haya na kufikia fainali kwa Timu ya Yanga, na kama ambavyo waswahili husema mwana hutazama uchogo wa mamaye, timu zimemuahidi kuendelea kuongeza jitihada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. Kwa hakika kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nikupongeze wewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza kwa busara kabisa na weledi Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ninawapongeza Wenyeviti wote, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile pamoja

na wewe mwenyewe Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kusimamia vema na kwa ustadi mkubwa kabisa mijadala ya kibajeti katika Bunge lako tukufu. Tumeona hakika mnaupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona zinduna na ambari iko nyuma yake, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri, michango na maoni yao kwa Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, papo kwa papo kamba hukata jiwe, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa Wizara wakiwemo viongozi na watumishi wa Wizara ambao leo asubuhi nimewatambulisha, tuko nao hapa, umoja ni nguvu. Natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu wa Wizara wakati wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu na mageuzi makubwa tunayoendelea nayo Wizarani na katika sekta zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma *a.k.a.* Makita wanakwambia Kwalakabu Mwana-FA, Naibu Waziri makini kabisa wa Wizara yangu, kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Saidi Yakubu, Katibu Mkuu, anayehakikisha mambo yanakwenda na mageuzi yanatokea. Nimshukuru pia Nicholas Mkapa, Naibu Katibu Mkuu mwenye jukumu la kuhakikisha ufanikishaji na kusonga mbele katika mageuzi makubwa ya tasnia za Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wanaofanya kazi kwa bidii usiku na mchana na wanahakikisha mambo yanatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuendelea kukushukuru wewe kama nilivyosema awali, lakini pia tunasema mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani, ninawashukuru wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Njombe, kwa kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu na kwa wakati wote kunipa ushirikiano. Naomba waendelee kuniamini kwani mwana hasahau mkono uliomlea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia dira ya Wizara, majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mipango, miradi na programu mbalimbali katika sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuendeleza shughuli za Utamaduni, Sanaa na Michezo na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na rasilimali watu Wizarani na kusimamia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania *(COSOTA),* na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Vilevile, Wizara inaratibu na kusimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ilikadiria kukusanya shilingi milioni mia tisa kutoka kwenye vyanzo viwili ambavyo ni mapato yatokanayo na Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru pamoja na ada za mafunzo na mitihani kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Vyanzo vyote vinatoka Idara ya Maendeleo ya Michezo. Hadi kufika mwezi Aprili, 2023 shilingi 688,839,509 sawa na asilimia 76.5 ya lengo zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni shilingi 5,396,455,000 ambapo kiasi cha shilingi 2,998,315,611 sawa na asilimia 55.5 ya lengo zilikuwa zimekusanywa hadi kufikia mwezi Aprili, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya shilingi 35,425,991,000 ambapo kati ya hizo mishahara ilikuwa shilingi 8,201,882,000, matumizi mengineyo ni shilingi 11,392,949,000 na miradi ya maendeleo ni shilingi 15,831,160,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 28,161,934,771 sawa na asilimia 79.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 9,561,380,999 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na taasisi sawa na asilimia 83.9 ya bajeti ya matumizi mengineyo. Shilingi 6,772,390,081 ni mishahara ya Wizara na taasisi sawa na asilimia 82.5 ya bajeti ya mishahara. Shilingi 11,882,163,690 ni miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 74.7 ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Sekta ya Utamaduni ina majukumu ya kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni, lugha na maadili ya Taifa, kuendeleza utambulisho wa Taifa, kuhimiza na kukuza utaifa kwa vijana na wananchi kwa ujumla, kukuza Lugha ya Kiswahili ambayo ni Lugha ya Taifa kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), kufanya tafiti katika uga wa sekta ya utamaduni hususan lugha za kijamii ambazo ni kibebeo cha urithi wa utamaduni wetu na kuratibu na kusimamia shughuli za Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanaendelea kunufaika na utamaduni wao, Wizara iliratibu tamasha kubwa la kitaifa la utamaduni lililofanyika kuanzia Tarehe 01 hadi 03 Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam. Tamasha hilo lilitoa fursa kwa wananchi wetu kufanya matembezi ya kiutamaduni, mashindano ya ngoma za asili, maonesho ya vyakula vya asili, maonesho ya kazi za mikono za kiutamaduni na ubunifu pamoja na kuuza kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ya Jamhuri ya Afrika Kusini iliratibu Tamasha la Msimu wa Utamaduni wa Tanzania na Afrika

Kusini lililofanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro kuanzia tarehe 18 Novemba, 2022 hadi tarehe 4 Desemba, 2022. Aidha, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ya Jamhuri ya Afrika Kusini inaendelea na maandalizi ya Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania linalotarajiwa kufanyika nchini Afrika Kusini mwaka 2023. Mwaka huu sasa watu wetu wa sanaa na utamaduni watakwenda Afrika Kusini. Lengo la tamasha hilo ni kuimarisha ushirikiano na kutangaza kazi za sanaa na utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika matamasha mbalimbali yaliyoandaliwa na wadau wa Utamaduni yakiwemo; Tamasha la 12 la Muziki wa Cigogo, Tamasha la Utamaduni baina ya Tanzania na India kuhusu Mapokezi ya Balozi wa Amani Duniani na Kiongozi wa Kiroho Ndugu Gurudev Sri Sri Ravi Shankar lilofanyika katika Jiji la Dar es Salaam tarehe 24 Agosti, 2022; na Tamasha la Utamaduni kutoka Mkoa wa Mbeya lijulikanalo kwa jina la *Tulia Traditional Dance* lililofanyika kuanzia tarehe 22 - 24 Septemba, 2022 Jijini Mbeya. Tunampongeza sana Mheshimiwa Spika kwa tamasha hili la *Tulia Traditional Dance* Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine ni Tamasha la Utamaduni la Jamii za Watu wa Mwanza tarehe 4 - 8 Septemba, 2022 lililofanyika katika viwanja vya Kisesa Magu Jijini Mwanza na Tamasha la Kwanza la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Jijini Arusha tarehe 9 - 16 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie BAKITA (Baraza la Kiswahili la Taifa). Majukumu ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kuimarisha Lugha ya Kiswahili nchini na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi; kuhimiza matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma; kuratibu utafiti wa Kiswahili kwa kushirikiana na wadau na kuhimiza matumizi fasaha na sanifu ya Lugha ya Kiswahili na kuzuia kimsingi upotoshaji wake. Katika kipindi hiki, mafanikio lufufu yamepatikana kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Lugha ya Kiswahili inazidi kukua na kuendelea, mwezi Agosti, 2022 BAKITA

kwa kushirikiana na wachapishaji liliandaa na kugawa vitabu 1,640 vyenye thamani ya Shilingi milioni 50 kwa Ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani na nchi zinazohudumiwa na ubalozi huo zikiwemo nchi za Polandi, Uswizi, Bulgaria, Hungary, Romania, Jamhuri ya Cheki, Jamhuri ya Slovakia na *Holly See* ambavyo vinakusudiwa kutumika katika vituo na vyuo vikuu vinavyofundisha Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vitabu hivi viligawiwa kwa Klabu ya Kiswahili inayofahamika kama Kijiwe cha Kiswahili nchini Ujerumani ambacho kimetambuliwa na BAKITA kama kituo rasmi cha kufundisha na kuendeleza Kiswahili nchini humo. Pia tumegawa Kamusi ya Kiswahili kwa kila Mheshimiwa Mbunge ndani ya Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni juhudi za kutoa elimu juu ya matumizi fasaha na sanifu ya Lugha ya Kiswahili, BAKITA liliandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 891 kupitia redio na televisheni mbalimbali. Vipindi hivi vililenga kuelimisha jamii kuzingatia matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, BAKITA katika kuimarisha Kiswahili kimataifa, limeendelea na mradi wake wa kuunda kongoo ya Kiswahili ambapo kwa sasa kongoo hiyo ina jumla ya maneno milioni 29, sawa na asilimia 58 ya malengo yake. Kongoo hili linatarajiwa kuwa na jumla maneno milioni 50 na lina manufaa makubwa katika uendelezaji wa lugha kiteknolojia na kuimarisha data, takwimu za uhifadhi wa lugha.

Katika kutekeleza jitihada za Serikali za kuongeza idadi ya wakalimani, BAKITA liliendesha mafunzo kwa wakalimani wa lugha za Kiarabu, Kifaransa na Kiingereza. Aidha, kwa sasa kanzidata ya wakalimani ina wataalamu wasiopungua 118 wa fani hiyo ambapo 25 ni wakongwe katika tasnia na 93 ni wapya ambao walipatiwa mafunzo baada ya Serikali kununua vifaa vya kisasa vya ukalimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fursa hii, napenda nitoe wito kwa Watanzania wote wenye ujuzi wa lugha mbalimbali kukaribia BAKITA kwa ajili ya kupata mafunzo hayo ya ukalimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile BAKITA lilihariri na kutoa ithibati kwa vitabu 94 na moduli saba za ujifunzaji na ufundishaji kwa madarasa ya awali. Vitabu hivi viliwasilishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania, Shirika la *Room to Read* na wachapishaji na waandishi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; heshima ya Taifa letu katika diplomasia, utu, uzalendo, umoja, maadili na utangamano, kimsingi chanzo chake kikubwa ni mchango wa Tanzania katika kuzikomboa nchi za Afrika hususan kusini mwa Bara la Afrika. Ndiyo maana leo hii nchi yetu inasonga mbele inakwenda vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi pekee ya Afrika iliyoanza kupokea wapigania uhuru wa nchi mbalimbali za Afrika. Licha ya vitisho vya udhalimu wa kikoloni, Tanzania ilisimama na Afrika. Hili linajidhihirisha katika Wimbo wa Taifa la Tanzania pamoja na Mwenge wa Uhuru. Mwaka 2011, Umoja wa Afrika, uliridhia kuipa heshima Tanzania ya kuanzisha na kuwa Makao Makuu ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, ambapo iliwekwa chini ya usimamizi wa Wizara yangu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Urithi wa Ukombozi kimeanzisha utalii wa maeneo ya kiukombozi yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika ambapo kwa mwaka 2022/23 zaidi ya watalii 60,152 walitembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo hiki licha ya kupokea watalii mbalimbali kimekuwa pia kikitembelewa na Viongozi mbalimbali waliohusika na mapambano ya ukombozi wa Bara la Afrika. Mfano mzuri tarehe 14 Aprili, 2023 Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Joacquim Chissano alitembelea eneo la makumbusho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa uzingatiaji wa maendeleo ya Utamaduni na Sanaa, Serikali imechukua jitihada za makusudi za kuhuisha Mfuko wa

Utamaduni na Sanaa mnamo tarehe 30 Septemba, 2020 kwa lengo la kukuza na kuendeleza Sekta ya Utamaduni na Sanaa kupitia utoaji wa mikopo au mitaji yenye masharti nafuu na mafunzo ili kuziwezesha kazi za wadau katika sekta hizi kukidhi vigezo vya mahitaji ya soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, Mfuko ulipokea maombi ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 9.2 kutoka kwa waombaji 219. Hadi kufikia tarehe Aprili, 2023 Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,077,000,000 kwa miradi 45 kutoka katika maeneo mbalimbali ya Sekta ya Utamaduni na Sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mikopo hiyo, jumla ya ajira 21,579 zimetengenezwa na miongoni mwa ajira hizo, ajira za kudumu ni 733 na ajira za muda ni 20,846. Aidha, Mfuko umekuwa kichocheo kikubwa kwa wadau katika eneo la urasimishaji kwani mfuko umewahamasisha kurasimisha shughuli zao katika mamlaka mbalimbali kama vile *TRA*, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA),* Halmashauri pamoja na mamlaka nyingine za udhibiti ili waweze kuendesha shughuli zao kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa mikopo hii na ili kupata njia iliyo rahisi ya kuwafikia wajasiriamali wengi wa sekta za Wizara hii, Wizara kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ipo katika hatua za mwisho za kuingia mkataba wa utoaji wa mikopo kupitia taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya Sanaa ni eneo lingine muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na inahusisha Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Taasisi ya Hakimiliki Tanzania na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha sanaa inatumika ipasavyo kulitangaza Taifa kikamilifu, Serikali kwa kushirikiana na BASATA, Kituo cha Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Tanzania (KISUVITA) yenye Makao Makuu yake Nevada, Marekani iliandaa na kuendesha kwa mafanikio makubwa kabisa Shindano la Kimataifa la Urembo na Utanashati kwa Viziwi *(Miss and Mr.*

*Deaf International)* kuanzia tarehe 23 – 31 Oktoba, 2022. Ikiwa ni mara ya kwanza kabisa Barani Afrika, mashindano haya yalifanyika katika Jiji la Dar es Salaam ambapo watu 147 kutoka nchi 43 duniani walishiriki, na kwa taarifa za makusanyo ya kadi, watazamaji 1,478 walifika ukumbini kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shindano hilo, Mtanzania Khadija Kanyama aliibuka Binti Mrembo Zaidi Kiziwi Duniani na Mtanzania Russo Songoro aliibuka Mwanamitindo Bora Zaidi wa Kiume Kiziwi Duniani na Mtanzania mwingine Rajan Ally alishinda nafasi ya pili Mwanaume Mtanashati Zaidi Kiziwi Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha vijana wote nchini wanapata fursa ya ajira na kuonesha vipaji vyao. Serikali kwa kushirikiana na BASATA na Asasi ya *The Music in Africa Foundation* imeratibu kufanyika kwa mara ya kwanza nchini Mkutano mkubwa wa wadau wa Muziki wa Afrika ujulikanao kama *The Music in Africa Conference for collaboration, Exchange and Show Case (ACCES)* uliofanyika kati ya tarehe 24 - 26 Novemba, 2022. Mkutano huo ulizileta nchini kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji, uelimishaji, usambazaji, utumiaji na uratibu wa muziki wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inaendelea na uratibu wa maandalizi ya ujenzi wa sanamu ya Mwalimu Nyerere inayotarajiwa kusimikwa Jijini Addis Ababa Ethiopia katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika ambapo hadi Aprili, 2023 hatua iliyofikiwa ni kuanza kwa ujenzi wa sanamu halisi baada ya Mkandarasi, Kampuni ya *Epitome Architects Limited* ya Tanzania kukamilisha ujenzi wa sampuli kifani *(prototype)* ya pili na kuridhiwa na Kamati ya Kitaifa kwa mujibu wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa (Na. 18) ya Mwaka 2004 na Kanuni zake za Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na mpango wake wa kuwapa fursa Wasanii wa Tanzania kuonesha vipaji vyao kupitia Tamasha la Serengeti *Music Festival*, ambalo kwa sasa linakwenda kufanyika Kimataifa. Tofauti na miaka iliyopita, kwa mwaka 2022/2023, Tamasha hili limeendeshwa kwa mtindo

tofauti kwa kupeleka makundi ya Sanaa na Wasanii mmoja mmoja nje ya nchi kushiriki shughuli za sanaa katika matukio makubwa yenye hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kikundi cha *Safi Theatre* kimeshiriki Maadhimisho ya Miaka 60 ya Umoja wa Afrika katika eneo la *Cradle of Humankind*, *Johannesburg* wakati kikundi cha Singeli cha Sholo Mwamba kikishiriki Tamasha la *African Music Days* ukumbi wa *Muffathalle, Munich* katika maadhimisho ya miaka 60 ya Umoja wa Afrika kati ya tarehe 24 - 25 Mei, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). BASATA limeendelea kuleta mageuzi ya kuboresha muziki wa kizazi kipya kwa kutengeneza Kivunge cha Mtozi *(Producers' Kit)* chenye zaidi ya vionjo 400 vyenye ladha ya asili ya kitanzania. Vionjo hivi vilirekodiwa kutoka kwenye ngoma za makabila mbalimbali ya Tanzania. Matokeo ya Kivunge cha Mtozi ni kuchochea mageuzi ya kuwa na muziki wa kitanzania wenye mdundo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BASATA limeendelea kuwezesha wasanii nchini kwa kuwasajili na kutoa vibali kwa wasanii binafsi 1,188; vikundi 201; kumbi za sherehe, starehe na burudani 261; kampuni 94 na vibali vya matukio 24. Aidha, BASATA limetoa vibali 307 vya wasanii wa Tanzania kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za sanaa pamoja na vibali 52 vya wasanii wasiokuwa Watanzania kuingia nchini kwa ajili ya kufanya shughuli za sanaa. Aidha, BASATA limetoa vibali 64 kwa taasisi vikiwemo vyama, mashirikisho asasi zisizo za Serikali na taasisi binafsi kujishughulisha na sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023. Baraza limendelea na mageuzi ya kiutendaji na kitaasisi ili kuwa mwezeshaji zaidi wa shughuli za sanaa badala ya kudhibiti zaidi. Hayo ndiyo maono ya Baraza la Sanaa Tanzania kuwa mwezeshaji zaidi badala ya kuwa mdhibiti zaidi. Katika utekelezaji huu baraza limeendelea kutokimbilia kuwafungia wasanii, bali kunapotokea changamoto zilizokithiri za kimaadili, Baraza limekuwa likielimisha zaidi wahusika na kuwaelekeza

marekebisho stahiki. Aidha, Baraza limekuwa likiwaita wasanii siyo tu pale wanapokosea, ila hata pale wanapofanya vizuri kwa kweli na kuwapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha wasanii kufanya vizuri katika kazi zao, BASATA limeendelea kutoa Tuzo za Muziki wa Tanzania *(TMA)* kwa mara ya pili mfululizo. Kimsingi Tuzo ya Heshima ilitolewa kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne. Aidha, Tuzo 52 zilitolewa kwa wasanii mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie Bodi ya Filamu Tanzania. Serikali kupitia Bodi ya Filamu ilitoa Tuzo za Filamu kwa wadau waliofanya vizuri katika fani mbalimbali kwenye Tasnia ya Filamu ambapo kilele chake kilikuwa tarehe 17 Desemba, 2022 Jijini Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kupitia programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa. Tunakwenda sasa mtaa kwa mtaa; michezo, mtaa kwa mtaa; Sanaa, mtaa kwa mtaa. Kwa hiyo, kupitia Programu ya Mtaa kwa Mtaa katika Tasnia ya Filamu, Bodi iliandaa mikutano na mafunzo kwa vitendo yaliyotolewa kwa wadau wa filamu na michezo ya kuigiza ambapo jumla ya wadau 750 waliweza kufikiwa na kupewa elimu kuhusu masuala yanayohusu filamu na michezo ya kuigiza katika mikoa 25 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na kuratibu utoaji wa mafunzo, kurudisha utamaduni wa kuonesha filamu kwenye kumbi za sinema ikiwa ni hatua ya kuongeza masoko ya filamu, kutoa leseni 180, uendeshaji wa shughuli za biashara ya filamu na michezo ya kuigiza, kuhakiki na kupanga madaraja ya filamu takribani 1,109 nalo lilikuwa limefanyika. Maelezo ya ziada kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Filamu yametolewa katika aya ya 85 hadi 95 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA*. Majukumu ya Taasisi ya *COSOTA* ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya wabunifu na kukusanya na kugawa mirabaha yao pale ambapo kampuni

binafsi za Wasanii na wamiliki wa hakimiliki na hakishiriki *CMOs* hazijaanza kazi. Aidha, *COSOTA* limeendelea kuandaa mazingira ya kusaidia Kampuni za wadau kuweza kuwa na mikataba na kampuni dada katika nchi mbalimbli ili kuwezesha ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha. Sasa hivi tayari tuna mikataba na nchi ya Liberia, Zambia na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* imeendelea na usajili wa kazi na wasanii, pamoja na kazi za waandishi na wabunifu wanaomiliki kazi za ubunifu. Kwa sasa usajili hufanyika kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha *www.hakimiliki.go.tz.* Aidha, ufafanuzi wa kina unapatikana kuanzia ukurasa wa 84 hadi 92 katika kitabu changu cha hotuba kilichowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hatuwezi kuendeleza sanaa bila kuwekeza katika utamaduni na utafiti. Jukumu la TaSUBa kutoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusiana na masuala ya Sanaa na Utamaduni nchini. TaSUBa ni Taasisi ambayo inatoa kozi mbalimbali za masuala ya Sanaa na Utamaduni; miongoni mwa kozi hizo ni pamoja na Filamu na Uzalishaji wa Vipindi vya Televisheni, Uzalishaji wa Muziki, Sauti na Sanaa za Maonesho na Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 TaSUBa imefanikiwa kuvuka lengo kwa kudahili wanachuo 684 wa kozi ndefu sawa na ongezeko la asilimia 14 ya lengo la wanachuo 600. Ongezeko hilo linatokana na uhamasishaji mkubwa uliofanywa na Taasisi. Kwa wanafunzi waliodahiliwa kozi fupi kwa kipindi hicho ni 222, sawa na asilimia 148 ya lengo la kundi hili

Mheshimiwa Mwenyekiti, TaSuBa iliendesha Tamasha la Kimataifa la 41 la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo lililofanyika tarehe 6 Novemba, 2022 ambalo hufanyika kila mwaka. Tamasha lilihudhuliwa na watazamaji wa ndani na nje wanaokadiriwa kufikia 30,000. Aidha, vikundi mbalimbali vya kutoka ndani na nje ya nchi vipatavyo 46 vilishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Michezo; Sekta ya Maendeleo ya Michezo hapa nchini ina jukumu la kuhakikisha inaweka mazingira bora na kuwezesha maendeleo ya michezo hususan kuzalisha ajira, kuimarisha afya za wananchi, pamoja na kuwaletea furaha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake, Serikali imeratibu mashindano ya Jumuiya ya Madola ambayo yalifanyika nchini Uingereza katika Mji wa Birmingham, mwezi Julai hadi Agosti, 2022. Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi Tanzania ilifanikiwa kupata medali tatu, ambapo moja ni ya fedha kutoka kwa mwanariadha Alphonce Simbu aliyoipata katika mbio za Marathoni na mbili za shaba kutoka kwa mabondia Yusuph Changarawe aliyemchapa bila huruma kwa *knockout* bondia Arthur Langlier wa St. Lucia na Kassim Mbundwike aliyepata medali hiyo baada ya kumcharaza kwa *knockout* bondia Marion Faustino Ah Tong kutoka visiwa vya Samoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Tanzania imeendelea kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa ambapo tarehe 10 Agosti, 2022 ilikuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 44 wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika *(CAF)*, ambao ulifanyika Jijini Arusha na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani *(FIFA)* Bw. Giani Infantino pamoja na viongozi wengine kutoka sehemu mbalimbali Afrika na Duniani kote walishiriki mkutano huo. Aidha, tarehe 24 Mei, 2023 Wizara imewasilisha Taarifa ya Tanzania kwa kushirikiana na nchi ya Kenya na Uganda, nchi zote zilizoko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu kuomba kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu barani Afrika *(AFCON 2027)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 2 – 4 Mei, 2023 nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Michezo wa Baraza la Michezo la Afrika Kanda ya *IV*, uliofanyika Jijini Arusha ambapo Viongozi kutoka Nchi 9 kati ya 14 wanachama wa Baraza hilo walishiriki. Aidha, kutumia Mkutano huo Tanzania ilitumia fursa hiyo vizuri kabisa kwa kuomba nafasi ya kuwa Makao Makuu ya Kanda ya *IV*, ambapo ilikidhi vigezo vyote vilivyotakiwa na hivyo kuifanya Tanzania kuchaguliwa kuwa Makao Makuu ya

Sekretarieti ya Baraza hilo *(African Union Sports Council Secretariat)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa na miundombinu ya michezo bora katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa sasa, wizara inaendelea na taratibu mbalimbali za Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo Mkandarasi ameanza ujenzi katika *Recreational and Sports Centres.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa maeneo hayo unatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 54.6 na utafanyika katika kipindi cha miezi 36. Serikali pia inaendelea na taratibu za ujenzi wa uwanja mkubwa wa michezo katika Mkoa wa Dodoma katika eneo la Nzuguni, ambapo zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi imetangazwa. Sambamba na ujenzi wa Uwanja wa Michezo Dodoma, pia Serikali inajiandaa kujenga Uwanja kama huo katika jiji la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BMT, Serikali kupitia BMT imewezesha kuzigharamia Timu za Taifa kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Serikali kupitia BMT, imewezesha jumla ya timu 15 kushiriki katika mashindano ya kimataifa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3.6 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Michezo, udhamini na harambee zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hizo ni pamoja na Timu za Michezo ya Riadha, Ngumi, Judo, Kuogelea na *Para powerlifting*, ziliwezeshwa kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika Birmingham nchini Uingereza. Katika mashindano hayo, Tanzania ilipata jumla ya Medali tatu katika mchezo wa Riadha na Ngumi. Timu ya Taifa ya vijana ya Mpira wa Miguu kwa Wanawake (Serengeti *Girls)*, iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini India kuanzia tarehe 11 hadi 30 Oktoba, 2022 ambapo timu hiyo ilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali. Hii iliwezekana baada ya timu yetu kuichapa timu ya

Taifa ya Ufaransa mabao (2-1) na kutoka sare dhidi ya Kanada (1-1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu (Tembo *Warriors)*, kuwezeshwa kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Uturuki kuanzia tarehe 30 Septemba hadi 10 Oktoba, 2022. Kwa hiyo, mafanikio ya idara ya michezo ni mengi. Kadhalika, wanamichezo wa Tanzania wameendelea kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na kupeperusha vema bendera ya Tanzania. Wachezji hao ni pamoja na Gabriel Gerald Geay ambae ameshika nafasi ya pili katika mbio kubwa Duniani za Boston Marathon na Valencia Marathon. Vile vile, mwanariadha Alphonce Felix Simbu, aliyeshika nafasi ya Tatu katika Mbio za Osaka Marathon na Yangzhou. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, imeendelea kudahili wanachuo na kadiri siku zinavyokwenda idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa inaongezeka. Mpango wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 umeainishwa kwa kina katika aya ya 159 mpaka aya ya 183 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kutokana na muda naomba niende moja kwa moja kwenye kuomba fedha. Kwa mwaka 2023/2024, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni moja. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na viingilio katika matukio ya michezo yanayofanyika katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, kukodisha kumbi na *gym* zilizopo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ada za mafunzo na mitihani ya Kitaifa kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo. Aidha, kwa upande wa Taasisi sita zilizo chini ya wizara kiasi kinatarajiwa kukusanywa ni shilingi bilioni 5.9, kinatarajiwa kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida ya Miradi, mwaka 2023/2024, Wizara imetengewa bajeti ya shilingi 35,445,041,000. Kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni shilingi 9,651,285,000. Matumizi mengineyo ni shilingi 13,962,596,000 na Miradi ya Maendeleo ni shilingi 11,831,160,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya fedha; ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2023/2024, naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2023/2024, yenye jumla ya shilingi 35,445,041,000. Kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi 9,651,285,000. Matumizi mengine ni shilingi 13,831,160,000 na Miradi ya Maendeleo ni shilingi 11,831,160,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwisho, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha wizara kufanikisha majukumu yake. Bila kumsahau Mheshimiwa Naibu Waziri (MwanaFA), mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2022/23 yametokana na ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa Mheshimiwa Spika na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHE. BALOZI DKT. PINDI HAZARA CHANA (MB.), WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupatia uzima na afya njema

na kutuwezesha kukutana tena hapa Bungeni, na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu, mshikamano na upendo.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara hii ni muhimu kwa nchi yetu, ambayo kwa maneno mengine naweza kusema ni Wizara yenye nguvu shawishi (***soft power***) ya nchi, kwa maana ya kuwa inawaleta wananchi wenye itikadi tofauti pamoja, inaimarisha mshikamano na ushirikiano, inaleta furaha miongoni mwa wananchi, inadumisha amani na inajenga na kuimarisha afya za wananchi. Pia, inatoa ajira nyingi kupitia michezo na sanaa. Aidha, chambilecho wahenga, chanda chema huvikwa pete, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa maendeleo ya nchi yetu. Pia, nimpongeze kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka miwili (2) ya Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta zetu ambayo yametokana na uongozi wake ulio mahiri, wenye weledi, umakini na upeo mkubwa unaoendelea kulishamirisha Taifa letu ndani na nje ya nchi. Sisi na wadau wetu wote wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo tunamuahidi kuendelea kumpa ushirikiano, kuchapa kazi kwa bidii na kwa weledi ili kuendana na fikra, maono, na falsafa yake ya "Kazi Iendelee". Aidha, nitumie fursa hii kumuombea kiongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu, awe na afya njema, Mungu aendelee kumpa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa namna alivyo mstari wa mbele kwa kuwa kichocheo cha ukuaji wa Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo hivi karibuni tumeshuhudia akiridhia Kocha wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kulipwa mshahara na Serikali. Aidha, ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wake katika michezo, Mheshimiwa Rais alinunua tiketi 2,000 wakati wa mchezo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes) uliofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam tarehe 28 Machi, 2023. Pia, amehamasisha Timu zetu za Yanga na Simba ambazo zimeshiriki mashindano ya kimataifa ngazi ya Afrika kwa kuwazawadia kila goli lililofungwa katika mashindano hayo Shilingi

Milioni Tano (Sh. 5,000,000) katika hatua ya makundi. Hamasa hiyo iliendelea kwa timu hizo zilipofika hatua ya robo na nusu fainali kwa kutoa zawadi ya Shilingi Milioni Kumi (Sh. 10,000,000) kwa kila goli lililofungwa.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya fainali tumeshuhudia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiongeza dau kwa kuzawadia kila goli Shilingi Milioni Ishirini (Sh. 20,000,000). Aidha, ameweza kununua tiketi 5,000 zenye thamani ya Shilingi Milioni Ishirini na Tano (Sh. 25,000,000) kwa ajili ya mashabiki kuingia kuishangilia Timu ya Yanga katika mchezo uliofanyika tarehe 28 Mei, 2023 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya USM Algiers. Pia ametoa usafiri wa ndege wa kuipeleka Timu ya Yanga na baadhi ya mashabiki wake nchini Algeria. Mchango wa Mheshimiwa Rais ndiyo chachu ya mafanikio ya timu za Simba na Yanga katika mashindano haya na kuiwezeshakufikia fainali kwa Timu ya Yanga na kama ambavyo Waswahili husema mwana hutazama uchogo wa mamaye, timu zinamwahidi kuendelea kuongeza jitihada. Hakika huyu ndiye mwanamichezo wa kweli na wa vitendo siyo wa maneno tu. Mheshimiwa Rais amekuwa akituunga mkono katika matukio na shughuli mbalimbali za Sekta zetu, ikiwemo Tamasha la Kimataifa la Michezo la Wanawake (*Tanzanite International Women Sports Festival*) na Mashindano ya Riadha kwa Wanawake ya *Ladies First*. Tunampongeza na kumshukuru sana.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake kwa hakika kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Viongozi hawa wamekuwa wadau mahiri katika sekta zetu ambapo wameshirikiana nasi kuzindua au kufunga matukio mbalimbali ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na kutupatia maelekezo pamoja na ushauri uliosaidia kuboresha sekta hizi. Ninawashukuru na kuwapongeza sana. Aidha, nizidi

kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba ya Bajeti yake iliyotoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2022/23 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2023/24. Wizara yangu inaahidi kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza kwa busara na weledi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelekezo na miongozo yako imekuwa msingi wa ufanisi mkubwa wa Bunge katika kuisimamia Serikali kutekeleza vema majukumu yake. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia na kukushauri vema katika majukumu yako ya kuliongoza Bunge. Nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb.) kwa kusimamia vema na kwa ustadi mkubwa mijadala ya kibajeti katika Bunge lako Tukufu.

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, kivuli cha mvumo huwafunika walio mbali, Wizara hii ni kubwa na muhimu kama nilivyosema hapo awali kwani ni Wizara yenye nguvu shawishi (*soft power*) ya kukusanya na kugusa maisha ya Watanzania wengi wapenda michezo na burudani, hivyo, kila mtu katika nchi hii anaguswa na Wizara hii kupitia sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais utendaji ulio bora na uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu aliyonikabidhi.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukiona zinduna na ambari iko nyuma yake, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge wa jimbo la Ubungo, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mbunge wa Viti Maalum), Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri, michango na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Maelekezo yao yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Wizara

itaendelea kuzingatia ushauri, maoni, mapendekezo na maelekezo yanayotolewa na Kamati kwa maendeleo ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** papo kwa papo kamba hukata jiwe mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa Wizara wakiwemo viongozi na watumishi wa Wizara. Natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu wa Wizara wakati wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu na mageuzi makubwa tunayoendelea nayo wizarani na katika sekta zetu. Nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mb.), kwa lakabu “Mwana-FA”, Naibu Waziri makini wa Wizara yangu kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Bw. Saidi Yakubu, Katibu Mkuu anayehakikisha mambo yanakwenda na mageuzi yanatokea; Bw. Nicholas Mkapa, Naibu Katibu Mkuu mwenye jukumu la kuhakikisha ufanikishaji na kusonga mbele katika mageuzi makubwa ya tasnia za Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wanaofanya kazi kwa bidii na wanahakikisha mambo yanatokea na mipango inatekelezwa kama ilivyopangwa na Waswahili tunaamini ya kuwa kofi halilii kwa kiganja kimoja na kwa hakika ushirikiano wao umefanikisha.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** mkono mmoja hauchinji ng’ombe niwashukuru kwa dhati watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, hatimaye kuleta tija na ufanisi kwa Wizara. Aidha, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wakiwemo mashirikisho, vyama, vilabu na kila mdau mmojammoja kwa nafasi zake katika sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuhakikisha Sekta hizi zinakua na zinaleta furaha kwa wananchi na kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa Sera.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani, ninawashukuru wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Njombe kwa kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu; na wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika Mkoa wetu

kwa lengo la kuwaletea maendeleo wanawake wa Mkoa wa Njombe. Ninawaahidi utumishi uliotukuka pamoja na ushirikiano wa dhati katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Naomba waendelee kuniamini kwani mwana hasahau mkono uliomlea.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni masikitiko yetu kwamba katika Bunge lako Tukufu lilipatwa na msiba wa mpendwa wetu Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge mwenzetu akiwawakilisha wananchi wa jimbo la Amani Zanzibar. Kwa niaba yangu binafsi, Wizara na wadau wetu wote, ninatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wote wa jimbo la Amani Zanzibar na Tanzania kwa ujumla wake. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aipokee na kuilaza roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Taifa letu pia limepoteza wadau mahiri na wa kutegemewa katika sekta zetu, wakiwemo wanamichezo, wanautamaduni na wasanii mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia za marehemu wote, ndugu, jamaa, marafiki na kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa kuwapoteza wapendwa wao "Tunaomba Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu wote na kuzilaza mahali pema peponi". Amina.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/23 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/24 aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 5 Aprili, 2023. Aidha, hotuba hii imezingatia Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 - 2025); Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 - 2025/26); na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya

Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu nane: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima, Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka 2022/23 na Sehemu ya Nne inabainisha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2023/24; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2023/24; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2023/24; na mwisho, Sehemu ya Nane ni shukurani kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

## 2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO, VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** dira ya Wizara ni ***''kuwa Wizara inayohakikisha ushiriki wa ushindani katika Utamaduni, Sanaa na Michezo kimataifa unaolenga maendeleo ya Taifa''*** na dhima ni ***''kukuza, kuwezesha na kuendeleza utambulisho wa Taifa kupitia maadili ya kiutamaduni, Sanaa na Michezo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Taifa''***.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendeleza shughuli za Utamaduni, Sanaa na Michezo na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Rasilimali Watu Wizarani na kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Vilevile, Wizara inaratibu na kusimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza na kuimarisha utendaji kazi, Wizara inaongozwa na misingi mitano ya kimkakati na kimageuzi ambayo ni Kuwafikia Wadau *(Outreach Programmes)*; Mageuzi ya Taasisi *(Institutional Reforms)*; Utawala Bora *(Good Governance)*; Uendelezaji wa Miundombinu *(Infrastructure Development)*; na Utafutaji wa Rasilimali *(Resources Mobilization)*.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya misingi hiyo, katika mwaka 2023/24 Wizara imejipanga kutekeleza maeneo mbalimbali ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na kukarabati, kuboresha, kujenga na kutunza miundombinu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; kukamilisha kutunga na kuhuisha Sera, Sheria, mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji katika sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa Timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuweka na kuboresha mazingira wezeshi na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kuratibu, kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ni kuziimarisha na kuziongezea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kusimamia na kutekeleza majukumu ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine katika utendaji kazi hususan zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Elimu, Afya, Maliasili na Utalii, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Sekta Binafsi katika maendeleo kwa kufadhili na kusukuma mbele gurudumu la Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022/23

### 3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

#### 3.1.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara

ilikadiria kukusanya Shilingi Milioni Mia Tisa (Sh. 900,000,000) kutoka kwenye vyanzo viwili ambavyo ni mapato yatokanayo na viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru pamoja na Ada za mafunzo na mitihani kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Vyanzo vyote vinatoka Idara ya Maendeleo ya Michezo. Hadi kufika mwezi Aprili, 2023 Shilingi Milioni Mia Sita Themanini na Nane, Mia Nane Thelathini na Tisa Elfu, Mia Tano na Tisa (Sh. 688,839,509) sawa na asilimia 76.5 ya lengo zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu za kutofikia lengo ni pamoja na kutokamilika kwa miundombinu ya kumbi zilizopo uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwemo vifaa; mwamko mdogo wa mashabiki kushabikia timu zilizopo nje ya kituo cha Dar es Salaam; na kutokuwasilishwa kwa wakati madai ya kodi ya pango katika eneo changamani la michezo Dar es Salaam.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya mapato ikiwemo kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu katika uwanja, ili kuwezesha kuvutia mashabiki wengi zaidi; kuongeza hamasa katika michezo ikiwemo zawadi mbalimbali kwa washindi ili kuhamasisha matokeo mazuri yatakayochochea ushabiki na hatimaye mapato; na ufuatiliaji wa karibu wa madai ya pango kwa mujibu wa mikataba ya upangaji.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Hamsini na Tano Elfu (Shilingi 5,396,455,000) ambapo shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Tisini na Nane, Mia Tatu Kumi na Tano Elfu, Mia Sita Kumi na Moja (Shilingi 2,998,315,611) sawa na asilimia 55.5 ya lengo zilikuwa zimekusanywa hadi kufikia mwezi Aprili, 2023. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikiwa malengo ni kutokana na wadau wengi wa filamu kufanya kazi zao bila ya kufuata utaratibu wa kisheria ikiwemo kukosa vibali na kuingiza filamu sokoni kabla ya kuhakikiwa; na kuchelewa kukusanywa na kugawanywa kwa mirabaha ya kazi za wabunifu. Fauka ya hayo, kwa upande wa vyuo, moja ya sababu ni wanavyuo kutokulipa ada kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali.

Wizara kupitia Taasisi inaendelea kutoa elimu kwa wadau na kufanya kampeni mbalimbali ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Kampeni hizo ni pamoja na kuhamasisha usajili na kufuata taratibu za uzalishaji na usambazaji wa kazi za sanaa; kuongeza kasi ya kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa taasisi; utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999; na kuhamasisha wanavyuo kulipa ada kwa wakati.

### 3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Ishirini na Tano, Mia Tisa Tisini na Moja Elfu (Sh. 35,425,991,000) ambapo kati ya hizo Mishahara ilikuwa Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili na Moja, Mia Nane Themanini na Mbili Elfu (Sh. 8,201,882,000), Matumizi Mengineyo (OC) shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Tatu Tisini na Mbili, Mia Tisa Arobaini na Tisa Elfu (Sh. 11,392,949,000) na Miradi ya Maendeleo (DEV) Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu (Sh. 15,831,160,000).

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Mia Moja Sitini na Moja, Mia Tisa Thelathini na Nne Elfu, Mia Saba Sabini na Moja (Sh. 28,161,934,771) sawa na asilimia 79.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tano Sitini na Moja, Mia Tatu Themanini Elfu, Mia Tisa Tisini na Tisa (Sh. 9,561,380,999) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 83.9 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Sabini na Mbili, Mia Tatu Tisini Elfu, na Themanini na Moja (Sh. 6,772,390,081) ni Mishahara ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 82.5 ya bajeti ya Mishahara; na Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane Ishirini na Nane, Mia Moja Sitini na Tatu Elfu, Mia Sita Tisini (Sh. 11,828,163,690) ni Miradi ya Maendeleo ambayo sawa na asilimia 74.7 ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2022/23

### 3.2.1 SEKTA YA UTAMADUNI

#### 3.2.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utamaduni ina majukumu ya kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni, lugha na maadili ya Taifa; kuendeleza utambulisho wa Taifa; kuhimiza na kukuza utaifa kwa vijana na wananchi kwa ujumla; kukuza lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya Taifa kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA); kufanya tafiti katika uga wa sekta ya utamaduni hususan lugha za kijamii ambazo ni kibebeo cha urithi wa utamaduni wetu na kuratibu na kusimamia shughuli za Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Sekta hii imetekeleza majukumu ambayo yamefafanuliwa kama ifuatavyo:

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanaendelea kunufaika na utamaduni wao, Wizara iliratibu Tamasha kubwa la Kitaifa la Utamaduni lililofanyika kuanzia tarehe 1 hadi 3 Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam. Tamasha hilo lilitoa fursa kwa wananchi wetu kufanya matembezi ya kiutamaduni, mashindano ya ngoma za asili, maonesho ya vyakula vya asili, maonesho ya kazi za mikono za kiutamaduni na ubunifu pamoja na kuuza kazi hizo. Jumla ya vikundi 24 vya ngoma za asili kutoka mikoa ya Tanzania Bara na vikundi viwili (2) kutoka mikoa miwili (2) ya Zanzibar vilishiriki katika Tamasha hilo. Vilevile, Maafisa Utamaduni, Machifu na Viongozi wa Kimila walishiriki katika Tamasha hilo. Aidha, Serikali iliadhimisha Siku ya Uanuai wa Utamaduni Duniani tarehe 21 Mei, 2023 kwa kuendesha Kongamano lililohusisha wanafunzi wa Vyuo Vikuu na vya Kati vya Mkoa wa Dodoma. Kongamano hilo lilifanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo mada zilizowasilishwa zilijikita katika Utamaduni na Maadili ya Mtanzania.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ya Jamhuri ya Afrika Kusini iliratibu Tamasha la Msimu wa Utamaduni wa Tanzania na Afrika Kusini

lililofanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro kuanzia tarehe 18 Novemba 2022 hadi 4 Desemba 2022. Tamasha hilo lilikuwa na lengo la kuimarisha ushirikiano wa kiutamaduni baina ya Tanzania na Afrika Kusini. Aidha, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Kushirikiana na Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ya Jamhuri ya Afrika Kusini inaendelea na maandalizi ya Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania linalotarajiwa kufanyika nchini Afrika Kusini mwaka 2023. Lengo la Tamasha hilo ni kutangaza kazi za Sanaa, Utamaduni, ubunifu kimataifa na asili ya Mtanzania na utamaduni wake.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** umuhimu wa lugha ya Kiswahili umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Kutokana na hilo, ni ukweli usiopingika kuwa, kwa sasa mawanda ya matumizi na maendeleo ya lugha adhimu na aushi ya Kiswahili yamekuwa makubwa kitaifa na kimataifa. Hii imesababisha Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano mapana katika nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Aidha, Kiswahili imekuwa Lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na ni Lugha rasmi na ya Kazi ya Umoja wa Afrika (AU). Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya lugha hii, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limepitisha tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani, ambayo kwa mara ya kwanza ilisherehekewa tarehe 7 Julai, 2022.




*Mkutano Mkuu wa 41 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), umepitisha Julai 7 ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani.*

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika matamasha mbalimbali yaliyoandaliwa na Wadau wa Utamaduni yakiwemo; Tamasha la Kwanza la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Jijini Arusha tarehe 9 - 16 Oktoba, 2022; Tamasha la Utamaduni la Jamii za Watu wa Mwanza tarehe 4 - 8 Septemba, 2022 katika viwanja vya Kisesa Magu Jijini Mwanza; Tamasha la 12 la Muziki wa Cigogo lililofanyika tarehe 23 - 25 Julai, 2022 Wilayani Chamwino - Dodoma chini ya usimamizi wa Kituo cha Sanaa cha Chamwino "Chamwino Arts Center (CAC)" ambapo wadau wa Utamaduni na Sanaa zaidi ya 600 walishiriki katika Tamasha hilo; Tamasha la Utamaduni baina ya Tanzania na India kuhusu Mapokezi ya Balozi wa Amani Duniani na Kiongozi wa Kiroho Mheshimiwa Gurudev Sri Sri Ravi Shankar lililofanyika tarehe 24 Agosti, 2022 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam; na Tamasha la Utamaduni kutoka Mkoa wa Mbeya lijulikanalo kwa jina la Tulia Traditional Dance lililofanyika kuanzia tarehe 22 - 24 Septemba, 2022 Jijini Mbeya. Matamasha haya hutoa fursa na nafasi kwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali nchini kuusherehekea na kuudumisha utamaduni wao. Hali hii huonesha uhai wa utamaduni wa Mtanzania.




*Tamasha la 12 la Muziki wa Cigogo lililofanyika tarehe 23 - 25 Julai, 2022 Wilayani Chamwino - Dodoma chini ya usimamizi wa Kituo cha Sanaa cha Chamwino "Chamwino Arts Center (CAC)"*



*Tamasha la Utamaduni baina ya Tanzania na India la Mapokezi ya Balozi wa Amani Duniani na Kiongozi wa Kiroho Mheshimiwa Gurudev Sri Sri Ravi Shankar lililofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwl. Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 24 Agosti, 2022.*

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa tunaendelea kudumisha utamaduni na utambulisho wa Taifa la Tanzania, Wizara iliunda Kamati ya Kitaifa ya upatikanaji wa Vazi la Taifa. Katika kipindi cha mwezi Julai mpaka Aprili, 2023, Kamati hiyo imekamilisha mapendekezo ya awali ya upatikanaji wa vazi hilo. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kukusanya maoni ya wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu vazi la utambulisho wa Taifa.

### 3.2.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kuimarisha lugha ya Kiswahili nchini na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi; kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma; kuratibu utafiti wa Kiswahili kwa kushirikiana na wadau na kuhimiza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili na kuzuia upotoshaji wake. Katika kipindi hiki mafanikio lufufu yamepatikana kama ifuatavyo:

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA iliandaa maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Kiswahili duniani yaliyofanyika tarehe 4 - 7 mwezi Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam. Maadhimisho hayo yalifana na yalihudhuriwa na jumla ya washiriki 1,514 wakiwamo wageni kutoka nchi za Ujerumani, China, Uingereza, Urusi, Misri, Uganda, Ghana, Afrika Kusini, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Kenya na Burundi. Mafanikio ya maadhimisho hayo ni pamoja na kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Afrika

Kusini katika Elimu ya Msingi na Ufundishaji wa Kiswahili. Vilevile, katika maadhimisho hayo *Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili* ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango tarehe 07 Julai, 2022. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, Baraza liliandaa *Mwongozo wa Maadhimisho ya Kiswahili Duniani* ambao ulisambazwa katika Balozi za Tanzania na kutumiwa na Balozi hizo katika kuadhimisha Siku hiyo. Hali kadhalika, Baraza lilituma mwakilishi katika ubalozi wa Ujerumani kushirikiana nao katika kuadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akizindua Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi wa mwaka 2022-2032 wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani iliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwl. Julius Nyerere Jijini Dar es salaam tarehe 7 Julai 2022.*

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inazidi kukua na kuendelea, mwezi Agosti, 2022 BAKITA kwa kushirikiana na wachapishaji liliandaa na kugawa Vitabu 1,640 vyenye thamani ya shilingi milioni 50 kwa ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani na nchi zinazohudumiwa na ubalozi huo zikiwemo nchi za Polandi, Uswizi, Bulgaria, Hungary, Romania, Jamhuri ya Cheki, Jamhuri ya Slovakia na Holly See ambavyo vinakusudiwa kutumika katika vituo na vyuo vikuu vinavyofundisha Kiswahili. Pia, vitabu hivi viligawiwa kwa Klabu ya Kiswahili inayofahamika kama **Kijiwe cha Kiswahili** nchini Ujerumani ambacho kimetambuliwa na BAKITA kama kituo rasmi cha kufundisha na kuendeleza Kiswahili nchini humo. Aidha,

katika kutekeleza azma ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kukuza Kiswahili kimataifa, BAKITA limeandaa na kusambaza vitabu vya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani. Pia, BAKITA liligawa vitabu kwa balozi 50 za Tanzania nje ya nchi ambapo kila ubalozi ulipewa vitabu 32 na vitabu vyote kwa ujumla wake viligharimu shilingi milioni 30. Vilevile, Baraza lilitembelea na kufanya mazungumzo ya uraghibishi na kushajiisha nia ya mmiliki wa *Good Hope Junior School* nchini Zimbabwe ya kutaka kuanzisha somo la Kiswahili na liliwakabidhi vitabu 50 vya kufundisha na kujifunzia Kiswahili ukiwamo *Mwongozo wa Taifa wa Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni*.



*Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani Dkt. Abdallah Possi (kulia) akikabidhi cheti cha utambuzi wa Klabu ya Kijiwe cha Kiswahili nchini Ujerumani mwezi Novemba, 2023.*

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha hakuna nchi inayoachwa nyuma kwenye harakati za kitaifa za kukisambaza Kiswahili, BAKITA limeendesha darasa la kwanza la Kiswahili kwa walimu 49 nchini Malawi mwezi Novemba, 2022 na walimu 38 nchini Burundi mwezi Desemba, 2022. Mafunzo haya yamejenga hamasa kubwa na kusababisha walimu wa Kiswahili katika nchi hizo kuhitaji mwendelezo wa mafunzo hayo. Kutokana na vuguvugu hilo, walimu wa Burundi wameanza harakati za

kuundwa kwa baraza litakalosimamia maendeleo ya Kiswahili nchini humo kutokana na hamasa waliyoipata. Aidha, BAKITA lilishirikiana na ubalozi wa Nigeria kufanikisha darasa la Kiswahili la Waandishi wa Habari 27 wa *Voice of Nigeria (VON)* mwishomi mwa mwezi Mei, 2023. Pia, Shirika hili limeanzisha ushirikiano wa kubadilishana wataalamu na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).




*Uongozi wa Chuo Kikuu cha Hebron nchini Malawi na baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wakiwa katika picha ya pamoja na Walimu wa Baraza la Kiswahili la Taifa Bi. Wema Msigwa (wa nne kutoka kushoto - waliokaa) na Onni Sigalla (wa tatu kutoka kulia - waliokaa) wakati wa Mafunzo ya Kiswahili kwa Wageni yaliyoendeshwa na BAKITA.*

**37. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, BAKITA liliandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 891 kupitia redio na televisheni za Redio One, TBC-Taifa, TBC1, Clouds Fm, Kiss FM, U-FM, WAPO Redio, MVIWATA FM na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa. Vipindi hivi vililenga kuelimisha jamii kuzingatia matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili. Aidha, BAKITA liliandaa makala 49 zilizochapishwa katika gazeti la HabariLeo toleo la kila siku ya Ijumaa. Vilevile, BAKITA lilitoa jarida la mtandaoni mara 7. Jarida hili linajulikana kama Lugha ya Taifa na linatoka mara moja kwa mwezi. Fauka ya hayo, Baraza lilirusha

maudhui mbalimbali yanayohusu sarufi na fasihi ya Kiswahili kupitia akaunti zake za mitandao ya kijamii ikiwemo; Twitter, Facebook, Instagram na channeli ya Youtube. (Facebook-bakitatz, Istagram - bakita_tz na Twitter–bakita_tz, Youtube – Kiswahili TV). Maudhui haya yamefanya BAKITA liwe na takribani wafuasi 64,000 wa akaunti zake kwa ajili ya kujifunza lugha na kujenga ulumbi wa lugha.

*Baadhi ya Nembo za Vyombo vya Habari vilivyotumika kurusha hewani Vipindi vya kuelimisha jamii kuzingatia matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili.*

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili kwa wageni ni sehemu ya utekelezaji wa *Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili*. Katika kipindi hiki, BAKITA lilitoa mafunzo kwa diaspora 42 katika nchi za Falme za Kiarabu za Abu Dhabi na Dubai, diaspora 14 katika nchi ya Italia, diaspora 28 katika nchi ya Uholanzi, diaspora 23 katika nchi ya Zimbabwe na diaspora kumi (10) nchini Nigeria. Mafunzo haya pia yanaendelea nchini Rwanda kuanzia tarehe 5 – 9 mwezi Juni, 2023 kwa wanafunzi 324 na mpango wa BAKITA ni kufikia balozi zote. Malengo ya mafunzo hayo ni kufanya diaspora wawe na uwezo wa kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kupitia vituo vilivyoanzishwa na balozi za Tanzania katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) na pia kufungua vituo kwa kuiga mfano wa Watanzania watatu wanaoishi nchini Zimbabwe waliofungua kituo cha Kiswahili na Utamaduni katika jimbo la Bulawayo. Fauka ya hayo, BAKITA lilitoa mafunzo ndani ya nchi kwa walimu 288 sawa na ongezeko la asilimia 476 ya lengo la kufundisha walimu 50 wa kufundisha wageni. Ongezeko hilo limetokana na mbinu iliyobuniwa na BAKITA ya kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wanaohitimu vyuo vikuu na lilianza kwa kuendesha kozi hiyo kwa wanafunzi 200 wa

Chuo Kikuu cha Dodoma na waliobaki 88 ni wale waliofundishwa kupitia kituo cha Makao Makuu cha Ofisi za BAKITA. Utaratibu huo utaendelezwa kwa vyuo vyote vinavyotoa shahada za Kiswahili nchini. Manufaa ya mafunzo haya ni kujenga uwezo wa nchi wa kuteka soko la Kiswahili ndani na nje ya nchi na kubaini wahitimu wa Kiswahili kwa kila mwaka kupitia vyuo vikuu nchini.



*Moja ya darasa la mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wahitimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma yaliyofanyika mwezi Julai, 2022.*

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali kadhalika, BAKITA katika kuimarisha Kiswahili kimataifa limeendelea na mradi wake wa kuunda kongoo ya Kiswahili ambapo kwa sasa kongoo hiyo ina jumla ya maneno 29,000,000 kati ya maneno 50,000,000 yanayotarajiwa, sawa na asilimia 58 ya malengo yake. Kongoo hili likikamilika litakuwa na manufaa makubwa katika uendelezaji wa lugha kiteknolojia na kuimarisha data ya uhifadhi wa lugha. Aidha, wataalamu na watu mbalimbali watakuwa na uwezo wa kulitumia kongoo hili kwa shughuli za uandishi wa kamusi, ujifunzaji wa Kiswahili na uandishi wa vitabu.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA lilitafsiri jumla ya kazi kubwa na ndogo 954. Pia, BAKITA lilithibitisha tafsiri 2,452 zilizofanywa na Mawakala wake. BAKITA lilitoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mikutano miwili ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu huko Banjul, Gambia. Aidha, BAKITA liliratibu huduma ya ukalimani katika mikutano mbalimbali ikiwemo; Mkutano wa Tatu

wa Dharura wa Baraza la Mawaziri la *Afican Diamond Producers Association* (ADPA), ulioandaliwa na Chama cha Wazalishaji Almasi Afrika uliofanyika Arusha, Tanzania mwezi Oktoba, 2022; Mkutano wa Baraza la Utendaji na Uratibu wa nne (4) wa nusu mwaka wa Umoja wa Afrika (AU) na *Regional Economic Communities* (RECs) uliofanyika Lusaka, Zambia mwezi Julai, 2022; Mkutano wa Bunge la Afrika uliofanyika Midrand, Afrika Kusini mwezi Agosti, 2022; Mkutano wa 18 wa Chama cha Wazalisha Pamba Afrika 2022 ulioandaliwa na Chama cha Wazalishaji Pamba Afrika uliofanyika Jijini Mwanza, Tanzania mwezi Agosti, 2022; Mkutano wa 8 wa Kamati ya Uendeshaji ya *African Flight Procedure Programme* (AFPP), ulioandaliwa na International Civil Aviation uliofanyika Dar es Salaam, Tanzania mwezi Oktoba, 2022; Mkutano wa kwanza wa Bunge la Sita la *Pan African Parliament* (PAP) uliofanyika Midrand Afrika Kusini mwezi Novemba, 2022; Mkutano wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ya Haki za Binadamu na Watu uliofanyika Banjul, Gambia mwezi Oktoba, 2022; Mkutano wa Uanuwai wa Viwanda na Uchumi uliofanyika Desemba, 2022, Jijini Dar es Salaam; Mkutano wa Wataalamu wa Methodolojia ya Rushwa, ulioandaliwa na Bodi ya Ushauri dhidi ya Rushwa ya Umoja wa Afrika uliofanyika Zanzibar, Tanzania mwezi Julai, 2022; Mkutano wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV uliofanyika Arusha tarehe 2-4 Mei, 2023, Kikao cha Kawaida cha 75 cha Kamisheni ya Haki za Binadamu na Watu uliofanyika Banjul, Gambia tarehe 3 -13 Mei, 2023 na Mkutano wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa Ethiopia mwezi Februari, 2023.




*Wakalimani wa Kiswahili - Kiingereza Bw. Petro Basil Mswahili na Amos Mjemah wakiwa katika chumba cha kutolea huduma ya Ukalimani wakati wa kikao cha Mkutano wa Feed The Future - USAID kilichofanyika Morena Hotel tarehe 11 Mei, 2023.*

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA lilitambua Vituo vitatu (3) vya kufundisha Kiswahili kwa wageni vikiwemo Kituo cha KKKT Shule ya Lugha Morogoro; Kijiwe cha Kiswahili cha nchini Ujerumani; Kituo cha Kiswahili na Utamaduni kilichopo Bulawayo nchini Zimbabwe na hivyo kuwa na jumla ya vituo 31 ambapo kati ya vituo, vituo 10 vilianzishwa kupitia balozi za Korea Kusini, Nigeria, Ufaransa, Italia, Sudani, Mauritius, Uholanzi, Havana, Abu Dhabi na Zimbabwe; na vituo 21 ni vituo vilivyo nje ya balozi ambavyo kati yake vituo 16 viko nchini na vitano (5) viko katika nchi za Afrika Kusini, Ethiopia, Italia, Zimbabwe na Ujerumani, **(*Kiambatisho Na.1*).** Fauka ya hayo, BAKITA limefanya utafiti na kubaini jumla ya vituo na vyuo 150 vinavyofundisha Kiswahili nje ya nchi na Watanzania zaidi ya 95 wanafanya kazi kupitia Kiswahili na taaluma zake husianifu huko ughaibuni.



*Baadhi ya Wanafunzi wageni wakihudhuria mafunzo ya lugha ya Kiswahili katika darasa la Kiswahili katika Kituo cha lugha cha KKKT kilichopo mkoani Morogoro mwezi Februari, 2023.*

**42. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jitihada za Serikali za kuongeza idadi ya wakalimani, BAKITA liliendesha mafunzo kwa Wakalimani wa lugha za Kiarabu, Kifaransa na Kiingereza. Aidha, kwa sasa kanzidata ya wakalimani ina wataalamu 118 wa fani hiyo ambapo 25 ni wakongwe katika tasnia na 93 ni wapya ambao walipatiwa mafunzo baada ya Serikali kununua vifaa vya kisasa vya ukalimani. Vilevile, BAKITA lilihariri na kutoa ithibati kwa vitabu 94 na Moduli saba (7) za ujifunzaji na ufundishaji kwa madarasa ya awali. Vitabu hivi viliwasilishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania, Shirika la *Room to Read* na wachapishaji na waandishi binafsi.



*Baadhi ya Wakalimani wakifuatilia darasa la Msasa kwa vitendo katika Ukumbi wa kutolea Mafunzo hayo wenye vifaa vya kisasa uliopo BAKITA. Mafunzo hayo yalitolewa Mwezi Agosti, 2022.*

### 3.2.1.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** heshima ya Taifa letu katika diplomasia, utu, uzalendo, umoja, maadili na utangamano chanzo chake kikubwa ni mchango wa Tanzania katika kuzikomboa nchi za Afrika hususan kusini mwa Bara la Afrika. Tanzania ni nchi pekee ya Afrika iliyoanza kupokea wapigania uhuru wa nchi mbalimbali za Afrika, licha ya vitisho na udhalimu wa kikoloni, Tanzania ilisimama na Afrika. Hili linajidhihirisha katika wimbo wa Taifa la Tanzania na Mwenge wa Uhuru. Kutokana na jukumu kubwa tulilolibeba kwa miaka 31 (1963-1994), mnamo mwaka 2011, Umoja wa Afrika, uliridhia kuipa heshima Tanzania ya kuanzisha na kuwa Makao Makuu ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, ambapo iliwekwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kimetekeleza majukumu yafuatayo: kukarabati jengo la yaliyokuwa Makao Makuu ya Ofisi ya Kamati

ya Ukombozi ya OAU ambapo ukarabati wa jengo hilo umefikia asilimia 95.



*Jengo lililokarabatiwa na Serikali lililopo Jijini Dar es Salaam ambalo lilitumiwa na Kamati ya Ukombozi ya OAU kuanzia mwaka 1963-1994.*

**45. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa maeneo yenye historia ya ukombozi wa Afrika yanahifadhiwa, kuenziwa na kutangazwa, Kituo cha urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kimeyatambua jumla ya maeneo 260 na kuweka mabango 80 ya kuyaelezea na kuyatangaza maeneo hayo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Morogoro na Lindi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kuyarasimisha kuwa urithi wa Taifa ili kuyalinda kisheria. Aidha, Kituo cha Urithi wa Ukombozi kimefanikiwa kukusanya nyaraka mbalimbali zilizotumika wakati wa harakati za ukombozi zipatazo 22,770; maktaba hai walioshiriki au kushuhudia harakati za ukombozi 284 wamehojiwa na kurekodiwa; vifaa mbalimbali kama pikipiki, toi la moyo, mhuri, sufuria, taipureta, sanduku la huduma ya kwanza viti na meza vilivyotumika wakati wa harakati za ukombozi 42 vimekusanywa; na elimu kwa umma kuhusu masuala ya harakati za ukombozi imetolewa kwa zaidi ya watu 500,000.

**46. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kukuza utalii nchini, Kituo cha Urithi wa Ukombozi kimeanzisha utalii wa maeneo ya kiukombozi yaliyotumiwa na wapigania

uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika ambapo kwa mwaka 2022/23 zaidi ya watalii 60,152 walitembelea maeneo hayo. Kati ya watalii hao, watalii zaidi ya 152 walitoka nje ya nchi na zaidi ya watalii 60,000 walitoka ndani ya nchi na maeneo waliyotembelea ni pamoja na Mazimbu na Dakawa - Morogoro; Kongwa -Dodoma; Masonya - Ruvuma; Farm 17 – Lindi; na Kituo cha Ukombozi – Dar es salaam. Aidha, Kituo cha Urithi wa Ukombozi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kimeratibu hatua za kutangazwa katika Gazeti la Serikali maeneo ya Urithi wa Ukombozi 15 ambapo kwa sasa yapo katika hatua za mwisho za kutangazwa. Lengo ni maeneo hayo kuwa Urithi wa Taifa na ili yaweze kulindwa, kutunzwa na kuwa kivutio cha utalii. Baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kutangazwa ni Kongwa, jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya OAU, Dakawa, Mazimbu, Masonya na Kaole.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika licha ya kupokea watalii mbalimbali kimekuwa pia kikitembelewa na Viongozi mbalimbali waliohusika na mapambano ya ukombozi wa Bara la Afrika. Mfano mzuri tarehe 14 Aprili, 2023 Rais mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Joacquim Chissano alitembelea eneo la makumbusho hayo na kusimulia namna walivyokuwa wakipokea misaada na mikakati ya kujikomboa kupitia Kamati ya Ukombozi ya OAU iliyokuwa na Makao Makuu yake nchini Tanzania. Pia, alitoa heshima kwa Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere kwa kukubali Kamati ya Ukombozi ya Afrika kutekeleza majukumu yake katika eneo hilo.



*Rais mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji wa Awamu ya Pili, Mhe. Joacquim Chissano (kulia) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb.) wakiangalia kumbukumbu za historia ya ukombozi alipotembelea Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika tarehe 14 Aprili, 2023 Jijini Dar es Salaam.*

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha historia hii inarithishwa kwa kizazi kijacho, Wizara imeshirikiana na Wizara ya Elimu kupitia Taasisi ya Elimu kuhakikisha uhuishaji wa mitaala ya kufundishia wanafunzi unaingiza maudhui ya historia ya Tanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika. Aidha, Kituo kwa kushirikiana na wadau kimeendelea na zoezi la kusambaza juzuu 9 za Hashim Mbita zinazoelezea Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Tayari Wizara imetafsiri juzuu 2 kwa lugha ya Kiswahili na hatua iliyobaki ni kushirikiana na Wizara ya Elimu ili vitabu hivyo viwe sehemu ya vitabu vya ziada kwa wanafunzi.

### 3.2.1.4 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**49.** ***Mheshimiwa Spika**,* Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa ni hali ya kuwapo kwa ongezeko la ushiriki wa watu katika shughuli za Utamaduni na Sanaa pamoja na kuimarika kwa ubora wa kazi za sekta hizo. Faida au manufaa yatokanayo na shughuli hizo ni pamoja na kukua kwa uchumi wa wasanii binafsi na Taifa kwa ujumla sambamba na kuimarika kwa maadili ya jamii. Aidha, maendeleo hayo yanajipambanua katika nyanja mbalimbali

zikiwemo ongezeko la idadi au wingi wa watu wanaojitokeza kushiriki katika shughuli mbalimbali za Utamaduni na Sanaa, wingi wa makundi yanayojumuishwa katika shughuli za Utamaduni na Sanaa kwa kuzingatia hali zao kama vile watu wenye ulemavu, watoto, jinsia na umri, namna Serikali na wadau wengine wa utamaduni na sanaa wanavyowasaidia watu kupata fedha za mitaji na kujiendeleza ili kukuza uwezo wao na kufikia viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika fani husika.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa uzingatiaji wa maendeleo ya Utamaduni na Sanaa, Serikali imechukua jitihada za makusudi za kuhuisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa tarehe 30 Septemba, 2020 kwa lengo la kukuza na kuendeleza Sekta ya Utamaduni na Sanaa kupitia utoaji wa mitaji yenye masharti nafuu na mafunzo ili kuziwezesha kazi za wadau katika Sekta hizi kukidhi vigezo vya mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Mfuko huu unatoa huduma katika maeneo ya urithi wa utamaduni, matumizi ya lugha na fasihi, sanaa za maonesho, sanaa za ufundi, utengenezaji wa filamu na makala, muziki, uandishi wa vitabu vya kukuza lugha ya Kiswahili, na miradi mingine ya kukuza Utamaduni, Sanaa na Maadili. Aidha, walengwa wa Mfuko ni watu binafsi, vikundi, vyama, mashirikisho, vituo vya elimu na mafunzo, asasi za kiraia na taasisi zinazojishughulisha na kazi za kukuza na kuendeleza kazi za Utamaduni na Sanaa.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, Mfuko ulipokea maombi ya mikopo yenye thamani ya Shilingi 9,262,096,578 kutoka kwa waombaji 219. Hadi kufikia tarehe Aprili, 2023 Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,077,000,000 kwa miradi 45 kutoka katika maeneo mbalimbali ya Sekta ya Utamaduni na Sanaa. Kutolewa kwa mitaji kwa miradi michache kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo waombaji kutorasimisha miradi yao, kutokuwa na uelewa wa uandishi wa miradi, kutokuwa na kumbukumbu za mapato na matumizi, kutokuwa na elimu ya fedha, usimamizi mbovu wa miradi, kutokuwa na elimu ya uwekezaji, kutokuwa na uhakika wa masoko ya kazi walizoziombea mitaji n.k.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika miradi 45 iliyowezeshwa, maeneo ya sekta yaliyowezeshwa na idadi yake katika mabano pamoja na thamani ya fedha iliyotolewa ni Filamu (miradi 17) iliyowezeshwa Shilingi 475,000,000; Muziki (miradi 14) iliyowezeshwa Shilingi 287,000,000; Sanaa za Ufundi (miradi 5) iliyowezeshwa Shilingi 105,000,000; Sanaa za Maonesho (miradi 3) iliyowezeshwa shilingi 30,000,000; na Sanaa ya Uandishi (mradi 1) uliowezeshwa Shilingi 10,000,000. Miradi hii imetoka katika mikoa saba (7) ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Mara, Iringa, Mwanza, Mtwara na Mbeya.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia miradi 45 ya Utamaduni na Sanaa kwa kipindi kilichotajwa kumekuwa na mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa. Miongoni mwa hayo ni uboreshaji wa Studio 21 zilizowezeshwa ikiwemo kununua vifaa vya kisasa vitakavyoweza kuzalisha kazi zenye ubora unaotakiwa. Kuwapo kwa Studio hizi umekuwa ni mkombozi kwa wasanii kwa kuwaondolea usumbufu na gharama za kusafiri nje ya nchi kwa ajili ya kutafuta sehemu za kuzalisha kazi zao. Mfuko umefanikisha ununuzi wa vitendea kazi kwa vyuo vitano (5) vinavyozalisha wadau wapya wa Utamaduni na Sanaa katika nyanja mbalimbali hususan U-DJ, mapambo, uibuaji wa vipaji vya uimbaji, urembo, mitindo, mapambo, upishi wa vyakula vya asili n.k. Vyuo vilivyowezeshwa ni Simba Scratch Academy, Koshuma Training Institute and Co., Mwanamboka Ujuzi-HUB, Dage School of Dressing, na AM Fashion. Vyuo hivi vinazalisha wadau wapya 332 kwa mwezi mmoja wanaojishughulisha na kazi za Utamaduni na Sanaa. Aidha, Mfuko umewezesha uandishi wa miswada 12 ya filamu na tamthilia, uzalishaji wa filamu mbalimbali kama vile JERAHA, LOLITA, REHANI, KICHUGUU, ANU, ASILI YETU n.k. zinazorushwa na zinazotegemewa kurushwa katika vituo mbalimbali vya redio na luninga nchini.

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya ajira 21,579 zimetengenezwa na miongoni mwa ajira hizo, ajira za kudumu ni 733 na ajira za muda ni 20,846. Aidha, Mfuko umekuwa kichocheo kikubwa kwa wadau katika eneo la urasimishaji kwani umewahamasisha kurasimisha shughuli zao katika mamlaka mbalimbali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni

(BRELA), Halmashauri pamoja na mamlaka nyingine za udhibiti ili waweze kuendesha shughuli zao kibiashara.

***55. Mheshimiwa Spika,*** kwa umuhimu wa mikopo hii na ili kupata njia iliyo rahisi ya kuwafikia wajasiriamali wengi wa sekta za Wizara hii, Wizara kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ipo katika hatua za mwisho za kuingia mkataba wa utoaji wa mikopo kupitia benki ya NBC. Kwa kuwa benki hii ipo katika mikoa yote ya Tanzania Bara ni imani ya Serikali itasaidia kufikisha huduma hii kwa walengwa katika mikoa yote badala ya hivi sasa ambapo imetolewa kwa mikoa michache.

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa wadau wa Utamaduni na Sanaa wanakidhi vigezo, kutumia mitaji katika madhumuni yaliyokusudiwa, wanasimamia miradi yao kitaalamu ili iweze kuwa na tija, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Mfuko umetoa mafunzo kwa wadau wa tasnia 4,534 kati ya hao wanawake walikuwa 1,896 na wanaume 2,638. Mafunzo yaliyotolewa yalihusisha mada mbalimbali miongoni mwa hizo ni elimu ya fedha, utunzaji wa kumbukumbu, uandishi wa miradi, urasimishaji wa kazi za Sanaa, usimamizi na uendeshaji wa miradi, uwekezaji, kuutambua mnyororo wa thamani wa kazi za Utamaduni na Sanaa na kujitambua. Mafunzo haya yamefanyika kwa awamu ya kwanza katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Pwani. Aidha, mipango ya kuwafikia wadau wengine katika mikoa yote ya Tanzania Bara inafanyika kwa lengo la kuwafikia wadau 6,000 kwa mwaka 2023/24.

### 3.2.2 SEKTA YA SANAA

#### 3.2.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

***57. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Sanaa ni eneo jingine muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na inahusisha Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (TFB), Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa).

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Sanaa inatumika ipasavyo kulitangaza Taifa kimataifa, Serikali kwa kushirikiana na BASATA, Kituo cha Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Tanzania (KISUVITA) na *International Deaf Cultural Arts Inc. (IDCA)* yenye Makao Makuu yake Nevada, Marekani iliandaa na kuendesha kwa mafanikio makubwa Shindano la Kimataifa la Urembo na Utanashati kwa viziwi *(Miss and Mr. Deaf International – MMDI, 2022)* kuanzia tarehe 23 – 31 Oktoba, 2022. Ikiwa ni mara ya kwanza kabisa Barani Afrika, mashindano haya yalifanyika katika Ukumbi wa Selous katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwl. Julius Nyerere *(Julius Nyerere International Convention Centre - JNICC)* Jijini Dar es Salaam ambapo watu 147 kutoka nchi 43 duniani walishiriki na kwa taarifa za makusanyo ya kadi, watazamaji 1,478 walifika ukumbini kutoka ndani na nje ya nchi. Katika shindano hilo, Mtanzania Khadija Kanyama aliibuka binti ***mrembo*** zaidi kiziwi duniani na Mtanzania Russo Songoro aliibuka mwanamitindo bora zaidi wa kiume kiziwi duniani na Mtanzania mwingine Rajan Ally alishinda nafasi ya pili mwanaume mtanashati zaidi kiziwi duniani. Kupitia shindano hili, Tanzania ilitangazwa kimataifa kama nchi ya fursa kwa wote bila kujali changamoto za kimaumbile walizonazo wanadamu na tayari waandaaji wa mashindano haya wamewasilisha na kukubaliwa ombi la kufanyika tena kwa mashindano haya kati ya tarehe 15 Novemba, na tarehe 3 Desemba, 2023 kutokana na mafanikio makubwa ya mwaka 2022 na heshima kubwa waliyopewa na nchi yetu. Kupitia mashindano hayo, washindi walipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Ngorongoro kama sehemu ya kuutangaza utalii wetu. Kwa mwaka 2023, Wizara inalenga kutangaza zaidi maeneo mengine muhimu na maandalizi yameanza.




*Bi Khadija Kanyama: Mtanzania binti mrembo zaidi kiziwi duniani aliyeshinda katika mashindano ya Miss and Mr. Deaf International yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam nchini Tanzania tarehe 23 – 31 Oktoba, 2022.*

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha vijana wote nchini wanapata fursa ya ajira na kuonesha vipaji vyao. Serikali kwa kushirikiana na BASATA na Asasi ya *The Music in Africa Foundation* imeratibu kufanyika kwa mara ya kwanza nchini Mkutano mkubwa wa wadau wa Muziki wa Afrika ujulikanao kama The Music in Africa Conference for collaboration, Exchange and Show Case (ACCES) uliofanyika kati ya tarehe 24 na 26 Novemba, 2022. Mkutano huo ulizileta nchini kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji, uelimishaji, usambazaji, utumiaji na uratibu wa Muziki wa Afrika kama vile Tune core, Siemens stiftung, Goethe Institute, Sauti za Busara, Womex , Smille, Media, Sound na *Africa Ari Lines Ziiki Media, Boomplay, Sportfy, The Orchard, Samcom, IOMMA, Sound Connect Fund, Action Music Academy,* COSOTA, BASATA, MaDJ, waandaaji wa matamasha, mapromota, mawakala wa muziki, Mameneja wa wasanii, Lebo za kurekodi muziki, Watangazaji, Waandishi wa Habari za Muziki, sound engineers, wenye shule za kufundisha muziki, wafanyabiashara wa kazi za muziki, wadau na wanamuziki wenyewe.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, mkutano huu ulikuwa ni wa awamu ya Tano baada ya ule wa Dakar, Senegal uliofanyika mwaka 2017, Nairobi, Kenya mwaka 2018, Accra, Ghana mwaka 2019, na Johannesburg, Afrika Kusini mwaka 2021 ambapo Wasanii wa Tanzania Barnaba, Sinaubi Zawose, Sholo Mwamba na Vitalis Maembe walitumbuiza sambamba na wanamuziki wenye ushawishi mkubwa kama vile Sampa the Great (Zambia), Mr. Eazi (Nigeria), Thandiswa Mazwai (Afrika Kusini), Sarkodie (Ghana), Banky W (Nigeria), Mulatu Astatke (Ethiopia), Baaba Maal (Senegal), Ebo Taylor (Ghana), Eric Wainaina (Kenya), Samini (Ghana), Cheick Lô (Senegal), Blinky Bill (Kenya) na Efya (Ghana). Kwa mujibu wa majumuisho ya Asasi zilizotajwa, wadau wapatao 1,120 kutoka nchi 45 ulimwenguni walishiriki na wadau hao wameuthaminisha mkutano huu kuwa wa mafanikio ya hali ya juu. Mafanikio katika maandalizi ya mkutano huu yameifanya Tanzania kuteuliwa mara ya pili kuwa mwenyeji wa Kongamano hili litakalofanyika tena tarehe 9 – 11 Novemba, 2023 hapa Nchini jambo ambalo halikuwahi kutokea huko nyuma nchi moja kuandaa mkutano huo miaka miwili mfululizo.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Mkutano huo, washiriki mashuhuri waliandaliwa ziara ya kiutalii ili wanapoondoka nchini wabaki na kumbukumbu ya Tanzania isiyofutika akilini mwao *(Tanzania: The Unfortgotable)*. Aidha, kupitia matukio kama haya, Tanzania sasa imeanza kuaminiwa na Asasi za Kimataifa kwa kuifanya nchi yetu kuombwa kuwa mwenyeji wa matukio makubwa duniani hasa upande wa Tuzo na ujenzi wa Akademia za muziki na filamu. Serikali inaendelea na majadiliano nao hasa kuhusu uwezeshaji wa kifedha katika matukio hayo.

**62.** ***Mheshimiwa Spika*** katika kuhakikisha Sekta ya Sanaa inakuzwa kuanzia ngazi ya chini na kurithishwa kwa watoto na vijana, Wizara kwa kushirikiana na BASATA iliratibu Mashindano ya Sanaa za Maonesho na Muziki wakati wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA yaliyofanyika Mkoani Tabora ambapo kwa upande wa UMITASHUMTA yalifanyika kuanzia tarehe 31 Julai hadi 06 Agosti, 2022, ambapo wanafunzi wa shule za Msingi kutoka mikoa yote ishirini na nane (28) Tanzania Bara na Zanzibar walishiriki. Mashindano haya yalihusisha kwaya, ngoma na Muziki wa kizazi Kipya. Aidha, mashindano upande wa UMISSETA

yalifanyika tarehe 09 hadi 19 Agosti, 2022 ambapo wanafunzi wa shule za Sekondari kutoka mikoa 25 Tanzania Bara na Kusini Unguja na kufanya jumla ya mikoa 26 kushiriki. Lengo la mashindano hayo ni kuibua na kukuza vipaji na kuviunganisha vipaji hivyo kwenye soko la ajira. Kwa mfano, baadhi ya washindi wa ngoma katika mashindano hayo walishiriki Tamasha la JAMAFEST nchini Burundi kama sehemu ya motisha ya ushindi walioupata. Sambamba na mashindano hayo, Wizara iliratibu ushiriki wa wananchi wa Tabora na viunga vyake ili kujionea vipaji vya vijana hao huku Wasanii hasa wa muziki wa Kizazi Kipya wakipenyeza ujumbe wa umuhimu wa michezo katika kujenga afya na manufaa ya kujitokeza kushiriki Sensa iliyofanyika mwezi Agosti, 2022 ikiwa ni sehemu ya programu pana ya Sensabika.

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na BASATA iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Tamasha lijulikanalo kama "Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festival" (JAMAFEST). Tamasha hilo huandaliwa kwa mzunguko miongoni mwa nchi wanachama kila baada ya miaka miwili. Kwa mwaka 2022 tamasha hili liliandaliwa na nchi ya Burundi na lilikuwa ni onesho la Tano tangu kuanzishwa kwake baada ya Rwanda (2013), Kenya (2015), Uganda (2017) na Tanzania (2019). Wizara kwa kushirikiana na wadau wake iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Tamasha hilo lililofanyika katika Jiji la Bujumbura kuanzia tarehe 04 hadi 12 Septemba, 2022 lililoongozwa na kaulimbiu isemayo "Kutumia Rasilimali za Utamaduni kukabiliana na Athari za UVIKO-19 kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki''. Katika maonesho hayo, Tanzania ilipeleka wajasiliamali 65 na vikundi vya sanaa 13 ambavyo vilionesha kazi zao na kujipatia kipato, ikiwa ndiyo nchi ya kwanza iliyopeleka washiriki wengi zaidi baada ya mwenyeji Burundi.

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inaendelea na uratibu wa maandalizi ya ujenzi wa Sanamu ya Mwl. Nyerere inayotarajiwa kusimikwa Jijini Addis Ababa Ethiopia katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika ambapo hadi Aprili, 2023 hatua iliyofikiwa ni kuanza kwa ujenzi wa Sanamu halisi baada ya Mkandarasi, Kampuni ya EPITOME ARCHITECTS LIMITED ya Tanzania kukamilisha ujenzi wa sampuli kifani ya pili na kuridhiwa na Kamati ya Kitaifa kwa mujibu wa

Sheria ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Chimbuko la Mradi huo ni mapendekezo ya Hayati Robert Mugabe la mwaka 2015 yaliyolenga kutambua mchango uliotukuka wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika ukombozi wa Bara la Afrika hasa Mataifa yaliyo Kusini mwa Bara hilo. Mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani 205,942 unajengwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Sekretarieti ya SADC, Mameneja Mradi kwa kushirikiana na familia ya Mwalimu Nyerere na kwa mujibu wa Mkataba uliopo, inatarajiwa kukamilika Desemba, 2023. Usimamizi wa Tanzania unalenga haswa kutimiza matakwa ya Kanuni ya 17 na 18 ya Kanuni za 2005 za Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya mwaka 2004 zinazoelekeza Sanamu inayojengwa kumuenzi mmoja wa Waasisi kufanana pasi na shaka na anayeenziwa.

***65. Mheshimiwa Spika***, Wizara pia iliandaa Tamasha la kimataifa la Muziki wa Taarabu lililofanyika katika ufukwe wa Bahari ya Hindi (Coco Beach) tarehe 3 Julai, 2022. Tamasha hili lilijumuisha vikundi tisa (9) vya muziki wa Taarabu kutoka ndani ya nchi, wasanii binafsi watano (5) na kikundi kimoja cha Taarabu kutoka nchini Burundi. Lengo la Tamasha hili lilikuwa kubainisha mchango wa muziki wa Taarabu katika kueneza lugha ya Kiswahili kuelekea Siku ya lugha hiyo duniani tarehe 7 Julai ya kila mwaka.




*Kikundi cha Taarabu kutoka nchini Burundi ambacho ni moja ya kikundi kilichotumbuiza katika Tamasha la Taarabu lililofanyika tarehe 03 Julai, 2022 katika ufukwe wa Bahari ya Hindi.*

***66. Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na mpango wake wa kuwapa fursa Wasanii wa Tanzania kuonesha vipaji vyao kupitia Tamasha la Serengeti Music Festival, ambalo kwa sasa linakwenda kufanyika Kimataifa. Tofauti na miaka iliyopita, kwa mwaka 2022/23, Tamasha hili limeendeshwa kwa mtindo tofauti kwa kupeleka makundi ya Sanaa na Wasanii mmoja mmoja nje ya nchi kushiriki shughuli za Sanaa katika matukio makubwa yenye hadhi ya kimataifa. Kwa mfano, Kikundi cha *Safi Theatre* kimeshiriki Maadhimisho ya Miaka 60 ya Umoja wa Afrika katika eneo la Cradle of Humankind, Johannesburg wakati kikundi cha Singeli cha Sholo Mwamba kikishiriki Tamasha la African Music Days ukumbi wa Muffathalle, Munich katika maadhimisho ya miaka 60 ya Umoja wa Afrika kati ya tarehe 24 - 25 Mei, 2023. Kikundi hicho hicho pia kimeshiriki Tamasha linaloandaliwa kila mwaka na *Asasi ya The Africa We Want e.V* la *German Pan-African Expo* nchini Ujerumani lililofanyika tarehe 1 - 4 Juni, 2023 mjini Tübingen. Katika matamasha hayo, Singeli imeonekana kukonga nyoyo za wazungu wengi na imetia fora kwa kufuatiliwa kwa kiasi kikubwa ndani na nje ya nchi. Vilevile, Msanii wa Vichekesho Mujuni Sylivery Bajwauka (Mpoki) ameshiriki kama MC

katika matukio ya Siku ya Tanzania na Siku ya Kiswahili yaliyoandaliwa na Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza na kufanyika tarehe 3 Juni, 2023 Jijini London.

### 3.2.2.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ni pamoja na kukuza na kuendeleza sanaa nchini; kufanya tafiti za fursa za masoko na masuala mbalimbali yanayohusu sanaa; kuandaa Kanuni za kusimamia ubora wa kazi za Sanaa; na kuandaa na kuendesha maonesho, mashindano, matamasha na biashara za sanaa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA imeendelea kukuza ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora kwa lengo la kuwawezesha wasanii kuwa wabunifu na kubuni kazi za sanaa zilizo bora. BASATA liliendelea na mageuzi ya kiutendaji na kitaasisi ili kuwa mwezeshaji zaidi wa shughuli za sanaa badala ya kudhibiti. Hivyo, BASATA limeshiriki kuratibu kutatua migogoro ya wasanii kuhusu mikataba waliyoingia ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 zaidi ya migogoro mikubwa mitano (5) imetatuliwa. Pia, BASATA limekuwa likiwaita wasanii siyo tu pale kwenye upungufu bali hata pale wanapofanya vizuri na kuwapongeza. Sambamba na hatua hii, BASATA limeendelea kutokimbilia kuwafungia wasanii kama ilivyokuwa awali bali kunapotokea changamoto zilizokithiri za kimaadili, kama alivyoagiza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Tamasha la Usiku wa Msanii Joseph Mbilinyi.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeendelea kuleta mageuzi ya kuboresha muziki wa kizazi kipya kwa kutengeneza Kivunge cha Mtozi yaani ***Producers' Kit*** chenye zaidi ya vionjo 400 vyenye ladha ya asili ya kitanzania. Vionjo hivi vilirekodiwa kutoka kwenye ngoma za makabila mbalimbali ya Tanzania. Matokeo ya Kivunge cha Mtozi ni kuchochea mageuzi ya kuwa na muziki wa kitanzania wenye midundo ya Taifa la Tanzania. Nawapongeza sana wanakamati.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeendelea kuwawezesha wasanii nchini kwa kuwasajili na kutoa vibali kwa wasanii binafsi 1,188; vikundi 201; kumbi za sherehe, starehe na burudani 261; kampuni 94 na vibali vya matukio 24. Aidha, BASATA limetoa vibali 307 vya wasanii wa Tanzania kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za sanaa pamoja na vibali 52 vya wasanii wasiokuwa watanzania kuingia nchini kwa ajili ya kufanya shughuli za Sanaa. Aidha, BASATA limetoa vibali 64 kwa Taasisi vikiwemo vyama, mashirikisho Asasi zisizo za Kiserikali na Taasisi binafsi kujishughulisha na Sanaa. Hatua hii inasaidia BASATA kutambua wadau wake pamoja na shughuli wanazofanya na kuwasaidia kutambulika na kusaidiwa zaidi na mamlaka nyingine za ndani na nje ya nchi.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA liliendesha warsha ya kuwajengea uwezo wasanii wa Tanzania katika kutumia fursa za kiteknolojia kupitia jukwaa la *Access Music*. Kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *Music in Africa* kutoka Afrika Kusini, liliwajengea uwezo wasanii 89 wa Tanzania katika kuziona fursa za kibiashara katika muziki ikiwemo matumizi ya fursa za kiteknolojia katika mitandao ya kijamii kuendesha kazi zao. Aidha, kwa kushirikiana na Kituo cha Sanaa cha Chamwino (Chamwino Art Center), limetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wasanii 38 kutoka katika vikundi 38 vya Sanaa wilayani Chamwino mkoani Dodoma. Mafunzo haya yalijikita katika masuala ya ubunifu katika kazi za Sanaa, Mikataba na masuala ya Hakimiliki, pamoja na masuala ya usajili. Katika mafunzo hayo BASATA lilishiriki katika kutoa mada zilizotajwa hapo juu kwa kushirikiana na walimu 3 wa shule za msingi na Sekondari pamoja na wataalamu 2 kutoka Kituo cha Sanaa cha Chamwino.



*Wataalamu wa Music in Africa kutoka Afrika Kusini wakiendesha warsha kwa Wasanii wa Tanzania wa Muziki jijini Dar es Salaam tarehe 24 – 26 Novemba, 2022.*

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni juhudi za kukuza na kuongeza ubora wa kazi za sanaa, Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na TaSUBa limetoa mafunzo ya sanaa kwa wasanii 37 ambao vipaji vyao viliibuliwa kwenye mashindano mbalimbali ikiwemo *Bongo Star Search* (BSS 2021) – washiriki 5, *Taifa Challenge Cup and Music* - washiriki 26 pamoja na washindi 6 wa ***Miss and Mr. Deaf Africa.*** Mafunzo yalifanyika katika Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) kuanzia tarehe 06 Agosti, 2022 hadi tarehe 03 Septemba, 2022. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo katika fani ya uimbaji, utunzi na matumizi ya jukwaa.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa BASATA na wasanii katika maonesho mbalimbali nchini, BASATA limeshiriki na kuratibu ushiriki wa Wasanii wa Sanaa za Ufundi katika Maonesho ya Sabasaba ya mwaka 2022 yaliyofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Juni hadi 13 Julai, 2022. Katika maonesho hayo, wasanii 24 wa Sanaa za Ufundi waliwezeshwa kuonesha bidhaa zao kupitia banda lililoandaliwa na BASATA. Vilevile, wasanii 364 walihamasishwa kushiriki maonesho ya Sabasaba katika mikoa ya Morogoro, Manyara, Tanga na Njombe. Aidha, BASATA lilihamasisha wasanii katika mikoa mingine kushiriki maonesho hayo ambapo jumla ya wasanii 364 walifanikiwa kuonesha bidhaa zao katika mikoa mbalimbali.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA imeendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za Sanaa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Baraza limewezesha kuanzishwa kwa Programu inayotambulika kwa jina la ***'Sanaa Mtaa kwa Mtaa'***. Lengo la programu hii ni kushirikisha na kuhamasisha jamii katika maeneo mbalimbali kuendesha shughuli za kukuza, kufufua na kuendeleza sanaa nchini na utekelezaji wake umefanyika katika Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Rufiji tarehe 16 Oktoba, 2022. Jumla ya wasanii na wadau wa Sanaa zaidi ya 452 walishiriki na jumla ya mitaa 16 ilipitiwa. Na pia imefanyika katika Mkoa wa Arusha mjini tarehe 09 na Wilaya ya Karatu tarehe 10 Disemba, 2022 kwa kushirikiana na uongozi wa Jiji la Arusha na Wilaya ya Karatu ambapo jumla ya wasanii na wadau wa Sanaa 497 walishiriki.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA imekuwa ikiimarisha shughuli za Sanaa kupitia Taasisi mbalimbali za elimu ikiwemo Shule za Msingi na Sekondari. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 BASATA kwa kushirikiana na Taasisi ya *Kukaye Moto Cultural Center* lilitoa mafunzo ya Sanaa kwa watoto 120 kutoka shule 6 za Msingi za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Mafunzo hayo yalihitimishwa kwa tamasha la watoto katika fani za ngoma, utambaji wa hadithi, Maigizo, Sarakasi na Muziki. Aidha, kupitia mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA 2022, BASATA limetoa mafunzo ya sanaa kwa wanafunzi ambapo mafunzo hayo yalijikita katika kufundisha namna bora ya kuendesha Sanaa za Maonesho hususan katika maeneo ya fani za maigizo, muziki na ngoma za asili. Jumla ya walimu 26 wa shule za Msingi na 26 wa Shule za Sekondari na wanafunzi 580 walipatiwa mafunzo hayo.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa taarifa na ushawishi kwa umma kuhusu masuala ya sanaa, BASATA limefanya ziara 21 katika Vituo vya Habari pamoja na kufanya Vikao 19 na waandishi wa Habari. Vile vile, BASATA limeendelea kutumia kurasa zake za mtandaoni za *Instagram* (basata.tanzania) na *Twitter* (Basata_Tanzania) kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa jamii kuhusiana na masuala ya sanaa. Katika kuhakikisha jamii inahabarishwa na kushauriwa katika

masuala yahusuyo Sanaa, BASATA limeendesha midahalo minne (4) ya Sanaa mkoani Arusha na Kagera, lengo likiwa ni kuimarisha utendaji wa wasanii na wadau wa sanaa nchini. Katika midahalo hii, Jumla ya wasanii na wadau wa sanaa 302 walishiriki.



*Moja ya vikao vya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Waandishi wa Habari kilichohusu kuimarisha utoaji wa taarifa na ushawishi kwa umma kuhusu masuala ya Sanaa kilichofanyika mkoani Dar es Salaam.*

**77. *Mheshimiwa Spika,*** BASATA limetoa ushauri kwa wasanii na wadau wa Sanaa wapatao 2,759 kutoka maeneo mbalimbali nchini. Ushauri huu ulitolewa katika maeneo ya masoko ya kazi za sanaa, uendeshaji wa matukio, utafutaji fedha kwa vikundi na Taasisi pamoja na masuala ya usajili na vibali. Ushauri huu ulitolewa kupitia vikao vya wadau, mawasiliano ya simu na mazungumzo ya wadau wanaotembelea Ofisi za BASATA.

**78. *Mheshimiwa Spika,*** BASATA liliendesha Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara, chenye lengo la kushirikisha jamii. Katika kuimarisha ushiriki wa mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kufufua, kukuza na kuendeleza sanaa nchini, BASATA limeendesha kikao kazi cha siku mbili cha Maafisa Utamaduni wa mikoa na Wilaya. Kikao kazi hiki kilifanyika mkoani Dodoma katika ukumbi wa African Dreams tarehe 26 na 27 Januari, 2023. Jumla ya Maafisa Utamaduni 143 walishiriki. Katika kikao kazi hicho mada mbalimbali zilijadiliwa

ikiwa ni pamoja na; Mwongozo wa Uendeshaji wa Kamati za Sanaa za Mikoa na Wilaya, Mwongozo wa Uendeshaji wa Programu ya Sanaa ya Mtaa kwa Mtaa, Mwongozo wa Usimamizi wa Maadili katika Sekta ya Sanaa, Mapitio ya Kanuni za BASATA, matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili (AMIS) pamoja na mada zingine kutoka katika Taasisi za COSOTA, Bodi ya Filamu, na Mfuko wa Fidia kwa Watumishi.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA kwa kushirikiana na Taasisi ya Afrofest (Shirika lisilo la Kiserikali kutoka Kanada linalojishughulisha na kukuza Muziki wa Afrika nchini Kanada) waliwezesha mafunzo ya wasanii 4 kutoka Kanada na kundi la Mjomba Bendi inayoongozwa na Mrisho Mpoto ambapo wasanii 8 walishiriki kwenye mafunzo hayo na kufanya maonesho ya pamoja katika Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Sanaa Bagamoyo mwezi Novemba, 2022. Kutokana na zoezi la kufanya maonesho kwa pamoja wasanii kutoka kundi la Mjomba Bendi chini ya uongozi wa Mrisho Mpoto na wasanii kutoka Kanada kila mmoja alijifunza kutoka kwa mwenzake na mwisho wa siku kila mmoja alijifunza.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu zoezi la Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, BASATA liliratibu tamasha kubwa lililotambulika kwa jina la Tamasha la SENSABIKA lililofanyika tarehe 21 Agosti, 2022 jijini Dar es Salam katika viwanja vya Leaders Club. Tamasha lilihusisha michezo mbalimbali na maonesho ya Sanaa za Maonesho, Ngoma, Muziki, Sanaa za Ufundi, na Filamu. Katika tamasha hili wasanii waliandaa kazi 107 zilizotumika kutoa elimu juu ya ushiriki wa wananchi katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Aidha, wasanii wapatao 442 walishiriki katika tamasha hilo.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeendelea kutoa Tuzo za Muziki wa Tanzania (TMA) kwa mara ya pili mfululizo. Tamasha la utoaji wa Tuzo hizi lilifanyika Dar es Salaam katika ukumbi wa Super Dome, Masaki Tarehe 29 Aprili, 2023. Utuoji wa Tuzo ulihusisha utoaji wa Tuzo maalumu zilizotolewa kwa Taasisi Nne (4) ambazo ni: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, Clouds Media Group na Sauti za Busara, Zanzibar. Lengo lilikuwa ni kutambua mchango wao wa kukuza tasnia ya muziki Tanzania. Tuzo ya Heshima ilitolewa kwa Dr.

Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne (4). Aidha, Tuzo 52 zilitolewa kwa wasanii mbalimbali. Vilevile tukio la utoaji wa Tuzo hizi lilihudhuriwa na waalikwa wapatao 1,500. Fauka ya hayo jumla ya vyombo vya habari 46 vilishiriki usiku wa Tuzo hizo na kufanya matangazo mubashara ikiwemo Azam TV; Clouds TV na Digital; Global online TV; Mwananchi Digital; TVE na vyombo vingine vya habari na mitandao ya kijamii, ambapo inakadiriwa jumla ya watu 19,865,064 walifuatilia matangazo ya usiku wa Tuzo mubashara ndani na nje ya nchi.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA likiwa kama msimamizi wa Sekta ya Sanaa nchini, lilishiriki katika utoaji wa Tuzo za AFRIMMA nchini Marekani ambapo Watanzania 19 walishiriki na watano kati yao kushinda Tuzo hizo. Wasanii walioshinda Tuzo ni pamoja na Diamond Platnumz (Best Live Act), Rayvanny (Best Male East Africa), Zuchu (Best Female East Africa), Mrisho Mpoto (Best Traditional Artist) na Joel Lwaga (Best Gospel). Pamoja na malengo mengine, ushiriki huo ulilenga kujifunza na kupata uzoefu katika maandalizi na uendeshaji wa Tuzo za Sanaa kutoka katika mataifa mengine. Aidha, kupitia ushiriki huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipewa Tuzo ya Heshima kama kiongozi mwenye kuleta mabadiliko na mapinduzi (Transformational Leader) katika kuendeleza Sekta ya Sanaa nchini Tanzania. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Uni Media limeendesha shughuli ya utoaji wa Tuzo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini. Tuzo hizo zilitolewa tarehe 04 Desemba, 2022 jijini Dar es Salaam ambapo jumla ya Tuzo 31 zilitolewa kwa washindi waliopatikana. Katika kutoa Tuzo hizi Baraza lilidhamini kwa lengo la kukuza vipaji vyuoni na kuwapatia vijana mafunzo ya namna ya kuanzisha na kuratibu utoaji wa Tuzo.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeanza kutumia mfumo wa Kielektroniki wa usajili na kutoa vibali kwa wasanii na wadau wa sanaa, lengo likiwa ni kuongeza makusanyo ya rasilimali fedha na kudhibiti mianya ya upotevu wa maduhuli ya Serikali pamoja na kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wasanii na wadau wa sanaa nchini. Mfumo huu unafanya kazi sanjari na mifumo mingine ya Serikali. Katika kuhakikisha mfumo huu mpya wa

kielektroniki wa usajili na vibali - AMIS unatambulika na kuweza kutumiwa na wasanii, BASATA limeendelea kutoa elimu na kuwajengea uwezo wasanii na wadau wa sanaa kuhusu matumizi ya Mfumo huu unaopatikana kwa kiungo cha https://sanaa.go.tz/.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, BASATA limeendelea kurejesha uhusiano baina yake na Taasisi zingine na Vituo vya Utamaduni vya Nchi za Umoja wa Ulaya na Marekani (Culture Development Partners) kwa kufanya vikao vya kuendeleza tasnia za Sanaa nchini. Aidha, BASATA limefanikiwa kuhuisha uanachama wake katika Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Sanaa na Utamaduni Duniani (IFACCA) ambapo kwa sasa Katibu Mtendaji wa BASATA anakuwa Mjumbe na aliiwakilisha Tanzania katika Mkutano wa Shirikisho la Mabaraza hayo uliofanyika Mjini Stockholm Sweden kuanzia tarehe 1 hadi 5 Mei, 2023 ambapo ulihudhuriwa na zaidi ya viongozi 400 kutoka kila kona ya Dunia. Ajenda kubwa ya Mkutano huo ilikuwa ni kuimarisha uhusiano wa wasanii katika ubunifu wa kazi za Sanaa.



*Mkutano wa Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Sanaa na Utamaduni Duniani (IFACCA) ambao Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ni Mjumbe na aliiwakilisha Tanzania katika Mkutano huo uliofanyika Mjini Stockholm Sweden tarehe 1 - 5 Mei, 2023.*

### 3.2.2.3 BODI YA FILAMU TANZANIA (TFB)

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Bodi ya Filamu ni pamoja na kusimamia na kuratibu kazi za filamu ikiwemo kuhakiki na kuzipanga katika madaraja; kutoa vibali vya usambazaji, maonesho ya filamu, michezo ya kuigiza, kampuni za usambazaji wa filamu, kumbi za maonesho ya filamu, maktaba za picha za filamu, studio za uandaaji wa filamu; pamoja na kujenga uwezo wa wadau waliojiajiri/kuajiriwa katika tasnia ya filamu.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bodi ya Filamu iliratibu uendeshaji wa Tamasha la Tuzo za Filamu na kutoa Tuzo kwa wadau waliofanya vizuri katika fani mbalimbali kwenye Tasnia ya Filamu ambapo kilele chake kilikuwa tarehe 17 Desemba, 2022 Jijini Arusha. Kupitia Tamasha hili, jumla ya Tuzo 45 zilitolewa kwa wadau wa filamu. Kati ya hizo, Tuzo 32 zilitolewa kwa washindi kwenye vipengele mbalimbali vilivyoshindaniwa, Tuzo 10 zilitolewa kwa wasanii/wadau wa filamu wakongwe, na Tuzo 3 zilitolewa

kwa viongozi wa Serikali akiwemo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua mchango wake katika kuilea na kuikuza Sekta ya Filamu nchini ikiwemo kufanikisha Tuzo hizo.



*Mshindi wa Tuzo ya kipengele cha Mwigizaji Bora wa Kike, Bi. Tunu Mwinyimbegu akikabidhiwa Tuzo hiyo na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Filamu kutoka Bodi ya Filamu Tanzania, Bw. Emmanuel Ndumukwa katika kilele cha Tuzo za Filamu Tanzania za mwaka 2022 tarehe 17 Desemba, 2022 Jijini Arusha.*

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kuratibu utoaji mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau wa filamu kupitia pragramu zake mbalimbali za mafunzo. Kwa mfano, katika kipindi hiki, kumefanyika mafunzo yaliyotolewa kwa mtindo wa uchambuzi wa filamu ijulikanayo kama ***Film Screening and Criticism***, ambapo kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, wadau 297 wamenufaika kupitia uchambuzi wa jumla ya filamu 19. Aidha, kupitia Programu ya kuwaendeleza wasanii chipukizi ijulikanayo kama ***The Coming Film Star*** iliwajengea uwezo wasanii chipukizi 60 katika masuala ya weledi, utawala wa fedha, pamoja na uwajibikaji. Pia, waandaaji wa filamu 16 walitembelewa katika maeneo yao ya kazi na kupata mafunzo kuhusu uboreshaji wa kazi za filamu. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na Chama cha Waigizaji Mkoa wa Morogoro iliandaa mafunzo yaliyotolewa kwa waigizaji 65 mkoani humo kupitia programu yake ya ***Taylor-made Training*** na kuwajengea uwezo katika fani ya uigizaji.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kuendelea kuimarisha uwezo wa tasnia ya filamu katika uzalishaji wa filamu Bodi ya filamu imeingia makubaliano na Asasi ya Busan Foundation for International Cooporation (BFIC) ya nchini Korea Kusini yenye lengo la kuanzisha shule ya filamu (Film Academy) nchini itakayotoa mafunzo kwa wasanii na wadau wetu ili kuwawezesha kuandaa filamu zenye ubora na shindani kimataifa. Aidha, jopo la wataalamu watano lilikuja nchini kutoka Korea Kusini kwa lengo la kufanya upembuzi yakinifu na kujua mahitaji halisi ya uanzishwaji wa shule hiyo.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** programu iitwayo *Mapping the Film Locations* yenye lengo la kutangaza mandhari za kipekee za upigaji picha za filamu zipatikanazo hapa nchini kama vile mbuga za wanyama, hifadhi, milima pamoja na miundombinu ya kisasa ya nchi, imeendelea kutekelezwa ili kuvutia wacheza filamu kutoka nje ya nchi kuja kutengeneza filamu zao hapa nchini. Maeneo hayo yanatangazwa kupitia makala fupi ya filamu iliyowekwa kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na Kihispania ili kuongeza wigo wa uelewa, na imesambazwa katika balozi 34 za Tanzania zilizopo katika nchi mbalimbali Duniani. Aidha, njia nyingine iliyotumika ni kupitia Taasisi mbalimbali, ikiwemo Kamisheni ya Filamu Nchini Namibia *(Namibia Film Commission)*, Kituo cha Utamaduni cha Irani *(Culture Center of Islamic Republic of Iran*), Chama cha Waendeshaji wa Biashara ya Utalii Tanzania *(Tanzania Association of Tour Operators),* Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kupitia Safari Chaneli pamoja na mitandao ya kijamii ya Bodi.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** kongamano (Symposium) la Wadau wa Filamu lililofanyika mwezi Desemba, 2022 Jijini Arusha liliandaliwa ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za kuweka mazingira ya wadau wa filamu kujadili masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya Tasnia ya Filamu. Kongamano hilo lilihudhuriwa na wadau wa filamu takribani 200 na lilihusisha mijadala ya masuala mbalimbali ya tasnia ikiwemo fedha, mitaji na weledi katika uandaaji wa filamu. Aidha, vikao 2 vilivyoshirikisha viongozi wa Shirikisho la Filamu Tanzania (TAFF) vilifanyika, ambapo masuala mbalimbali yanayohusu uongozi na mipango ya kuendeleza Tasnia ya Filamu kupitia vyama vinavyounda Shirikisho hilo yalijadiliwa. Vilevile, Bodi

iliwezesha maandalizi na kufanyika kwa Tuzo za Filamu kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu mbalimbali zijulikanazo kama UNI-AWARDS zilizotolewa tarehe 4 Desemba, 2022 jijini Dar es Salaam, ambapo jumla ya Tuzo 30 zilitolewa kwa wanafunzi hao.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** mkakati maalumu wa kurudisha utamaduni wa kuonesha na kutazama filamu kwenye kumbi za sinema ikiwa ni hatua ya kuongeza na kuwezesha masoko ya filamu za Kitanzania na kuboresha mapato ya kazi za filamu umeendelea kufanyika. Kwa kutumia utaratibu huo filamu ya **The Green Tanzanite** ilizinduliwa na kuoneshwa katika ukumbi wa Mlimani City tarehe 21 Aprili, 2023 na Mheshimiwa. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb.), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo watazamaji 222 walihudhuria. Vilevile, filamu nyingine zilizozinduliwa na kuoneshwa kupitia mkakati huu ni pamoja na filamu ya **Ugonjwa wa Kifo** iliyooneshwa eneo la wazi Tabata jijini Dar es salaam na filamu ya jina la **Dodoma** ambayo ilioneshwa katika ukumbi wa Mlimani City.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Bodi imeweza kutoa leseni za uendeshaji wa shughuli za biashara za filamu na michezo ya kuigiza 180, ambayo ni sawa na asilimia 300 ya lengo la kutoa leseni 60 katika kipindi hicho. Leseni hizo zilitolewa ikiwa ni hatua za urasimishaji wa shughuli na biashara ya filamu nchini. Aidha, Vitambulisho 271 ambayo ni sawa na asilimia 22.6 ya lengo la vitambulisho 1,200 vilitolewa kwa wadau wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki pekee jumla ya miswada na maombi 286 ya vibali vya kutayarisha filamu yamepokelewa na kuchambuliwa, ambapo kati yake, maombi 69 yalikuwa ya watayarishaji kutoka nje ya nchi, na maombi 217 ni ya watayarishaji kutoka ndani ya nchi (Watanzania). Aidha, jumla ya filamu 1,109 zilihakikiwa na kupangiwa madaraja, sawa na asilimia 73.9 ya lengo la filamu 1,500 kwa mwaka mzima. Kati ya filamu hizo, filamu za ndani ya nchi zilikuwa 1,097 na za nje ya nchi zilikuwa 12.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu Tanzania iliendesha Operesheni 35 kati ya 36 sawa na asilimia 97.2 ya oparesheni

zilizopangwa kufanyika kwa mwaka mzima katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na mikoa ya Tabora na Mwanza pamoja na mji wa Kahama mkoani Shinyanga. Operesheni hizo zilihusu ufuatiliaji wa vibali vya Bodi ya Filamu katika filamu zinazozalishwa na kusambazwa pamoja na kuwapo kwa ithibati za uendeshaji wa biashara za filamu zinazotolewa na Bodi ya Filamu. Aidha, hatua mbalimbali zimechukuliwa dhidi ya baadhi ya wadau wanaokiuka Sheria ikiwa ni pamoja na kuwaita wahusika ili watoe maelezo kuhusiana na uvunjifu wa Sheria pamoja na kuwaelimisha mambo ya kuzingatia wanapojihusisha na uzalishaji, usambazaji pamoja na biashara nyingine zinazohusisha kazi za filamu. Faida ya zoezi hili ni pamoja na kulinda haki za wamiliki na walaji wa mazao ya filamu pamoja na kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kupitia programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa katika Tasnia ya Filamu, Bodi iliandaa mikutano na mafunzo kwa vitendo yaliyotolewa kwa wadau wa filamu na michezo ya kuigiza ambapo jumla ya wadau 750 waliweza kufikiwa na kupewa elimu kuhusu masuala yanayohusu filamu na michezo ya kuigiza katika mikoa 25 ya Tanzania Bara.

### 3.2.2.4 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Ofisi ya COSOTA ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, na wachapishaji, kukusanya na kugawa mirabaha au ujira unaotolewa kulingana na haki zao zilizofafanuliwa katika Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999. Ukusanyaji na ugawaji mirabaha ni kwa kipindi ambacho Kampuni Binafsi za Wasanii na wamiliki wa hakimiliki na hakishiriki hazijaanza kazi. Aidha, COSOTA pia ina majukumu ya kutunza rejesta za kazi za ubunifu, usanii na vyama vya watunzi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti zilizorekodiwa, watangazaji na wachapishaji, kutoa elimu katika masuala ya hakimiliki, kusimamia uanzishwaji na uendeshwaji wa kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha ya wasanii na wamiliki wa hakimiliki na hakishiriki, kushughulikia migogoro ya hakimiliki ili kubainisha umiliki na kukuza ushirikiano na mashirika na ofisi za kimataifa

zinazohusiana na masuala ya hakimiliki na miliki bunifu kwa ujumla.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya shilingi 1,350,000,000 zilipangwa kupatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za Sanaa; leseni 419; Mirabaha toka kwa watumiaji wa kazi za sanaa; Ada ya Wanachama na usajili wa Hakimiliki; na Mapato ya Uendeshaji. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei 17, 2023 jumla ya shilingi 302,760,823, sawa na wastani wa asilimia 22.43 ya lengo zilikusanywa. Mapato mengine yalitegemewa kukusanywa kutokana na chanzo kipya cha mapato kutoka kwenye vibebeo vya kazi za ubunifu yaani *blanktape devices* ambapo hadi sasa taarifa ya utekelezaji wake kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) bado haijapokelewa.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea na usajili wa kazi na wasanii, waandishi na wabunifu wanaomiliki kazi za ubunifu. Kwa sasa usajili huo hufanyika kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha *www.hakimiliki.go.tz.*

Ili kuboresha usimamizi wa kazi za hakimiliki, COSOTA imepandisha kazi hizo katika mfumo wa kidigiti kwa utambuzi ili kujulikana zinapotumika kwenye mitandao mbalimbali. Inatarajiwa fedha kutokana na matumizi mbalimbali ya kazi hizo kuwasilishwa COSOTA kutoka katika Kampuni ya *Composers, Authors and Publishers Association* (CAPASSO) ya Afrika Kusini kwa ajili ya kupewa wasanii na wadau wa kazi husika. Jumla ya kazi 22,203 za muziki zilipandishwa kwenye mfumo baada ya kuhakikiwa na kusajiliwa katika mfumo wa WIPOCOS ili wasanii wanufaike na mgao wa kazi zao kwa njia ya kidigitali. Taarifa hizo zitawezesha Ofisi ya Hakimiliki kuweza kupokea fedha ya mirabaha kutokana na haki za matumizi ya Kidijitali (Digital Mechanical Rights) zinazosimamiwa na Taasisi hiyo iliyoko nchini Afrika Kusini.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na usajili na matumizi ya kazi nje ya nchi, COSOTA imeendelea na kufuatilia ushirikiano na Vyama dada kwenye mataifa mbalimbali. Ofisi imefanya mawasiliano na Ofisi za Hakimiliki katika nchi tatu (3) ambazo ni DR Congo *(Bureau Congolais du Droit dÁuteur - BCDA),* Liberia *(Copyright Society of Liberia - COSOL)* na Gambia *(Copyright*

*Society of Gambia - COSOG)* ili kuboresha ushirikiano wa usimamizi wa Hakimiliki. Kutokana na mabadiliko ya sheria kuanza kutambua kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha, COSOTA inatarajia kusaidia Kampuni husika kusaini mikataba na kampuni kama hizo kwa nchi mbalimbali ili kuwezesha ukusanyaji na ugawaji mirabaha. Katika kipindi hiki, COSOTA pia imekuwa na ushirikiano ambao umeendelea kupitia Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization -WIPO) na Shirika la Miliki Ubunifu Afrika (African Regional Intellectual Property Organization - ARIPO) na Shirikisho la Watunzi na Waandishi Duniani (Confederation of Authors and Composers Societues - CISAC), Shirikisho la Waandaaji wa kazi (International Federation of Phonograms Industries - IFPI) na Shirikisho linalohusika na uchapishaji (International Federation for Reprographic Rights Organizations -IFRRO).

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Ofisi ilipokea Migogoro 29 kwa ajili ya kufanyiwa usuluhishi na kati ya migogoro iliyopokelewa, iliyotatuliwa na kuhitimishwa ni migogoro 23 na 6 iliyobaki inaendelea na utaratibu wa utatuzi. Aidha, elimu ya hakimiliki ilitolewa kwa wateja 476 ambapo wateja 425 walitoka Dar es Salaam na wateja 51 walitoka Arusha. Kutokana na mageuzi ya taasisi (Institutional Reform) inayotokana na Marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki Na 7/1999 yaliyofanyika Julai, 2022 kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022, COSOTA pia imetoa elimu kwa wadau mbalimbali ikiwemo Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo tarehe 20 Septemba, 2022 na tarehe 18 Mei 2023. Vilevile, tarehe 30 Mei, 2023 COSOTA ilifanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ulinzi wa Hakimiliki za Kazi za Ubunifu.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, elimu pia imetolewa kwa Shirikisho la Sanaa za Maonesho, Shirikisho la Muziki Tanzania, Shirikisho la Filamu na Chama cha Wachapishaji Tanzania. Elimu kwa umma imefanyika kwa kushirikiana na wadau kama Benki ya NBC, Ziiki Media na Wasafi Media, Kampuni ya Multichoice Tanzania, Kampuni ya Azam Media, Taasisi za WUSM, Viwanja vya

Sabasaba (Tanzania Trade Development Authority - TANTRADE), ABC Initiative na *ABC Attorneys, Tanzania Music Foundation, Bongo Star Search* na *Tanzania Cosmetology Association* na Kadogoo *Club*.

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, COSOTA pia imeshirikiana na Kamati ya Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo iliyoundwa kwa ajili ya kukusanya maoni ya wadau kuhusu namna bora zaidi ya usimamizi wa hakimiliki nchini. Maoni na elimu kuhusu hakimiliki ilitolewa kwa Kanda sita (6) ambazo ni Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Kusini (Mtwara), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam). Matokeo ya kazi ya Kamati hiyo ni marekebisho ya Kanuni, kutolewa elimu kwa wadau, na mabadiliko ya muundo wa COSOTA. Mabadiliko ya Kanuni yamepelekea kuwapo na nafasi ya kuundwa kwa kampuni binafsi za wasanii (Collective Management Organizations – CMOs) ambazo zitahusika na ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wasanii. CMOs hizi zitaundwa na wasanii wenyewe.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuwa Kanuni za kuanzishwa kwa CMOs hizo zimepitishwa mwezi Mei, 2023, kwa sasa COSOTA ipo katika harakati za kuhamasisha na kutoa elimu kwa wadau wanaohusika kujiunga na kuunda CMOs zao. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwahimiza na kuwahamasisha wadau wote wanaohusika na hakimiliki kujiunga na kuunda CMOs zao kwa maslahi yao.

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na marekebisho ya kanuni ya leseni iliyoingizwa katika mfumo wa Government electronic Payment Gateway (GePG), COSOTA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imefanya maboresho ya mfumo wa usajili na utoaji wa leseni unaopatikana <u>*www.hakimiliki.co.tz*</u> kwa lengo la kuwezesha mfumo kutumika kwa urahisi zaidi. Marekebisho hayo ni pamoja na uwekaji wa viwango vipya vya leseni (Tariffs). Matokeo ya marekebisho hayo ya mfumo ni pamoja na kuongezeka kwa usajili wa wanachama 576; kusajiliwa kwa kazi 1,074 na leseni 6.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imehuisha Muundo wa Taasisi (Organisation Structure) baada ya marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki. Marekebisho hayo yalifanyika kwenye majukumu ya Idara ya Leseni na Uharamia, Idara ya Kumbukumbu pamoja na kuanzishwa kwa Kurugenzi ya Sheria na Vitengo vyake ambapo hapo awali kilikua Kitengo kimoja. Rasimu ya Muundo huo imewasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa hatua zaidi za utekelezaji.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji, COSOTA imefanya ukaguzi dhidi ya warusha maudhui kwa njia ya waya wasio na leseni na kutumia maudhui ya wazalishaji/wamiliki kinyume na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na.7/1999. Ukaguzi huo ulifanyika kwa kushirikiana na wadau yaani Kampuni ya Multichoice Tanzania; Kampuni ya Azam Media; na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika mikoa ya Arusha, Geita, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Mtwara na Pwani. Kutokana na ukaguzi huo, kesi tano (5) zilifunguliwa na mmiliki mmoja wa *cable* mkoani Katavi alipewa barua ya onyo kwa kuzuia maafisa ukaguzi kutekeleza majukumu yao. Vilevile, ukaguzi umefanyika kwa wanaogoma kulipia leseni kwa mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Arusha. Ukaguzi kama huo utaendelea kufanyika katika mikoa mingine ya Tanzania Bara iliyobaki, hadi mikoa yote itakapofikiwa.

### 3.2.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatuwezi kuendeleza sanaa bila kuwekeza katika utaalamu na utafiti; TaSUBa ni Taasisi inayotoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusiana na masuala ya Sanaa na Utamaduni nchini. TaSUBa ni Taasisi ambayo inatoa kozi mbalimbali za masuala ya Sanaa na Utamaduni, miongoni mwa kozi hizo ni pamoja na Filamu na Uzalishaji wa Vipindi vya Televisheni (Film and TV Production); Uzalishaji wa Muziki na Sauti (Music and Sound Production); na Sanaa za Maonesho na Ufundi (Performing and Visual Arts). Aidha, Taasisi inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya kozi mpya ambazo ni Usimamizi wa Sanaa na Masoko katika Sanaa (Arts Management and Marketing); Urithi wa Utamaduni na Utalii (Cultural Heritage and Tourism); na Muziki (Music). Mafunzo ya kozi hizo yataanza mara tu baada ya kukamilisha mahitaji ya NACTVET ambayo yako katika hatua za

mwisho kukamilishwa. Kazi zote zitatolewa katika ngazi ya Astashahada na Stashahada (Certificate and Diploma).

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 TaSUBa imefanikiwa kuvuka lengo kwa kudahili wanachuo 684 wa kozi ndefu sawa na ongezeko la asilimia 14 ya lengo la wanachuo 600. Ongezeko hilo linatokana na uhamasishaji mkubwa uliofanywa na Taasisi. Kwa wanafunzi waliodahiliwa kozi fupi kwa kipindi hicho ni 222, sawa na asilimia 148 ya lengo la kudahili wanafunzi 150. Aidha, Taasisi imefanikiwa kuendesha semina mbili (3), warsha tatu (5) na kongamano moja (1). Kongamano lilifanyika wakati wa Tamasha la Kimataifa la 41 la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ambapo washiriki walitoka nje na ndani ya nchi, hivyo lilifanyika kwa mafanikio makubwa kutokana na mahudhurio ya washiriki na mada zilizojadiliwa katika kongamano hilo.

**109. Mheshimiwa *Spika***, pia Taasisi imefanikiwa kuandaa Mitaala na kuiwasilisha kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (The National Council for Technical and Vocational Eduction and Training - NACTVET) kwa ajili ya kupata Ithibati. Mitaala hiyo ni: Urithi wa Utamaduni na Utalii - Cultural Heritage and Tourism; Muziki – Music; na Usimamizi wa Sanaa na Masoko - Art Management and Marketing.

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi iliendesha Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo ambapo Taasisi hii ni muanzilishi na mwenyeji wa Tamasha hilo lililofanyika tarehe 10 - 12 Novemba, 2022, ambalo hufanyika kila mwaka mara moja. Mgeni rasmi siku ya ufunguzi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tamasha lilihudhuriwa na watazamaji wa ndani na nje wanaokadiriwa kufikia 30,000. Aidha, vikundi mbalimbali vya sanaa kutoka ndani na nje ya nchi vipatavyo 46 vilishiriki. Kati ya hivyo, vikundi vya ndani vilikuwa 40 na vya nje 6 kutoka nchi za Zambia (vikundi 4); Canada (kikundi 1); na Visiwa vya Mayotte – Ufaransa (kikundi 1).



*Onesho la Sanaa la Wakufunzi na Wanachuo katika Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo lililofanyika tarehe 10 Novemba, 2022 Bagamoyo, Pwani.*

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, TaSUBa imeendelea Kuimarisha Mtandao (Networks) kati ya Taasisi na Wadau wa Sanaa Nje na Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na wadau wa ndani wafuatao ambao tayari makubaliano ya ushirikiano (MoU) yamesainiwa. Miongoni mwa wadau wa ndani ni pamoja na *Good Neighbours Tanzania;* Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania *(Tanzania Correction Training Academy -TCTA); Tanzania House of Talent (THT);* na *Naweza Foundation*. Wadau wa nje ambao Taasisi inashirikiana nao na makubaliano ya ushirikiano (MoU) yamesainiwa ni pamoja na *Bagamoyo Friendship Society* (Ujerumani); *Musicians for a Better Life* (Ujerumani); na *Volkshochschule Ahlen* (VHS Ahlen - Ujeremani). Taasisi inaendelea na mazungumzo na taratibu za kusaini ushirikiano na *Pedagogical Studies & Arts Teacher's Pedagogical Studies - University of the Arts Helsinki* Finland; *Teaching Artist Institute - TAI* (Marekani); na *Media for Development International Inc*. (Marekani).

### 3.2.3 SEKTA YA MICHEZO
### 3.2.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Michezo hapa nchini ina jukumu la kuhakikisha inaweka mazingira bora na kuwezesha Maendeleo ya Michezo hususan kuzalisha ajira, kuimarisha afya za wananchi pamoja na kuwaletea furaha Watanzania. Sekta hii kwa sasa inatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 ambayo imetengenezewa mkakati wa Utekelezaji wa mwaka 2022. Sekta hii ni miongoni mwa mihimili inayotoa ajira na kuchangia katika uchumi wa mtu mmoja mmoja na kwa Taifa kwa ujumla. Aidha, sekta hii inahusisha Idara ya Maendeleo ya Michezo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Katika kutekeleza majukumu yake Wizara kupitia Sekta hii imetekeleza majukumu ifuatavyo:

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeratibu mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika mwezi Julai hadi Agosti, 2022 nchini Uingereza katika mji wa Birmingham. Timu mbalimbali kutoka Tanzania zilishiriki zikiwemo timu za michezo ya Riadha, Ngumi, Judo, Kuogelea na Kunyanyua Vitu Vizito (Powerlifting). Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi Tanzania ilifanikiwa kupata medali tatu (3), ambapo moja (1) ni ya fedha kutoka kwa mwanariadha Alphonce Simbu aliyoipata katika mbio za Marathon na mbili (2) za shaba kutoka kwa mabondia Yusuph Changarawe aliyemchapa bila huruma kwa *knockout* bondia Arthur Langlier wa St. Lucia na Kassim Mbundwike aliyepata medali hiyo baada ya kumuadhibu kwa *knockout* bondia Marion Faustino Ah Tong kutoka visiwa vya Samoa.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu mashindano ya Taifa Cup, Ili kuhakikisha Mashindano hayo yanakuwa na hadhi ya Taifa, Serikali kupitia Wizara imeelekeza mashindano hayo kuanzia katika ngazi ya chini kabisa ya Mtaa. Dhana hii ndiyo inayofahamika kama Mashindano ya Taifa Cup Mtaa kwa Mtaa. Mashindano haya yaliyozinduliwa katika Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani tarehe 16 Oktoba, 2022 na baadaye Jijini Arusha tarehe 9 Desemba, 2022 ambapo pia yalizinduliwa katika Wilaya ya Karatu tarehe 10 Desemba, 2022 na aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Mohamed O.

Mchengerwa (Mb.). Mashindano haya yanaanzia ngazi ya Mtaa na kuendelea hadi ngazi ya Taifa. Lengo la mashindano hayo ni kuibua vipaji vya michezo na sanaa kuanzia ngazi ya mtaa. Kutokana na mpango huo Serikali imefanikiwa kupata vifaa vya michezo vitakavyotumika katika mashindano hayo, kutoka kwa wafadhili nchini China ambavyo vitagawiwa kwa Halmashauri ikiwa ni hatua ya kuyawezesha mashindano hayo kuwa na hamasa na kuvutia washiriki wengi zaidi katika ngazi zote.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ina dhamira ya kweli ya kuinua michezo, ambapo imeendelea kuziwezesha Timu za Taifa kwa kadri bajeti inavyopatikana. Katika kipindi cha mwaka 2022/23 Timu ya Taifa ya Wanawake (Serengeti Girls) iliwezeshwa kukaa kambi ya maandalizi ya wiki mbili nchini Uingereza katika jiji la Southampton kabla ya kushiriki fainali za kombe la dunia nchini India. Aidha, Serikali iligharamia kambi ya maandalizi ya miezi sita iliyofanyika ndani ya nchi na wiki mbili nchini Uturuki Timu ya Wanaume ya mpira wa miguu ya Watu Wenye Ulemavu (Tembo Warriors) kushiriki mashindano ya fainali za Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Uturuki. Aidha, Serikali iliisaidia Timu ya *Fountain Gate* ya Mpira wa Miguu iliyopo Jijini Dodoma kushiriki mashindano yaliyoandaliwa na CAF kwa shule za Sekondari ya Bara la Afrika kwa Wasichana yaliyofanyika Durban Afrika Kusini mwezi Aprili, 2023 na Timu hiyo ilitwaa Ubingwa wa Bara la Afrika.

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania imeendelea kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa ambapo tarehe 10 Agosti, 2022 ilikuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 44 wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ambao ulifanyika Jijini Arusha na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) Bw. Giani Infantino pamoja na viongozi wengine kutoka sehemu mbalimbali Afrika na Duniani walishiriki mkutano huo. Aidha, tarehe 24 Mei, 2023 Wizara imewasilisha Taarifa ya Tanzania kwa kushirikiana na nchi ya Kenya na Uganda kuhusu kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu barani Afrika (AFCON 2027). Taarifa ya kuomba zabuni ya kuwa mwenyeji wa mashindano hayo imeshawasilishwa CAF na kura ya uamuzi wa nani ameshinda zabuni hiyo itapigwa mwezi Julai, 2023. Fauka ya hayo, nchi zinazoshindania uenyeji wa mashindano hayo ni pamoja na Botswana, Misri, na Algeria.

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 2 - 4 Mei, 2023 nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Michezo wa Baraza la Michezo la Afrika Kanda ya IV uliofanyika Jijini Arusha ambapo Viongozi kutoka Nchi 9 kati ya 14 wanachama wa Baraza hilo walishiriki. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alituma salamu, naomba ninukuu. "*Huu ni mkutano wa kwanza wa kihistoria wa Kanda ya IV kufanyika katika ardhi ya Tanzania. Tunawakaribisha Wajumbe wote wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV hapa nchini kwetu ambayo ni Nchi ya amani na ukarimu ikiwa na vivutio vingi vya Utalii Bora Duniani*". Mwisho wa kunukuu.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, mgeni rasmi katika mkutano huo alikuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kati ya mambo aliyoyasema, miongoni ni pamoja na, naomba ninukuu "*kuwekeza kwenye kujenga uwezo wa kitalaamu ili kuzalisha wanamichezo wanaoweza kuleta mageuzi kwenye Sekta ya Maendeleo ya Michezo na Maendeleo kupitia Michezo. Tusikubali kushika mkia kila siku na wala tusikubali kurudi nyuma. Lengo la kila taifa ni kuona timu yake inashinda makombe ya Kimataifa hasa Kombe la Dunia. Tukiamua kuwekeza kwenye miundombinu ya michezo na ujuzi pamoja na kushirikiana tunaweza kufikia malengo makubwa kwenye sekta ya michezo*". Mwisho wa kunukuu.



*Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Mkutano wa Mawaziri wa Michezo wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV uliofanyika Jijini Arusha tarehe 2 - 4 Mei, 2023.*

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutumia Mkutano huo, Tanzania ilitumia fursa hiyo vizuri kwa kuomba nafasi ya kuwa Makao Makuu ya Kanda ya IV ambapo ilikidhi vigezo vyote ambavyo Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV vilitakiwa na hivyo kuifanya Tanzania kuchaguliwa kuwa Makao Makuu ya Sekretarieti ya Baraza hilo. Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV linahusisha nchi za Comoros, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Madagascar, Mauritius, Rwanda, Sychelles, Somalia, Sudan, Sudani Kusini, Uganda na Tanzania. Kwa kuwa Ofisi za Makao Makuu ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV imepitishwa kuwa Tanzania, itasaidia kudumisha uhusiano na mataifa wanachama na itatoa ajira kwa vijana wa Kitanzania hususan katika sekta ya michezo lakini pia itasaidia kuhamasisha upatikanaji wa wataalamu zaidi wa michezo.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na mafanikio kadhaa yaliyopatikana katika kipindi ambacho Serikali ilitia mkono wake katika kuziunga mkono Timu za Taifa zinapokwenda kwenye

mashindano ya Kimataifa, Serikali itaendelea kuziunga mkono Timu zote za Taifa zitakazofuzu kushiriki mashindano ya Kimataifa. Ili kuhakikisha hilo linatekelezwa, Serikali itaendelea kutenga bajeti ya kuhudumia Timu za Taifa kujiandaa na kushiriki Mashindano ya Kimataifa. Mfano, mwaka 2019/20 Serikali ilitenga Sh. 270,000,000; mwaka 2020/21 ilitenga Sh. 431,000,000; mwaka 2021/22 ilitenga Sh. 1,320,000,000; mwaka 2022/23 ilitenga Sh. 1,446,900,000; na mwaka 2023/24 Serikali imetenga Sh. 1,066,895,000.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa na miundombinu ya michezo bora katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa sasa, Wizara inaendelea na taratibu mbalimbali za Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi (Recreational and Sports Centres) katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo mikataba ya ujenzi imesainiwa kwa maeneo ya Dar es Salaam na Dodoma. Mkandarasi amekabidhiwa maeneo na ameanza hatua za awali za ujenzi (mobilization stage). Ujenzi wa maeneo hayo unatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 54.6 na ujenzi utafanyika katika kipindi cha miezi 36. Serikali pia inaendelea na taratibu za ujenzi wa uwanja mkubwa wa michezo katika Mkoa wa Dodoma katika eneo la Nzuguni ambapo zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa uwanja huo imetangazwa. Sambamba na ujenzi wa Uwanja wa Michezo Dodoma, pia Serikali inajiandaa kujenga Uwanja kama huo katika jiji la Arusha kwa ajili ya kujiandaa na michezo ya AFCON 2027 endapo nchi za Afrika Mashariki zitashinda zabuni ya kuandaa michezo hiyo.



*Muonekano wa Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi kitakavyokuwa mara baada ya kukamilika kujengwa katika jiji la Dodoma eneo la Nanenane Nzuguni.*

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeanza kukarabati miundombinu ya Michezo katika shule Teule za Michezo Nchini. Shule hizi 56 za Sekondari zinahusisha shule mbili kwa kila Mkoa, kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara ikiwa na lengo la kuendeleza vipaji vya michezo mbalimbali vinavyoibuliwa kutoka katika ngazi ya shule za msingi. Miundombinu ya Michezo kwenye shule zilizoteuliwa inahitaji ukarabati na ujenzi. Utekelezaji wa mpango wa kuboresha miundombinu hiyo utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo kwa awamu ya kwanza, imefanyika tathmini ya miundombinu ya michezo katika shule saba (7) kutoka katika mikoa ya Tabora, Tanga, Dodoma, Manyara, Pwani na Mtwara. Mshauri mwelekezi kwa ajili ya kusimamia mradi huu amepatikana ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na kwa sasa kwa kushirikiana na Wizara anaendelea na zoezi la kukamilisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kutekeleza mradi huo.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa (OR-TAMISEMI) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliandaa Mwongozo kwa ajili ya maandalizi na uendeshaji wa Michezo ya Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) na Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) Kitaifa.

Mwongozo unabainisha masuala mbalimbali ikiwemo utaratibu wa uteuzi wa Kamati ya Kitaifa ya uratibu, Udhamini, mgawanyo wa bajeti na ugharamiaji wa mashindano hayo. Kwa mwaka 2022/23 mashindano hayo yaliyofanyika mkoani Tabora kuanzia tarehe 29 Julai, 2022 hadi 19 Agosti, 2022 jumla ya wachezaji na viongozi 3,920 wa shule za msingi walishiriki, na wachezaji na viongozi 4,200 wa shule za Sekondari kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani walishiriki. Mashindano haya yamekuwa na manufaa makubwa kwa kuwaunganisha wanafunzi na ni njia mojawapo ya kuibuwa vipaji kwa ajili ya timu zetu za Taifa na vilabu mbalimbali nchini.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwongozo wa uendeshaji wa mashindano ya UMISSETA, UMITASHUMTA na *Federation of East Africa Secondary School Sports Associations* (FEASSSA) umekamilika na umesambazwa katika Sekretarieti za mikoa na Wizara zenye dhamana na Elimu, Michezo na OR-TAMISEMI. Aidha, mwongozo huo umezinduliwa wakati wa uzinduzi wa michezo UMISSETA na UMITASHUMTA ya tarehe 04 Agosti, 2022. Aidha, mashindano hayo kwa mwaka 2023 yamezinduliwa tarehe 03 Juni, 2023 na yanafanyikia mkoani Tabora, ambapo mashindano ya FEASSSA yatafanyika mwezi Agosti, 2023 nchini Rwanda, baada ya kumalizika kwa mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA.



*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia) akizindua Mwongozo wa Michezo ya UMISSETA, UMITASHUMTA na FEASSSA tarehe 04 Agosti, 2022.*

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na mbinu haramu za matumizi ya dawa za kuongeza na kusisimua misuli michezoni, Serikali kupitia Wizara ilipokea fedha dola za Marekani 21,025.06 mwezi Septemba, 2022 kutoka Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) kwa ajili ya kuwezesha mafunzo ya kukabiliana na matumizi ya dawa na mbinu haramu michezoni. Kutokana na fedha hizo masuala yaliyofanyika ni pamoja na wajumbe 2 kutoka Tanzania walihudhuria Mkutano wa Kanda ya Tano wa *Antidoping* nchini Uganda mwezi Oktoba, 2022; kuwezesha kuendesha mafunzo ya Wakufunzi (ToT) kwa Maafisa 30 kutoka Wizarani, BMT, Vyama vya Michezo na Maafisa Michezo wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam; mafunzo ya uelewa kuhusu *antidoping* kwa viongozi 180 wa vyama vya kitaifa vya Michezo; mafunzo kwa wadau na waendeshaji wa mashindano ya michezo 100 kuhusu umuhimu wa kuwapo kwa Sheria ya *antidoping*; na mafunzo kwa Maafisa Michezo 38 wa mikoa, BMT na Wizara yaliyofanyika Jijini Dodoma tarehe 31 Novemba hadi 1 Desemba, 2022.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekuwa ikiimarisha na kuwashirikisha watu wenye mahitaji maalumu katika michezo. Kwa mwaka 2022/23 katika michezo ya UMISSETA na UMITASHIMTA kwa mara ya kwanza watoto wenye mahitaji maalumu walishiriki michezo hiyo iliyofanyika katika mkoa wa Tabora. Aidha, kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Timu ya Taifa ya Mchezo wa Tennis (Wheel Chair Tennis) imewezeshwa kupata eneo la kujenga Miundombinu ya michezo jijini Dar es Salaam katika Wilaya ya Kigamboni; Timu ya Wanawake ya Basketball (Wheel Chair Basketball) ilishirikishwa katika Tamasha la Wanawake lijulikanalo kwa jina la *Tanzanite International Women Sports Festival* lililofanyika tarehe 20 hadi 22 Oktoba, 2022 Jijini Dar es Salaam; na Timu ya Taifa ya Walemavu wanaocheza mpira wa miguu (Tembo Warriors) waliwezeshwa kifedha na kiutaalamu hadi kufika robo fainali ya mashindano ya Kombe la Dunia kwa mchezo huo yaliyofanyika nchini Uturuki kuanzia tarehe 30 Septemba hadi 10 Oktoba, 2022.

### 3.2.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kusimamia aina

zote za michezo ya ridhaa na kulipwa kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo; kusajili Vyama vya Michezo; kutoa Tuzo kwa Wanamichezo wanaofanya vizuri katika mashindano ya Kitaifa na kimataifa; na kuamsha ari ya wananchi kupenda aina zote za michezo.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT limewezesha kuzigharamia Timu za Taifa kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Serikali kupitia BMT, imewezesha jumla ya timu 15 kushiriki katika mashindano ya kimataifa ambapo kiasi cha shilingi 3,636,512,694.90 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Michezo, udhamini na harambee zimetumika. Timu hizo ni pamoja na Timu za michezo ya Riadha, Ngumi, Judo, Kuogelea na Parapowerlifting ziliwezeshwa kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika Birmingham nchini Uingereza. Katika mashindano hayo Tanzania ilipata jumla ya medali tatu katika mchezo wa Riadha na Ngumi; Timu ya Taifa ya vijana ya Mpira wa Miguu kwa Wanawake (Serengeti Girls) iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini India kuanzia tarehe 11 hadi 30 Oktoba, 2022 ambapo timu hiyo ilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali. Hii iliwezekana baada ya timu yetu kuichapa timu ya Taifa ya Ufaransa mabao (2-1) na kutoka sare dhidi ya Kanada (1-1).

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu (Tembo Warriors) iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Uturuki kuanzia tarehe 30 Septemba hadi 10 Oktoba, 2022 ambapo timu hiyo ilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali na kushika nafasi ya saba (7) duniani. Pia, Timu hiyo ilifanikiwa kuziadhibu nchi kubwa duniani kama Japan (3-1) na Uzbekistan (3-0) na kutoka sare na nchi ya Uhispania (0-0). Aidha, baada ya mashindano hayo, timu hiyo ilifanikiwa kuuza wachezaji 10 katika vilabu vya nchini humo. Wachezaji waliobahatika kupata ajira katika Timu za nchini Uturuki ni pamoja na Alfan Kyanga, Juma Kidevu, Habibu Likoike na Shedrack Hebron waliosajiliwa kwenye klabu ya Sisli Yeditepe. Wengine ni Abdulkarim Amiri na Salimu Bakari waliosajiliwa na klabu ya Keysari, Ramadhan Chomelo

aliyejiunga na klabu ya Konya na Frank Ngailo klabu ya Izmir BBSK na Mudrick Azzan na Richard Swai kwenye klabu ya Mersin.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23 Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo mpira wa miguu ambapo hivi karibuni timu zetu za Simba na Yanga zimeweza kufika katika hatua nzuri katika michezo ya Klabu Bingwa na Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Timu ya Yanga kwa mara ya kwanza katika historia ya michezo ya Shirikisho imekuwa ya kwanza kufuzu kucheza fainali baada ya kuiondoa timu ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini kwa mabao 4-1 katika hatua ya nusu fainali. Aidha timu ya Simba ilifanikiwa kuingia robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuibuka mshindi wa mabao 7-0 dhidi ya timu ya Horoya ya Guinea.

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio hayo yamechochewa na maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alichangia kwa kuziongezea morali timu zetu kwa kununua magoli ya ushindi, ambapo alianza na Sh. 5,000,000 katika hatua ya makundi na robo fainali; Sh. 10,000,000 katika hatua ya nusu fainali; na Sh. 20,000,000 na kutoa usafiri wa ndege katika hatua ya fainali. Kutokana na hamasa hiyo ya Mheshimiwa Rais, Timu ya Simba imeweza kupata jumla ya magoli 11 katika hatua ya makundi na robo fainali na kujikusanyia jumla ya Sh. 55,000,000 wakati Timu ya Yanga imeweza kupata magoli 16 katika hatua ya makundi, robo, nusu fainali na fainali na kujikusanyia jumla ya Sh. 115,000,000. Mafanikio hayo ni makubwa na ya kihistoria kwa nchi yetu kwa kuwa inaimarisha ubora wa ligi yetu na kuitangaza Tanzania nje ya mipaka yetu.

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, kadhalika wanamichezo wa Tanzania wameendelea kufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania. Wachezaji hao ni pamoja na Gabriel Gerald Geay aliyeshika nafasi ya pili katika Mbio kubwa Duniani za Boston Marathon na Valencia Marathon, mwanariadha Alphonce Felix Simbu aliyeshika nafasi ya Tatu katika mbio za Osaka Marathon na Yangzhou Jianzhen Half Marathon. Aidha, Timu ya Taifa ya Mchezo wa kuogelea ilishiriki Mashindano ya kualikwa nchini Afrika ya Kusini yaliyoshirikisha nchi

10 na kunyakua jumla ya medali 74 na kushika nafasi ya pili. Katika Nyanja za masumbwi, mabondia wa Kitanzania wameendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa. Mabondia waliofanya vizuri katika kipindi hiki ni pamoja na;

(i) Twaha Kiduku ambaye alimcharaza bondi Lago Kiziria kutoka nchini Georgia katika pambano lililofanyika mkoani Morogoro tarehe 22 Aprili, 2023;

(ii) Hassan Mwakinyo ambaye alimbamiza bondia Murdochee Kuvesa Katembo kutoka nchini Congo DRC katika pambano lililofanyika jijini Dodoma tarehe 23 Aprili, 2023;

(iii) Ibrahim Class ambaye alimchakaza bondia Gustavo Pina Melger kutoka nchini Mexico katika pambano lililofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 30 Septemba, 2022;

(iv) Mwanadada Fatuma Yazidu alimcharanga bondia Consolata Musanga kutoka nchini Kenya katika pambano lililofanyika Nairobi Kenya tarehe 25 Machi, 2023; na

(v) Bondia machachari Karim Mandonga alimchanachana bondia Kenneth Lukyamuzi kutoka nchini Uganda katika pambano lililofanyika Nairobi Kenya tarehe 25 Machi, 2023.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Timu ya Taifa ya Netiboli iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Afrika ya kufuzu kushiriki Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Afrika Kusini mwezi Agosti, 2022. Vilevile Timu ya Taifa ya Wanawake ya Gofu iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Afrika ya *All Africa Challenge Trophy* yaliyofanyika mwezi Septemba, 2022 ambapo Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mashindano hayo na kuibuka mshindi wa jumla wa tatu. Mafanikio mengine ni pamoja na Shirikisho la Michezo Vyuo Vikuu Tanzania kushiriki Kambi ya wanavyuo vya Afrika Mashariki; na Timu ya Taifa ya Kuogelea iliwezeshwa kushiriki mashindano ya ubingwa wa Kanda ya tatu, ambapo Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mashindano hayo na timu ya Tanzania iliibuka mshindi wa kwanza kati ya nchi 12 zilizoshiriki.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, mashindano ya Afrika Kanda ya Tano ya mpira wa mikono (handball) ambayo yalifanyika tarehe 25 hadi 30 Aprili, 2023 jijini Dar es Salaam na kushirikisha nchi 9 ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Somalia, Ethiopia, Sudan Kusini na Djibouti yamewezeshwa. Vilevile, mashindano ya Judo ya Kanda ya Tano Afrika Mashariki ambayo yalifanyika kuanzia tarehe 29 hadi 30 Aprili, 2023 jijini Dar es Salaam na kushirikisha nchi za Tanzania Bara, Zanzibar, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Somalia na Congo DRC yamewezeshwa. Pia, mashindano ya kimataifa ya Mpira wa Kikapu kwa Watu wenye Ulemavu (wheelchair basketball) yaliyofanyika tarehe 5 – 7 Mei, 2023 jijini Dar es Salaam na kushirikisha nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Ethiopia yaliwezeshwa. Aidha, Baraza liliwezesha mashabiki wa klabu ya Yanga kwenda nchini Afrika Kusini kushuhudia mechi ya nusu fainali ya kombe la Shirikisho baina ya Yanga na Klabu ya Marumo Gallants.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mazingira na amani iliyopo katika nchi yetu, imekuwa ni kuvutio kwa nchi za Afrika na dunia kwa ujumla kutaka kuendesha mashindano ya michezo mbalimbali katika nchi hii. Hivi karibuni tumepokea maombi kutoka Chama cha Kriketi Tanzania (TCA) la kuwa mwenyeji wa mashindano ya Kriketi ya kufuzu Kombe la Dunia kwa timu za vijana waliochini ya umri wa miaka 19 kwa nchi za Afrika. Mashindano hayo yatafanyika tarehe 21 - 30 Julai, 2023 jijini Dar es Salaam. Tunavikaribisha vyama vingine vya michezo kutoka duniani kote kuja Tanzania kufanya michezo yao, kwani ni sehemu sahihi wala hawatajutia maamuzi watakayokuwa wameyafanya ya kuichagua Tanzania.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Serikali kupitia BMT imefanikiwa kusajili Vyama 5, Vilabu 109, Akademi 8, Vituo 10, Mawakala 4 na Wakuzaji 17. Aidha, mapitio ya Katiba ya Shirikisho ya Karate Tanzania (Tanzania Sports Karate – Do Federation), Chama cha Mchezo wa Gofu (Tanzania Golf Union) na Chama cha Mpira wa Miguu kwa Wanawake Tanzania yamefanyika. Pia, marekebisho ya Katiba ya Chama cha Morogoro Region Basketball Association na Katiba za Vilabu vinne (4) ambavyo ni Tanganyika Kigoma Football Club, Copco

Football Club, Ceassia Queens Football Club, na Rock Solution Football Club yamefanyika.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT limefanikiwa kujenga Mfumo wa Usajili wa kidigitali (Online Registration) wenye lengo la kurahisisha utaratibu wa usajili kwa watendaji na wadau wa michezo. Mfumo huu utasaidia shughuli za usajili kufanyika kidigitali. Mfumo huu utawarahisishia wadau wa michezo kufanya usajili mahali popote walipo na kuwezesha kufanya malipo kwa kupata namba ya kumbukumbu ya malipo (control number). Kadhalika, mfumo huu utasaidia kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli. Kwa sasa mfumo upo kwenye hatua ya majaribio.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwapo kwa wataalamu wa kutosha wa Michezo, BMT liliendesha mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo wanamichezo. Mafunzo hayo yalitolewa kwa michezo na viwango tofauti ambavyo ni BMT kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa liliratibu na kusimamia mafunzo kwa wataalamu wa Ngumi za Kulipwa wakiwemo Makocha, Waamuzi na Wakuzaji wa Ngumi za Kulipwa nchini. Jumla ya wataalamu 100 walipata mafunzo hayo. Lengo ni kuwajengea uwezo wataalamu wa Ngumi kutekeleza majukumu yao kitaalamu kuendana na wakati. Aidha, kwa kushirikiana na Vyama vya Mchezo wa Riadha, Mpira wa Miguu na Netiboli Baraza liliratibu mafunzo kwa Walimu wa Shule teule 56 za Michezo za Sekondari kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara. Jumla ya walimu 57 walipata mafunzo ya Mpira wa Miguu, Netiboli na Riadha. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea walimu uwezo wa kwenda kuibua na kuendeleza vipaji vya vijana kupitia shule hizo.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT liliendesha mafunzo kwa walimu wa Shule za Sekondari wapatao 48 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mafinga mkoani Iringa. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu kuibua na kuendeleza vipaji vya watoto katika shule. BMT pia limesimamia Utawala Bora kwa Vyama vya Michezo. Katika kuendeleza dhana ya utawala bora kwa vyama, BMT limeweka mikakati mbalimbali ikiwemo kuandaa Katiba za mfano kwa vyama, vituo, wakuzaji, mawakala wa michezo, kufanya chaguzi za vyama mbalimbali vya michezo. Vyama vilivyofanya chaguzi ni pamoja na Tanzania Baseball & Soft Ball

Association (TaBSA); Tanzania Rugby Union (TRU); Tanzania Table Tennis Association (TTTA); Tanzania Hockey Association (THA); Tanzania Golf Union (TGU), Tanzania Ladies Golf Union (TLGU), Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Chama cha Baiskeli Tanzania (CHABATA)na Athletics Tanzania (AT).

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT iliratibu vikao kazi vya kamati za utendaji za Vyama na Mashirikisho ya Michezo ili kuwashauri na kuwajengea uwezo wa kiutawala na uongozi ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 vikao vya vyama 15 vimefanyika kama ifuatavyo: Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu (TAFF); Shirikisho la Ngumi za Wazi Tanzania (OBFT); Chama cha Baseball & Softball Tanzania (TaBSA); Chama cha Kabaddi Tanzania; Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA); CHANETA NA CHANEZA; Riadha Tanzania (RT); Umoja wa wachezaji wa Soka wa Zamani (UMSOTA); PAN AFRICA; SIMBA SC; TFF & DRFA; Special Olympics; Chama cha Kriketi Tanzania (TCA); Chama cha WUSHU Tanzania; na Chama cha Tenisi Tanzania (TTA).

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT lilifuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za michezo katika mikoa 26, Wilaya 52, Vyama vya Michezo 54 na Taasisi za Michezo 15. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza liliendesha kikao kazi cha ufuatiliaji na tathmini kilichohusisha Makatibu wa Kamati zote za Michezo Tanzania Bara. Kikao hicho kilihudhuriwa na Makatibu kutoka mikoa 24 ya Tanzania Bara. Vilevile, Baraza lilifanya vikao kama hivyo na Vyama 28 na Taasisi tatu (3) za Michezo. Katika vikao hivyo ilisisitizwa kuendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa shughuli za michezo katika ngazi za mikoa na Wilaya ikiwemo kuhamasisha ushiriki wa jamii katika michezo, kusimamia uendelezaji wa viwanja na miundombinu ya Michezo, kuibua vipaji, na kusimamia vyama na Vilabu vya Michezo katika ngazi za mikoa na Wilaya.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT lilifanya ufuatiliaji wa mashindano mbalimbali ya Kitaifa yanayoandaliwa na Vyama na Mashirikisho ya Michezo ikiwemo SHIMMUTA – Tanga, SHIMIWI – Tanga, SHIMISEMITA – Morogoro, UMISSETA na UMMITASHUMTA – Tabora. Riadha – Arusha, Dodoma na Dar es Salaam, CHANETA –

Morogoro na Dar es Salaam na kubaini kuwa mashindano hayo yanaleta hamasa kubwa na kusaidia ukuzaji na uendelezaji wa vipaji pamoja na kupunguza maradhi yasiyoambukiza. Pia yanahamasisha mshikamano, uzalendo na umoja miongoni mwa washiriki.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika Michezo, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, Baraza liliratibu Tamasha la Kimataifa la Michezo la Wanawake (Tanzanite International Women Sports Festival) likihusisha Kongamano na Mashindano ya Michezo mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi. Jumla ya wanamichezo 712 kutoka vyama vya michezo 13 ikiwemo Mpira wa Miguu wanawake, Mpira wa Kikapu kawaida, Mpira wa Kikapu kwa Watu wenye Ulemavu, Mpira wa Wavu, Netiboli, Ngumi za Ridhaa, Ngumi za Kulipwa, Michezo ya Jadi, Riadha, Karate, Kabaddi, Mpira wa Mikono na Power Arts kutoka nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Zambia walishiriki. Aidha, wananchi na wadau mbalimbali wa michezo wapatao 3,000 walihudhuria Tamasha hilo.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Shirikisho la Riadha Tanzania waliandaa mashindano ya mchezo wa riadha kwa wanawake (*ladies First*) kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la mashindano hayo ni kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo. Kutokana na matamasha na mashindano hayo kumeshuhudiwa kuhamasika kwa hali ya juu kwa wanawake kushiriki katika michezo mbalimbali.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuendelea kutambua vipaji vya wanamichezo na vilabu mahiri na wanaofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, BMT liliandaa tukio la utoaji Tuzo kwa wanamichezo na vilabu ambapo tuzo hizo zilitolewa tarehe 17, Machi, 2023 ambapo wanamichezo na vilabu mbalimbali vilipewa tuzo mbalimbali kulingana na sifa ya mhusika.




*Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb.) akikabidhi Tuzo ya Wimbo Bora wa Mwaka 2022 kwa mwakilishi wa mwanamuziki Jay Melod kwenye Usiku wa Tuzo za Muziki Tanzania zilizofanyika tarehe 29 Aprili, 2023 Jijini Dar es Salaam.*

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Serikali wamejiunga na programu maalumu ya Mpira wa Miguu kwa Shule "Football for Schools(F4S)" inayodhaminiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu la Dunia (FIFA) ambapo Tanzania itapokea mipira takriban elfu sitini na nne (64,000) kwa ajili ya programu hiyo. Mipira hiyo itapelekwa katika shule za Msingi zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar ambapo kila Mkoa utapokea mipira takriban elfu mbili (2,000). Aidha, programu hiyo itahusisha pia utoaji wa mafunzo kwa walimu na makocha wa ngazi za chini "grassroot level" kutoka kwa wataalamu wa FIFA, hii ikiwa ni pamoja na kupata mbinu za kufundishia kupitia mfumo maalumu wa kidigitali ambao utatumiwa na walimu hao mara baada ya kupata mafunzo hayo. Programu hii itasaidia sana katika kuibua na kuendeleza vipaji kwa kuwa inahusisha upatikanaji wa mipira, mbinu za kufundishia na wataalamu wa kutosha.

### 3.2.3.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni chuo pekee kinachotoa mafunzo ya michezo kwa wataalamu wa michezo nchini. Chuo hiki kipo mkoani Mwanza katika Wilaya ya Kwimba. Jukumu kuu la chuo hiki ni kufundisha taaluma ya michezo, kutafiti na kutoa ushauri kuhusu masuala ya maendeleo ya michezo.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya imeendelea kudahili wanachuo katika masomo ya Michezo. Katika juhudi hizo, Chuo kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanachuo ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 kilifanya usajili wa wanachuo 154 kwa mwaka wa kwanza ambapo Wanaume ni 108 na Wanawake ni 46 ukilinganisha na usajili wa wanachuo 130 katika mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 18. Kwa upande wa mwaka wa pili Chuo kina wanachuo 107, Wanaume 83 na Wanawake 24. Hivyo jumla ya wanachuo waliosajiliwa katika Chuo kwa mwaka 2022/23 ni 261 ikilinganishwa na jumla ya wanachuo 221 waliosajiliwa mwaka 2021/22.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23 Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimetoa mafunzo ya muda mfupi katika vituo viwili vya Dar es Salaam na Chuoni Malya ambapo aina ya mafunzo yaliyotolewa ni kuhusu Mpira wa Mikono, Lishe, Tiba na Kinga, uandaaji na uratibu wa matukio mbalimbali ya michezo *(sports event management)*, utafutaji wa masoko katika michezo *(sports marketing)*, Mpira wa Miguu, Mpira wa wavu, Netiboli na Mpira wa Kikapu kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo/Mashirikisho nchini, jumla ya washiriki 538 wameshiriki na kuhitimu mafunzo hayo, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 79.3 ya lengo la washiriki 300 lililowekwa.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimehuisha mitaala ya ufundishaji wa kozi ndefu na kuboresha mbinu za ufundishaji *(teaching pedagogy)* ili kukidhi haja ya ualimu wa michezo kwa lengo la kuongeza weledi wa ufundishaji michezo katika shule za msingi na sekondari nchini. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Idara ya Michezo ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam kinaendelea na utafiti kuhusu kutofanya vizuri

kwa Timu za Taifa katika mashindano ya kimataifa *(An Assessment of "Critical Success Factors Influencing Performance of the Tanzanian National Teams in the International Sporting Competitions")*. Kufanyika kwa utafiti huo kutasaidia kupata suluhu ya kufanya vizuri kwa Timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wanachuo, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kuendelea na ujenzi wa hosteli za wanachuo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, shughuli mbalimbali zimefanyika kwa upande wa ujenzi wa hosteli za wanafunzi, shughuli hizo ni pamoja na ujenzi wa msingi katika hatua ya sakafu; ujenzi wa nguzo na ngazi kuelekea ghorofa ya kwanza; ujenzi wa sakafu ya ghorofa ya kwanza; ujenzi wa nguzo kuelekea ghorofa ya pili; ujenzi wa sakafu ya ghorofa ya pili na ujenzi wa nguzo kuelekea ghorofa ya tatu.



*Muonekano wa Ujenzi wa Hosteli za Wanafunzi unaoendelea katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Hosteli hiyo itakuwa na jumla ya ghorofa nne (4) itakapokamilika.*

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ujenzi wa Akademia ya Michezo (National Sports Academy) katika Chuo cha Maendeleo

ya Michezo (Mshauri Elekezi *(*Consultant*)* amelipwa kwa mujibu wa Mkataba. Mradi huu unatarajiwa kuwa Kituo pekee katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa na viwanja vya michezo, hosteli, bwawa la kuogelea, madarasa, jengo la utawala, multipurpose *hall,* gymnasia na uwanja wa riadha, ambapo viwanja vyote hivi vinajengwa kukidhi viwango vya Olimpiki. Hadi kufikia Aprili, 2023 kazi zilizokamilika ni pamoja na maandalizi ya eneo la ujenzi wa kituo; kuhuisha mipaka ya eneo kwa ajili ya kulitambua; kuchora michoro ya mradi; na kutangazwa kwa zabuni ya ujenzi. Mradi huu utakapokamilika unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 33 za Kitanzania.

### 3.2.4 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Wizara iliratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za ofisi ikiwepo matengenezo ya magari; ununuzi wa mafuta ya magari kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uendeshaji wa ofisi; kuwezesha utoaji wa huduma za usafi na ulinzi wa ofisi, Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru na kwenye makazi ya viongozi; kulipa pango la Ofisi katika jengo la PSSSF Jijini Dodoma; kulipa umeme katika Ofisi za Mtumba, PSSSF, Ofisi za Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru. Aidha, imewezesha upatikanaji wa shajala na vitendea kazi vingine vya ofisi ikiwemo samani, magari na kompyuta.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilisimamia upatikanaji wa stahili mbalimbali za viongozi na watumishi ikiwemo malipo ya nauli za likizo, posho za kujikimu, na vibali vya likizo. Pia, imeendelea kuratibu safari za viongozi na watumishi za ndani na nje ya nchi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipokea kibali cha ajira cha watumishi 17 wa kada mbalimbali wakiwemo Maafisa Utamaduni, Michezo, Ugavi, Wachumi na Watakwimu. Mchakato wa kuwapata maafisa hao unaendelea ambapo Wizara imewasilisha kibali hicho katika Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira kwa ajili ya kukamilisha suala hilo.

## 4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2022/23, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:

(i) Mtiririko wa mahitaji ya fedha kutoendana na mahitaji ya Wizara hususan kwa miradi ya maendeleo. Aidha, ukomo mdogo wa bajeti ya Wizara ikilinganishwa na maelekezo makubwa ya kutekeleza shughuli za kutangaza Taifa, Kikanda na Kimataifa.

Wizara iliendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa kwa Wizara ambayo awali hayakupangiwa bajeti. Aidha, Wizara imeendelea kufanya mazungumzo na Balozi mbalimbali nchini zikiwemo za Saudi Arabia, China, Qatar, Uswizi, Ujerumani, Ufaransa, Uhispania, Falme za Kiarabu (UAE) na Uturuki ili kushirikiana katika maeneo mahsusi.

(ii) Kukosekana kwa mifumo thabiti ya kiteknolojia ya kufuatilia matumizi na mapato ya watumiaji wa kazi za sanaa na ubunifu zinazosimamiwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya mwaka 1999.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufanyika kwa marekebisho ya sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura 218 na kutokana na maandalizi ya Kanuni za uanzishwaji wa kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha (CMOs) zitakazoanzisha mifumo ya upatikanaji wa taarifa za mapato na matumizi ya kazi za muziki zitakazotumika katika kukusanya na kugawa mirabaha. Aidha, COSOTA ipo katika hatua ya kuwa na mfumo unaojitegemea utakaosaidia katika kuhakiki taarifa za kampuni wakati wa kugawa mirabaha;

(iii) Upungufu wa vitendea kazi vikiwemo magari kwa upande wa Wizara pamoja na Taasisi zake.

Wizara imeendelea kuandaa maandiko ya miradi kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Wadau na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi;

(iv) Uelewa mdogo wa jamii hususan vijana kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kuenzi urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika na nafasi ya Tanzania kama kitovu cha harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika.

Wizara kupitia Kituo cha Programu ya Urithi wa Ukombozi imeendelea kutoa elimu kupitia makongamano, mitandao ya kijamii na kufanya maonesho mbalimbali ya kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulinda urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

(v) Upungufu wa watumishi katika kada mbalimbali za michezo na utamaduni hususan katika Halmashauri nchini. Pamoja na kufanikiwa kuanzishwa kwa Vitengo vya utamaduni na Michezo katika Halmashauri, kumekuwa na changamoto ya Vitengo hivyo kukosa wataalamu wanaostahili. Pia Vitengo kutokupewa kipaumbele katika Halmashauri na kutokupangiwa bajeti ya kutekeleza majukumu yao ya kibajeti.

Katika kutatua changamoto hizo, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeongeza mtaala wa elimu ya cheti na vituo vya mafunzo ili kuongeza idadi ya wataalamu mbalimbali wa michezo, na Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo pia kimeongeza kiwango cha udahili ili kuongeza idadi ya Maafisa Utamaduni nchini. Aidha, Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kujaza nafasi ambazo hazina wataalamu sahihi na pia Wizara inaendelea kuwasiliana na OR – TAMISEMI kuzielekeza Halmashauri kuviwezesha Vitengo kwa kuvitengea bajeti.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nilifahamishe Bunge lako tukufu kuwa Vitengo hivi ni muhimu sana katika jamii yetu kwa sababu vina kazi kubwa ya kuihimiza na kuielimisha jamii yetu kuzingatia na kufuata maadili ya Kitanzania. Kwa sasa kumekuwa na kasi

kubwa sana ya jamii yetu kuvamiwa na utamaduni wa kimagharibi ambayo ni hatari sana kwa jamii yetu kupoteza utamaduni na maadili yetu. Niwaombe Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuvitengea Vitengo hivi bajeti na majukumu yanayostahili.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Utamaduni ni utambulisho, kielelezo cha uhai na utashi wa watu katika Taifa. naomba niwakumbushe kauli ya Baba wa Taifa hili Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere aliyoitoa wakati alipokuwa aKifungu a kwa mara ya kwanza Wizara ya Utamaduni mwaka 1962 alisema, nanukuu "***Nchi inayokosa utamaduni wake ni sawa na mkusanyiko wa watu usiokuwa na roho na hivyo kukosa sifa ya kuitwa Taifa kamili***". Mwisho wa kunukuu. Kwa nukuu hiyo ni dhahiri kuwa Sekta ya Utamaduni ni muhimu sana kuliko kitu chochote tunachokifanya na ndiyo maana kwa kutambua hilo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizipa umuhimu wa kipekee Sekta hizi ikiwa ni pamoja na kuzitenga na Idara ya Habari-MAELEZO ili ziweze kutambulika kwa wananchi na kujipambanua katika majukumu yanayotekelezwa na Sekta hizi. Hivyo, Watanzania kwa pamoja tuungane kulinda maadili na utamaduni wetu.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2023/24 Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) (2020-2025); Ahadi na Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/22 - 2025/26. Aidha, utekelezaji wa majukumu utazingatia pia malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 katika maeneo yanayohitaji kuchukuliwa hatua na Wizara, pia utazingatia Mwongozo wa Bajeti wa mwaka 2023/24. Majukumu yatakayotekelezwa yanaainishwa kama ifuatavyo kwa kila Sekta.

## 5.1 SEKTA YA UTAMADUNI

### 5.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni kuratibu na kuendesha vipindi vya Redio na Televisheni, makongamano na midahalo kuhusu namna ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini; kufanya Tamasha la Kitaifa la Utamaduni pamoja na kuratibu Matamasha ya Kiutamaduni katika Kanda saba (7) za Utamaduni ili kusherehekea Uanuai wa Urithi wa Utamaduni; kuratibu vikao vitatu (3) vya wadau wa Sekta ya Utamaduni vya kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Utamaduni ya mwaka 1997 pamoja na kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wake; na kukamilisha zoezi la upatikanaji wa Vazi la Taifa. Majukumu mengine ni pamoja na kutafiti, kukusanya na kuhifadhi elementi za Urithi wa Utamaduni Usioshikika na kuandaa ripoti ya miaka minne ya utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 2003 unaohusu Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika; kuratibu na kushiriki katika mikutano, makongamano, maadhimisho na matamasha ya kiutamaduni ya kitaifa, kikanda, na kimataifa; kuandaa mkutano wa wadau kuhusu kuanzisha mchakato wa Sheria ya Taifa ya Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika; kufanya Vikao Kazi viwili (2) vya Maafisa Utamaduni nchini; kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Baraza la Kiswahili la Taifa; Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; na kuratibu shughuli za Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

### 5.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuratibu maadhimisho ya pili ya Siku ya Kiswahili Duniani; kutekeleza *Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili* wa mwaka 2022 – 2032 kwa kutoa mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa diaspora 150, kuchapisha vitabu 2 vya kufundishia na kujifunzia Kiswahili; kuimarisha Kiswahili nchini na kukitangaza kimataifa; kutoa elimu ya matumizi sanifu na fasaha ya lugha ya Kiswahili kwa kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 700 kupitia redio na televisheni. Pia, makala 30 zitachapishwa katika magazeti na maudhui mbalimbali kuhusu Kiswahili yatatolewa kupitia mitandao ya kijamii ambayo ni YouTube, Facebook na Twitter; kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili

kwa wageni kwa wataalamu 250 kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania; na kutoa semina kuhusu matumizi bora ya Kiswahili kwa waandishi na watangazaji kutoka vyombo vya habari duniani. Majukumu mengine ni kutoa ithibati kwa miswada 85 ya vitabu vya kiada na ziada; kuendesha mafunzo kwa wakalimani 30 wa lugha mbalimbali; kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka 700 na kuthibitisha tafsiri 3,000 zinazofanywa na wakala wake; kutambua na kusajili jumla ya wataalamu 400 katika kanzidata ya wataalamu wa Kiswahili; na kutambua na kutoa ithibati ya vituo 3 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni.

### 5.1.3 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umepanga kutoa huduma zake kwa kuzingatia makundi maalum, mgawanyiko kisekta na mikoa ya Tanzania Bara. Aidha, Mfuko utawezesha miradi ya Utamaduni na Sanaa 650 kiasi cha Shilingi bilioni 9.5 kwa wastani wa miradi 25 kwa kila Mkoa. Kipaumbele kitawekwa kwa miradi inayomilikiwa na makundi maalumu yaani wanawake, vijana na wenye ulemavu ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuchangia katika Pato la Taifa. Mfuko umepanga kutoa mafunzo kwa wadau 6,000 nchini. Aidha, mkazo utawekwa katika eneo la usimamizi wa miradi, utunzaji wa kumbukumbu, utamaduni wa kujiwekea akiba, uwekezaji, urasimishaji na maadili. Aidha, Mfuko umekwisha andaa mpango wa kuzishirikisha taasisi za fedha katika utoaji wa huduma ambapo mpango huu utasaidia kusogeza huduma katika maeneo ambapo wananchi wanaishi. Jumla ya Ajira 59,150 zinatarajiwa kuzalishwa kupitia miradi 650 itakayowezeshwa ambapo ajira za kudumu zinatarajiwa kuwa 19,700 na ajira za muda 39,450.

## 5.2 SEKTA YA SANAA

### 5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali kupitia Wizara itaendelea na Maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Sanaa; kusimamia maboresho ya Sheria na Kanuni za sekta; kusimamia Ujenzi wa Sanamu ya Mwalimu Nyerere katika Jiji la Addis Ababa nchini Ethiopia; kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wadau wa Muziki wa Afrika (Music in Africa Conference (ACCES);

kuratibu Mashindano ya Kimataifa ya Urembo na Utanashati kwa Viziwi na Tamasha la Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Duniani; na kuratibu matumizi ya Sanaa kutangaza utekelezaji wa Serikali wa shughuli za maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kuratibu kutangaza vipaji vya Wasanii wa Tanzania kitaifa na kimataifa kupitia Tamasha la Serengeti Music Festival; kuratibu shughuli za Burudani katika Maadhimisho ya Siku za Uhuru na Muungano; kuratibu mashindano ya Sanaa kwa vijana kupitia UMMISETA, UMITASHUMTA, Taifa Cup na mashindano mengine; na kuratibu Tamasha la Sauti za Busara, Masai Festival, Usiku wa Taarabu, kuratibu kutumia sanaa kuhamasisha vijana kushiriki kilimo, na shughuli nyingine za Kitaifa na Kimataifa kwa kushirikiana na wadau.

### 5.2.2 BODI YA FILAMU TANZANIA

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kusimamia maudhui ya filamu nchini kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja filamu 1,500; kurasimisha shughuli/biashara za filamu na kutoa leseni 200 za uendeshaji wa shughuli/biashara hizo; kushughulikia maombi na kutoa vibali 1,300 vya uandaaji wa filamu nchini; kuwatambua wadau wa filamu na Michezo ya Kuigiza kwa kutoa vitambulisho 1,200 kwa wadau hao; kuendesha Tamasha la Kitaifa la utoaji wa Tuzo za Filamu; kuendesha programu/mafunzo kwa lengo la kuwajengea uwezo wadau wa filamu; kuendelea na mkakati wa kuyabaini na kuyatangaza maeneo ya upigaji picha za filamu nchini; na kuendelea kuwawezesha wadau kutumia huduma za Bodi kupitia mfumo wa Utambuzi wa wadau (Arts Management Information System-AMIS) pamoja na kuwasajili.

### 5.2.3 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kuimarisha ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora; kuimarisha mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI; kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa mahala pa kazi; kuimarisha Utawala bora katika kutekeleza shughuli za Baraza na uendeshaji wa Sekta ya Sanaa; kuimarisha na kuongeza mapato ya Baraza; kukarabati na kujenga vituo vya sanaa na Ofisi za Baraza; kuimarisha utoaji habari, mawasiliano ya Umma na ushawishi; kusimamia maslahi ya wasanii yasiyo ya hakimiliki au hakishiriki;

kuendesha elimu na shughuli za sanaa katika shule za Msingi na Sekondari; kusimamia matumizi ya sanaa za jadi; na kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za Sanaa.

### 5.2.4 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kusimamia Makampuni ya Wasanii wenyewe yaliyoidhinishwa kukusanya na kugawa miraba; kutoa leseni/kukusanya mirabaha kwa watumiaji wa kazi za ubunifu katika maeneo ambayo hayatakuwa chini ya CMOs; kukusanya mapato kutoka katika vibebeo tupu (blanktape devices); kusajili kazi za ubunifu na wasanii, waandishi na wabunifu; kukagua uharamia wa kazi za wabunifu; kutatua migogoro na utaoji msaada wa kisheria; na kufanya kampeni kubwa kwa kutoa Elimu kwa Umma kuhusu hakimiliki na hakishirikishi.

### 5.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Juni, 2024 imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo; Kudahili wanachuo wapatao 750 kwa kozi ndefu na 250 kwa kozi fupi; kuendesha semina 4, warsha 4 na kongamano 1; kuendelea na ukarabati wa ukumbi mkuu wa maonesho, ukumbi wa “flexible”, Jukwaa la Mwembeni, nyumba ya Mkuu wa Chuo, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kununua vifaa vya jukwaa la kuendeshea Tamasha, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na Kununua Samani za Ofisi; kupata ithibati kwa mitaala mipya mitatu (3); kununua na kusimika mitambo ili kuanza kurusha matangazo katika Kituo cha Redio na TV; kuanza mchakato wa kupata eneo la kuanzisha kampasi ya mafunzo Dodoma; kuendesha Tamasha la 42 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo; kuimarisha mtandao (Networks) kati ya Taasisi na wadau wa sanaa nje na ndani ya nchi; na kuandaa Mpango Mkakati wa Kutangaza Taasisi (Communication Strategy).

## 5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

### 5.3.1 IDARA YA MICHEZO

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Juni, 2024, Serikali kupitia Wizara itatekeleza majukumu mbalimbali, miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na kujenga na

kukarabati miundombinu ya michezo; kuandaa kongamano la wadau wa Sekta ya michezo; kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na Mashindano ya Afrika (AAG) na michezo ya Afrika Mashariki; kusambaza na kutoa elimu kuhusu Mkakati wa Maendeleo ya Michezo kwa wadau wa Sekta; kupambana na dawa na mbinu haramu katika michezo; na kuratibu kikao kazi cha mwaka cha maafisa michezo. Majukumu mengine ni pamoja na kuratibu mashindano ya Kitaifa ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; kuratibu mashindano ya *Tanzanite International Women Sports Festival* na Taifa Cup mtaa kwa mtaa kwa kushirikiana na BMT; kuratibu matunzo na matumizi ya eneo changamani la michezo la Taifa (viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru); kutoa huduma ya kinga na tiba kwa wanamichezo; kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa inayohusu sekta ya michezo; na kuratibu mashindano ya Fainali ya Mpira wa Miguu Bara la Afrika (AFCON 2027) kwa kushirikiana na nchi ya Kenya na Uganda.

### 5.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 majukumu yaliyotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuwezesha na kuzigharamia Timu za Taifa 15 kushiriki mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo na usimamizi kwa wataalamu 150 ili kupata wataalamu wa michezo nchini; kuendelea kusajili Vyama/Mashirikisho na vilabu vya michezo vipatavyo 200; kuratibu matamasha mawili ya Michezo ya Wanawake (Tanzanite); kuendelea kuhamasisha Utawala Bora katika vyama na mashirikisho ya michezo 48; kuratibu na Kusimamia Mfumo wa Usajili wa kidijitali (Online Registration); kuidhinisha vibali 180 vya matukio mbalimbali ya michezo; na kuendelea kutoa tuzo kwa wanamichezo bora kwa michezo yote inayochezwa Tanzania, kuendelea kufanya ufuatiliaji wa Kamati za Michezo ngazi za mikoa na Wilaya ili kusimamia kikamilifu programu za kuinua na kuendeleza vipaji katika ngazi za chini.

### 5.4 MIRADI YA MAENDELEO

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara

la Afrika, katika mwaka wa fedha 2023/24 umetengewa jumla ya shilingi 450,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya O.A.U pamoja na kufanya ukarabati wa makaburi na mahandaki yenye urithi wa ukombozi wa Afrika; kutambua na kukusanya kumbukumbu na taarifa za Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika unaoshikika na usioshikika ndani na nje ya Nchi; kutayarisha na kuchapisha vitabu vya mashujaa wa ukombozi wa Afrika; R.M. Kawawa, S.A. Salim, J.S. Warioba, na Br. Gen. H. Mbita; kuratibu maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika (Machi 23) na Siku ya Afrika (Mei 25), kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika; na kufanya ziara kwenye Matawi ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika katika Nchi za Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kutoa mwongozo wa uendeshaji wake.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, katika mwaka wa fedha 2023/24 umepangiwa jumla ya shilingi 1,600,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na utoaji wa mikopo, ruzuku na mafunzo kwa wadau wa sekta ya utamaduni na Sanaa; kuunda Mfumo wa Kielektroniki wa kanda ili kuweza kutoa huduma kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kazi na kuwafikia walengwa wengi kwa urahisi.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kupitia Mradi wa Kuimarisha BAKITA na Kukibidhaisha Kiswahili umetengewa jumla ya shilingi 300,000,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kuanzisha vituo 8 vya kufundisha Kiswahili kupitia balozi za Tanzania nje ya nchi na kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa diaspora na wenyeji katika nchi husika na kuandaa Kongamano la Kiswahili nje ya nchi.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na mradi wa ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, katika mwaka 2023/24 umetengewa jumla ya Shilingi 610,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Hosteli za wanafunzi; na kukarabati madarasa matatu (3).

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya kwa mwaka 2023/24 umetengewa jumla ya Shilingi 470,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Akademia utakaohusisha miundombinu ya msingi ya viwanja vya michezo, vyumba vya kubadilishia nguo na hosteli.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma, katika mwaka wa fedha 2023/24 umetengewa Shilingi 60,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kupata Mshauri Elekezi na kuhuisha upembuzi yakinifu wa mradi utakaohusisha uhuishaji wa michoro, gharama za ujenzi, utafiti wa athari za mazingira na andiko la biashara (business plan). Aidha, pamoja na kujenga uwanja mpya jijini Dodoma, Serikali itajenga uwanja mwingine wa kisasa jijini Arusha, ambao unatarajiwa kutumika katika mashindano ya AFCON 2027 endapo nchi za Afrika Mashiriki zitashinda zabuni ya kuandaa mashindano hayo.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi (Recreational Centre) katika mwaka 2023/24 umetengewa Shilingi 4,760,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha awamu ya kwanza ya vituo vya mazoezi na kupumzika wananchi katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma. Awamu hiyo itahusisha ujenzi wa hosteli zenye uwezo wa kuchukua watu 50; viwanja vya michezo ikiwemo uwanja wa mpira wa miguu wa nyasi halisi na nyasi bandia; ujenzi wa viwanja vya mpira wa kikapu, pete, na wavu.

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa Ujenzi wa *Sports and Arts Arena* katika mwaka 2023/24 umetengewa jumla Shilingi 130,000,000 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kupata Mshauri Elekezi na kufanya upembuzi yakinifu wa mradi utakaohusisha michoro, gharama za ujenzi, utafiti wa athari za mazingira na andiko la biashara (*business plan*).

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ni mradi ambao utatekelezwa katika mwaka 2023/24 na umetengewa jumla ya Shilingi 101,160,000 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni kuendelea kugharamia timu za

Taifa ikijumuisha makocha; kutoa mafunzo kwa wataalamu wa michezo nchini; kuratibu mashindano ya Kitaifa na kimataifa; kutekeleza programu za kuendeleza michezo kwa wanawake; na kuendelea kuboresha na kukarabati miundombinu ya michezo.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam katika mwaka 2023/24 umepangiwa jumla ya Shilingi 1,120,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kufanya ukarabati mkubwa wa uwanja wa Benjamin Mkapa katika eneo la kuchezea (pitch), mfumo wa umeme, mfumo wa zimamoto, mfumo wa maji, kubadilisha maeneo ya mashabiki, na majukwaa ya watu mashuhuri; kuendelea kufanya ukarabati mkubwa wa uwanja wa Uhuru katika maeneo ya kuweka viti vya watazamaji, kuweka *Score Board (Big Screen)*, kuweka mfumo wa sauti (*Sound system*) katika uwanja, kuboresha na kujenga vyumba vya kubadilishia nguo, kubadilisha paa la Uwanja kwa kuweka mabati mapya katika mzunguko, kuboresha Mfumo wa Maji Taka, na kuweka mfumo wa Ulinzi wa CCTV na kukarabati viwanja vitano (5) vya majiji ya Mwanza, Arusha, Dodoma, Tanga na Mbeya.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo kwa mwaka 2023/24 umepangiwa Shilingi 1,360,000,000 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo katika shule teule 56 za michezo.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), katika mwaka 2023/24 umetengewa Shilingi 570,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ukarabati wa ukumbi mkuu wa maonesho, ukumbi wa "flexible", Jukwaa la Mwembeni, nyumba ya Mkuu wa Chuo, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na Kununua Samani za Ofisi; kununua na kusimika mitambo ili kuanza kurusha matangazo katika Kituo cha Redio na TV; na kuendesha na kuimarisha miundombinu ya Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu ni mradi utakaotekelezwa katika mwaka 2023/24 ambapo umetengewa Shilingi 100,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanza maandalizi ya mradi kwa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina wa mradi na kuandaa andiko la kibiashara (*business plan*); na kuanza hatua za maandalizi ya ujenzi.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa katika mwaka 2023/24 umepangiwa Shilingi 200,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa wazi wa Sanaa katika eneo la Ilala Shariff Shamba Jijini Dar es Salaam; na kununua vifaa vya sauti na taa kwa ajili ya ukumbi.

### 5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi. Kwa mwaka 2023/24 shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi ikiwemo matengenezo na mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, kulipa pango la ofisi, umeme na simu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali na samani za ofisi. Aidha, Wizara itaendelea na uratibu na kuwezesha mazoezi ya wafanyakazi wote wa Wizara kila wiki mara moja; kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za wafanyakazi ikiwemo uhamisho, likizo, safari za kikazi n.k. na kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi. Pia Wizara itaendelea na kuratibu ushiriki wa Wizara katika sherehe za Mei Mosi, Siku ya Wanawake Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na Michezo ya SHIMIWI; na kuratibu mafunzo, ajira na upandishwaji vyeo kwa watumishi.

## 6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

### 6.1 MAPATO

**184.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2023/24 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi Bilioni Moja (Shilingi 1,000,000,000) kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na viingilio katika matukio ya michezo yanayofanyika katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, kukodisha kumbi na *gym* zilizopo katika Uwanja wa Benjamin

Mkapa na ada za mafunzo na mitihani ya Kitaifa kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, kwa upande wa Taasisi sita (6) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tisa Sabini, Mia Nne Ishirini na Nane Elfu (Shilingi 5,970,428,000). ***Kiambatisho Na. 2*** ni mchanganuo wa mapato yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2023/24.

## 6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2023/24 Wizara imetengewa bajeti ya **shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Arobaini na Tano, na Arobaini na Moja Elfu** (Shilingi 35,445,041,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita Hamsini na Moja, Mia Mbili Themanini na Tano Elfu** (Shilingi 9,651,285,000), Matumizi Mengineyo ni **shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Tisa Sitini na Mbili, Mia Tano Tisini na Sita Elfu** (Shilingi 13,962,596,000) na Miradi ya Maendeleo ni **shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu** (Shilingi 11,831,160,000). ***Kiambatisho Na. 3*** kinaonesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2022/23

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2023/24 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2023/24 yenye jumla ya **shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Arobaini na Tano, na Arobaini na Moja Elfu** (Shilingi 35,445,041,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita Hamsini na Moja, Mia Mbili Themanini na Tano Elfu** (Shilingi 9,651,285,000), Matumizi Mengineyo ni **shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja na Sitini Elfu** (Shilingi 13,831,160,000) na Miradi ya Maendeleo **ni shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu** (Shilingi 11,831,160,000).

## 8.0 MWISHO NA SHUKURANI

**187.** ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia

kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2022/23 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali, taasisi za fedha, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa wadau siyo rahisi kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache nikianza na wadau wa ndani, ambao ni Kampuni za Azam Media; Multichoice Tanzania; Airtel Tanzania; Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF); Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Benki ya NMB. Wengine ni Tanzania National Park (TANAPA); Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCA); Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); Benki ya CRDB; Tanzania House of Talent (THT); Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC); na Makumbusho ya Taifa. Aidha, wadau wengine ni pamoja na Shirika la Bima la Taifa (NIC); Programu ya kudhibiti UKIMWI (NACP); Wakala wa Serikali Mtandao (eGA); Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC); Shirika la Culture and Development East Africa (CDEA); Wakala wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Kampuni ya Startimes; Hotel ya Onomo Dar es Salaam; Kampuni ya Wanene Entertaiment; Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Kituo cha Televisheni cha DSTV; na Vituo vya Redio vya CLOUDS Media group, EFM na Wasafi.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa wadau wa nje, naomba nianze na Balozi zote za Tanzania katika mataifa mbalimbali, Serikali ya Mji wa Busan nchini Korea ya Kusini; Bagamoyo Friendship Society (Ujerumani); Musicians for a Better Life (Ujerumani); Alwaleed Philanthropies kutoka Saudi Arabia; Jamhuri ya Watu wa China; na Umoja wa Ulaya.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo mahsusi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa maelekezo na ushauri katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Utamadui, Sanaa na Michezo. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo ya mara kwa mara yaliyowezesha kuboresha utendaji wa Wizara.

**191.** ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushuru sana. *(Makofi)*

Ahsante sana sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu na Michezo kwa niaba yake Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Sekiboko karibu.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa hii ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu Utamaduni na Michezo, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza hotuba yangu nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati, Kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi na kazi kubwa kwa uwekezaji mkubwa anaoufanya katika sekta ya michezo

nchini, hali ambayo tumeiona dhahiri inakwenda kupunguza na kutatua kero nyingi zilizoko kwenye sekta ya michezo na mwisho wa siku kufuta kabisaa ile kauli ya kwamba Tanzania ni 'Kichwa cha Mwendawazimu'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukutaarifu kuwa, kwa kuzingatia Kanuni ya 6(7)(b) na ya 7(1)(a), pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilishughulikia Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na taasisi zilicho chini ya Wizara hiyo. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tarehe 23 na 24 Februari, 2023, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 96 – Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa yetu yote iingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard) kama ilivyowekwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii inazingatia maeneo matatu yafuatayo yaliyofanyiwa kazi na Kamati:

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

(b) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024; na

(c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika eneo hili kamati ilishughulikia mambo mawili makubwa. Mambo haya ni Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2022/2023. Taarifa fupi ya maeneo haya ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; Kamati ilikagua miradi miwili ya maendeleo, iliyoidhinishiwa fedha

na Bunge lako tukufu katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa ujumla wake Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi hii. Hata hivyo, Kamati ilisisitiza Serikali kupeleka fedha katika mradi namba 4353, unaohusu ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa). Utekelezaji wa mradi huu umekuwa ukisuasua kwa kuwa serikali imekuwa haipeleki fedha zinazoidhinishwa katika bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023; Kamati ilichambua utekelezaji wa bajeti ya wizara hii kwa kuzingatia uzingatiwaji wa maoni na ushauri wa kamati, ukusanyaji wa maduhuri na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kutoka Hazina na kubaini yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa yake kuhusu Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo 14 kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji iliyowasilishwa na Wizara na kubaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Wizara imetekeleza sehemu kubwa ya ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikadiria kukusanya Maduhuli ya shilingi 6,296,445,000.00, ambapo Wizara yenyewe ilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 900, sawa na asilimia 14.29 na Idara na Taasisi zilizo chini yake zilikadiriwa kukusanya shilingi 5,396,445,000, sawa na asilimia 85.71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari 2023, Wizara, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya shilingi 3,119,647,946, sawa na asilimia 49.55 ya lengo la makusanyo. Kamati ilihimiza Wizara kusimamia Idara na Taasisi zake katika kuhakikisha kuwa, lengo la ukusanyaji wa Maduhuli linafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara kupitia Fungu 96 pamoja na Taasisi zake, iliidhinishiwa shilingi 35,425,991,000. Kati ya fedha hizo Mishahara ni shilingi 8,201,882,000, sawa na asilimia 21.15. Matumizi Mengine ni

shilingi 11,391,949,000 sawa na asilimia 32.15 na shilingi 15,831,160,000, sawa na asilimia 44. 68 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mwezi Februari, 2023, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, jumla ya shilingi 16,036,220,372.00, sawa na asilimia 45.3 ya bajeti yote, kwa mchanganuo ufuatao:

i. Shilingi 5,383,725,304 kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 33.6 ya fedha zote zilizopokelewa.

ii. Shilingi 5,627,327,687 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*OC),* sawa na asilimia 35.1 ya fedha zilipokelewa; na

iii. Shilingi 5,025,167,381 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 32 ya fedha zilipokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilitengewa kiasi cha jumla ya shilingi 15,831,160,000 tu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kiasi hiki ni kidogo sana kulinganisha na majukumu na umuhimu wa Wizara yenyewe katika kukuza, kulinda na kuendeleza utambulisho wa Mtanzania kwenye nyanja za ubunifu, utamaduni, sanaa na michezo. Hata hivyo, bado fedha hizo kidogo zimekuwa hazitolewi kwa wakati, hali inayokwamisha utekelezaji wa majukumu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, Wizara imepanga kutekleleza vipaumbele nane kwa bajeti ya shilingi bilioni 35.455. Kati ya fedha hizo, misharaha (*PE*) ni shilingi 9,651,285,000 sawa na asilimia 27.2. Matumizi mengineyo (*OC*) yanaombewa shilingi 13,962,596,000 sawa na asilimia 39.4 na miradi ya maendeleo inaombewa shilingi 11,831,160,000 sawa na asilimia 33.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa, pamoja na mambo mengine, bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii imepungua ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaoshia Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haijaridhishwa na Wizara kupunguziwa bajeti ya miradi maendeleo. Hatua hii haiendani kabisa na nia ya Serikali na hususani maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kukuza na kuimarisha sekta ya utamaduni, sanaa na michezo nchini. Aidha, hatua hii haiakisi hamasa kubwa iliyopo hasa ya Watanzania ya kupenda na kukumbatia sekta hizi muhumu. Kwa hivyo basi, Kamati inashauri Bunge lako Tukufu, kuitaka Serikali iongeze bajeti ya miradi ya maendeleo ya Wizara angalau ifike ile ya mwaka 2022/2023 au zaidi ili kuingozea Wizara hii nguvu ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kuinua sekta nzima ya utamaduni, sanaa na michezo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, makadirio ya matumizi ya maendeleo yameshuka kwa shilingi bilioni nne, sawa na asilimia 25.3, kutoka shilingi 15,831,160,000 mwaka 2022/2023 hadi shilingi 11,831,160,000 mwaka 2023/2024, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; Kamati inatoa ushauri, maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (*TaSUBa*). Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ina nafasi kubwa ya kuchangia katika maendeleo ya sanaa na utamaduni nchini kwa kunoa vipaji vya vijana wetu waliopo katika tasnia ya sanaa. Aidha, chuo hiki kingeweza kuwa tanuru la kutafiti, kuchakata na kuwa makavazi *(achieve)* ya utamaduni wa Taifa letu. Hata hivyo, chuo kimeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa sababu fedha ambazo zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimekuwa hazipelekwi kwa wakati kwa zaidi ya miaka kumi mfulululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

i) Serikali kuiwezesha taasisi kutekeleza majukumu kwa kuipatia fedha zote zinapangwa katika Bajeti.

ii) Wadau wa sanaa na utamaduni nchini kuungana na Serikali katika kukiendeleza, kuenzi na kuitumia taasisi katika kuendeleza tasnia za sanaa na utamaduni nchini.

iii) Taasisi ibuni na kuanzisha kozi mbalimbali zenye kuwasaidia wasanii kujiajiri mara baada ya kumaliza mafunzo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Maduhuli wa Taasisi zinazosimamiwa na Wizara. Ukiacha Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Wizara na Taasisi zake zimeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa maduhuli yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa mfano, hadi Kamati inachambua taarifa za Wizara mwezi Februari 2023, Ofisi ya Haki Miliki *(COSOTA*) ilikuwa imekusanya asilimia 14.9 tu ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1.35. Ni wazi kuwa kuna kulegalega katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia Wizara hii na Taasisi zake. Ni maoni ya Kamati kwamba Wizara na Taasisi zake ziongezeke juhudi katika kusimamia ukusanyaji wa Maduhuli, kwa kuwa inaaminika kwamba tasnia ya sanaa na utamaduni ni mgodi ulio juu ya ardhi ambao unaweza kutumika kuzalisha mapato na ajira nyingi kwa vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kushughulikia changamoto zilizojitokeza kwenye ukusanyaji wa maduhuli na kurasimisha tasnia ya sanaa na utamaduni kwa ujumla, Kamati inashauri hatua zifuatazo:-

i. Uongozi wa Wizara uimarishe usimamizi wa Taasisi zake katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli.

ii. Wizara ifanye tathmini maalum kwa *COSOTA* ili kujua sababu za taasisi hii kushindwa kukusanya maduhuli kama ilivyopangiwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, na kurekebisha kasoro zilizopo kimfumo, kisheria na kiutendaji.

iii. Serikali ifanye tafiti na kisha kuandaa mkakati maalumu juu ya kuimarisha na kusimamia sekta ya tasnia ya sanaa na utamaduni kama sekta muhimu ya uzalishaji mapato na kukuza ajira nchini

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Upatikaji wa Fedha za Maendeleo. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ndiyo ambayo inaitambulisha na kuitofautisha nchi yetu kimataifa, lakini kwa masikitiko makubwa Kamati inaona Wizara hii bado haijapewa kipaumbele hasa katika mgawanyo wa Bajeti. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kutumia shilingi trilioni 15.2 kama fedha za maendeleo ambapo Wizara hii imepangiwa shilingi bilioni 11.8 sawa na asilimia 0.08 ya Bajeti yote ya maendeleo kwa mwaka huo wa fedha. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, bajeti ya matuimizi ya maendeleo kwa Wizara hii imeshuka takribani asilimia 25 ikikadiriwa na ile ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya maendeleo kwa Wizara inashuka katika kipindi ambacho Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameipa msukumo mkubwa Tasnia ya Sanaa, utamaduni na michezo hadi kuunda Wizara maalumu kwa ajili ya Tasnia hizi. Aidha, bajeti hii inashuka katika kipindi ambacho Wizara imejielekeza kutekeleza vipaumbele vikubwa saba, ikiwa ni pamoja na kuwezeha ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano ya kimataifa na kukarabati Uwanja wa Benjamin Mkapa na viwanja vingine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika muktadha wa maelezo ya hapo juu, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i. Kuongeza fedha ya bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ili iweze kufikia angalau kama ile ya mwaka wa fedha 2022/2023 kwani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 bajeti ya miradi ya maendeleo katika Wizara hii imepungua kwa takribani asilimia 25.

ii. Kuhakikisha fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii zinatoka kabla ya mwaka wa huu wa fedha 2022/2023 kukamilika ili kuisaidia Wizara kutekeleza malengo ambayo imejiwekea.

iii. Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu mchango mahsusi wa sekta ya sanaa, utamaduni na michezo katika Pato la Taifa na jinsi ya kuchochea sekta hiyo ili iweze kukua na kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Uwanja wa Michezo wa Taifa (Benjamin Mkapa); Kamati imebaini kutokuwepo kwa ubora wa miundombinu katika Uwanja wa Taifa hali ambayo inapelekea wasiwasi mkubwa kwa matumizi ya uwanja huo wakati wa michezo ya kimataifa na Kitaifa kwa vilabu na timu zetu ya Taifa. Aidha, pamoja na Serikali kuchukua hatua mbalimbali, bado Kamati inaona sehemu ya kuchezea *(pitch)* imeharibika kutokana na mfululizo wa matumizi bila kuwepo kwa mpango bora wa kufanya marekebisho *(repair and maintenance)* kwa wakati. Katika kutatua changamoto hii Kamati inashauri yafuatayo: -

i. Wizara iwe na mkakati wa dhati wa kutumia viwanja vingine vyenye ubora ili kupunguza mzigo kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, hasa katika mashindano ya ndani.

ii. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ihakikishe kunakuwa na viwanja vingi vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi katika Uwanja wa Taifa (Benjamin Mkapa).

iii. Kamati inaipongeza Wizara kuendelea kukusanya mapato kupitia michezo na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa kwenye Uwanja wa Taifa na ule wa Uhuru Jijini Dar es Salaam. Kwa kuwa uwanja wa Benjamin Mkapa unahitaji kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara ili kulinda hadhi yake ni maoni ya

Kamati kuwa Serikali ije na mpango mkakati wa kubakiza *(retain)* sehemu ya mapato yanayokusanywa katika uwanja kuliko ilivyo sasa ambapo mapato yote yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

iv. Kamati inashauri Serikali kuona namna ya kuanzisha utaratibu wa kubakisha asilimia ya Makusanyo ya fedha zinazokusanywa kwenye uwanja wa Taifa kwa ajili ya kufanya matengenezo madogo madogo panapotokea uharibifu.

v. Kamati inasikitishwa na hali ya miundombinu ya Uwanja hususan miundombinu ya umeme iliyopelekea kukatika kwa umeme kwa mechi zilizokuwa zinazochezwa usiku. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inasimamia Menejimenti ya Uwanja wa Benjamini Mkapa ili uwe unafanyiwa matengenezo na marekebisho ya mara kwa mara kwa ajili ya kuzuia hali kama iliyojitokeza tarehe 28 Machi, 2023 na tarehe 30 Aprili, 2023 ya umeme kukatika wakati mechi zikiwa zinaendelea ikihusisha Timu ya Taifa ya Tanzania *(Taifa Stars)* na Timu ya Taifa ya Uganda, pia na timu Yanga dhidi ya *Rivers United* ya Nigeria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania *(Gaming Board of Tanzania)*. Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa tarehe 1 Julai, 2003 kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya Mwaka 2003. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Bodi hii ni kuratibu, kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa sekta ya michezo ya kubahatisha nchini ili iweze kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020, inataka Wizara ya Utamaduni, Sanaa, na Michezo kupokea asilimia 5 ya mapato yatokanayo na kubashiri matokeo ya michezo *(Sports Betting)* inayosimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza maoni mahususi katika eneo hili kama ifuatavyo: -

i. Serikali kupitia Wizara itoe ukomo *(ceiling)* ya fedha hizi ili kuiwezesha Wizara kufanya mipango na hivyo kuonekena kwenye Randama ya Wizara Fungu 96; na

ii. Fedha hizi zitolewe kadiri ya zinavyokusanywa kwa kila mwezi ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa katika eneo la kuendeleza shughuli za michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Viwanja vya Michezo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya Chuo cha Michezo Malya. Aidha, Kamati inaona mazingira wezeshi katika michezo ni msingi bora na inapanua wigo wa kukuza vipaji na ajira. Katika kuinua na kuibua vipaji, Wizara inashirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia UMITASHUMTA na UMISETA. Hata hivyo, Kamati bado inaona haitoshi kwani uendelezaji na ulezi wa vipaji hivyo unatakiwa uwepo wa taasisi maalum ya kusimamia. Kwa hali hiyo, Kamati inashauri ifuatavyo: -

i) Serikali iweke mkakati wa kuongeza idadi ya vyuo vya utamaduni, sanaa na michezo nchini ili kuweza kuongeza idadi ya wataalamu; na kupitia vyuo vya elimu, michezo iingizwe kama somo rasmi ili kupata walimu bora na wabobevu; na

ii) Serikali iweke utaratibu wa kushirikiana na vyama vya michezo kupitia na kuangalia maendeleo ya vijana wenye vipaji na kuwaingiza katika madaraja ya timu za Taifa kulingana na umri wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Mpira wa Miguu kwa Ngazi za Chini. kwa lengo la kukuza vipaji vya mpira wa miguu nchini, Kamati inaishauri Serikali kupitia Baraza la Michezo Tanzania kuimarisha utendaji kazi wa Kamati za michezo za Mikoa

na Wilaya ili ziweze kutekeleza vizuri wajibu wao wa kuratibu michezo kwenye ngazi za kata, vijiji na mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchakato wa Upatikanaji wa Vazi la Taifa. Kwa muda mrefu sasa, tangu Mwaka 2003, Serikali imekuwa katika mchakato wa kutafuta Vazi Rasmi la Taifa. Mchakato huu umechukua takribani miaka 20 na bado hakuna dalili yoyote ya mafanikio ya kupata vazi hilo. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato huu kwa kupata Vazi Rasmi la Taifa au kutangaza rasmi kuachana na mchakato huo kama imeonekana jambo hilo haliwezekani kutokana na mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mirabaha ya Wasanii. Mirabaha ni fidia anayopewa mbunifu kwa kazi yake aliyoiingiza sokoni kutumika kibiashara ikiwa ni tofauti na fedha za mauzo ya moja kwa moja ya kazi zake za ubunifu. Wingi wa kutumika kwa kazi za msanii ndio unaotofautisha ukubwa wa mapato ya mrabaha kati ya msanii mmoja na msanii mwingine. Aidha, iwapo kazi ya msanii haijatumiwa kibiashara hata kama ameiuza na ipo sokoni kwa wingi basi hana haki ya mrabaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (*COSOTA*) ina jukumu ya kusimamia na kulinda wamiliki wa hakimiliki na hakishiriki nchini pamoja na kukusanya na kugawa mirabaha kwenye maeneo ya watumiaji ambayo kampuni zitakuwa hazijaanzishwa. Hata hivyo, Kamati inaona *COSOTA* bado haitekelezi ipasavyo majukumu yake ya kusimamia na kukusanya mirabaha ya wasanii ya ndani na nje ya nchi kwa mujibu wa Kifungu cha 47 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999. Kamati inashauri hatua zifuatazo katika kuimarisha makusanyo ya mirahaba kwa wasanii: -

i. Serikali kuharakisha kukamilisha utaratibu wa kukusanya mirahaba kupitia kwa ukusanyaji wa pamoja yaani *Collective Management Organizations* ili wasanii waanze kufaidika kikamilifu kupitia kazi zao za ubunifu; na

ii. Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni Mswaada wa Sheria wa kudhibiti wizi wa maudhui ya kazi za wasanii *(content conspiracy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho; napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru sana Mhesshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi kwa kushiriki vyema katika vikao vya Kamati ikiwemo cha Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua majina yao yote lakini kwa sababu muda niende moja kwa moja kwenye hitimisho la taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana wewe, Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu vyema, hakika ninyi ni viongozi wa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Said Othman Yakubu, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Nicholas Merinyo Mkapa pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipatia Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu ya Kamati kiufanisi. Pamoja naye, napenda kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, *ndc,* na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu, Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndugu Waziri Kizingiti na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Happiness Christopher Ndalu na

Ndugu Eunike Shirima, kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Utamaduni, Sanaa na Michezo(Fungu 96) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Msingi wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** Ninapenda kukutaarifu kuwa, kwa kuzingatia Kanuni ya **6 (7) (b)** na ya **7 (1) (a),** pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilishughulikia Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na taasisi zilicho chini ya Wizara hiyo. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tarehe 23 na 24 Machi, 2023, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 96** – Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inazingatia maeneo matatu yafuatayo yaliyofanyiwa kazi na Kamati:

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(b) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024; na

(c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 117 (1), cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, na kama sehemu ya kutathimini utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, tarehe 18-19 Machi 2023, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kukagua miradi miwili iliyotengewa fedha na kutekelezwa na Wizara ambayo kwa pamoja ikiwa imetengewa jumla ya **Shilingi 15,831,160,000.00**. Taarifa fupi ya ukaguzi wa miradi hii ni kama ifuatavyo:

**1.2.1 Mradi Namba 4353: Ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianza kutekelezwa Mwaka wa Fedha 2010/11 ukiwa na makadirio ya gharama ya **Shilingi 8,544,000,000.00**. Hata hivyo, baada ya Serikali kupitia upya gharama halisi za mradi kwa wakati uliopo, mradi huu sasa unakadiriwa kugharimu jumla ya **Shilingi 12,300,000,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 chuo kilitengewa **Shilingi 550,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukarabati wa miundombinu, ununuzi wa vifaa kwa ajili ya vituo vya redio na televisheni na ununuzi wa jukwaa la kisasa la chuma *(Truss Stage)*.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Februari 2023, jumla ya **Shilingi 101,959,300.00** zilishatolewa, ikiwa ni sawa na **asilimia 18.5** ya bajeti ya mradi huu kwa mwaka husika.

**1.2.2 Mradi Namba 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa katika Mkoa wa Dar es Salaam na unahusisha ukarabati wa jengo la iliyokuwa Makao Makuu ya Ofisi ya Kamati ya Ukombozi ya Afrika **(OAU)**, utafiti wa

kutambua na kuhifadhi maeneo zaidi ya **260** yaliyotumiwa na Wapigania uhuru wa Afrika yaliyopo nchini**.** Aidha, mradi unahusisha kuongeza wigo wa utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi wa urithi wa ukombozi wa Afrika, kwa kubadili jina kutoka kuwa Ofisi ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Kuwa Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Mradi ulitengewa jumla ya **Shilingi 515,000,000.00**. Hadi kufikia Februari, 2023 mradi ulipokea jumla ya **Shilingi 515,00,000.00** sawa na **asilimia 100** ya fedha zote zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu. **Kamati inapenda kuipongeza Serikali na kuiomba kuendelea kuhakikisha Fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatolewa kwa wakati ili kukamilisha miradi hiyo kwa ufanisi na tija inayokusudiwa.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa, pamoja na ujenzi wa kituo hiki kukamilika kwa asilimia **100,** programu hii inakabiliwa na kukosekana kwa mfumo rasmi wa kisheria wa kusimamia urithi wa ukombozi wa Afrika. Hali hii inaweza kusababisha mchango wa Tanzania katika kuongoza mapambano ya kupigania uhuru na kupinga ubaguzi wa rangi kwa Afrika kutotambulika kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Kituo cha Ukombozi wa Urithi wa Afrika ili isaidie kufanya yafuatayo: -

(a) Kuweka mfumo rasmi wa kisheria na miongozo inayosimamia Urithi wa Ukombozi wa Afrika;

(b) Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhifadhi wa Kumbukumbu za Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; na

(c) Kubadili matumizi ya baadhi ya miundombinu ya Urithi wa Ukombozi ambayo inatumika kwa shughuli nyingine.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Katika kikao kilichofanyika tarehe 24 Machi, 2023, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023. Uchambuzi wa taarifa ulifanywa katika maeneo matatu, ikiwa ni pomoja na kuzingatia kwa maoni na ushauri wa Kamati, ukusanyaji wa maduhuli; na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Taarifa fupi ya maeneo haya ni kama ifuatavyo:-

### 2.1 Kuzingatiwa kwa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika Taarifa yake kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kumi na nne (14) kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji iliyowasilishwa na Wizara na kubaini kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imetekeleza sehemu kubwa ya ushauri na mapendekezo yaliyotolewa.

### 2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo - **Fungu 96** ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 6,296,445,000.00,** ambapo Wizara yenyewe ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 900,000,000.00, sawa na asilimia 14.29** na Idara na Taasisi zilizo chini yake zilikadiriwa kukusanya **Shilingi 5,396,445,000, sawa na asilimia 85.71**.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Wizara, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya **Shilingi 3,119,647,946** sawa na **asilimia 49.55** tu ya lengo la makusanyo. Makusanyo ya maduhuli kwa Wizara yalikuwa **Shilingi 574,236,691**, sawa na **asilimia 63.8** ya lengo. Wakati huo huo Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya **Shilingi 2,545,411,255** sawa na **asilimia 47.2** ya lengo la makusanyo kama inavyooneshwa katika Kielelezo Namba 1(a) na (b).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limefanikiwa kukusanya **Shilingi 489,132,298** sawa na **asilimia 71.4** ya **Shilingi 685,000,000** ya makadirio ya makusanyo yaliyoidhinishwa. Hata hivyo, Kamati iligundua kuwa chanzo cha mafanikio hayo ni kutokana na utaratibu, usimamizi mzuri na udhibiti uliowekwa na Serikali kupitia BMT. **Kamati inaipongeza BMT kwa kufuata miongozo ya Serikali, hali iliyopelekea ukusanyaji wa mapato kuwa wenye ufanisi.**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Haki Miliki Tanzania (COSOTA) hadi kufikia mwezi Februari, 2023, walikuwa wamekusanya **Shilingi 200, 812, 000. 00** sawa na **asilimia 14.9** tu ya lengo la kukusanya **Shilingi 1,350,000,000.00** iliyoidhishwa na Bunge lako Tukufu. Hiki ni kiasi kidogo sana hasa ukizingatia kuwa COSOTA na Bodi ya Filamu Tanzania ni miongoni wa Taasisi inayotengemewa katika ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara hii.

Kielelezo Namba 1 (a): **Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Mwaka 2022/2023 na kiasi kilichokusanywa hadi Februari, 2023**

| CHANZO | JUMLA YA MAKADIRIO YA WIZARA | MAKADIRIO KWA TAASISI | ASILIMIA | MAKUSANYO KWA TAASISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| Wizara ya Maendeleo ya Michezo | | 900,000,000 | 14.29 | 574,236,691 | 63.8 |
| Taasisi zilizo chini ya Wizara | | 5,396,455,000 | 85.71 | 2,545,411,255 | 47.2 |
| JUMLA | 6,296,445,000.00 | 6,296,455,000 | 100 | 3,119,647,946 | **49.55** |

***Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati***

### 2.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara kupitia **Fungu 96** pamoja na Taasisi zake iliidhinishiwa **Shilingi 35,425,991,000.** Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 8,201,882,000**, sawa na **asilimia 21.15,** Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 11,391,949,000** sawa na **asilimia 32.15** na **Shilingi 15,831,160,000** sawa na **asilimia 44. 68** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi Februari, 2023, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina jumla ya **Shilingi 16,036,220,372.00** sawa na **asilimia 45.3** ya bajeti yote, kwa mchanganuo ufuatao:-

i. **Shilingi 5,383,725,304** kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 33.6** ya fedha zote zilizopokelewa;

ii. **Shilingi 5,627,327,687** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na **asilimia 35.1** ya fedha zilipokelewa; na iii. **Shilingi 5,025,167,381** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na **asilimia 32** ya fedha zilipokelewa.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilitengewa kiasi cha jumla ya Shilingi 15,831,160,000 tu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kiasi hiki ni kidogo sana kulinganisha na majukumu na umuhimu wa Wizara yenyewe katika kukuza, kulinda na kuendeleza utambulisho wa Mtanzania kwenye nyanja za ubunifu, utamaduni, sanaa na michezo. Hata hivyo, bado fedha hizo kidogo zimekuwa hazitolewi kwa wakati, hali inayokwamisha utekelezaji wa majukumu katika Wizara hii.

**Kielelezo Na.2: Ulinganisho wa upokeaji wa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi Februari, 2023**

| MAELEZO | | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Mishahara ya Watumishi | Wizara | 3,326,321,000 | 2,140,969,716 | 64.36 |
| | Taasisi chini ya Wizara | 4,875,561,000 | 3,242,755,588 | 66.51 |
| **Jumla Ndogo** | | **8,201,882,000** | **5,383,725,304** | **65.64** |
| Matumizi Mengineyo (OC) | Wizara | 8,334,371,000 | 3,751,139,347 | 45.01 |
| | Taasisi chini ya Wizara | 3,058,578,000 | 1,876,188,340 | 61.34 |
| **Jumla Ndogo** | | **11,392,949,000** | **5,627,327,687** | **49.39** |
| Miradi ya Maendeleo | Wizara | 14,981,160,000 | 4,543,208,080 | 30.33 |
| | Taasisi chini ya Wizara | 850,000,000 | 481,959,301 | 57.60 |
| **Jumla Ndogo** | | **15,831,160,000** | **5,025,167,381** | **31.74** |
| **JUMLA KUU** | | **35,425,991,000** | **16,036,220,372** | **45.27** |

***Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati***

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imejiwekea malengo mbalimbali kwa kuzingatia Mipango na Sera za Kitaifa na Kimataifa ambazo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

(2021/2022 – 2025/2026) pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020) na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/2022 -2025/2025 - 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni **:-**

(i) Kutafiti, kukusanya na kuhifadhi elementi za Urithi wa Utamaduni Usioshikika na kuandaa ripoti ya miaka minne ya utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa Mwaka 2003 unaohusu Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika;

(ii) Kukamilisha ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya O.A.U pamoja na kufanya ukarabati wa makaburi na mahandaki yenye urithi wa ukombozi wa Afrika;

(iii) Kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa Timu za Taifa katika michezo na michuano mbalimbali sambamba na kuhamasisha wadau kusaidia ushiriki wa timu, vilabu na wawakilishi mbalimbali wa kitaifa katika michezo na michuano ya kimataifa;

(iv) Kuendelea kufanya ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Benjamin Mkapa katika maeneo ya uwanja *(pitch),* mfumo wa umeme, mfumo wa zimamoto, mfumo wa maji, kubadilisha eneo la mashabiki na majukwaa ya watu mashuhuri;

(v) Kuratibu na kuendesha vipindi vya Redio na Televisheni, makongamano na midahalo kuhusu namna ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini;

(vi) Kufanya Tamasha la Kitaifa la Utamaduni pamoja na kuratibu Matamasha ya Kiutamaduni katika Kanda saba (7) za Utamaduni ili kusherehekea Unuani wa Urithi wa Utamaduni;

(vii) Kuratibu mashindano ya Sanaa kwa vijana kupitia UMMISETA, UMITASHUMTA, Taifa Cup na mashindano mengine; na

(viii) Kuratibu Tamasha la Sauti za Busara, Masai Festival, Usiku wa Taarab na matamasha mengine ya Kitaifa na Kimataifa kwa kushirikiana na wadau.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika sehemu hii upo katika maeneo matatu kama yavyofafanuliwa hapa chini.

**3.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia **Fungu 96** inakadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 6,970,428,000.** Makadirio haya yameongezeka kwa **Shilingi 673,974,000** sawa na **asilimia 10.7** ukilinganisha na yale ya mwaka 2022/2023, kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 3a na 3b.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara na Idara zake zinatarajiwa kukusanya **Shilingi 1,000,000,000** sawa na **asilimia 14.7** ya makusanyo yote**.** Makusanyo haya ni ongezeko la **Shilingi 100,000,000**, ikilinganishwa na lengo la kukusanya **Shilingi 900,000,000** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika, Taasisi sita zilizo chini ya Wizara zinatarajia kukusanya** Shilingi 5,970,428,000 **sawa na** asilimia 85.3 **ya lengo la Makusanyo ya Wizara nzima. Makusanyo haya ni ongezeko la** Shilingi 573,973,000 **ikilinganishwa na makusanyo ya** Shilingi 5,396,455,000 **kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.**

**Kielelezo Na 3a: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Mwaka 2022/2023 na 2023/2024 - Makao Makuu ya Wizara (Idara ya Maendeleo ya Michezo)**

| Maelezo | Makadirio y Maduhuli 2022/23 | Makadirio ya Maduhuli 2023/24 | Ongezeko/Pungufu kwa asilimia |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru na Benjamin Mkapa) | 640,000,000 | 907,696,000 | 42 |
| Ada za Mafunzo | 259,998,000 | 92,302,000 | 64 |
| Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | 1,000 | 0 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | 1,000 | 0 |
| Jumla | 900,000,000 | 1,000,000,000 | 11 |

*Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati*

**Kielelezo Na. 3b: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Taasisi Zilizo chini ya Wizara (Fungu 96) katika Mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

| Na | Jina la Taasisi | Makadirio ya Maduhuli 2022/23 | Makadirio ya Maduhuli 2023/24 | Ongezeko/ Pungufu,kwa asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 416,750,000 | 480,228,000 | 15.23 |
| 2. | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 720,000,000 | 800,000,000 | 11.11 |
| 3. | Bodi ya Filamu Tanzania | 1,359,642,000 | 1,460,000,000 | 7.38 |
| 4. | Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 685,068,000 | 950,200,000 | 38.70 |
| 5. | Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 1,350,000,000 | 920,000,000 | 32 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 1,025,000,000 | 1,360,000,000 | 33 |
| **Jumla** | | **5,396,455,000** | **5,970,428,000** | **11** |

***Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati***

**3.2 Makadirio ya Matumizi**
**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kupitia **Fungu 96** Wizara inakadiriwa kutumia **Shilingi 35,445,041,000.00.** Kati ya fedha hizo, Misharaha (PE) ni **shilingi 9,651,285,000.00** sawa na **asilimia 27.2**. Matumizi Mengineyo (OC) yanaombewa **Shilingi 13,962,596,000.00** sawa na **asilimia 39.4** na Miradi ya Maendeleo inaombewa **Shilingi 11,831,160,000.00** sawa na **asilimia 33.4.**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi Kamati imebaini kuwa bajeti ya mwaka 2023/2024 imeongezeka kwa **Shilingi 19,050,000**, (sawa na **asilimia 0.05)** ukilinganisha na Bajeti ya mwaka 2022/2023.


**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi unaonesha kuwa katika Mwaka 2023/2024 makadirio ya mishahara yameongezeka kwa **Shilingi 1,449,403,000,** kutoka **Shilingi 8,201,882,000** mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 9,651,285,000** mwaka 2023/2024; sawa na ongezeko la **asilimia 17.7.** Matumizi Mengineyo (OC) iliongezeka kwa **Shilingi 2,569,647,000,** kutoka **Shilingi 11,392,949,000** Mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 13,962,596,000** mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la **asilimia 22.6**.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, makadirio ya matumizi ya maendeleo yameshuka kwa **Shilingi 4,000,000,000,** sawa na **asilimia 25.3,** kutoka **Shilingi 15,831,160,000** Mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 11,831,160,000** mwaka 2023/2024 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 4.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na Wizara kupunguziwa bajeti ya Miradi Maendeleo. Hatua hii haiendani kabisa na nia ya serikali na hususan maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kukuza na kuimarisha sekta ya utamaduni, Sanaa na michezo nchini. Aidha, hatua hii haiakisi hamasa kubwa iliyopo sasa ya watanzania ya kupenda na kukumbatia sekta hizi muhumu. **"Kwa hiyo basi,**

**Kamati inashauri Bunge lako Tukufu, kuitaka Serikali iongeze Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara angalau kufikia ile ya mwaka 2022/2023 au zaidi ili kuingozea Wizara hii nguvu ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na kuinua sekta nzima ya utamaduni, sanaa na michezo kwa ujumla wake."**

Kielelezo Na. 4: **Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi (Fungu 96) kwa mwaka 2022/2023 na mwaka 2023/2024**




## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa Ushauri, Maoni na Mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 4.1 Umuhimu wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo kina nafasi kubwa ya kuchangia katika maendeleo ya sanaa na utamaduni nchini kwa kunoa vipaji vya vijana wetu waliopo katika tasnia ya sanaa na utamaduni. Aidha, chuo hiki kingeweza kuwa tanuru la kutafiti, kuchakata na kuwa makavazi (museum) ya utamaduni wa taifa letu. Hata hivyo, chuo kimeshindwa

kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa sababu fedha zilizokuwa zikitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zimekuwa hazipelekwi kwa wakati zaidi ya Miaka kumi mfulululizo .

***Mheshimiwa Spika***, Kamati inatoa ushauri ufuatao:

i) Serikali kukiwezesha chuo hiki kutekeleza majukumu kwa kukipatia fedha zote zinapangwa katika Bajeti.

ii) Wadau wa sanaa na utamaduni nchini kuungana na Serikali katika kukiendeleza, kukienzi na kukitumia chuo hiki katika kuendeleza tasnia za sanaa na utamaduni nchini.

iii) Chuo kibuni na kuanzisha kozi mbalimbali zenye kuwasaidia wasanii kujiajiri mara baada ya kumaliza mafunzo yao. Kozi zitakazotolewa ziweze kuwasaidia kubuni miradi na kuiendesha kwa ufanisi na tija.

**4.2 Ukusanyaji wa Maduhuli wa Taasisi zinazosimamiwa na Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** ukiacha Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Wizara na taasisi zake zilishindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa maduhuli yaliyopangwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kwa mfano, hadi Kamati inachambua taarifa za wizara mwezi Februari 2023, Ofisi ya Haki Miliki (COSOTA) ilikuwa imekusanya asilimia 14.9 tu ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1.350. Ni wazi kuwa kuna kulegalega katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kupitia wizara hii na taasisi zake. Ni moni ya Kamati kwamba Wizara na Taasisi zake ziongezeke juhudi katika kusimamia ukusanyaji wa Maduhuli, kwa kuwa inaaminika kwamba tasnia ya sanaa na utamaduni ni mgodi ulio juu ya ardhi ambao unaweza kutumika kuzalisha mapato na ajira nyingi kwa vijana nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kushughulikia changamoto zilizojitokeza kwenye ukusanyaji wa maduhuli na kurasimisha tasnia ya sanaa na utamaduni kwa ujumla, Kamati inashauri hatua zifuatazo:

i) Uongozi wa Wizara uimarishe usimamizi wa taasisi zake katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli

ii) Wizara ifanye tathmini maalum kwa COSOTA ili kujua sababu za taasisi hii kushindwa kukusanya maduhuli kama yalivyopangwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kurekebisha kasoro zilizopo kimfumo, kisheria na kiutendaji

iii) Serikali ifanye utafiti na kisha kuandaa mkakati maalumu juu ya kuimarisha na kurasimisha sekta ya tasnia ya sanaa na utamaduni kama sekta muhimu ya uzalishaji mapato na kukuza ajira nchini

**4.3 Upatikaji wa Fedha za Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ndiyo ambayo inaitambulisha na kuitofautisha nchi yetu Kimataifa, lakini kwa masikitiko makubwa Kamati inaona Wizara hii bado haijapewa kipaumbele hasa katika mgawanyo wa Bajeti. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali imepanga kutumia **Shilingi Trilioni 15.2** kama fedha za Maendeleo ambapo Wizara hii imepangiwa **Shilingi Bilioni 11.8** sawa na **asilimia 0.08** tu ya Bajeti yote ya Maendeleo kwa Mwaka huo wa Fedha. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, bajeti ya matuimizi ya maendeleo kwa wizara hii imeshuka takribani **asilimia 25** ukilinganisha na ya mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya maendeleo kwa Wizara inashuka katika kipindi ambacho Mheshimiwa Rais ameipa msukumu mkubwa tasnia ya sanaa, utamaduni na michezo mpya kabisa hadi kuunda wizara maalumu kwa ajili ya tasnia hizi. Aidha, bajeti hii inashuka katika kipindi ambacho wizara imejielekeza kutekeleza vipaumbele vikubwa saba, ikiwa ni pamoja na kuwezeha ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano ya kimataifa na kukarabati Uwanja wa Benjamin Mkapa na viwanja vingine nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika muktadha wa maelezo ya hapo juu, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

i) Kuongeza Fedha ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ili iweze kufikia angalau kama ile ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwani kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo katika Wizara hii imepungua kwa takribani **asilimia 25;**

ii) Kuhakikisha fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii zinatoka kabla ya Mwaka wa huu wa Fedha 2022/2023 kukamilika ili kuisaidia Wizara kutekeleza malengo ambayo imejiwekea

iii) Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu mchango mahsusi wa sekta ya sanaa, utamaduni na michezo katika pato la taifa na jinsi ya kuchochea sekta hiyo iweze kukua na kuleta tija zaidi.

**4.4 Uwanja wa Michezo wa Taifa (Benjamin Mkapa Stadium)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kutokuwepo kwa ubora wa miundombinu katika Uwanja wa Taifa hali ambayo inapelekea wasiwasi mkubwa kwa matumizi ya uwanja huo wakati wa michezo ya Kimataifa na Kitaifa kwa vilabu na timu zetu ya Taifa. Aidha, pamoja na Serikali kuchukua hatua mbalimbali, bado Kamati inaona sehemu ya kuchezea *(Pitch)* imeharibika kutokana na mfululizo wa matumizi bila kuwepo kwa mpango bora wa kufanya marekebisho *(repair and maintenance)* kwa wakati. Katika kutatua changamoto hii Kamati imeshauri yafuatayo: -

i) Wizara iwe na mkakati wa dhati wa kutumia viwanja vingine vyenye ubora ili kupunguza mzigo kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa hasa katika mashindano ya ndani.

ii) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ihakikishe kunakuwa na viwanja vingi vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya Kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi katika Uwanja wa Taifa (Benjamini Mkapa Stadium).

iii) Kamati inaipongeza Wizara kuendelea kukusanya mapato kupitia michezo na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa kwenye Uwanja wa Taifa na ule wa Uhuru Jijini Dar es Salaam. Kwa kuwa uwanja wa Benjamin Mkapa unahitaji kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara ili kulinda hadhi yake. **Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ije na mpango mkakati wa kubakiza *(retain)* sehemu ya Mapato**

**yanayokusanywa katika uwanja kuliko ilivyo sasa ambapo mapato yote yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.**

iv) Kamati inashauri Serikali kuona namna ya kuanzisha utaratibu wa kubakisha asilimia ya Makusanyo ya fedha zinazokusanywa kwenye uwanja wa Taifa kwa ajili ya kufanya matengenezo madogo madogo ya uharibifu.

v) Kamati inasikitishwa na hali ya miundombinu ya Uwanja hususan miundombinu ya umeme iliyopelekea kukatika kwa umeme kwa mechi zinazocheze usiku. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inasimamia Menejimenti ya Uwanja wa Benjamini Mkapa ili uwe unafanyiwa matengenezo na marekebisho ya mara kwa mara kuzuia hali liyojitokeza tarehe 28 Machi, 2023 na tarehe 30 Aprili, 2023 ya umeme kukatika wakati mechi zikiwa zinaendelea ikihusisha Timu ya Taifa ya Tanzania *(Taifa Stars)* na Timu ya Taifa ya Uganda, pia na timu Yanga dhidi ya Rivers United ya Nigeria.

### 4.5 Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania *(Gaming Board of Tanzania)*

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania *(Gaming Board of Tanzania - GBT)* ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa tarehe 1 Julai, 2003 kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya Mwaka 2003 ya Michezo ya Kubahatisha. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Bodi hii ni kuratibu, kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa Sekta ya Michezo ya kubahatisha nchini ili iweze kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020, inataka Wizara ya Utamaduni, Sanaa, na Michezo kupokea **asilimia 5** ya mapato yatokanayo na kubashiri matokeo ya michezo *(Sports Betting)* inayosimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza maoni mahususi katika eneo hili kama ifuatavyo:

i. Serikali kupitia hazina itoe ukomo (ceiling) wa fedha hizi ili kuiwezesha Wizara kufanya mipango na hivyo kuonekena kwenye Randama za Wizara Fungu 96; na

ii. Fedha hizi zitolewe kadiri ya zinavyokusanywa kwa kila mwezi ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa katika eneo la kuendeleza shughuli za michezo.

**4.6 Kuimarisha Viwanja vya Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya Chuo cha Michezo Malya. Aidha, Kamati inaona mazingira wezeshi katika michezo ni msingi bora na inapanua wigo wa kukuza vipaji na ajira. Katika kuinua na kuibua vipaji, Wizara inashirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia UMITASHUMTA na UMISETA. Hata hivyo, Kamati bado inaona haitoshi kwani uendelezaji na ulezi wa vipaji hivyo unatakiwa uwepo wa taasisi maalum. Kwa hali hiyo, Kamati inashauri ifuatavyo: -

i) Serikali iweke mkakati wa kuongeza idadi ya vyuo vya utamaduni, sanaa na michezo nchini ili kuweza kuongeza idadi ya wataalamu na kupitia vyuo vya elimu, michezo iingizwe kama somo rasmi ili kupata walimu bora na wabobevu; na

ii) Serikali iweke utaratibu wa kushirikiana na vyama vya michezo kupitia na kuangalia maendeleo ya vijana wenye vipaji na kuwaingiza katika madaraja ya Timu za Taifa kulingana na umri wao.

**4.7 Usimamizi wa Mpira wa Miguu kwa ngazi za chini**

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kukuza vipaji vya mpira wa miguu nchini, Kamati inaishauri Serikali kupitia Baraza la Michezo Tanzania kuimarisha utendaji kazi wa Kamati za michezo za Mikoa na Wilaya ili ziweze kutekeleza vizuri wajibu wao wa kuratibu michezo kwenye ngazi za kata, vijiji na mitaa.

### 4.8 Mchakato wa Upatikanaji wa Vazi la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa, tangu Mwaka 2003, Serikali imekuwa katika mchakato wa kutafuta vazi rasmi la Taifa. Mchakato huu umechukua takribani miaka 20 na bado hakuna dalili yoyote ya mafanikio ya kupata vazi hilo. ***Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato huu kwa kupata vazi la Taifa au kutangaza rasmi kuachana na mchakato huo kama imeonekana ni jambo lisilowezekana kutokana na mazingira yetu.***

### 4.9 Mirabaha ya Wasanii

**Mheshimiwa Spika**, mirabaha ni fidia anayopewa mbunifu kwa kazi yake aliyoiingiza sokoni kutumika kibiashara ikiwa ni tofauti na fedha za mauzo ya moja kwa moja ya kazi zake za ubunifu. Wingi wa kutumika kwa kazi za msanii ndiyo unaotofautisha ukubwa wa mapato ya mrabaha kati ya msanii mmoja na msanii mwingine**.** Aidha, iwapo kazi ya msanii haijatumiwa kibiashara hata kama ameiuza na ipo sokoni kwa wingi basi hana haki ya mrabaha.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ina majukumu ya kusimamia na kulinda wamiliki wa hakimiliki na hakishiriki nchini pamoja na kukusanya na kugawa mirabaha kwenye maeneo (watumiaji) ambayo kampuni zitakuwa hazijaanzishwa. Hata hivyo, Kamati inaona COSOTA bado haitekelezi ipasavyo majukumu yake ya kusimamia na kukusanya mirabaha ya wasanii ya ndani na nje ya nchi kwa mujibu wa Kifungu cha 47 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999. Kamati inashauri hatua zifuatazo katika kuimarisha makusanyo ya mirahaba kwa wasanii:

i) Serikali kuharakisha kukamilisha utaratibu wa kukusanya mirahaba kupitia kwa ukusanyaji wa pamoja yaani *Collective Management Organizions* (CMOs) ili wasanii waanze kufaidika kikamilifu kupitia kazi zao za ubunifu; na

ii) Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni Mswaada wa Sheria wa kudhibiti wizi wa maudhui ya kazi za wasanii (content conspiracy).

**SEHEMU YA TANO**

**5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti - Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb pamoja na Wajumbe wote wa Kamati, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi kwa kushiriki vyema katika vikao vya Kamati ikiwemo cha Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mb - M'kiti
2. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - M/M'kiti
3. Mhe. Mwanahamisi Kassian Said, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Aloyce John Kamamba. Mb - Mjumbe
5. Mhe. Nusrat Shaban Hanje, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Esther Edwin Maleko, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Yahaya Abdulwakili, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Janejely James Ntate, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Dkt. Thea Ntara, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb - MJumbe
16. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Khamis Ali Kassim, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe na Naibu Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Hakika ninyi ni viongozi wa mfano.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo – Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb), Naibu Waziri - Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii - Ndg. Said Othman Yakubu, Naibu Katibu

Mkuu - Ndg. Nicholas Merinyo Mkapa pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipatia Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu ya Kamati Kiufanisi. Pamoja naye, napenda kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndugu Michael Chikokoto, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu - Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndg. Waziri Kizingiti na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee, tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Happiness Christopher Ndalu na Ndg. Eunike Shirima, kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Utamaduni, Sanaa na Michezo - **Fungu 96** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

**Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mb**
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**
**06 JUNI, 2023**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Husna Sekiboko Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni na Michezo nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge kuna wageni waliopo Bungeni muda huu, wageni wa Waheshimiwa Wabunge wageni 65 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Mbunge ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana, Ajira na wenye Ulemavu ambao ni Chawa wa Mama kutoka Kasulu Mjini, Mkoa wa Kigoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile Mbunge ambao ni viongozi na walimu wa *Scout* kutoka Kigamboni Mkoa wa Dar es Salaam, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Justine Nyamoga, ambao ni watumishi kutoka Huduma ya Yerusalemu na Waumini kutoka Kilolo, Mkoa wa Iringa, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Waheshimiwa Profesa Kitila Kumbo na Mheshimiwa Issa Mtemvu, ambao ni Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi ya Wilaya ya Ubungo na Wajumbe wa Baraza la Wazee kutoka Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Hamisi Taletale kutoka Jijijni Dar es Salaam, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wapo wanafunzi 29 na Walimu nane kutoka Shule ya Ben Carson ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni kwenye Jukwaa la Spika ambaye ni Ndugu Imani Kajula ambaye ni *CEO* wa Klabu ya *Simba Sports, a*hsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.  Sasa tunaanza mjadala, hapa ninayo orodha ya wachangiaji, tutaanza na Profesa Kitila Alexander Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwanza nimpongeze *CEO* wa Simba kwa kuwa na roho ngumu kuwepo humu ndani leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye Kamati yetu, niongeze sauti kidogo kwenye eneo moja la utamaduni na nataka kuzungumia umuhimu wa utamaduni. Kwa kweli utamaduni ni dhana muhimu sana katika kufikia Tanzania ambayo tunaitaka kimaendeleo. Changamoto nyingi ambazo tunakumbana nazo tungeweza kuzitatua kama tukizingatia dhana hii ya utamaduni. Mara nyingi tukizungumzia utamaduni watu wanazungumzia habari za sanaa, maigizo, nyimbo ngoma za asili, hizo ni sehemu muhimu, lakini sio utamaduni pekee, ni sehemu muhimu ya utamaduni, lakini haiwezi kuwa pekee yake, lakini muhimu ni kwamba utamaduni kwa kweli ni mtindo wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo yale mawazo, desturi, tabia ya kijamii, mkusanyiko wake ndio tunapata utamaduni. Kwa mfano, tunapozungumzia ubunifu, ili tuweze kuwa na ubunifu maana yake tunahitaji kujenga utamaduni wa ubunifu, kwa mfano kuwa na tabia ya kujaribu na kutokuogopa kukosea. Kama tukisema kupambana na rushwa, sheria pekee yake haitoshi, lazima tujenge utamaduni wa kukataa kwa mfano *shortcut* na ujanja ujanja katika Maisha, ni utamaduni. Ukiwa na jamii ambayo utamaduni wake ni ujanja ujanja, *shortcut* hata utunge sheria ngumu namna gani, bado rushwa itakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo utamaduni ni jambo la msingi sana katika kukamilisha ambayo tunayataka. Hata sasa hivi Mheshimiwa Rais anapanua mambo ya demokrasia, maridhiano na yenyewe inahitaji kujenga utamaduni wa kidemokrasia, ikiwemo utamaduni wa kupingana kwa hoja bila kuchukiana, utamaduni wa kustahimiliana tunapotofautiana na utamaduni wa kuheshimu sheria na haki za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo utamaduni wa kuheshimu sheria ni muhimu sana, unaweza ukawa na sheria nzuri, lakini kama hamna utamaduni huo itakuwa ni changamoto. Kwa sasa hivi lazima tupongeze kwamba nchi yetu ina utamaduni

mzuri kwenye michezo. Tuna timu mbili kubwa Yanga na Simba tunashindana, tunataniana, tunacheka, hatugombani, jambo jema ni utamaduni mzuri sana. Hata kama wenzetu ndio hivyo tena lakini tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na umuhimu wa utamaduni nchi yetu hii tangu tulipoanza, hotuba ya kwanza ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo Tanganyika kama *Republic* katika Bunge Mkutano wa Tano wa Bunge, tarehe 10 Desemba, Mwalimu Nyerere alitangaza kufanya mabadiliko makubwa mawili katika Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badiliko moja ambalo alifanya aliamua kuanzisha Wizara Maalum ambayo wakati huo aliita *Ministry of National Culture and Youth,* baadaye wakatafsiri wengine wakaita Wizara ya Mila za Taifa na Uongozi wa Vijana. Kwa hiyo, ukienda Waziri wa kwanza wa Wizara hii alikuwa anaitwa Bwana Kundya, Mbunge wa Singida alikuwa anaitwa Waziri. Mheshimiwa Sima, Mbunge wako wa kwanza alikuwa Kundya huyo na alikuwa Waziri wa Mila za Taifa na Uongozi wa Vijana. Kwa hiyo, Mwalimu aliamua kuanzisha Wizara Maalum, baadaye wakafuata wengine akina Chedya na kadhalika, lakini hatimaye akaja Meja Jenerali Sarakikya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo kwa muda mrefu tukawa na hii Wizara na katika historia ya nchi yetu ni mara mbili tu tumekuwa na Wizara *dedicated* kwa ajili ya utamaduni na sanaa. Mara ya kwanza ni hiyo ilikuwa tarehe 10 Desemba, 1962, mara ya pili ni mwaka jana tarehe 8 Januari, 2022. Pale ambapo Mheshimiwa Rais aliamua kuunda Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kwa hiyo, ni uamuzi ambao ni mkubwa na unaakisi malengo yale ambayo Mwalimu Nyerere aliyatanganza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale aliposema Makamu Mwenyekiti sisi Kamati hatuwezi kuelewa, katika kipindi ambacho Mheshimiwa Rais ameamua kufuata nyayo za Baba wa Taifa 1962 tukiwa watu milioni 10, inawezekanaje tumeunda Wizara Maalum watu milioni 61 halafu unapunguza bajeti ya maendeleo, hili haliwezi kueleweka. Kwa hiyo tuombe sana Serikali ilione jambo hili kwamba ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende katika jambo la pili, *of course* siwezi kumaliza hotuba yangu bila kuipongeza Timu ya Yanga kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Wameijengea heshima nchi, dunia imeona, nchi imeona, lakini Mheshimiwa Rais ameona jambo kubwa sana hili. Kwa hiyo, tunawapongeza na nadhani mambo mazuri huwa yanaigwa, nishauri kwa mfano, pale Dar es Salaam tuna Mkuu wa Mkoa pale, Albert Chalamila, mahiri sana, machachari, pengine angeweza kuamua wale ambao wamefika robo fainali awaandalie *lunch* ya Mkuu wa Mkoa pale. Kwa hiyo, mtu akiingia robo fainali Mkuu wa Mkoa anaandaa *lunch,* akiingia fainali *dinner* kwa Mheshimiwa Rais, tatizo liko wapi? Kwa hivyo jambo hili watu wasiwe na nani na nini, inakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pale Ubungo tuna mabingwa 30 wa ndondi, 30 Jimbo la Ubungo pekee yake kwenye mambo ya ngumi. Nataka niwapongeze vijana hawa na kwa niaba yao niwataje wachache tu kwa sababu ya muda. Nimtaje Binti yetu Amina Mohamedi, hongera sana; Mariam Macho, hongera sana; Iddi Pialali, hongera sana; Hassan Ndoga, hongera sana, Mfaume Mfaume, hongera sana kwa kazi kubwa ambayo ameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wasanii wote kutoka Jimbo la Ubungo wanamuziki ambao walishinda tuzo za muziki nimpongeze sana kupitia kwake Ndugu yetu Dulla Makabila ambaye aliibuka kuwa msanii bora wa kiume wa singeli, hongera sana Dulla Makabila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni ombi kwa Mheshimiwa Waziri, Dar es Salaam na hasa Wilaya ya Ubungo tuna mashindano ya *Ndondo Cup*. Tunayo maombi mawili, ombi la kwanza atusaidie sana Mheshimiwa Waziri, vile Viwanja wa Kinesi na *TP* ni viwanja muhimu ambavyo vinatumika kwa ajili ya mashindano ya *Ndondo Cup,* lakini havijakaa vizuri. Tumwombe sana, tena sasa Mwenyekiti anaaongea, amwangalie Mwenyekiti wake aweke kiwanja pale, jambo jema kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, suala la *Ndondo Cup* tunaomba liingie katika mfumo rasmi wa kiligi litambuliwe. Kwa

sababu linaibua vipaji vya vijana wengi sana, *otherwise* Mheshimiwa Waziri sisi kama Kamati kama alivyosema mwenzangu tunampongeza kwa kazi nzuri, ana hamasa nzuri, juzi amewatia vijana wetu hamasa nzuri sana pale Algeria, ile tumeshinda lakini tumeshindwa kikanuni. Kimchezo tulishinda, lakini kikanuni tukashindwa, lakini Waziri amechangia sana kwa hamasa zako. Tunashukuru kwa hamasa kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa, vijana wanawaka moto na tunaamini mwaka huu timu zetu zaidi ya mbili zitaenda vizuri katika Mashindano ya Kombe la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kitila. Waheshimiwa Wabunge muda wa kuchangia ni dakika saba, kwa sababu orodha ni ndefu. Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete na Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara hii ya Michezo, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kile alichokifanya kwenye hii Wizara kutuletea Mawaziri majembe. Kikubwa ambacho naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Waziri kutoka Tanga, Ndugu yangu Hamis Mwinjuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anachaguliwa nakumbuka nilikuwa Marekani, lakini Waziri alikuwa na kidevu cheusi kabisa hakina mvi hata moja, alikuwa anakicheka cha kwangu, Mheshimiwa Waziri leo hii ana kidevu cheupe kwa sababu ya mzigo mzito wa Wizara aliyopewa. Wizara kubwa, Wizara ambayo inachangia furaha ya nchi nzima, Wizara ambayo Bunge lako lina furaha kwa sababu ya hii Wizara, ila Wizara hii inatia aibu, tunakaa hapa mbele Wizara ina bajeti ndogo kuliko Wizara yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ana mapenzi ya dhati na hii Wizara, tuseme wazi ameingia madarakani Mheshimiwa Rais akaelekeza watu wa michezo ya kubashiri

wapeleke pesa asilimia tano inayopatikana. Yote hayo ni kupambana na hii Wizara ili ikapate pesa. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ambao tunasimamia hii Wizara, ni aibu kusema mengi, Wizara haina pesa hii, tunamtia mvi ndugu yangu Mwana FA na dada yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niongee kidogo, leo hii hawa Wizara imeletewa Fungu bilioni 900 Mwezi wa Pili, mwaka huu. Ukimuuliza Waziri hapo hajui hiyo miiloni 900 ya nini, tuseme ukweli kwa heshima niliyonayo…

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, … kwako na …

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamisi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nampongeza anachangia vizuri Mheshimiwa Taletale, lakini nataka tu aweke rekodi vizuri sio bilioni 900 ni milioni 900, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Hamisi taarifa unaipokea?

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea na nimezoea kuzungumza kuhusu ma-b kumbe kuna ma-mi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inapelekewa milioni 900 ya kitu ambacho wao hawajui, leo dada yangu Mheshimiwa Waziri, leo naondoka na shilingi yake, ikiwezekana akamtafute Waziri wa Fedha, maana yake hapo mbele hayupo. Tujue je, hiyo milioni 900 anayopewa, inawezekana hata Mheshimiwa Rais ameelekeza hii

*five percent* iende kwao, lakini pia hajui hiyo milioni 900 waliyopewa ya mchanganuo gani. Kwa hiyo, niombe tunataka kujua hizo pesa zinazokuja kwenye Wizara yetu ya Michezo zinakuja kwa utaratibu upi, kwa namba ipi? Maana ukisema leo hii Wizara imeletewa milioni 900 Mwezi wa Pili, wakati watu wa michezo ya kubashiri kila mwezi wanatoa pesa, kwa hiyo, wananyimwa haki yao. Nani wa kusimamia haki yao kama sio sisi kama Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kingine hapa, maendeleo ya michezo tuangalie wenzetu kama Senegal, Senegal ni nchi ambayo ina wananchi milioni 16, Tanzania tuko zaidi ya milioni 60, Senegal ukitazama mashindano makubwa ya ndani ya Afrika yote Senegal wamechukua. Sisi tupo tu, tunahangaika kubebesha mzigo kuipa *TFF*. Nimpongeze sana Ndugu yangu Karia na timu yake, tunahangaika kubebesha mzigo kumpa Mama Samia. Jamani juzi nimesema mimi ni kipenzi cha yule mama, wanamtia presha mama yangu. Watafuteni utaratibu, watafute njia ya kuangalia jinsi gani hii Wizara itapata pesa, tuwe wawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakae, hii ni michezo ya kubashiri, waibebe kama ilivyo waipeleke Wizara ya Michezo, wanashindwa nini? Leo hii tunakuja kuzungumzia michezo hapa, kuna Wizara ina zaidi ya trilioni tatu, Wizara ya Michezo ina bilioni 35, ni udhalilishaji huo, ni aibu kwa Wizara na ni aibu kwa Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia. Kama tunataka kumsaidia Rais *positively,* lazima tuangalie tunakwama wapi? Lazima tuangalie tuna dhamira gani, dhamira ya kutaka kumsaidia Rais, hii michezo ya kubashiri…

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu, Nchi kama Uingereza labda tuseme ni nchi kubwa wao wana michezo ya kubashiri ya nchi, wanasema *Gaming Board* ya Nchi, lakini ile michezo ya kubashiri inapeleka *50 percent* kwenye Wizara ya Michezo, tunaona inaendelea. Basi nizungumzie nchi ya jirani yetu hapo Kenya, utaratibu wao wamesema mpaka 2030 watatoa bilioni 11 kwenye Wizara ya Michezo, hiyo ni kwa mwezi, lakini tazama sisi tuna bilioni 35, humo kuna mshahara wa Mwana *FA* sijui kuna mshahara wa nani, khaa! Kuna vitu vingine vinaumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna dhamira ya kuisadia hii Wizara ambayo nimeona jana Mheshimiwa Rais amesimama anatamba kwamba ana dhamira ya dhati ya kuisaidia Wizara ya Michezo, lakini leo hii sisi tunashindwa kukaa, kujadili jinsi gani Wizara ya Michezo itasonga mbele. Tuongee wazi, leo hii mimi na ujana wangu na kutembea tembea kwenye baadhi ya nchi, Wizara za Michezo zinatazamwa, lakini leo hii kwenye Bunge lako Tukufu tuongee ukweli ndio Wizara ambayo tumeipuuza, hatutaki kuisika, inadhalilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme neno langu la mwisho, nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kama sijaelezewa ile asilimia tano aliyoelekeza Mheshimiwa Rais inakuja kiasi gani mpaka amepata milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Naomba nianze kwa kumshukuru Mungu, hatimaye nitumie fursa hii kuwapongeza Wizara hii ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Balozi Pindi Chana pamoja na Naibu Waziri wake, Hamis Mohamed Mwinjuma, Mwana *FA,* bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, nataka nimrejee Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Mwasisi wa Taifa letu la Tanzania, alisema kwamba *"Nchi isiyokuwa na utamaduni wake ni sawa na Taifa lililolokufa, yaani Taifa mfu"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana ya kuyarejea haya maneno na hapo kabla sijaipongeza Timu ya Yanga. Naipongeza Timu ya Yanga kwa hatua waliyofikia pamoja na kwamba mimi sio Yanga. Mimi naipenda Timu ya Simba lakini ninaposimama kwenye jukwaa hili au kwenye Bunge lako Tukufu, nasimama

nikiamini kwamba Tanzania kwanza, ndio maana nimetumia fursa hii kuipongeza Timu yetu ya Yanga kwa hatua nzuri waliofikia, lakini Waswahili wanasema usione vinaelea bali vimeundwa. Waundaji sio wengine ni Mama shupavu, Mama hodari, Mama ambaye ana maono makubwa sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hongera sana mama kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, niongelee kuhusu utamaduni. Utamaduni ndiyo kitu kinachomtanabaisha mwanadamu, wapi alikotoka, wapi alipo na wapi anakokwenda, tamaduni ni maisha ya kila siku. Sasa kwa muktadha huo bajeti hii ambayo imepewa Wizara hii ni bajeti ndogo ndogo kupita kiasi. Hakuna chochote hapa ambacho wanaweza kufanya ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa muktadha wake ndiyo Wizara inayobeba Taifa ukiachana na Wizara nyingine. Ndiyo Wizara inayotutambulisha sisi kama Watanzania. Kuna mambo mengi na makubwa ya kufanya kwa bajeti hii wanafanya nini hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala la michezo. Michezo ni lazima tuwajenge watoto wakiwa mashuleni, hapa mashuleni kote unakokwenda hakuna viwanja vizuri vya kuchezea, hakuna wataalam ambao wanaweza wakawafundisha hao Watoto, na kule mashuleni ndiko tunakoweza kuwaibua wachezaji kama leo wakina Mayele hao ndiyo tunawaibua kule. Kama bajeti ni ya namna hii tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na hiyo kwa sababu ka muda kenyewe ni kadogo sana nataka nielezee TaSUBa. TaSUBa ni Tamasha la Utamaduni na Sanaa Bagamoyo, hapa kama ambavyo wamesema ndani ya miaka 10 bajeti haijaenda, lakini tutambue kwamba hapa ndipo wanapozalishwa vijana wenye vipaji maalum katika Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na uzalishaji huo, Mama Samia Suluhu Hassan ametangaza *Royal Tour* na

Bagamoyo ni Mji wa kihistoria katika Taifa hili na duniani kwa ujumla, duniani kote wanaijua Bagamoyo, angalia leo unakwenda kwenye Chuo cha Sanaa Bagamoyo hata ukuta hakuna! Ukuta hakuna, hivi mtu anatoka huko anakotoka anasema anaenda kukiona chuo ambacho kinawazalisha wasanii, ndiyo chuo chenyewe hiki? Hapa ni lazima tujipange, tujipange ili tuoneshe na sisi kama Taifa kuna chemchem ya kuibua hivi vipaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekuwa mdogo nilikuwa na mambo mengi ya kusema lakini sasa nitafanya nini dakika zenyewe ni dakika saba? Basi itoshe tu hayo hayo niliyoyasema yanatosha lakini nilikuwa na mambo mengi nitaandika. Nilikuwa na mambo mengi na ushauri bila kukosa kukisemea Kiswahili. Kiswahili ni lugha, ni lugha adhimu, ni lugha yenye mashiko na lugha inayowatambulisha Watanzania, chimbuko la Kiswahili ni Tanzania. Sasa nina ushauri juu ya Kiswahili hiki. Kuna Chama kinaitwa CHAUKIDU (Chama cha Ukuzaji Kiswahili Duniani). Hivi vyama hivi ni lazima Wizara kama Wizara kuna CHAUKIDU na CHALUFAKITA. Hivi Wizara ni lazima mviweke ndani ya bajeti yenu, Wanapofanya makongamano Wizara ishiriki katika kuvisaidia hivi vyama katika kukitangaza Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma Kikwete tunakushukuru sana.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri lakini cha pili nimpongeze Mheshimiwa

Rais kwa jinsi alivyoweka mguu wake asilimia 100 kwenye suala la michezo Tanzania, nina kila sababu ya kujivunia kama mdau wa michezo nchini kuona kwamba Mheshimiwa Rais ameweka asilimia 100 mguu wake kuona ana-*support* michezo nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimpongeze sana Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Michezo na kuna mambo nitakayomshauri hapa, lakini nimpongeze pia ndugu yetu Mapana kwenye BASATA. Naenda haraka kwa sababu dakika ni chache na hii inaonyesha kwamba hii Wizara pia kuna changamoto, huu muda ilitakiwa tuchangie mambo mengi sana kwa ajili ya ku-*support* Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Mapana wakati kuna siku mimi nilisimama hapa nilisema, "BASATA imegeuka kuwa mahakama ya wasanii" lakini Dkt. Mapana ameibadilisha BASATA sasa imekuwa ni sehemu ambayo wasanii wanapata haki zao. Kwa hiyo ninampongeza sana Mtendaji Mkuu wa BASATA kwa kile ambacho anakifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina hoja zangu. Kabla ya hapo pia niipongeze Yanga kwa yale ambayo wameyapata kule Algeria na ni wamefanya kitu kizuri na kwa sababu ya Yanga pia hata Simba tumeweza kuhudhuria jana kwenye mwaliko wa Mheshimiwa Rais na wanamichezo wengine, kwa hiyo, tunawapongeza. Pia niipongeze timu ambayo pia ni sehemu ya uongozi timu ya Singida *Big Stars* kwa kuingia kwenye michuano ya Shirikisho, mwakani *Big Stars* Singida tunaingia kwenye Shirikisho Barani Afrika na tuwahakikishie Watanzania tutafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya kwanza iko kwenye michezo kwenye viwanja. Mheshimiwa Waziri mwaka jana tulitenga bajeti hapa ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa viwanja. Hakuna sehemu inasomeka kwenye bajeti yenu suala la shilingi bilioni 10 popote pale halisomeki. Sasa mimi niwape tu ushauri kwa bajeti ya shilingi bilioni 35 hii hamuwezi kufanya kitu chochote, lazima mtoke *out of the box* kwenye kutafuta ni namna gani mtasaidia ujenzi wa viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fanyeni kama Zambia niliwashauri, jambo la kwanza, tunajenga mradi wa *SGR,* mradi wa *SGR* Mkandarasi yule ilitakiwa *CSR* yake tumpe kazi ya kujenga uwanja mmoja, angeweza kuwasaidia na mkaondokana na changamoto hii. Tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, *CSR* ya ujenzi wa Mwalimu Nyerere mngempa kazi ajenge bwawa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zambia walifanya hivyo kwenye *coper belt* wamejenga viwanja vyao kule kwamba *CSR* inayotokana na migodi tunajenga viwanja. Sisi kwa shilingi bilioni 35 hapa tutaendelea kupigana chenga, kwa sababu gani Mheshimiwa Waziri? Shilingi bilioni 35 itaenda kujenga nini kwenye viwanja vyetu vya nchi yetu? Nikuombe tokeni nje, tafuteni watu, tafuteni wadau waweze kuwa-*support* kujenga viwanja. Tafuteni fedha kwenye makampuni haya. Mgodi kama wa *Barrick* mwaka huu wametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mashule, Makete nimepokea karibu shilingi milioni 540. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Barrick* wapeni *task* wajenge angalau uwanja mmoja. Nendeni pale *GGM,* pale *Geita Gold* wajenge uwanja mmoja. Mimi nawapa mbinu tu za kuweza kupata fedha ili muweze kusaidia kujenga viwanja nchi hii, tofauti na hapo ni danadana tutamaliza miaka mitano kwenye Ilani tutakuwa hatujatekeleza kitu na mpango wa Mheshimiwa Rais ku-*support* michezo nchini utakuwa haujafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ni kwenye suala la *reforms.* Kuna sheria ambazo zipo ndani ya *TFF* na taratibu. Moja kati ya jambo ambalo ningetamani *TFF* na Watanzania ni suala la kwenye makato kwenye mapato ya viwanja kwa wachezaji wetu. Hizi timu zinatumia gharama kubwa sana kwenye uendeshaji. Sasa inapotokea timu imeenda kwenye mechi imecheza, yale makato ya mapato kwa maana ya *gate fee* ni lazima Serikali ione, lazima *TFF* waone jinsi gani ya kuzi-*support* timu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea tu mfano kwenye ule mchezo ambao ulipita mchezo wa *Simba Sports Club* dhidi ya Yanga ambapo kwenye mchezo wa *Simba Sports Club* dhidi ya

Yanga zilipatikana jumla ya shilingi 410,000,000 lakini Simba wameenda kuambulia shilingi 183,000,000. Angalia mgawanyo pale, kuna *VAT,* kuna gharama ya tiketi shilingi milioni 22, kuna uwanja shilingi milioni 47, kuna *FA* (Chama cha Mkoa) shilingi milioni 18, kuna Bodi ya Ligi shilingi milioni 25, kuna *TFF* shilingi milioni 12. Saidieni hivi vilabu. Mheshimiwa Waziri nikikwambia bajeti ya kuifanya klabu ikae *camp. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikikaa *camp Simba Sports Club* kwenye mchezo wa Yanga *they are spending* zaidi ya shilingi milioni 100. Sasa leo unaenda kupata zaidi ya shilingi milioni 410 kwenye mchezo wao wanaenda kupata shilingi milioni 138 tu, zaidi ya shilingi milioni 300 zimeenda kwenye mifuko ya watu wengine. Mheshimiwa Waziri mimi nimekuwepo kwenye mpira, ukienda hawa watu ambao wanapatiwa hizi fedha wana udhamini kutoka Azam. Azam anavyotoa udhamini kuna fedha inaenda Bodi ya Ligi. *NBC* anavyotoa udhamini kuna fedha zinaenda Bodi ya Ligi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wana faini kwa wachezaji kila siku unasikia sijui Morrison kafungiwa analipa shilingi milioni tatu, sijui ukisikia Simba imefanya nini, imelipa shilingi milioni tano, ukisikia sijui Yanga imefanya jambo gani inalipa shilingi milioni 10. Hawa watu *they accumulating a lot of money.* Hizi fedha zingine waweze kuvisaidia vilabu vyetu vikaendesha kwenye mambo yao ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ambalo nataka kukushauri, kwanza kukupongeza ni jinsi gani ambavyo sekta ya uigizaji Tanzania inafanya vizuri, ninakuomba Mheshimiwa Waziri BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania wanafanya jambo zuri sana, hapa nitoe *complement* yangu kwa huyu mtu anaitwa Leah Mwendamseka (Lamata) amefanya jambo moja kwenye uigizaji, anatengeneza *series,* amefanya jambo zuri sana sasa Tanzania inaenda kutambulika angalau kwenye uzalishaji wa *series* umeenda kwenye jambo zuri, anazalisha vizuri. Huyu mtu tumpongeze na tuone hata wadau wengine ambao wanafanya hii kazi ya uzalishaji kwenye Bongo *Movie* na kwenye uigizaji tuweze jinsi ya kuwa-*support. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hawa waigizaji wakienda sehemu kuigiza, vibali vya kupata vya kuigizia maeneo fulani ya Serikali inakuwa ni ngumu kupata. Tuweze kutengeneza mazingira ambayo inaweza kuwasaidia ili filamu zetu Tanzania ziweze kuzalishwa katika ubora. Kwa hiyo, ninatoa *complement* kwa Lamata kwa jinsi alivyoifanya Jua Kali na kampuni inavyofanya vizuri na kwenye nyanja za Kimataifa nadhani katika uzalishaji ameenda vizuri sana. Kwa hiyo, nipende kupongeza kwenye hilo na niombe Mheshimiwa Waziri waigizaji nchini waweze kuangaliwa kwa jicho la karibu ili mazingira yao ya kufanya kazi yawe katika ubora, hasa maeneo ya kuigizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ni jambo la shule. Mlisema mnajenga shule za michezo nchini na tunaye Leonard Tenga hapa yuko hapo juu, anajua kabisa tulikuwa na Makongo ikazalisha wachezaji wengi ambao wamekuja kulisaidia Taifa letu. Leo hii alipita hapa Waziri Bashungwa huyo hapo nyuma, alituahidi kwamba mnajenga shule, akapita Waziri Mchengerwa akaahidi anajenga shule, unakuja wewe anaahidi mnajenga shule, hamna shule iliyojengwa hata moja, shule za michezo nchini ambazo zinaenda kuzalisha *specific* kwa ajili ya kuzalisha soka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makongo ilizalisha wachezaji wengi kwenye Taifa letu. Fanyeni mchakato wa kujenga shule, hata mkianza na mbili za mfano, sisi wadau wa michezo watajisikia amani kuona kwamba mnaenda kulisaidia Taifa letu. Kwa hiyo ni vema….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kw Amuda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana muda wetu umeisha.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya pili?

**MWENYEKITI:** Ee ndiyo, unga mkono hoja muda wako umeisha Mheshimiwa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme naunga mkono hoja lakini nilikuwa na jambo kubwa sana kuhusu mfuko wa maendeleo. Wanakusanya fedha lakini hatujui ni kiasi gani kimekusanywa hadi leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Utaleta kwa maandishi.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami niongee mawili katika hii Wizara ambayo ni moja kati ya Wizara kubwa bahati mbaya sana tunaweza tusiwe tunaona ukubwa wake. Ukubwa wake hauonekani, moja katika bajeti kwa sababu bajeti ina-*signify* au bajeti inaonesha ni kwa kiwango gani watu mnachukulia *serious* Wizara husika ambayo mnaisemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni inapaswa kuwa ndiyo *definition* halisi ya sura ya nchi lakini leo na bahati mbaya sana wakati ninatafakari nikafikiria pengine Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni tunaichukulia kama Wizara ya Michezo, yaani tunai-*qualify* kwamba ni mchezo na ndiyo maana tunafanya mchezo na ndiyo maana bajeti yetu inakuja ikiwa ya mchezo mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize, hivi shilingi bilioni 35 unaweza ukafanya nini, unaongelea fedha ya maendeleo shilingi bilioni 11 imeeleza vizuri Kamati hapa unaweza ukafanya nini? Siyo hiyo tu, tumeona hata bajeti iliyokuwa imetengwa mwaka jana haijaenda kwa asilimia 100. Kwa hiyo ni vitu ambavyo moja ni vichekesho, mbili inatuonesha hata sisi tunaochangia hatuko *serious* tunafanya sanaa kama Wizara tunavyoiita ya sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema siyo sahihi? Moja, mnachopaswa kujua, michezo, utamaduni ni moja kati ya vitu ambavyo tunaweza kupata *foreign currency*. Ni maeneo ambayo nchi ikiamua kuwekeza vizuri, leo ukiitaja Marekani inajulikana Marekani kwa kucheza *rugby*. Ukitaja Marekani inaonekana kwa kucheza *basket,* ukiongelea Kenya wanajulikana kwa kukimbia kwa riadha. Leo ukiitaja India kwa mbali utasikiliza utafikiria *Bollywood*. Ukiitaja Nigeria utaongelea *Nollywood*. Sisi tunajulikana kwa lipi? Hatuwezi kukimbiza kuku, hatuwezi kukimbia, hatuwezi kufanya chochote, *is it true?* Siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vyote tunaweza kuvifanya. Tumekosa utashi wa kufanya hayo yote. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba sisi ukitutaja tunajulikana kama *Swahiliwood. (Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia taarifa unaipokea?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo mbaya hata kuwa *Swahiliwood* siyo mbaya ni lugha kama ambavyo wengine ni *Englishwood* ni *Indianwood* lakini *we have to go far,* lazima tuende mbali na hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikabidi niitafute dira, dira ipi inatuongoza kufanya kazi? Dira ipi imekuwa *instrument* ya Wizara, tena nimesoma ikawa, "Kuwa Wizara inayohakikisha ushiriki wa ushindani katika michezo, sanaa na utamaduni wa kitaifa unaolenga maendeleo ya Taifa." Nikataka niwaulize ninyi mmeisaidiaje hizi tasnia kuwa washiriki wenye ushindani?

Mmesaidiaje michezo kwa maana ya mipira kuwa kwenye ushindani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Yanga niwapongeze watani wangu Yanga mmejaribu baada ya miaka 30 ya Simba leo mmejaribu. Niwapongeze Yanga, mmeona Yanga wamewekeza wakaleta wachezaji wazuri wamepata walichokipata. Vivyo hivo kwenye michezo mingine wanasema *numbers don't lie, eh?* Ukiwekeza unapata matokeo, wamewekeza wamepata matokeo. Tunataka tupate matokeo gani kwenye Wizara ya Sanaa na Michezo tukiwa tumewekeza shilingi bilioni 35? Tukiweka hela ya maendeleo ambayo ni shilingi bilioni 11 kwenye bajeti amesema hapa msemaji anasema *out of 15 trillion* ya fedha za maendeleo, sisi tumeweka shilingi bilioni ngapi, bilioni 11 ambayo ni 0.08 kwenye fedha za maendeleo. Hivi tunataka maajabu kutoka nchi gani tuweze kufanikisha hii sera? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini ninasisitiza umuhimu wa Wizara hii? Moja ni *source* kubwa ya kupata ajira. Mbili; ni *source* kubwa ya kupata fedha za kigeni. Tatu; ni *source* kubwa ya kusaidia hata vipato vya kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mchango wa Wizara hii katika Pato la Taifa ni 0.03! Siyo sawa, tunaweza kufanya vizuri kama tukiamua. Mimi ningekutana na Mheshimiwa Rais kama ananisikia ni lazima tufanye *overhaul.* Yaani tufanye *a total transformation.* Moja; jinsi ambavyo tunaitafsiri michezo katika hii nchi. Hatuwezi kuchukulia michezo kama kitu eti tunataka kufurahisha watu, tumeshaenda zaidi ya kufurahisha watu, tunataka kupata fedha, kupata utajiri kutoka kwenye vipaji vyetu. Kwa hiyo, nitamshauri Mheshimiwa Rais afanye *transformation.* Pia hii Wizara aipe uzito kama zilivyo Wizara nyingi na kubwa katika nchi hii. Yaani ukiacha Wizara ambayo tunaiona ni kubwa, ya pili inapaswa kuwa Wizara ya Michezo, Utamaduni na Sanaa kwa sababu ya umuhimu na ukubwa wake kugusa watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikaje hapo. Moja; ni lazima turudi sasa kwenye tulivyoanza miaka ile, tufungue vyuo mbalimbali vya michezo. Tu-*train* walimu wa kutosha wa michezo.

Ni lazima tu-*recruit*. Serikali ina maana ni vitu viwili; sera na uwekezaji wa Serikali. Kama sera yetu ikijikita ikaendana sambamba na uwekezaji wa Serikali tutafika tunakokutaka na hapo tunakuja kuongelea mambo ya *scouting*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna vipaji kadha wa kadha mitaani. Nitatoa mfano Mheshimiwa Waziri. Kuna baadhi ya vijana niliwatoa Kyerwa kuja kuwasaidia kwenye *academy* mbalimbali kwenye hii nchi. Nataka nikwaambie nimehangaika hata kuwatafutia timu za ku-*train* mpaka nimechoka. Yaani huwezi hata kupata timu hata kama kijana ana uwezo wa kiasi gani wa kucheza mpira, kupata hata timu ya kuchezea ni changamoto kubwa sana, na hao ni watu ambao *at least* wanamjua Mbunge, vipi wale ambao hawana hata wa kuwashika mkono? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, walimu uwaandaliwe wa kutosha kwenye vyuo, lakini hivyo vyuo kuna baadhi ya *academy* leo zina-*train* michezo. Moja; zipewe ruzuku kidogo lakini zipunguziwe gharama ili ziweze kuwekeza zaidi katika ku-*spot* na kutengeneza walimu na wanamichezo vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Lazima tutafute *partnership*. Bahati nzuri wanamichezo tulipata ridhaa ya kwenda *Southern Sudan*. Tuliona *Southern Sudan* wanajiandaaje kushika dunia ya michezo. Kila ulikoenda wamefungua *academy* za *basketball,* za *football,* za *netball,* sisi tunafanya nini hapa? Viwanja vya michezo vilivyokuwepo kwenye maeneo yetu leo vyote vimevamiwa. Maeneo ya wazi yote leo watu wameyafanya mabaa, watu wamejenga na hakuna anayeongelea tena na Wizara hapa sijaona inaelezeaje tunawezaje ku-*promote* michezo bila kuwa na viwanja vya michezo hususan mpira wa miguu naongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuna safari ya kwenda, tuna safari ya kwenda kabla ya kujua tunafikaje kule na hiyo inaanza na *total transformation* na hiyo inaanza na kubadilisha *mindset* na hiyo inaanza na *political will* ambayo sasa hiyo ni bajeti ya Serikali. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa sababu ya muda naomba niende moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nataka nirejee watu wawili muhimu sana. Kwanza ni Mwalimu wangu marehemu Mheshimiwa Dkt. Agustino Mahiga pale *National Defense College* pia na *American Political Scientist* Joseph Nye. Hawa watu wawili walizungumza jambo moja kubwa sana. Ukitaka nchi iwe na usalama na amani lazima mambo mawili makuu uweze kuyasimamia. Moja ni *hard power* lakini jingine *soft power*. Walimaanisha nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *hard power* walimaanisha Majeshi lakini kwenye *soft power* walikuwa wanamaanisha *cultural values* (tuna maanisha sanaa, utamaduni na michezo) kila kitu. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha dhahiri kwamba sasa anahitaji ku-*promote* eneo hili la *soft power* (nguvu laini) eneo la michezo na sisi tumejionea tangu mashindano yameanza Mheshimiwa Rais ameonesha uwezo mkubwa sana, lakini mpaka juzi anaamua ndege isafiri kwenda Algeria zaidi ya shilingi milioni 200 zimegharamia ndege ile kwenda, ameonesha dhahiri kwamba anahitaji eneo hili la *soft power,* eneo hili ambalo linagusa jamii kwa ukubwa wake liweze kuwa *promoted*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ninayoiona hapa nikirudi kwenye bajeti, wamesema Kamati na wachangiaji wengine, inasikitisha sana; fedha za maendeleo ambazo ndiyo tunatarajia Wizara hii ifanye vizuri, mwaka 2022 tulitenga Shilingi bilioni 15, mwaka huu tunatenga Shilingi bilioni 11. Sababu gani ya msingi iliyotumika kupunguza fedha hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nataka niwaombe sana wenzetu wa Wizara ya Fedha, hili jambo walifanyie kazi.

Haiwezekani Wizara hii ambayo tunaitegemea iweze kutengeneza mazingira mazuri kwa Watanzania. Ameeleza vizuri hapo Mheshimiwa Anatropia kwamba sasa inatoa ajira na inafanya kila jambo, lakini hebu mathalani tufanye tu kwamba hakuna sanaa, hakuna michezo, hakuna maigizo hakuna chochote nchini. Nchi haiwezi kutawalika. Ndiyo maana tunazungumza kwamba Wizara hii ndiyo *soft power* ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wewe ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na ndio Mwenyekiti wa leo kwenye kiti hiki. Unayo mamlaka ya kuagiza kwenda kufanya *supplementary budget* ili turudi hapa. Maana yake kwenye bajeti kuu fedha iwe imeongezwa. Hatuwezi tukawa tunazungumza habari hii ambayo siyo nzuri kutafsirika kwa Watanzania kwamba Wizara muhimu kama hii imepunguziwa bajeti. Tutashindwa kutoa maelezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili muhimu sana. Tumezungumza hapa kuhusu *sport betting*. Tumetunga sheria wenyewe, inatengwa 5% kwenye makusanyo hayo ya michezo ya kubashiri. 5% inakwenda Wizarani kwa maana ya Baraza la Michezo Tanzania. Hii 5% haiendi kwa wakati. Siyo tu kwenda kwa wakati, haijulikani. Hata kiwango kile ambacho kinapatikana, kinachopelekwa kule hakijulikani. Maana yake nini? Hapa tunaleta changamoto. Nami nitakwenda baadaye kushauri vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa tunaowapa 5%, hata kuandaa mpango kazi wa hiyo 5% wanashindwa, kwa sababu hawana uhakika na hiyo fedha inakuja wakati gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri, nawaomba *TCRA* tuweke jambo hili wazi, kwa nini lijifiche? *TCRA* watoe *link* kwa Baraza la Michezo Tanzania wawe wanaona kila kinachoingia ili wajue 5% yao ni kiasi gani, waweze kupanga mpango ambao sisi Wabunge tunaweza kujadili, kwa nini tumeshindwa kutekeleza hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michezo hii ya kubahatisha, jambo moja muhimu sana ni suala la maadili. Hayuko mtu huku chini; sasa hivi kila nyumba mtu anaweza kwenda kuweka mashine, watu wakaamua kucheza kwenye nyumba za watu, watoto wadogo, kila mtu. Nani ana jukumu la kusimamia maadili kwenye eneo hili la michezo ya kubahatisha? Tunatengeneza Taifa la namna gani hapo kesho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ni muhimu sana kwenye eneo la maadili. Fedha hii 5% ipelekwe kule ili pia waweke mpango wao wa kuweza kuhakikisha kwamba suala la maadili tuwashirikishe na Wizara ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie uwanja wa Taifa. Mheshimiwa Waziri aliunda Tume, nami nataka nimwambie, Tume haikuwa na haja. Jambo lile liko wazi, hatuitaji kuunda Tume. Tume inaenda kufanya *compromise*. Watatuletea majibu ambayo tunayajua. Tangu Uwanja wa Mkapa umejengwa haujawahi kufanyiwa marekebisho, haujawahi kufanyiwa chochote na hatujawahi kutengeneza bajeti hapa kuweka fedha ambayo inaenda kuhakikisha kwamba tunakarabati Uwanja wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wetu tumeujenga zaidi ya miaka 15 lakini hakuna ukarabati, wala huhitaji *mechanism* hapa. Suala la umeme kukatika litegemee, suala la maji kutokuwepo litegemee, na wala hatuwezi kuja kuwabana Mawaziri hapa kwa sababu hatujatenga bajeti. Ninatachotaka kushauri hapo, jambo la kwanza, wala hatuhitaji Tume hapa. Serikali itenge bajeti kila mwaka kwa ajili ya Uwanja wa Benjamini Mkapa na ndiyo uwanja tunaoutegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunao wadau ambao wamewekeza kwenye michezo. Wako *AZAM, NBC, AIRTEL* na wengine wote. Wadau hao wote waitwe washirikishwe. Tunapata aibu kwa pamoja, nao wameweka mabango yao pale. Kwa sababu umeme ukizimika, mabango hayawezi kuwaka. Hao pia waitwe washirikishwe ili kuhakikisha kwamba uwanja huu haturudi huku tulikotoka. Hii adha kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nilichangie muhimu sana, Serikali inatenga maeneo. Huko kwenye Mipango Miji, Halmashauri zetu zinatenga maeneo ya viwanja. Sasa maeneo ya viwanja yanaitwa maeneo wazi. Viwanja vinaitwa maeneo ya wazi. Hapa nataka wakitenga viwanja washirikishe wenzetu wa *TFF,* ndio wanaojua *standard* ya viwanja inatakiwa iweje? Nawapongeza sana *TFF,* wamekuwa na mstari wa mbele kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie eneo moja muhimu sana. Nawashukuru sana Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, nawapongeza sana *Dar Young African,* wameleta heshima kwenye nchi hii. Nawapongeza *TFF,* nawapongeza sana kwa kazi kubwa waliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami niendelee na kuwapongeza Wizara Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza sekta zote zinazohusiana na Wizara yao. Pia napenda kukushukuru Mheshimiwa Waziri, kwani kwetu kule Zanzibar anajitahidi sana kuweka ushirikiano wa pamoja na kutoa msukumo katika mazingira yote ya utamaduni na kuhakikisha yanakwenda sambamba na Tanzania Bara. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, aendelee na juhudi zake hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda inabidi moja kwa moja nichague moja la kusema hapa. Najielekeza kwenye lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswali ni ajira, lugha ya Kiswahili ni rasilimali na pia lugha ya Kiswahili inaitangaza Tanzania katika Sekta ya Utalii. Kuna utalii sasa unafanyika kupitia lugha ya Kiswahili, kwamba watalii wanakuja kusikia hiyo lugha ya Kiswahili, kuona nchi yenyewe ambayo imeanzisha Kiswahili na kuona utamaduni wa Mswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye hiyo hiyo lugha ya Kiswahili; ili kukamata soko la ajira ni lazima Wizara hii iongezewe fungu la fedha katika kuwaandaa vijana wetu kwa soko la ajira la ukalimani na ualimu, kwa maana ya kwamba tuwaongezee uwezo na idadi ya lugha ambazo ataweza kwenda kutafsiri na kufanya ukalimani, isiwe tu Kiswahili na Kiingereza, bali na lugha nyingine za kigeni wawe wanazimudu ili kudhibiti hili soko la ajira lisije likachukuliwa na mataifa mengine ambao sasa hivi wao ndio wanajifunza Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili chetu kinajulikana Afrika, kinajulikana duniani sasa hivi na kinaipaisha Tanzania, lakini tukiimarishe Kiswahili chetu kiwe imara. Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha mbalimbali duniani; Kiarabu, Kiingereza, Kiajemi na lugha nyingine. Kwa maana hiyo, Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha. Neno lenyewe Swahili, linatokana na neno la Kiarabu, kwamba ni pwani, pwani. Pia Waturuki wanatumia neno hilo hilo swahil kwa maana ya pwani. Kwa hiyo, ni lugha ya Pwani na utamaduni wa pwani ukaenea duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 nilisema na leo narudia tena kwa uchache tu. Kuna maneno tunayatumia ambayo yameungana; Kiswahili, Kiarabu, Kiingereza, mfano taabani, kanuni, madrasa, dhuluma, Askari, barafu; haya ni Kihindi, Kiarabu na Kiswahili tunayatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikwambie sasa, bendera na safari ni neno la Kihispania; vurumai ni neno la Kigiriki, tunalitumia; pashiani, reshani Kijerumani kuna hela, kuna zahanati. Hapa natoa mfano mdogo tu tuone. Hoja yangu ni kwamba tunapotunga haya maneno ya Kiswahili tutumie maneno rahisi na mepesi kama lugha yenyewe, isiwe sasa hivi Kiswahili ni kigumu. Kimekuwa kigumu sana na hapo wanapokaa kuyatunga haya maneno, ushirikishwaji unakuwaje kwa pande zote mbili; Baraza la Sanaa, Baraza la Kiswahili la Taifa na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKITA na BAKIZA)? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki sasa hivi kimemaliza muda, naishauri Serikali itapokiunda, iangalie upya muundo wake kama unakidhi vigezo vya sasa na kuitangaza Kiswahili duniani?

Kama haukidhi, tufanye marekebisho, tutafute Waswahili wabobezi ambao wapo, waingie kwenye hizi sekta waweke sawa Kiswahili chetu ili kiendane na hadhi na ubora unaotakiwa, kuliko kujaza tu maneno hata hayaeleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshatoa mfano kwamba Kiswahili ni mchanganyiko wa maneno. Lugha nyingi zinategemeana kwenye maneno mbalimbali yenyewe huko kwenye Kijerumani, Kifaransa, Kigiriki na Kitaliano, yanaingiliana siyo kwenye lugha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, nataka nitoe mfano mdogo kwa watu ambao wamekineemesha Kiswahili, wamekitangaza Kiswahili duniani na kukistawisha. Nina wengi, lakini kwa uchache tu, napenda kumtaja Prof. Mohamed na Dkt. Abdallah, hawa walikuwa walimu katika Vyuo Vikuu vya Uganda na Kenya ambao wanafunzi wao sasa wameshalikamata soko la Ghana na Nigeria, wanasomesha huko Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya utangazaji kuna watu wamekichangia Kiswahili tangu miaka ya 50 na 60 nchi mbalimbali. Mfano, Watangazaji kuanzia miaka ya 1950, kuna Bwana Ahmed Rashid Ally, Sauti ya Afrika, Sauti ya Ukombozi, Cairo; kuna Maimuna Fassy, sauti ya Marekani; Abdulrahim Kaktan, *Radio Deutsche* Welle; Abdala Mbamba, sauti ya *America*; Ahmed Rajab *BBC* na wengine *Radio* Moscow Abdul Wahidah Hassan Shehe. Tukiendelea, *Radio* Japan, Rahman Mohamed Dahman, ambaye alitokea *Radio* Deutsche Welle; Umul Kheir; hao ni wengi na baadhi tu akiwemo Bw. Ramadhani Ally ambaye alitangaza Idhaa ya Kiswahili Czechoslovakia Idhaa ya *Prague*, pia alitangaza Berlin na baadaye *Radio Deutsche* Welle, mpaka akastaafu. Mwingine *Radio* Beijing, Miraji Mpatani, Haroub Othman; tukiendelea, kuna na wengi Radio China. Naomba tuwaenzi, tuwatambue. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, mwisho niseme hivi, neno la Tanzania lina nuru na linapaa duniani. Aliyetunga jina la Tanzania alikuwa ni mwanafunzi kwa wakati huo, ametumia kipaji chake na uwezo wake. Kama ingewapendeza, miaka 60 ya Muungano, Jamhuri ya Tanzania akaletwa huyu mtu tukamwona na Taifa

likamtambua kutokana na jambo zuri aliyotufanyia Taifa letu, Tanzania inapaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kutokana muda ulioko mbele yetu kwa mujibu wa Kanuni ya 34 (2), naongeza muda ili tumalize shughuli iliyo mbele yetu. Haya Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nitakuwa na sehemu kama tatu. Kwanza, pongezi; pili, nitazungumzia Baraza la Kiswahili la Taifa; na tatu, soka letu na nne, nitazungumzia uingiaji salama katika Uwanja wa Taifa na mwisho utawala bora katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameongeza hamasa katika michezo. Zile shilingi milioni tano, tano alizokuwa anazitoa kwa magoli yanayofungwa kwenye *club* bingwa na kwenye shirikisho, imeleta heshima sana na ikaleta hamasa kubwa sana. Kwa hiyo, tunampongeza sana na tunapongeza vilabu vyote ambavyo vimeshiriki kimataifa, Simba pamoja na Yanga ambao walituheshimisha kwa kufika fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza utajielekeza kwenye Baraza la Kiswahili la Taifa. Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza sana. Tumesema kwamba tutafanya Kiswahili kuwa bidhaa na watu wengi wanadhani kwamba ukijua tu Kiswahili kama hivi ambavyo tunaongea, basi unaweza ukawa Mwalimu wa Kiswahili au mkalimani. Kumbe sivyo, lazima ujifunze Kiswahili kama lugha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka pia kukifanya Kiswahili bidhaa kwa maana ya kwamba kikafundishwe huko nje, lazima pia tujifunze na lugha za mataifa mengine. Kwa hiyo,

nawapongeza sana BAKITA, wana kitabu hapa *English,* Kiswahili na *Portuguese* cha mtu ambaye anajifunza Kiswahili ambaye ni Mreno. Sasa ili aweze kufundishika vizuri, ndani yake pia kuna sehemu ya Kiingereza. Pia wamekuja na Mwongozo wa Taifa wa Ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni hatua ya awali, kati na juu. Hii kweli wanathibitisha kwamba BAKITA wapo kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, wana kitabu kinaitwa furahia Kiswahili, Kiswahili kwa wageni. Kwa hiyo, tunaona jitihada ambazo BAKITA wanazifanya katika kuhakikisha kwamba Kiswahili kweli kinakuwa ni bidhaa kama ambavyo tumesema. Sasa nami nitoe wito kwa Wizara ya Elimu na Vyuo Vyetu Vikuu, navyo viwekeze nguvu katika kufundisha siyo tu Kiswahili, lakini kufundisha Kiswahili kama lugha ambayo baadaye inakuwa bidhaa, kufundisha wakalimani wa kutosha, na kufundisha katika namna ile ambayo kweli watu watapata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tulisikia *South Africa* wanataka walimu 1,000 lakini huwezi kwenda *South Africa* kufundisha Kiswahili kwa sababu tu unajua Kiswahili, lazima ujue Kiswahili kama lugha, lazima ujue Kiingereza, lakini ikibidi lazima ujue lugha za wenyeji wa maeneo yale. Kwa hiyo, nawapongeza sana BAKITA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilisema kwamba suala la pili nitazungumzia kuhusu soka letu. Katika timu nne ambazo zimeingia fainali ya shirikirikisho na fainali ya *club* bingwa Afrika, *Al Ahly* wao katika timu yao *first eleven* walikuwa wana wachezaji wa kigeni watatu tu. Wale Wydad ambao waliwatoa Simba walikuwa na wachezaji wawili tu. Hawa *USM* Alger, walikuwa na wachezaji wawili tu. Yanga walikuwa na wachezaji wazawa sita. Maana yake ni nini? Hatusemi kwamba vilabu visiwe na wachezaji wa kigeni, lakini hii ni kwa sababu hatuwekezi kwenye soka la vijana kuanzia *under seventeen, under twenty, under twenty-three. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ushiriki *World Cup au Afcon* kila mwaka, uwe na uhakika, ni lazima tuwekeze kwenye soka la vijana. Hapa kuna mambo mawili; kuna Serikali na wadau. Kwa

hiyo, Serikali wajibu wake: moja, kujenga miundombinu ya viwanja; pili, kupitia sera za kikodi kuhakikisha kwamba tunapunguza kodi katika vifaa vya michezo. Leo hii ukimpeleka mtoto kama pale *Fountain Gate* au *Magnet* au Kambiyaso, ile *kit* yake tu, kwamba vifaa kwa maana ya viatu, soksi, jezi na mpira wa kuchezea, *minimum* labda unazungumzia Shilingi laki moja na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuweze kuwa na Timu ya Taifa itakayokuwa shindani, lazima tuwe na wachezaji wazawa wa kutosha, lakini ili tuwe na wazawa wa kutosha, lazima tuwekeze kuanzia hiyo *under seventeen* na kuendelea. Kwa hiyo, hilo nimeona niliseme vizuri. Kwa hiyo, kuna wajibu wa Serikali na wajibu wa wadau. *(Makofi)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo ni muhimu niliseme ni kuhusu uingiajia wa pale uwanjani. Mmeona juzi tunatoa pole kwa ile familia, lakini lazima tufike wakati tujifunze wakati wa mechi kubwa *management* ya namna ya kuingia uwanjani iwe ni salama. Haiwezekani mechi inachezwa saa 10.00, unatakiwa uende uwanjani saa 12.00 asubuhi. Tuwekeni utaratibu mwema wa jinsi ya kuingia pale uwanjani.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kapinga.

**TAARIFA**

**MHE. BENAYE L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji juu ya uingiaji salama katika Uwanja wetu wa Taifa. Kwa utaratibu wa uwanja ule, una mageti, lakini kwa bahati mbaya sana utaratibu uliozoeleka, mageti yanayofunguliwa ni matatu tu; lile la Simba, lile la Yanga, na lile kubwa, lakini uwanja ule wote umezungukwa na mageti, lakini sasa wananchi wanasongamana kiasi kwamba wanasababisha ile hali inayotokea pale na mauaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa sababu inaboresha namna ya kuingia katika uwanja na kwa usalama na kwenda uwanjani isiwe kama kero, isiwe kama adha. Maana yake tunasema kuna kitu Mheshimiwa Jesca huwa anasema afya ya akili. Michezo na burudani ni mojawapo ya tiba nzuri sana ya hiyo mnayoita afya ya akili. Kwa hiyo, mtu kwenda uwanjani ni kutaka kupata *entertainment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema lingine nitazungumzia utawala bora katika soka. Nilisema mwaka 2022, Chama cha Mpira cha Wanawake mpaka leo hawajafanya uchaguzi. Walipofanya uchaguzi, ulivurigika, walisema kwamba wapigakura wamekuwa wengi, wakasema watafanya baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri, wewe kama mama kwa kukosekana ule uchaguzi maana yake tunakosa uwakilishi wa wanawake kwenye Kamati ya Utendaji wa *TFF*. Kwa hiyo, nawaomba Baraza la Michezo, Msajili wa Vyama za Michezo na Wizara kwa ujumla, jambo hili ni muhimu. Kama tunazungumzia kunyanyua wanawake, na timu zetu za wanawake zinafanya vizuri, tufanye uchaguzi wa chama cha soka cha wanawake hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, ajiandae.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii kuchangia katika Wizara hii ambayo na-*declare interest* kwamba nahusika, mimi ni mdau mkubwa wa hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu katika Wizara ambayo anaonyesha mapenzi ya dhati kabisa, kuwapenda kabisa ni Wizara hii. Ndiyo

maana sasa hivi naona hamasa kubwa katika hii Wizara, tayari ameishaonesha dira kabisa kwamba hii Wizara ni watoto wangu, wanahitaji kulelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tayari Mheshimiwa Rais ameshaonesha dhamira ya dhati katika Wizara hii, Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge waanze kuangalia Wizara hii kwa mnajili mpya kabisa, tukianzia hasa kwenye masuala ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri. Kusema kweli, mimi ni kati ya watu ambao nilishangaa kumwona Bakhresa amekuja kwenye hii Wizara, Mama ana jicho la mbali sana, lakini naanza kuona sasa namna gani umeanza ku-*cope* vizuri na wanasanii na wanamichezo. Tayari tunaanza sasa kuona siku ile kwenye Tuzo tulikuwa tunacheza sana pale, tunaanza kuona sasa Wizara imempata mtu ambaye anaweza akaifanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze Mheshimiwa Rais pia kwa kumchagua kaka yangu Kipenzi Mheshimiwa Hamis Mwinjuma tayari huyu ambaye ana-*idea* anajua kabisa, anajua shida na chnagamoto za Wizara hii naamini kabisa kwa sababu yeye ni mwanamichezo lakini pia ni mwanamuziki ataenda kuleta ukombozi katika wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la bajeti. Kwa kuangalia zamani wakati nasoma tulifundishwa *basic needs* katika maisha na wakawa wanasema kwamba malazi, mavazi, usafiri ikawa ni kitu kama *luxury* sasa hivi usafiri siyo *luxury* tena ni lazima. Leo hii katika hii wizara tunaangalia kama *entertainment* kwamba hii Wizara ni kwa ajili ya *entertainment* hapana siyo kweli. Hii Wizara inaenda kuwa mkombozi mkubwa wa kupunguza ajira katika nchi hii. Kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ikiweka mikakati mizuri kama ambavyo alivyoweka mikakati kaka yangu Bashe katika *BBT*. Hii Wizara italeta heshima ya kupata bajeti kubwa sana na kuweza kuendeleza Wizara hii katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niambie Waheshimiwa Mawaziri hao wawili ambao tayari wamepewa dhamna katika wizara hii muhimu sana katika nchi yetu waangalie namna gani ya kuja kuwa–*convince* wabunge hawa waangalie mikakati gani waipange katika nchi hii, ili iweze kuondoa hii *isuue* ya bajeti. Leo hii bilioni 35 ni bajeti ndogo sana, ni bajeti ya aibu najisikia vibaya kwa sababu hii wizara ambayo inanihusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Rais Wizara hii imeweza kutoa mikopo kwa badhi ya wasanii mnaweza kuona namna gani Mheshimiwa Rais anaipenda hii wizara, lakini leo hii Wizara ina bajeti ya bilioni 35, nazungumza hapa wasanii wakiwepo pale, nazungumza hapa wanamichezo wako humu ndani bilioni 35 inaenda kusaidia kitu gani katika hii Wizara? Tuangalie namna nyingine ya kufanya uwekezaji katika Wizara hii ili iweze kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine Mheshimiwa Waziri mimi ni mmoja ya watu ambao tulikuja kwenye tuzo za wanamuziki pale the *The Dom* Masaki. Mheshimiwa Waziri na Wizara yako naomba niwapongeze sana mwaka jana hii shughuli imeanza na sasa hivi mwaka huu mmefanya kazi nzuri sana, lakini naomba niulize au niwaambie ni namna gani ya kufanya kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri umewaandalia wasanii tuzo. Wasanii hawa ambao wameandaliwa tuzo. Tuzo zinatangazwa pale kwa ajili ya wasanii kupewa tuzo hawapo na wengine hawajaandaa hata wapokeaji wa tuzo hizi sasa unajiuliza ni kwamba *lack of coordination* ama ni shida iko wapi? Je, wasanii hawajazipokea hizi tuzo ama Mheshimiwa Waziri na jopo lako hamjaweza kuzitangaza hizi tuzo vizuri au kuwapa tarehe nzuri ya kujua tuzo ni tarehe fulani na wasanii wote wanapaswa kuwepo. Mimi sijawahi kuona huko nje kina Beyonce wakakosa kwenye tuzo, sijawahi kuona kina Rihanna wakakosa kwenye tuzo, kwa sababu ndiyo sehemu pekee ya kuonesha *appreciation* ya kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unaenda pale unakuta nusu ya wasanii ambao wanaenda kupewa tuzo hawapo hii inaondoa hamasa na Ladha ya tuzo zetu za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tafuta namna ya kukaa na wasanii wako. Wasanii ni wasikivu na wanakuheshimu, wanaheshimu Serikali ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan. Fanya warsha mbalimbali, fanya semina mbalimbali, waelimishe mambo ambayo unataka kuwafanyia, waoneshe njia waoneshe upendo. Nina uhakika hao wasanii wako watakuwa wanashiriki kila tukio ambalo wewe na Wizara yako inaandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi nilijisikia vibaya naona hadi wasanii ambao juzi tu wametoka eti na yeye hayupo. Ukiuliza yuko wapi? hujui. Yaani haijulikani yuko wapi nasema sasa hii tuzo ameandaliwa nani? Kama siyo wasanii. Kwa hiyo, tuangalie *either* kama shida iko kwa wasanii basi zungumzeni nao, lakini kama shida iko kwene menejimenti ya Wizara basi fuatilieni hili jambo mjue namna gani ya kuweza Kwenda kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nataka nizungumze kuhusu mmomonyoko wa madili. Naisema huku kwa sababu wizara hii au tasnia hii ni sehemu mojawapo ya mmomonyoko wa maadli katika Tanzania yetu. Nasema hivi kwa sababu nimetokea huko nafahamu vizuri jinsi gani mtu anaona kwa namna moja au nyingine kwamba ili mimi niwe msanii lazima nivute bangi, ili niwe msanii lazima ninywe madawa ya kulevya, ili niwe msanii lazima ninywe pombe, ili niwe msanii lazima nicheze uchi yaani kuna vitu vingi sana katika wizara hii ambavyo Mheshimiwa Waziri kwa weledi wako, kwa muonekano wako, kwa namna yako na uzoefu wako utawaweza Kwenda kuvifanyia kazi, ili hii wizara au hivi vipaji wazazi huko nyumbani waweze kuruhusu watoto wao kutaka kuwa wasanii tulinde utamaduni wetu. Tulinde asili yetu tulinde utanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utamaduni unaweza ukaona sasa hivi dunia ilivyo badilika masuala ya utandawazi mambo yamebadilika. Watu tumepita kwenye

*phases* za kubadilisha nywele, *phases* za kuweka kope za kujichubua…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** …lakini sasa hivi kuna *phases* ambayo ni mbaya sana ya kubadilisha maumbile.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Tunabadilisha maumbile yetu leo hii huyu mtu mwembamba hana *shape* lo hii kesho kutwa unamuona ana *shape* kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako…

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Kwa hiyo naamini hii Wizara ya kuelimisha vijana wetu, watu wetu…

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha Mheshimiwa Khadija, ahsante sana.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa hii lakini Serikali iangalie namna gani ya kusaidia vizazi vyetu Tanzania inaenda kunagamia kwa namna hii. Ahsante sana nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija tunashukuru sana**.** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii, na mimi naomba moja kwa moja nianze kwa kuunga mkono hotuba hii na niwashauri Waheshimiwa Wabunge tuipitishe hii bajeti bila ya ukakasi lakini bajeti hii lazima iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kwenda katika mchango wangu rasmi ningempongeza kwanza Mheshimiwa Rais ana maono mazuri sana, ana ndoto nzuri sana ametueleza jana wakati tulivyokuwa katika hafla ile ya kuipongeza klabu kubwa kabisa yenye historia kubwa katika nchi hii klabu ya Yanga ambayo imeshakuwa mabingwa sasa mara 29 wanakwenda kutawazwa leo jioni hii kuwa mabingwa wa 29 katika *Premier League*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amejipambanua kutaka masuala ya michezo utamaduni, yaweze kupewa kipaumbele stahiki na ameona kwa kupitia *sports diplomacy* kwamba kumbe Tanzania inaweza ikapata *recognition* ikatambuliwa nchi za nje kupitia michezo na nimefurahi sana tuliupokuwa kule Algiers Mheshimiwa Waziri alipata nafasi ya kuweza kukutana na wenzake wa pale Algiers, Algeria Mawaziri wenzake kuizungumzia habari ya Tanzania na michezo. Vilevile nimeona *seriousness* ya Serikali katika kupeleka mawaziri wawili, Waziri wa Serikali ya Muungano lakini Waziri Mwita kutoka Zanzibar. Hii inaonesha kabisa dhamira ya Mheshimiwa Rais kupeleka nguvu ya kutosha katika michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuchukizwa na jambo la kupeleka bajeti ndogo. Mwaka jana tumepeleka billion 35.4, mwaka huu tunaomba tena 35.4 haya maono ya Rais yatafikiwa vipi? Ndoto ya Rais inafikiwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi hata siku moja na hata ukiangalia dhima ya Wizara. Dhima ya Wizara ni kukuza kuwezesha na kuendeleza utambulisho wa Taifa, maadili ya kiutamaduni, sanaa na michezo na wenyewe wakasema kabisa ili wafikie malengo haya lazima wawafikie wadau wafanye mageuzi kwenye taasisi wafanye utawala bora na uendelezaji wa miundombinu ya michezo huwezi ukafanya mambo hayo kwa bajeti hii tutakuwa tunataniana humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wengi waliozungumza kuhusu bajeti, lakini vile vile kamati imesisitiza suala la bajeti. Sasa kwa nini sasa Bunge lako hili lisiichukue hoja hii kama hoja mahususi ikapelekwa mbele ya Kamati ya bajeti ili

Kamati ya bajeti itakapofanya majumuisho na kujadiliana na Serikali suala la kuongeza bajeti likawa ni moja kati ya mambo yaliyoibuliwa kutokana na mijadala hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba kwa kuwa michezo ya kubahatisha kwa sehemu kubwa sana inategemea *sports*, inategemea michezo. Iwe kwenye *betting* ama kwenye *casino* au michezo mingine kutokana na hili nataka nikupe *figures* hadi Mei 2023 hadi Mwezi uliopita, Serikali imekusanya bilioni 146.9 na imevuka malengo ya kukusanya bilioni 131.5 sasa kwa fedha zote hizi zinatokana na *sports* unapelekaje 35.4? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hayo mambo hayaendi na kwa hali hiyo, napendekeza suala la michezo ya kubahatisha iwe chini ya Wizara ya Michezo nafikiri ni suala muafaka. Yawezekana tumechelewa lakini Serikali ilichukue suala hili, michezo hii ipelekwe chini ya Wizara ili fedha zote hizi zipelekwe kwenye michezo. Huwezi kuwa na kitu kinachozalisha bilioni 146na hadi Juni watafika hawa bilioni 170 halafu ukawape bilioni 35 ni mzaha. Hata Rais ndoto zake hazitaweza kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine. *Sports betting* inategemea sana mpira wa miguu sana. Hapa Tanzania 90% ya wanaocheza *betting* wana *bet* katika michezo ya mpira wa miguu hivyo *industry* ile inafaidika na mpira wa miguu. Tunarudisha nini na kwa hali hii nilikuwa nashauri Serikali ichukueni hili suala kwamba iwe ni sharti la kikanuni ya kupata leseni kwamba Kampuni ya *Betting* ili ipate leseni ilazimike kudhamini *premier league clubs* ama *championship club* hapo tutakwenda kusaidia nchi yetu katika michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili hatuna budi kupongeza zile kampuni ambazo zimejitokeza sasa hivi, kuweza kudhamini *clubs* zetu mbalimbali naomba nizitaje chache tu. *M-Bet* wanaidhamini *club* moja iko hapa Msimbazi inaitwa nini? Simba, kuna kampuni inaitwa *Meridian* wanadhamini timu ya *KMC*, kuna Kampuni ya *Ten Bet* inadhamini Dodoma Jiji. Lakini bingwa wao *Sports* Pesa wanadhamini *Young Africans,* wanadhamini Namungo, wanadhamini Singida *Big Stars*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa lakini Wizara toeni *recognition* kwa hawa watu ambao wanafanya vizuri ku-*sponsor* michezo yetu nchini. Naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara hii. Kwa sababu ya muda mfupi naomba kuungana na wenzangu wote waliochnagia kuhusu bajeti ya Wizara hii, kwa sababu haswa ndio kilichofanya nisimame kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunathamini maana saa nyingine tunasema hii Wizara ipo kwa bahati mbaya au kwa kitu gani? Michezo, Sanaa na utamaduni ni jambo mtambuka inayowagusa kuanzia watoto wa miaka miwili, mitatu, ukiona wale watoto wadogo mpaka wana-*act* namna gani, Mayele anafunga goli na wengine wana-*act* kama Joti anavyotembea ina maana wame wa-*inspire* watoto toka wakiwa wadogo, lakini mpaka wazazi mpaka wazee huku tunashabikia michezo, tunafatilia tamthiliya ili tupate amani, lakini ukiangalia bajeti inayotengwa kwenye Wizara hii kwa kweli inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemei bajeti kuu ya bilioni 35, naangaliaga bajeti ya maendeleo kwa sababu Serikali kama imeajiri watendaji sehemu ya mishahara ikaenda kama mishahara zingine kama *oc* zinaenda akama *oc*. Lakini bajeti hii ya maendeleo ambapo kwa mwaka uliopita ilitengewa bilioni 15 lakini mpaka mwezi Februari wizara hii imepata bilioni 5 peke yake na sijui kama sasa hivi wameongezewa sawa na 31%. Tunaongea habari ya kuboresha viwanja, tunaongea habari ya kujenga vyuo, tunaongea habari ya kufufa chuo cha sanaa cha Butimba sijui wizara inaweza kufanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea habari ya kuweza kuhifadhi urithi wa ukombozi wa Afrika kwa bajeti hii ndogo kwa sababu Waziri wa Fedha yupo na Serikali hii iko hapa, nafikiri hilo watakuwa wameshalichukua. Lakini vinginevyo nampongeza sana Waziri, nampongeza pia na Naibu wake pamoja na watendaji wa Wizara kwa kweli tuseme kama ni upele umepata mkunaji. Tumeona kwa namna gani michezo Tanzania inapanda, hawa ni wachapakazi nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaona ni kwa kiwango gani amepaisha michezo Tanzania. Mama Samia Suluhu Hassan Mungu ampe uwezo, Mungu amlinde kwa sababu kwa kweli watanzania wameona kwa namna gani ametoa motisha kubwa. Kila mtu anafahamu ameanza ku-*motivate* wachezaji mara milioni tano, ameongeza dau milioni 10 ameongeza dau milioni 20, ametoa usafiri, anakaa na wachezaji wanakaa wanakula pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa sana la kuiga kutoka kwa viongozi wetu. Nampongeza sana lakini siyo yeye tu nawapongeza na Mawaziri. Nampongeza Waziri Mkuu kule kwake utasikia Namungo *FC,* nawapongeza Mawaziri huku ukienda kwenye majimbo yao michezo mingi, vipaji vingi vya wachezaji vinabebwa na Wahehsimiwa wengi Wabunge pamoja na Mawaziri. Ukienda huku utasikia Gekul *Cup* utasikia Issaay *Cup,* utasikia sijui Massay *Cup*. Wanatoa jezi, wanatoa mipira, chakula na nafikiri Wabunge wengi kwenye maeneo yetu ndio tunachokifanya na kuwasaidia wasanii kurekodi miziki na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawapongeza sana lakini kwa kweli bajeti iongezwe tuone ni namna gani wanaweza wakafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuwa–*support* tumeona michezo Tanzania nawapongeza hata wanayanga wameweza kuibeba sifa ya nchi kwa kuweza kuingia fainali hongera sana, tunaendelea kupongeza timu nyingi wamekuja huku *Serengeti Girls* tumewapongeza wamepata sifa ya kuingia

kwenye *World Cup*, Tembo *Worriors,* wamekuja vijana wa riadha Gabriel Geay, kina Isumbi yaani kwa kweli nawapongeza, hii yote ni kwa sababu tunawa–*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba vipaji hivi vinaanza toka utotoni. Hawa watoto wadogo kama timu kubwa inapata makocha hivi kwa nini hawa watoto wadogo tusianze kuwajenga kuanzia leo. Sisi zamani tulikuwa na maeneo ya wazi ambayo tunacheza michezo kama rede sijui hata inapotelea wapi? Lakini ni michezo ya kuwajenga watoto hasa kwa akili. Sasa maeneo yote yale ya wazi yamejengewa hakuna maeneo ambayo watoto wanacheza wanafungiwa ndani. Michezo ingesaidia Watoto kuwajengea akili pamoja na kuweka mahusiano na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Waziri katika kuhitimisha pengine uwaelekeze sasa kama ni Wakurugenzi au kwenye maeneo yote huko ya kata ya vijiji, waendelee kutenga maeneo wazi watoto wanacheza barabarani, wengine wanafungiwa ndani. Ili kutoka pale waendelee kujengewa uwezo lakini wapo taluma ya michezo, sanaa na utamaduni waanze kufundisha, waingie kwenye mitaala wafundishwe kuanzaia shule za msingi, sekondari, mpaka vyuo vikuu. Tuweze kupata vipaji kwa sababu hii ni ajira tosha. Ukichukua vijana watano wa Tanzania ukaambiwa chagua wangapi Kwenda shamba wengine kwenye michezo, kwa kweli watatu wataenda kwenye michezo. Kwa hiyo, michezo ni ajira kwa vijana wengine wanapotea kwa kukosa *support* na kwa hiyo hii ingia kwenye mitaala vijana wafundishwe, wawe-couch kuanzia huku chini siyo timu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kusemea ni bahati tuliyopata Tanzania ya kuwa *center* ya kuhifadhi urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika. Hapa naomba tu kwamba tunamuenzi Baba wa Taifa yeye ndio aliyesema Tanzania haiwezi kuwa huru, mpaka Afrika yote iwe huru na kwa heshima hii, sisi tumekuwa *center* ya kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tujenge hili ambalo limeanza kujengwa kutoka 2003 kwa msaada wa *UNESCO* na Tanzania kwa kweli ni *center* nzuri ya utalii wa kiutamaduni na

tunapata wageni wengi wa kuja kujifunza kwetu, hasa hawa ambao sisi tumewasaidia katika Ukombozi wa Bara la Afrika hasa nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watakwenda kupata kumbukumbu zao kuna maeneo mengi ya kuhifadhi ikiwepo Dar es Salaam, Mazimbwi, Kongwa pamoja na sehemu zingine. Kwa hiyo, kote huku kuhifadhiwe ijengwe kumbukumbu nzuri, wahifadhi makaburi, watafute zile *documents* za zamani kuwe na maktaba kubwa na ukumbi ili wenzetu wakute hizi historia. Tanzania ni nchi ya pekee iliyokuwa na uzalendo kusaidia nchi za Afrika Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa uletwe Muswada wa kisheria wa kuweza kuhifadhi hizi kumbukumbu za kiutamaduni ili utamaduni huu usiweze kupotea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa fursa ya kuchangia leo katika bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumpongeza Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya, kuipa uzito suala zima la michezo. Wote tutakuwa mashahidi baada ya kuona kazi kubwa inayofanyika na hasa kwenye sekta ya michezo, Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa amewekeza ametoa *support* kubwa kumaanisha kwamba sekta ya michezo imeshika hatamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Rais kwa uzalendo wa kutoa fedha lakini pia kutoa ndege kuisafirisha Timu

ya Yanga kwenda kushiriki mashindano ya shirikisho. Na hivyo nitumie fursa hii kuwapongeza sana Wananchi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuliletea heshima Taifa letu hili. Yanga wamefanya kazi kubwa sana ya kutuheshimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme, na niwe mkweli hapa, kuna watu wanausemasema ushindi wa Yanga; naomba nikwambie kwamba ushindi Yanga tulivyoshinda ni tofauti na ushindi huo wanaouzungumzia enzi za Ukoloni, utaona kabisa Yanga tumeshinda *aggregate,* maana yake tumeshindwa kikanuni tu. Kwa hiyo niwapongeze sana wachezaji wote wa Timu ya Yanga, lakini niupongeze uongozi mzima na mashabiki wote wa Yanga, kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nataka nijikite hasa kwenye suala zima la sanaa na michezo kwenye Halmashauri zetu hizi za Msalala, Ushetu, Kahama na nyingine. Kwa suala zima la sanaa sisi tunaotoka kwenye maeneo megine, na hili nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, mama yangu, utakapokuja kusimama hapa, mtueleze, hivi hili suala la sanaa, michezo, wasanii kwa maana ya Bongo Fleva, waigizaji; hivi ni Dar es Salaam tu, maeneo mengine hatutambuliki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote ni mashahidi hapa, mtaona, wasanii wetu kwenye maeneo yetu wana vipaji vikubwa mno lakini hawana *support.* Lakini leo hii utaona vipaji vyote vinatoka Dar es Salaam, yaani ili mtu aweze kutoka kuwa msanii bora, ni lazima aende Dar es Salaam. Sasa wale wanaotoka kwenye maeneo yetu ni lini hasa watakuwa; ni lini hasa Serikali itatengeneza utaratibu mzuri, mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba na wale wanaotoka kwenye maeneo ya vijijini waweze kukua?

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hamisi Taletale.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe taarifa babu yangu, Mheshimiwa Sheikh Iddi Kassim, kwamba hawa wasanii ambao tunawaona Dar es Salaam siyo kana kwamba wanasaidiwa na Wana-Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano msanii kama *Diamond* anatokea Morogoro na Kigoma, amejisaidia mwenyewe kufika pale. Tusiupe mzigo Serikali kwamba watu wanaobakia Morogoro wasaidiwe na watu wa Morogoro. Kwa hiyo taarifa yangu ni kwamba, ndugu yangu, Mheshimiwa Iddi, kama unataka kuhamia Morogoro ili utoke karibu Morogoro, mlezi wa vipaji ni mimi hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim, taarifa unaipokea?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo mimi siipokei kabisa kwa sababu ninao akina Babu Tale zaidi ya 20. Narudia; ninao akina Babu Tale zaidi ya 20 wako Kata ya Bulyanhulu, wana uwezo wa kusimamia wasanii kwenye maeneo yale. Tunao wasanii bora kwenye maeneo yetu, hasa Kata ya Bulyanhulu na maeneo mengine Kahama, tunao. Tunao waandaaji tuzo, wapo wengi, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu. Sasa msitufanye sisi tunaotoka kwenye mikoa huko kuwa ni maeneo tu ya Mawaziri kuja kuzindua *Doto Cup, Iddi Cup, Saashisha Cup* na kubaki maeneo mengine ni Dar es Salaam tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Wizara iweke mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba…

**MHE SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha.

**TAARIFA**

**MHE SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ni kweli nchi hii ina vipaji vya wasanii wengi. Pale Jimbo la Hai tuna Jukwaa la Wasanii, wasanii wengi, na Mheshimiwa Naibu Waziri tulikwenda naye, aliona vipaji vikubwa na yeye mwenyewe akashangaa, akauliza hapa ni Hai au tuko wapi. Kwa hiyo ni kweli tuna vipaji vingi Mheshimiwa Waziri washuke watambue vipaji hivi na kuvisaidia, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Iddi Kassim, taarifa unaipokea?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo naipokea kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano; tunaye msanii mmoja anaitwa Issa Jim, yupo Kahama. Msanii huyu ni *professional boxer,* anamiliki mikanda miwili, ameshinda *International UBO,* anao mkanda huo Kahama; ameshinda pia mashindano ya Afrika Mashariki *(WABA);* ameshiriki mashindano matano, manne ameshinda moja ametoa *draw,* yupo Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini toka anaanza kuandaa mashindano haya hakuna *support* ya aina yoyote ile aliyopewa na wala hatambuliki na wala hata hapa hajaalikwa. Leo tunawaona akina Mandonga wako hapa, lakini kwenye maeneo yetu kule hamuwaaliki. Ni lazima tusimame na tuseme kwamba Watanzania wote tuna haki sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara pelekeni, waelekezeni maafisa utamaduni kwenye maeneo yenu huko kuhakikisha kwamba wanashiriki kuibua vipaji, kusaidia wasanii ili na wao waweze kufika kwenye maeneo haya. Kaka yangu, Mheshimiwa Babu Tale, amesema hapa, *Diamond* ametokea Kigoma. Leo hii Wana-Kigoma angekuwa Kigoma kule leo tungekuwa tunamhesabu ni mtu wa Kigoma. Tunahitaji tusambaze keki hii kwenye maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri, dada yangu, mhakikishe ya kwamba mnakwenda kuwaelekeza hawa maafisa utamaduni kwenye maeneo yetu ili wafanye kazi. Wasanii hawapewi ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho; leo hii utaona ofisi hizi; BASATA, *COSOTA*, zote ziko Dare es Salaam. Leo hii msanii anayetoka Kata ya Bulyanhulu anaandaa kazi yake. Ili apate kibali maana yake ni kwamba aandae kazi akiwa Bulyanhulu, apande gari aende akapate kibali Dar es Salaam, na mwisho wa siku akirudi huku bado hawa watu wa *COSOTA* anakuwa hana hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini mkazi wa Bulyanhulu atatoka aende Dar es Salaam kupata kibali; kwa nini msifungue ofisi hizi au mkawakaimisha hawa maafisa utamaduni kwenye maeneo yale ili kuhakikisha kwamba wawasaidie wasanii wetu kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za usafiri, msanii anatoka hana ndugu wala rafiki Dar es Salaam, anajichanga changa anakwenda mwenyewe Dar es Salaam, matokeo yake ni nini, anaingia kwenye mambo mabaya ambayo yatamhatarishia maisha yake. Kwa hiyo niombe sana kwamba wasanii wetu hawa wanahitaji kupewa ushirikiano kwenye maeneo yao hayo ya huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kodi mbalimbali. Leo hii tumeona ili mtu aandae kibali, tamasha, kwa mfano pale Shinyanga kuna taasisi inaitwa *HolySmile*. *HolySmile* yeye mwenyewe amejichanga changa ameamua kuanzisha sasa tuzo mbalimbali, kutafuta ni nani msanii bora na ni nani mwimbaji bora. Lakini ili apate kibali, gharama yake anatakiwa alipe 1,500,000. Hebu punguzeni, pia muone namna ya kupunguza gharama hizi, ni kubwa sana kwa wasanii hawa wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo mnayotoa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie la mwisho; mikopo hii mnayotoa mnawapa wasanii wakubwa, kwa nini hamuwapi hawa wasanii wanaochipukia huku chini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. Lakini kwa kumalizia ninaomba pia Mheshimiwa Waziri aongee na Kampuni ya Barrick kama alivyosema Mheshimiwa Sanga hapa, waweze kutujengea uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze kwa uteuzi, dada yangu, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, nimetoka naye mbali UVCCM kule, najua uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Binamu, rafiki yangu, wasanii wanasema ile *Master's* ya Uingereza walikuchangia, kwa hiyo wanataka waone matunda yake. Wanajua uko sehemu sahihi ya kubadilisha *industry* yao lakini na uwe mfano kama kijana wa Kitanzania ambaye umepitia huko unajua changamoto zao, matokeo wanataka wayaone; mimi sina shaka na wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kwanza nianze na jambo moja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunaomba, hii michezo ya kubahatisha iende kwenye Wizara husika. Tunalia hapa watu hawana bajeti, wewe una vyanzo vingi vya fedha; una majengo,

una mambo ya matrilioni huko, mabilioni, sasa hawa ambao vyanzo vyao vidogo hata michezo ya kubahatisha? Kwa sababu hata hicho kinachokwenda kinakwenda kama hisani, wapewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge, tupambane humu ndani hii Wizara iheshimike kama tulivyoipambania Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Hii Wizara itatengeneza ajira mpya, hii Wizara ikipewa fedha za kutosha Taifa litakuwa na furaha. Watanzania wanapenda michezo, tutapata Timu bora ya Taifa; haviwezi kuja hivihivi kama tusipowekeza. Lazima Wizara hii ipewe fedha ya kutosha iwe na vyanzo vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Mheshimiwa Tarimba hapa, wanakusanya mabilioni kwenye michezo ya kubahatisha halafu wanapewa vipesa vidogo, haiwezekani. Hicho ni chanzo chao cha sahihi, wapewe waweze kuwekeza maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waheshimiwa hapa wanasema tunawaona tu wasanii wakubwa, ni kweli, huko mikoani kuna wasanii wengi. Kama Wizara haina fedha itawezaje kutengeneza mazingira mazuri ya kuwasaidia wale wasanii wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mara tuna wasanii bwana; kuna *Lady Jay Dee* pale Bunda, lakini alifika hapo kwa taabu, hatuhitaji wengine wa-*suffer* kama *Lady Jay Dee*. Tuna Isha Mashauzi, Mkurya wa kwanza kuimba taarabu. Tunahitaji Wakurya wengine kule tuwaibue waimbe taarabu. Tuna Getrude Mwita, ‘Kibibi’, anaigiza vizuri. Tunahitaji hii Wizara iwezeshwe ili watokee akina Kibibi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bila kuwekeza, siyo kwenye *football* peke yake, kwenye sanaa, kwenye utamaduni, hii Wizara ikiwekeza vizuri tunaamini tutapata wasanii wengi walio mikoani huko watatambulika na hii nchi itajivunia wasanii mbalimbali kutoka pande mbalimbali za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara sasa hivi Mungu ametujalia tuna timu mbili kwenye Ligi Kuu; tuna *Biashara United.* Lakini Uwanja wa Musoma ni mbovu, unahitaji ukarabati, una jukwaa moja tu, zikichezwa pale timu kubwa mapato yanakuwa madogo, kwa hiyo klabu inakosa mapato ya kutosha, tunahitaji uwanja ukarabatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunda tuna Uwanja wa Sabasaba, tuna *Bunda Queens,* wameshinda kucheza Ligi Kuu ya Wanawake, lakini Uwanja wa Sabasaba hohehahe; ni lini mtaukarabati Uwanja wa Sabasaba ili Timu ya *Bunda Queens* iwe na uwezo wa kucheza uwanja wa nyumbani? Hayo mambo tunahitaji majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabondia wetu wanahitaji na wenyewe wawe na viwanja vyao. Zamani ukisikia bondia anapigana unasikia *DDC*, viwanja vyao. Watengenezewe mazingira mazuri, na tunapata mapromota hapa akiwemo Mheshimiwa Mwakagenda, mabondia wamechoka kwenda kupigania kwenye viwanja vya mpira; hilo ni jambo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo la msingi, sasa hivi wakipata matamasha kwenda kupigana nje ya nchi anatakiwa kwenda peke yake; anawezaje kushinda bila kocha? Iwe kama timu za mpira wa miguu, inaposafiri timu inakuwa na kocha na benchi la ufundi. Ukienda wasanii akisafiri anakuwa na meneja wake na *dancers* wake. Kwa nini kwa upande wa mabondia anatoka yeye, yaani atoke Mwakinyo peke yake bila benchi lake la ufundi, bila kocha wake; hii haiwezekani. Mchezo wa ngumi umekua hivyo lazima upewe thamani yake; hilo ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujue mchaka wa Vazi letu la Taifa umeishia wapi? Iliundwa kamati, imeyeyukia wapi? Yaani Watanzania wakiwa wanadai Vazi la Taifa ndiyo mnaanza kuwakusanya wanamitindo mbalimbali. Mchakato wa Vazi la Taifa umeishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani sasa hivi kila mtu anaamua tu anachagua vazi analolipenda, mimi na mwili wangu najua

nikivaa Kihindi hapa nikipiga Sari, Punjabi ntakaa sawa, mwingine anachagua tu Vazi la Uganda, Vazi la Rwanda. Jamani, Taifa hili lina historia yake, tuna mavazi mengi, tupendekeze tukija humu Bungeni hata siku moja moja na sisi kama Wabunge tuna Vazi letu la Taifa. Lazima muweke historia ya kumaliza mchakato wa Vazi la Taifa; hilo ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Mheshimiwa Mwana FA na Mheshimiwa Waziri, wewe ume-*perform* nchi mbalimbali, tunahitaji *arenas*. Leo hii msanii mkubwa ndiye mwenye uwezo wa kwenda kukodi pale *Mlimani City.* Ukumbi ule si chini ya milioni 30, bajeti yake ili aweze kuandaa tamasha anatakiwa atenge kama milioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na *arenas* nyingi hata ya watu 20,000, tukiwa na *arenas* za kutosha ushindani utakuwa mkubwa, hata bei itapungua. Watakaoukuwa na uwezo wa ku-*meet standard* ya kwenda kwenye *arena* watakuwa wengi, gharama itapungua…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** …lakini leo kwenye kumbi kubwa tunawaona akina Marioo, tunawaona akina…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester, muda wako umekwisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa; *a very vital thing.*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia. Na mimi niungane na

wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi lakini bajeti ni ndogo, mambo ni mengi na muda nao ni mdogo, nitajaribu kwenda kwa harakaharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na wazo la Mheshimiwa Sanga la kuangalia namna ya kutumia *CSR* za makampuni kuwekeza katika michezo. Kwa kifupi tu bajeti wanayopewa leo ya milioni 35 haiwezi kujenga moja ya tatu ya ule Uwanja wa Mkapa. Nimeangalia kwenye dodoso hapa ule uwanja ni dola milioni 56, ni kama bilioni 133. Kwa hiyo hiyo bajeti yenyewe hata kiwanja kama kile haiwezi, ukiacha mambo ya watumishi huko na vitu vingine. Kwa hiyo ninaomba sana tuangalie namna ya kuiwezesha Wizara iwe na hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitoe mfano; Moshi tuna Uwanja wetu wa Majengo, kila mwaka tunatenga bajeti ikinyesha mvua kubwa barabara zikiharibika wakiangalia mahali pa kutoa tunasema toa kule kwenye michezo, yaani michezo nchi hii imeendelea kuwa nayo ni mchezo, yaani michezo ni mchezo. Lakini kwenye Baraza la Madiwani lililopo sasa Moshi Mjini, mwaka jana tumetenga milioni 300 na mwaka huu milioni 300 na Uwanja ule wa Majengo tayari tunakwenda kuutengeneza, tayari *pitch* imeshawekwa, tunaweka uzio na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Wizara; na kwa sababu sasa hakuna hela ya kusiadia kule Majengo nashindwa niioombeje, lakini hata kama mtatembeza bakuli mkipata chochote kwenye Halmashauri kama ya Moshi ambayo tumepeleka milioni 600 kwenye uwanja na sisi tunakuwa wa mfano, basi mtusaidie kutuongezea hela ili uwanja wetu ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mpango wa kujenga viwanja viwili *(arenas)*. Naona mmoja unajengwa Dar es Salaam, mwingine walisema ni Dodoma. Mimi naomba niwaambie, ili michezo iendelee kukua ni lazima tu-*diversify*. Ni vizuri mmoja ukijengwa Dodoma huo mwingine ujengwe ama

Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini au kule kusini Mbeya, maeneo ambayo yanafikika, ili tuweze kupanua huu mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Moshi Mjini sisi tuna eneo pale, lina ukubwa wa mita za mraba 157,000, unaweza kuweka *arena* pale. Kanda ya Kaskazini tuna Uwanja wa Ndege wa Kimataifa pale Hai, Moshi Mjini tuna uwanja mdogo, ule uwanja unafikika. Kwa hiyo ni vizuri tu-*diversify,* siyo viwanja vyote vijengwe Dar na Dodoma halafu kwingine kusiwe na viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *aspect* ya kwamba michezo ni utalii, na nilikuwa nataka kulichangia hili katika Wizara ya Utalii lakini ni vizuri nililete hapa. Sisi Moshi Mjini tuna mashindano makubwa ya kukimbia, *Kilimanjaro Marathon,* inaleta watu karibu 8,000 kutoka nchi zaidi ya 51. Wale watu wakishamaliza kukimbia huwa wanakwenda mbugani, wanapanda mlima, wanakwenda Zanzibar, wanaingiza fedha kwenye utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yapo maeneo Wizara ya Michezo ikiwekeza vizuri inaweza kusaidia sekta nyingine na ili hizi sekta sasa na zenyewe zichangie kwenye michezo. Hii *Kilimanjaro Marathon* ni mfano, lakini tunaweza kuwa na Mchezo wa *Golf* wa kimataifa, tunakwenda ku-*lobby* na *PGA*. Kuna moja ilikuwa ifanyike kule *Kili Golf,* kuna kiwanja ambacho kipo katikati ya Mlima Meru na Mlima Kilimajaro, *Kilimanjaro Golf,* unaitwa *Kili Golf;* unaweza ukaleta yale mashindano pale, yatatangazwa dunia nzima lakini wale washiriki pia watapata nafasi ya kwenda kwenye mbuga za wanyama kwenda kutalii ili watuingizie fedha. Hiyo ni pamoja na *cycling tour.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote hayaji tu. Kule Rwanda kuna *Tour De Kigali;* hayaji tu, lazima ukafanye *lobbying* na vile vyama vya *cycling* vya kimataifa. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri mkitushirikisha sisi tunaweza kuungana kuweza kufanya hiyo *lobbying*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanja vya *golf*, na ninasema *golf* kama mchezo mmoja, lakini kwa michezo mingine yote. Tume-*concentrate* sana kwenye mpira wa miguu, ni vizuri tukumbuke kwamba ndondi nayo sasa hivi imeanza kutupia

kimataifa, muziki unatuaisha kimataifa, riadha juzi kuna mkimbiaji wetu amemshinda mpaka Kipchoge. Kwa hiyo ni vizuri tuangalie namna ya kukuza hii michezo yote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *golf* Moshi pale tuna uwanja wetu wa *golf*, Uwanja wa kwanza *golf* Tanzania, *Moshi Club,* tuna denii kubwa sana la *land rent.* Sisi hatutaki tusamehewe, tunaomba Mheshimiwa Waziri uongee na Waziri wa Ardhi waondoe *interest*, sisi tuko tayari kulipa ile *land rent* yote ili kuweza kusimamia ule Uwanja wa kihistoria wa *Moshi Club.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la riadha. Kuna ulazima wa kutengeneza kambi maeneo ya nyanda za juu, maeneo ya *Rift Valley* kama kule Karatu, na maeneo ya *West Kilimanjaro* ili watu waje wa-*train*. Kule Kenya kuna eneo linaitwa Iten ambalo mpaka wakimbiaji wa nje wanakuja ku-*train* wiki mbili, wiki tatu kabla ya mashindano makubwa. Sisi tuna maeneo yanafaa, kule *West Kilimanjaro* kunafaa, kule Karatu kunafaa, itengenezwe kambi watu waje wawekeze nyumba za kulala ili wakimbiaji waje washiriki huku, na ni utalii pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye *incentives*, kampuni ambazo zimeshasaidia michezo mpaka sasa, sijajua Serikali inazisaidiaje; Azam kama mfano mzuri, *GSM*, *Mohamed Enterprises, CRDB* ambao wana-*sponsor* Mchezo wa *Basketball* wa Taifa, *NMB;* ni namna gani Serikali inatia chachu kwa kampuni hizi ili kampuni nyingine nazo ziwekeze kwenye michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Moshi tulikuwa na mashindano makubwa sana ya *volley ball*. Yalikuwa yanakuwa *sponsored* na *Bonite Bottlers*. Sijaona ni namna gani Serikali inasaidia makampuni binafsi ambayo yanawekeza kwenye michezo ili kuvutia makampuni mengine nayo yapate hamu ya kuwekeza kwenye michezo. Kwa hiyo nadhani kuna kitu cha kufanya ili tuweze kusukuma gurudumu hili mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antipas atafuatiwa na Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Mimi pamoja na mambo mengine ni mwanataaluma wa Michezo, Wizara hii nasema inanihusu sana. Mimi ni Mwalimu wa Mpira wa Miguu kwa taaluma, nina Diploma C ya *CAF*. Kwa hiyo nachangia kama mdau wa michezo sio tu wa siasa peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea napenda nitoe pongezi kwa rafiki yangu Paul Nonga ambaye ni kocha mwenzangu, mchezaji wa *Mbeya City*. Leo ni siku yake ya mwisho kuwa kama mchezaji wa mpira. Ametumikia nchi hii zaidi ya miaka kumi kucheza mpira Yanga na timu zingine pamoja na Timu ya Taifa ya Tanzania. Kwa hiyo namtakia Kheri katika maisha yake mapya ya ualimu na menejimenti ya mpira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze ndugu yangu Waziri, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuchukua nafasi ya kuendesha Wizara hii. Mimi nina matarajio makubwa kwao na nawapongeza, naamini kabisa watafanya kitu kutusogeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nina machache tu nataka niwapitishe Waheshimiwa Mawaziri, ni *highlights,* lakini kubwa zaidi wanafahamu kuna changamoto hii ya jana au juzi kulikuwa na tuzo hizi za wasanii, Mheshimiwa Khadija hapa amezungumzia. Wasanii kutokuwepo ukumbini, kwangu mimi hilo sio kubwa sana, lakini la kwangu nimesikia uvunguni watu wanalialia kwamba tuzo zilikuwa mikono mitupu hazikuwa na chochote. Mwaka jana watu walipata fedha kidogo angalau motisha, lakini mwaka huu kulikuwa hamna kitu, imesikia, wanalalamika uvunguni. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba alifanyie kazi, kama sio sasa hivi basi wakati ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuzungumza na Baraza la Michezo la Taifa. Najua kuna masharti ya usajili wa vyama vya michezo. Mimi ni mdau wa mchezo wa kuvuta kamba, nimekuwa Mwalimu wa kamba Timu

ya Bunge na nimewezesha timu hii kuweza kushinda Ubingwa wa Afrika Mashariki kwa upande wa Mabunge kule Arusha, nadhani wengi watakuwa wanakumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sasa ni matamanio yangu kusajili Chama cha Mchezo wa Kamba. Masharti yanataka kila wilaya kuwe na vyama na nini iendelee mpaka juu, nafikiri ndio sheria, wako sahihi, lakini naomba tuombe kama *special case,* michezo isiyo maarufu iweze kuanza na tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nina mambo mawili makubwa ya kuchangia leo. La kwanza, ni namna ya kupata Timu ya Taifa kwa baadaye kwa maana ya kutengeneza watoto wetu, lakini la pili, manung'uniko yangu au *discomfort* kwa namna ambavyo Chama cha Mpira Tanzania wanafanya. Kabla ya kwenda popote niwapongeze tu hao watu wa *TFF,* menejimenti ya sasa wakati wao tunaona *achievement* kubwa kwa mpira wetu wa Tanzania. Timu ya Walemavu, Timu ya Wanawake, Timu za Simba na Yanga zimekwenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Yanga juzi ametoka fainali bahati mbaya hakuchukua, tunawapa pole, lakini tunawapongeza kwa hatua. Kwa hiyo yote haya mazuri ambayo yanasemwa ni wakati wa Menejimenti hii ya *TFF*. Kwa hiyo nawapongeza sana wale *seating leaders*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Baraza la Michezo la Taifa, kiongozi yupo pale mtendaji Neema Msita binti mdogo na timu yake, wengine wote kiujumla nawapongeza kwa sababu haya yote mazuri ya nchi hii yametokea wakati wao wako madarakani. Kwa hiyo niseme tu wanastahili pongezi nawashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusu Timu za Taifa; nadhani tuafahamu wachezaji wengi tunawaona wakiwa wameshakuwa maarufu kwenye Vilabu vya Ligi Kuu, tunawaita *National Team,* lakini sidhani kama kuna mtu anawajua wachezaji wa Timu ya Taifa ambao wapo leo, lakini miaka kumi iliyopita au kumi na moja tulikuwa tunawafahamu wakiwa wadogo, ukweli

hatukuwafahamu. Kwa hiyo kulingana na uchache wa muda naomba tu nishauri machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niombe jambo hili la kutengeneza *future* ya Timu yetu ya Taifa liwe la Serikali kiujumla kwa maana ya TAMISEMI na Wizara ya Michezo na Wizara ya Fedha tulichukue liwe jambo la kwetu. Napendekeza Halmashauri zote nchini zielekezwe na Serikali kuwa na *academies*, kuwe na timu za watoto *under twelve, under seventeen* zisimamiwe na halmashauri wenyewe. Watu wa *TFF* au watu wa Serikali kwa maana ya Wizarani watatoa tu utalaam kule chini. Watakuwa na timu ya wataalam kwenda kuangalia *facilities* ziweje.

**MHE.FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgungusi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Sanga.

**MHE.FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokizungumza *Coach* wangu pale ni kitu *right* kabisa. Kwa Afrika *the best development modal* ya soka iko Zanzibar ambayo wameitumia Ghana, wameitumia Nigeria, wameitumia Cameroon. Kwa hiyo mfumo mzuri wa kuzalisha wachezaji, upo kwa majirani zetu Zanzibar ambao tunaweza tukautumia na tukazalisha wachezaji wazuri kwa kuwa na *academy* kwenye kila eneo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgungusi, taarifa unaipokea?

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni hilo nilikuwa nakazia tu. Kuna kila sababu ya zile halmashauri zetu ziweze kuwa na timu. Tunatenga fedha mapato ya ndani kufanya vitu kama zahanati na vingine vingi vya msingi, lakini jambo la michezo kuwa na timu za watoto kwenye halmashauri ni jambo la msingi. Tunajua

unaweza kuwa mzigo mkubwa sana kwa halmashauri, lakini Wizara ya Michezo, Wizara ya Fedha iweze ku-*subsidize*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapelekewa kule chini fedha za maendeleo hata fedha ya kulea hizi *academy* kule halmashauri ziwepo. Tuna Walimu wengi wanazalishwa na *TFF,* hawa watu wanasoma i*ntermediate level* wengine wanasoma *preliminary* ualimu, wengine *diploma C,* wapo mtaani wanazurura wangeweza kupata ajira kwenye halmashauri zote kuwatengeneza watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mtoto anatengenezwa, *professionally* tangu akiwa mdogo ana miaka 12, ana miaka 10, akifika huko juu anakuwa na uelewa mkubwa kuliko leo, mtu anatokea mtaani amejilea mwenyewe, anakuja kukutana na *Coach Professional* akiwa tayari mkubwa amezeeka, hafundishiki. Ni changamoto kubwa, wengine watalaumiwa wahuni, hawazingatii, hawafundishiki kwa sababu ya mazingira kama hayo. Kwa hiyo naomba hilo tu nishawishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, tumwombe Mheshimiwa Rais kama tunakwama. Ametoa fedha tumejenga madarasa nchi nzima. Miundombinu mingine mingi ya Barabara, kila Jimbo limepata fedha, amesaidia, sidhani kama atashindwa kutusaidie kujenga viwanja vile vya *standard* nzuri kwenye kila halmashauri, halafu mambo ya malezi tutafanya wenyewe kama halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni suala la manung'uniko yangu. Kutokuwa na furaha na amani namna ambavyo ndugu zangu *TFF* ya leo wanaendesha hii hali ya mpira wetu. La kwanza kabisa, tunafahamu na wenyewe wanafahamu na Wizara pengine inafahamu kumekuwa na malalamiko mengi dhidi yao. Pengine najua wako kwenye nafasi nzuri kama hizo za maendeleo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha, malizia sentensi.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naam.

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili imelia, kwa hiyo muda wako umekwisha.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sekunde chache nimalizie.

**MWENYEKITI:** Sekunde thelathini, malizia.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Waziri, naomba asimamie, kuna wataalam ambao ni Walimu wetu wa mpira wanadai *TFF* fedha waweze kulipwa, lakini kuna watu wengine nafikiri wanafungiwa fungiwa, *TFF* wanashindwa kuwavumilia, naomba awasaidie.

la mwisho, kuna suala la uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Wanawake amezungumzia Mheshimiwa Chumi, naomba *TFF* walifanyie kazi. Wizara naikabidhi tutaonana Bunge la Septemba, tutazungumnza vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, ambaye ni Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho katika wachangiaji wa Bajeti yetu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Moja kwa moja nitangulie kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kuhamasisha na kuwekeza fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia mchezo wa soka hasa kwa Vilabu vyetu vya Simba na Yanga ambavyo mwisho wa siku vimepata mafanikio makubwa. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na nimwombe tu Mheshimiwa Rais huko anakonisikia aendelee kutuunga mkono katika mchezo huu ambao unapendwa zaidi kuliko michezo yote duniani ili tuweze kusonga mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia hapa hamasa ambayo imetolewa na Mheshimiwa Rais wetu imepelekea kushuhudia Vilabu vyetu vikifanya vizuri ndani na nje ya nchi kwenye mechi zake. Kwa mara ya kwanza tumeshuhudia Timu za Simba na Yanga zote kwa pamoja zikifanya vizuri katika medani ya soka. Pia tumeona Yanga imekwenda fainali, hongera sana, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Club ya Simba ikiwa na *consistency* kwa zaidi ya miaka mitano ikifanya vizuri na hivyo kupandisha kiwango cha soka kwa vilabu vyetu kwenye *ranking* za *CAF*. Kwa *Club* ya Yanga kutoka nafasi ya 63 hadi kwenda nafasi ya 18, kwa Club ya Simba kutoka nafasi ya 12 kwenda nafasi ya tisa na hivyo kupelekea *Club* ya Simba kutunukiwa nafasi ya kucheza *Super League* ya Afrika. Kwa taarifa nilizonazo nyepesi nyepesi hivi karibuni mashindano hayo yatafanyika na huenda yakafanyika nchini Tanzania. Hii itatuongezea fursa nyingine ya kuweza kuongeza zile fursa zilizotokana na *royal tour*. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uwezeshaji wake kwa hamasa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nihamie kwenye eneo la Sanaa. Sanaa yetu bado kuna maeneo haijafanya vizuri japokuwa juhudi kubwa zimewekezwa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita. Katika Nchi za Uturuki, Marekani na hata Afrika Kusini, hapa Afrika kumekuwa na zile sinema au filamu zinazoendana na historia. Ukienda Uturuki kuna filamu ambazo zinatamba sana sasa hivi za akina Osman, Ertugrul Bey lakini hata Marekani kuna zile filamu za kivita za akina Rambo, Michael *Dudikoff* na zingine. Niliwahi kushuhudia sinema au filamu inayohusiana na utawala wa *King Shaka* kule *South Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri wakati umefika hivi sasa kwa Serikali yetu kuwekeza kwa wasanii wetu kwa ajili ya kucheza picha ambazo zinaendana na historia. Kwa mfumo huu tutaweza kuongeza ajira katika filamu, lakini pia tutaongeza hisia za kizalendo, tutadumisha utamaduni zikiwemo lugha za asili ambazo Tanzania hapa zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hainingii akilini kuona wale wasanii wetu hawawezi kucheza filamu ile ya Mtwa Mkwawa wakati alipowaongoza Wahehe kupambana na Wajerumani na akawashinda katika awamu ya kwanza na yule Jemedari Zelewski akauawa. Vijana wetu hawawezi hizo lakini hawawezi kucheza sinema ya Vita vya Maji maji ambavyo wananchi wa Kabila la Wamatumbi waliwaongoza wananchi wa kabila zingine kupambana na Wajerumani na katika *battle* la kwanza waliweza kuwashinda Wajerumani siku 31 mwezi Julai mwaka 1905, pale katika Kijiji cha Kibata. Je, hawawezi vijana wetu kucheza picha zenye mvuto ambazo za wale Walugaluga kule wakiongozwa na Chief Milambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa wakati huu sinema za namna hii zimekuwa maarufu sana duniani na zimekuwa zikiingiza kipato sio tu kwa nchi hadi kwa msanii mmoja mmoja. Kwa hiyo niwaombe Serikali tuweke mkakati mzuri, tuwezeshe hizi taasisi zetu za BASATA, *COSOTA*, TaSuBa pamona na Mfuko huu wa Wasanii Tanzania au Mfuko wa Sanaa tuwezeshe fedha kwa sababu tunajua sinema za namna hii au filamu za namna hii zinagharimu fedha nyingi. Tuwekeza, fedha itolewe ruzuku kwa sababu hili jambo lina manufaa ya kitaifa sio tu kwa msanii mmoja mmoja ili tuweze kuendeleza hizi filamu za namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapa majuzi nilikuwa namsikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo akizungumza na *Deutsche Welle* kuhusiana na fidia kwa waathirika wa vita mbalimbali ambazo Wakoloni wa Kijerumani walipambana na wananchi au mababu zetu. Alizungumzia Vita vya Maji Maji, akazungumzia vita vya Mtwa Mkwawa na Wajerumani, lakini ilitolewa mifano kule Namibia kulikuwa na Waherero na Wamakwa walipambana na Wajerumani, walilipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Wizara itakapokuja ku-*wind up* kuhusiana na hii hotuba ambayo imetolewa, waje watuambie mkakati walionao katika kudai fidia, lakini sio fidia tu kudai pia zile malikale ambazo zilitaifishwa na Wakoloni wa Kijerumani kama *dinosaur* ambaye alitolewa kule

Tendeguru, Lindi lakini pia hadi mafuvu na sijui wanayatumia kwa shughuli gani mpaka leo, yarudishwe nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ije itupe taarifa wamefikia wapi katika mkakati huo. Vile vile ningeomba jamii zilizo husika na vile vita katika kudai fidia washirikishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(nation competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza wanamichezo wote kwa kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa. Kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hamasa na msukumo alioweka katika michezo yote na hasa mafanikio makubwa ya timu ya Yanga katika mashindano ya Kombe la Shirikisho *(CAF Confederation Cup)*. Napenda pia kuwapongeza Klabu ya Yanga kwa kushinda ugenini Algeria katika raundi ya pili ya fainali na kufanya jumla ya magoli mawili kwa mawili kushika nafasi ya pili kikanuni ya Kombe la Shirikisho *(CAF Confederation Cup)*. Kutokana na hamasa ya Mhe. Rais, Klabu ya Yanga imeandika historia na kuipa nchi yetu heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inastahili pongezi kwa mkakati wake katika kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa timu za Taifa na vilabu katika michezo na michuano mbalimbali ya kimataifa na kikanda. Kama sehemu ya mkakati huo Wizara iweke msukumo zaidi wa kuhamasisha kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya viwanja vya michezo hususani vya mpira wa miguu. Viwanja vingi vya mikoani vipo katika hali mbaya na kwa kiasi kikubwa ni sehemu ya changamoto katika maendeleo ya michezo nchini. Michezo na sanaa ni muhimu sana katika kujenga sura na sifa ya Taifa letu *(nation brand)*. Hivyo ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha inaweka umuhimu mkubwa wa ushiriki wa timu zetu za Taifa na kuwepo kwa mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha timu zetu za Taifa na vilabu zinafanya vizuri kwenye mashindano ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu katika michezo na sanaa ni nguzo muhimu katika kutekeleza Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Serikali itenge bajeti ya kutosha kuhakisha tija katika ushiriki wetu katika mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuboresha miundombinu ya viwanja, Wizara ijikite katika kuibua vipaji mbalimbali vya michezo na sanaa kwa kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine hususani Elimu na TAMISEMI. Pamoja na kutokuwepo kwa miundombinu rafiki, mikoa mingi imekuwa inatoa wachezaji wenye vipaji vikubwa katika mpira wa miguu,

riadha na hata sanaa mbalimbali. Imefika muda sasa wa kuwepo kwa mkakati wa kuibua na kuendeleza vipaji hivyo ambavyo vimekuwa vinaonekana kikanda zaidi kama vile riadha kwa Mikoa ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Mikoa ya Kati. Pia kwa upande wa mpira wa miguu kumekuwepo na mikoa kadhaa ya vipaji vikubwa na huko ndio Serikali iweke msukumo zaidi wa kuibua na kuendeleza hivyo vipaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa wasanii, kuna Mikoa imekuwa inatoa idadi kubwa ya vipaji kwenye uigizaji, uimbaji ikiwemo nyimbo za injili ambazo zinapata umaarufu sana duniani. Kutokana na vipaji vingi vya michezo hususani mpira wa miguu na riadha, napendekeza Shule ya Sekondari Santilya ya Wilaya ya Mbeya iongezwe kwenye orodha ya shule teule za michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Kiswahili kuwa Lugha rasmi Kimataifa, napendekeza uwekezaji zaidi katika kuitangaza na pia kuwezesha Ulimwengu kujua kuwa mizizi na ustawi wa Kiswahili ni Tanzania pekee na wengine wanaigiza kwetu. Serikali iendelee kuchukuwa hatua zaidi ya kukistawisha Kiswahili katika Mataifa mengine Barani Afrika na kwingineko kwa kushirikisha vyuo vikuu hapa nchini na vyuo vikuu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana (Mb) na Naibu wake Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb), Katibu Mkuu Bwana Saidi Yakubu, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Nicholaus Mkapa pamoja na timu ya wataalam kutoka Wizarani kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye utekelezaji wa agizo la Rais wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kujadiliana na mamlaka husika kurudisha mafuvu ya vichwa vya machifu wetu na vyombo vya sanaa vilivyochukuliwa kikatili na kupelekwa Ujerumani na wakoloni. Agizo hili alilitoa kwenye uzinduzi wa Tamasha la Utamaduni Kilimanjaro lililoandaliwa na

uongozi wa machifu wa mkoa huo tarehe 22 Januari, 2022. Suala hili linazihusu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mamia ya mafuvu ya binadamu yaliyochukuliwa na Wajerumani kutoka makoloni yake ya zamani ikiwemo Tanzania. Inakadiriwa kuwa kuna mafuvu zaidi ya 200 kutoka Tanzania ambayo yako Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mafuvu ya watu maarufu ni pamoja na majemedari wa kabila la Wangoni wajulikanao kama Nduna na Mbano kutoka Songea. Wengine ni Machifu maarufu kama Mkwawa wa Iringa, Sina wa Kibosho, Meli wa Old Moshi na wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuvu hayo yalichukuliwa na Wajerumani kutoka kwenye maeneo ya maziko hasa makaburi. Mengine yalichukuliwa kutoka kwenye maeneo ya kunyongea watu yaliyokuwa yameasisiwa na Wajerumani hapa Tanzania. Kwa mfano, eneo alikonyongewa Mangi Meli wa Old Moshi katika Jimbo la Moshi Vijijini limehifadhiwa kama sehemu ya makumbusho kule Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mangi Meli aliuawa mwaka 1900 kwa kupambana dhidi ya utawala wa ukoloni wa Ujerumani. Baada ya kuuawa mwili wake ulikatwakatwa na kichwa chake kikasafirishwa kwenda nchini Ujerumani. Pia kichwa cha Chifu Mkwawa kilikatwa na kupelekwa Ujerumani akiwa kwenye mapambano na wakoloni wa Kijerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kilio kikubwa hapa nchini Tanzania kutoka kwa makabila yenye mashujaa hawa kutaka masalia ya mafuvu ya wapendwa wao kurudishwa nchini. Kilio hiki ni pamoja na kurudisha mafuvu wa Machifu Sina wa Kibosho na Meli wa Old Moshi ambao wametokea Jimbo la Moshi Vijijini, hili ni jimbo langu la uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika tamasha la Utamaduni, Kilimanjaro

lililoandaliwa na uongozi wa machifu wa mkoa huo tarehe 22 Januari, 2022 aliagiza majadiliano ya kurudisha mafuvu ya vichwa vya machifu wetu yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakfu wa urithi wa kitamaduni wa Prussia huko Berlin, Ujerumani umeridhia kurejesha mabaki kadhaa ya binadamu na kazi za sanaa ambazo ziliibwa na Wajerumani walipokuwa wanatawala baadhi ya nchi za Kiafrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa zinazoeleza kuwa watafiti wa Ujerumani wameshafanya utafiti wa kuyatambua mafuvu kutoka Tanzania. Kwa mfano, katika utafiti huo, mjukuu wa Mangi Meli kutoka Old Moshi alifanyiwa vipimo vya kinasaba *(DNA)* ili kusaidia kusaka fuvu la babu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, wawakilishi kutoka Ujerumani walilitembelea Bunge letu hapa Dodoma na wanashauku kubwa ya kukamilisha zoezi hili. Ninaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Maliasili na Utalii walivalie njuga jambo hili kwa pamoja na kukamilisha zoezi la kurudisha mafuvu ya mashujaa wetu nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mheshimies Rais kwa kuhamasisha michezo, utamaduni wetu na sanaa. Pili nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayofanya. Nampongeza anavyohamasisha, mkononi mwako tumeshuhidia ushindi kwa vijana wetu wa *Fountain Gate School,* lakini pia hatua iliyofikiwa na timu ya Yanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Naibu Waziri - mtu mwema, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote, niwapongeze pia kwa kuwa na utaratibu wa mikopo kwa ajili ya kukuza utamaduni na sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ni ndogo mno, ni vyema iongezewe ili kuwezesha maendeleo ya majukumu yaliyokusudiwa. Nyasa tumeanza kujenga uwanja wa mpira, mnatuchangia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu na Serikali yetu nzima ya Awamu ya Sita kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020 & 2025 kwa kila sekta, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Pindi Chana - Waziri, Naibu Waziri na watendaji wakuu wa Wizara hii kwani kuna mafanikio makubwa sana katika Wizara hii muhimu kwa ajili ya kuibua vipaji vya Watanzania na kuchochea fursa ya ajira kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wenzangu wote kuipongeza sana timu yetu ya Yanga kwa kweli wametuheshimisha mbele ya kimataifa hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia hotuba ya mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, na maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, Serikali iangalie utaratibu wa kuweka kalenda ya mashindano mbalimbali za vipaji kupitia makundi kwenye ngazi za wilaya. Hata hivyo kuna vijana wengi walioko katika ngazi za shule zetu za sekondari na msingi nchini ambao wanakabiliwa na chagamoto mbalimbali katika kufikia ndoto zao

mara nyingi. Kwa hiyo, kuna haja kubwa ya kuimarisha Kamati za Michezo ngazi za Wilaya na Mikoa ili kuelekeza mpango kazi zao kila mwaka na kushirikisha washiriki wa vipajj ngazi za chini ili kufanikisha mpango wa Taifa wa kuwa na washiriki wenye uwezo mkubwa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie uwezekano wa kila halmashauri nchini kuwa na walimu wa fani ya michezo ili kuendeleza vipaji kwa vijana wetu shuleni. Aidha, Serikali ielekeze halmashauri kama mdau wa sekta hii kutenga fedha za utamaduni, sanaa na michezo kupitia mapato yake ya ndani katika bajeti ya mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa sana katika Taifa letu wa kulinda, kuendeleza, kutunza na kustawisha lugha ya Kiswahili kuwa rasilimali tulizonazo kitaifa na kutumia kukipigania ukuaji wake Kimataifa na hapa tuna kila sababu ya kumkumbuka, kumuenzi na kumwombea Hayati Mheshimiwa Julius Kambarage Nyerere Baba wa Taifa letu kwa kutuunganisha sisi Watanzania kutumia lugha moja Kitaifa na kuwa nchi ya mfano Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe na *data bank* ya maeneo ya michezo nchini kuanzia ngazi za vijiji, wilaya, mikoa, na kuzipima na kuendeleza maeneo hayo. Nayasema hayo kwa sababu maeneo mengi yamevamiwa na kutumika kinyume na matarajio ya awali hali itakayohatarisha maendeleo ya sekta ya michezo nchini kutoweka na athari kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa michezo, utamaduni na sanaa ni fursa kubwa ya ajira nchini tunaiomba Serikali yetu iongeze bajeti ya Wizara hii na kutafuta wadau watakaotuunga mkono ili kupata mafanikio makubwa sana Kitaifa. Aidha, kuna haja ya kuendeleza miundombinu ya michezo nchini na kupangia matumizi kikanda na kimikoa ili kuchochea tasnia ya utamaduni, sanaa na michezo. Naomba pia Serikali yetu itusaidie kutuma wataalam wa Wizara kwa ajili ya kuendeleza na kukarabati *Nyerere stadium* iliyoko Jimbo la Mbulu Mjini, ni uwanja mkubwa katika mkoa wetu wa Manyara ili kupata mpango mkakati wa kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu naomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ombi langu la kuwa mgeni rasmi katika fainali ya Kombe la Mashindano ya Jimbo la Mbulu Mjini mwezi wa Julai 2023 ambayo kwa miaka saba sasa kombe hilo huanzia ngazi ya vijiji mwezi Aprili, ngazi ya kata mwezi Mei, ngazi ya tarafa mwezi Juni na kuhitimishwa ngazi ya Jimbo mwezi Julai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Mawaziri/Naibu Mawaziri waliotangulia kwa ushirikiano wao katika kuhitimisha kombe hilo kila mwaka kwa jinsi walivyoshiriki na kutambua mchango wa wananchi na wadau wa michezo katika Jimbo la Mbulu Mjini, asanteni sana, na karibuni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ione namna ambavyo itakuza utamaduni kwenye maeneo ambayo yanapakana na mbuga zetu au maeneo ambayo watalii wengi hutemebelea kwa nia ya kusaidia kukuza utalii na kuongeza ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Iringa kama lango la utalii liangaliwe pia hasa ukizingatia historia ya watu wa Iringa na Chifu Mkwawa. Pia kuanzisha matukio mbalimbali kama mashindano ya ngoma, mbio na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ibuni njia muhimu za kushirikiana na wadau kuinua utamaduni wa sehemu husika na kuibua vivutio mbalimbali vilivyopo kwenye miji nchini ili kuimarisha ustawi wa afya ya jamii miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia katika mada ambayo iko mbele yetu. Kwanza naunga mkono hoja ya Waziri aliyoiweka hapa mezani. Pili, niseme tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, Wizara hii ya Michezo, Utamaduni pamoja na Sanaa ni Wizara mojawapo kati ya Wizara za kipaumbele. Niwaombe waendelee kuiona katika sura hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tuna Mheshimiwa Rais ambaye ni mwanamichezo kweli kweli, tena sio tu mwanamichezo ni mwanamichezo ambaye pia maono yake yana baraka, unaweza ukaona namna ambavyo timu zetu zilivyoweza kufanya vizuri. Taja timu zote ambazo umeona Mheshimiwa Rais ameweka mkono zimeweza kufanya vizuri sana ukianza na timu za wanawake, uje timu za vijana, uje timu za ngumi, taja kila aina ya mchezo unaweza ukaona ambavyo umefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja tu ambalo linaweza likawa linatofautiana kwa nadharia halafu mpaka ikaonekana labda bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana. Ni mategemeo ya Serikali na ni uelekeo wa Serikali ambapo tumeona vile vitu ambavyo vinaweza vikafanywa kwa ufanisi tuna Sekta binafsi, sio lazima Serikali iweke fungu kutoka kwenye Bajeti Kuu. Hii ni kwa sababu ya kukua kwa mahitaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwambia *experience* nzuri tu ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa mifano hapa katika nchi zingine nyingi tu ambazo wamefanikiwa kwenye michezo, waliweka dirisha linalotoa fursa kwa sekta binafsi kwa makampuni yaweze kushiriki katika shughuli za michezo na kile watakachokuwa wamekitoa kwenye michezo kinakuwa *deducted* kwenye kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenyewe walipitisha mwaka jana, jambo hilo lipo kwenye hatua zetu za kikodi. Kwa maana hiyo ni vile ambavyo labda hamasa

haijaweza kukolea lakini jambo hili Bunge lako lilipitisha na huu ndio utaratibu mzuri ambao duniani kote sekta ya michezo inakuwa *financed* kwa namna hiyo, kwa hiyo nitoe rai kwa makampuni yashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tutakuwa hatuitendei haki sekta binafsi, tukitaka hata magoli ya uwanja kwamba lazima yatengewe fedha kutoka Mfuko Mkuu. Kuna vitu vingi ambavyo tunaweza tukavifanya ambavyo sekta binafsi haiwezi ikafanya, lakini kwenye haya ya michezo tuna fursa nyingi ambapo sekta binafsi inaweza ikafanya na ika-*complement* bajeti ya sekta hii ikawa kubwa tu. Kwanza masuala ya michezo kwa jinsi yalivyo siyo mambo ambayo unaweza ukaya-*streamline* halafu ukaachia kila wakati yatoke Mfuko Mkuu. Kwa hiyo, nasema kwamba tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pongezi hizi mnazoona mwaka jana, mwaka juzi hata hii *five percent* ambayo inaenda kwenye Sekta ya Michezo haikuwepo. Tumshukuru Mheshimiwa Rais mwaka jana akasema tutoe *five percent* ikaenda kule, lakini akaweka na ahadi nyingine kwamba tunapoenda kwenye Bahati Nasibu ya Taifa tutaweka kiwango kingine ni vile tu hatujapata *total figure* ni kiasi gani, lakini mchakato wa manunuzi utakapokamilika tutakaa na Wizara kwa sababu hilo linatarajiwa lianze tunapoenda *mid-year review,* tutakaa na Wizara tuwaongezee kiasi kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu, tumekaa na Wizara tumewapa fursa *EPC+ F* kwenye ukarabati na ujenzi wa viwanja ambayo ni bajeti kubwa tutaisemea tunavyokuja kwenye bajeti kubwa ile inayokuja, lakini tulishatoa fursa kwenye bajeti hii inayomalizika wanayo hiyo *commitment* ili Wabunge waweze kuona ni kwa namna gani Serikali inaweka uzito kwenye jambo hili ambalo wameliongea…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa bajeti ni mchakato, tumesikia maoni yote haya kwa ujumla wake, tunakokwenda mbele tutaendelea kuboresha ili tuweze kuya-*incorporate* haya maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha michezo. Mheshimiwa Rais ni mwanamichezo, mimi mwenyewe ulevi pekee nilionao ni huo wa michezo na nazitakia kila la heri timu zote, nikiipongeza Yanga, sisi ni Mabingwa na nitatoa mwondoko, mabingwa wanaondokaje, Mabingwa wa Afrika nitakapokuja kutoa Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Mheshimiwa Naibu Waziri, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kibali kilichotuwezesha wote kuwepo hapa leo, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama yangu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa anayoendelea kuwa nayo juu yetu na ahadi yangu ni ile ile, hatutamwangusha, tutafanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha Sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ya nchi hii inaacha alama wakati huu wa utawala wake wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa miongozo mingi ambayo amekuwa akinipa, Mama yangu *experience* yake na yeye inanifaa mpaka mimi sasa. Kwa kweli namshukuru sana najifunza mengi kutoka kwake na naamini naiva zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu yangu Saidi Yakubu na Naibu Katibu Mkuu Ndugu yangu Nicholas Mkapa na Watendaji wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Vilevile, naishukuru sana familia yangu, mapenzi ni mengi kwa kweli na wananchi wenzangu wa Muheza kwa kuendelea kuniunga mkono, kuniongoza na kunipa ushirikiano wa hali na mali, ninyi ni

vyuma kweli kweli na Muheza inarudi kwenye ramani vizuri kama ambavyo tulikuwa tumekubaliana ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuzipongeza timu zetu. kwanza kabisa, ninaipongeza timu ya Dar es Salaam *Young Africans* ambao wamekuwa washindi wa pili, niseme tu kikanuni kwa sababu Yanga hawakufungwa kwenye hizi mechi mbili za fainali bali walishindwa tu kuchukua ubingwa kwa sababu ya kanuni. Kwa hiyo, tunakubaliana wamefanya vizuri sana na wameiletea sifa kubwa nchi na hata zile fedha ambazo Mheshimiwa Rais alikuwa anatoa pamoja na ndege matunda yake yameonekana. Hongereni sana Dar es Salaam *Young Africans. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Klabu ya Simba kwa kufika robo fainali ya ligi ya Mabingwa wa Afrika. Robo fainali ya ligi ya Mabingwa wa Afrika siyo nafasi ndogo na Simba imekuwa wakirudia mara kwa mara kiasi kwamba lengo sasa hivi ni kuivuka na ninaamini mkijipanga vizuri msimu huu unaokuja pengine tunaweza kuona maajabu. Vilevile, niwapongeze kwa *outstanding performance consistently* kwa miaka mitano iliyopita iliyosababisha mpate nafasi ya kushiriki *Super League. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *Super League* ni *league* ya vilabu vya Afrika ambavyo vinahusisha timu nane. Tuna nchi Hamsini na kitu kwenye Bara hili lakini vilabu ni nane tu vilivyopata nafasi ya kushiriki. Ni vile vilabu ambavyo *performance* zao zinaonekana zina mashiko kweli kweli na vigezo vingine vingi ambavyo wameviweka, Klabu ya Simba imevifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kama timu ya Yanga na yenyewe itaendelele na *performance* iliyoifanya mwaka huu basi pengine tutakuwa na timu mbili kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Afrika wakati naongea nae kwamba, tuna vigezo Klabu ya Yanga inatakiwa ivifikie ili tuwe na timu mbili. Kwa hiyo kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujibu hoja kadhaa ambazo zimetangulizwa na Waheshimiwa Wabunge kabla Mheshimiwa Waziri kuja kuhitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na hoja ya Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwamba utamaduni ni mtindo wa maisha na ni zile kawaida za watu na namna tunavyoishi, kwamba matatizo mengi ambayo tunayo yangeweza kuondoka kama tungeyatengenezea utamaduni na kuusimamia ukatekelezwa, hili nakubaliana nae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tuna mambo mengi na miongoni mwa mambo ambayo yamesemwa ni kuhusiana na taasisi zetu kushindwa kufikisha yale malengo ya maduhuli ambayo tulikuwa tumepanga kwamba tutayakusanya. Sasa kwa sababu ya muda nitoe mfano wa taasisi yetu moja tu ya *COSOTA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumekubaliana kwamba *COSOTA* mwaka 2022 itakusanya shilingi bilioni 1.35 lakini walishindwa kufikisha na sababu zipo wazi. Sababu moja ni kwamba mazingira na sheria ambazo zilikuwa zimetumika kuweka matazamio yale wakati ule yalikuja kubadilika hapo katikati na yakwafanya wawe chini ya kiwango kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 2022 ambayo yalikuwa yanatuelekeza kwamba tutaaanza kukusanya zile kodi kwenye *devices* ambayo haijaanza mpaka sasa hivi lakini yenyewe tuliijumlisha kwenye makusanyo yao. Vilevile elimu kwa wale ambao wanatakiwa kulipa ile mirabaha na ushirikiano mdogo ambao tunaupata, lakini hilo ndugu zangu Wabunge tunalishughulikia na hasa wana Kamati ambao walilileta. Miongoni mwa mambo ambayo tumeyafanya hivi karibuni kwa maelekezo ya Waziri, nimewaomba *COSOTA* wanipe majina na idadi ya fedha wanazodai kutoka kwa wale wadaiwa wao sugu na wamefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitumie Bunge lako tukufu kutoa salamu kwa wale ambao ni wadaiwa sugu kwa *COSOTA* kama wanaona kwamba kutumia kazi za sanaa ni halali yao bila kuwalipa hawa wasanii waliozifanya kazi hizi wajiandae. Bunge hili litakapokwisha mimi kwa maelekezo ya Waziri nitakwenda mwenyewe mtaani kuhakikisha kwamba tunazifungia sehemu hizi na hazifanyi shughuli zinazozifanya za kutumia kazi za

sanaa za nchi hii bila kuwalipa wasanii ambao wametoa machozi, jasho na damu katika kuzitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niihakikishie Kamati kwamba hili tutalifanya na mimi kama msanii sitakaa hapa nione kwamba wasanii wengine wanadhulumiwa na haki zao hazipatikani kwa sababu tu ya matakwa ya watu kutotaka kutoa ushirikiano. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ilikuwa ni hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Sanga kuhusiana na *CSR* za kampuni zinazotekeleza miradi mikubwa nchini zitusaidie kutengeneza miundombinu ya michezo kwenye nchi hii. Huu mpango sijui Mheshimiwa Sanga umeupata wapi lakini ni kweli kwamba sisi tulikuwa nao tayari sijui ni kidege gani kimekuibia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina maelekezo ya kujenga *stadiums* mbili Arusha na Dodoma, miongoni mwa vyanzo vya mapato ni *CSR* za miradi mikubwa katika sekta ya fedha, nishati na madini. Sasa, tayari Wizara imeanza kufanya mawasiliano na Wizara husika nilizozitaja hapo na nikuhakikishie mawasiliano yanaendelea vizuri na tutalifikia lengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine ambayo tumeipanga ni kuhimiza *Corporate Social Investment,* Wawekezaji wafanye uwekezaji wa kijamii ambapo unaweza kujenga viwanja ukavipa jina la Kampuni yako na kadhalika. Hilo nalo tunalifanyia kazi na nikuhakikishie tuko katika hatua nzuri na hili tutafanikiwa. Kazi tuliyopewa ni kujenga viwanja na hizi *Arena* na Mheshimiwa Sanga hizi fedha tutazipa na *Arena* na *Stadium* zitajengwa katika nchi kama ambavyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais yametoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mgao wa mapato wa viingilio. Hili ningetaka kujibia. Hili ni suala la kisheria na kikanuni Mheshimiwa Sanga na kitu ambacho hakiwezi kubadilika ni ile asilimia 18 ya *VAT* na asilimia tatu ambayo inakwenda kwa *BMT*. Hayo mengine ni ya kikanuni ambayo *TFF* inakaa na wadau wake ambao ni vilabu kabla ya msimu kuanza na wanakubaliana. Sasa kwa maoni yako na maoni ya Wabunge wengine wengi ambao

walishayatoa kuhusiana na jambo hili, sisi tutaielekeza *TFF* wakati inakaa na wadau wake ambao ni vilabu kabla ya msimu ujao kuanza, waangalie haya makato kuona namna amabayo wanaweza wakawapunguzia vilabu vyetu mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli mimi kwa sababu ya kuwa mtu wa mpira humu ndani ndani, nafahamu namna ambavyo vilabu vinaingia gharama kubwa za kuendeshwa na namna ambavyo zinapitia wakati mgumu hata wakati mwingine kufika kituo kingine kwa ajili ya kucheza mechi zao. Kwa hiyo, tutafanya kadri tunavyoweza *TFF* waliangalie wasiwape mzigo vilabu vyetu na yale ambayo yanaweza kuongeleka na yakabadilika yatabadilika mtuachie sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la shule za michezo ulisema Mawaziri wawili wamepita. Nikuhakikishie Waziri Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana anakwenda kufanya miundombinu ile kwenye shule zetu za michezo hilo halitashindikana. Hivi ninavyokuambia tenda itatangazwa hivi karibuni ya marekebisho kwenye viwanja vyetu vya michezo na ujenzi wa viwanja vipya vya michezo kwenye zile shule zetu 56 utaanza. Kwa hiyo, kama lilishindikana huko sasa hivi halishindikani kaa utulie uone muziki ndugu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dada yangu Mheshimiwa Khadija (Keisha), alizungumzia kuhusiana na tuzo. Hili nalo nililiombea ruhusa maalum kabisa kwa Mheshimiwa Waziri ya kwamba hili suala la tuzo Mheshimiwa Waziri niachie mimi na nimekwishakabidhiwa. Tutakapomaliza Bunge hili la Bajaeti naanza kushughulika nalo kwa ajili ya tuzo zinazofuata. Kwa hiyo, hili niachie mimi wala usiwe na wasi wasi nalo na tutalipatia suluhisho. Tuzo za mwakani nikuahidi Dada yangu zitakuwa za aina yake na zitakuwa za picha tofauti kabisa na ilivyokuwa huko nyuma. *(Makofi)*

*(Hapa kengele I;ilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mambo mengine ya kusema lakini naamini Mheshimiwa Waziri ameya – *capture* na atayasema wakati wa kuhitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namuita mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Waziri wetu wa Utamaduni, Sanaa na Michezo aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kushukuru maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya Elimu, Utamaduni na Michezo lakini pia nitumie nafasi hii kuwashukuru wachangiaji wote. Tumepata wachangiaji takribani 16 na michango hii yote tutaiwasilisha kwa maandishi kila hoja. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa hapa kwenye Wizara yetu ni habari ya bajeti. Mambo mengi mazuri yamezungumzwa yafanyike, *reforms* na kikubwa kabisa ambacho kimezungumzwa hapa ni suala zima la bajeti. Hili ni kweli kabisa, bajeti upande huu wa masuala ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ndiyo hii ambayo leo tumekuja kuomba Bunge letu bilioni 35. Kama alivyosema Waziri mwenzangu Mheshimiwa Mwigulu, kwamba hili ni eneo ambalo kimsingi tunaendelea kuangalia namna gani tuendelee kuliboresha kwa kushirikisha sekta binafsi na wachangiaji wengi wamesema tuone namna gani tunashirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tutakwenda kukarabati uwanja wetu wa Benjamin Mkapa. Hivi sasa kuna mechi ambayo tunaisubiri kati ya Tanzania na Niger itachezwa mwisho wa Mwezi wa Sita na niwatangazie Watanzania kwamba, mara baada ya mechi hii kukamilika tutafunga uwanja huu tayari kwa ukarabati. Ninashukuru sana kwa maoni ya Kamati walivyosema kwamba tubakize Benjamin Mkapa kwa ajili ya mechi kubwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tunautumia uwanja huu ambao una uwezo wa viti takribani 60,000 hata kwa ajili ya shughuli mbalimbali za matamasha kama vile mahubiri, sala mbalimbali tulikuwa tunatumia lakini sasa tutatumia viwanja mbadala na uwanja huu ubaki kama hazina na alama ya Taifa letu. Kwa hiyo, tutakwenda kukarabati uwanja huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukarabati tunatarajia kujenga recreation center pale nyuma ya uwanja wa Benjamin Mkapa *na recreation centre* nyingine itakuwa hapa Dodoma, itakuwa ni viwanja viwili Dodoma pamoja na Dar es Salaam, kama alivyosema Naibu Waziri tayari Mkandarasi amekwisha kabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunakwenda kujenga *arena,* wamezungumza hapa watu wanahitaji *arena,* haya ni maeneo ya kipaumbele, tayari tuna eneo la Kawe pale tutajenga arena pia tutajenga *stadium* mbili hapa Dodoma na nyingine tunatarajia kujenga Arusha ikiwa ni maandalizi pia ya kuwa wenyeji wa mashindano ya *AFCON* 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ukidhi *AFCON* tunahitaji viwanja nane vya Kimataifa, lakini kwa kuwa tumeomba pamoja na Kenya na Uganda ukichanganya na wanatatarajia kuja Wakaguzi *(Inspectors)* kutoka Makao Makuu ya *CAF* hivi karibuni, tayari nimeongea na Waziri wa Michezo wa Kenya na Waziri wa Michezo wa Uganda tunaona namna gani ya kuhakikisha kwamba tunakidhi vigezo na masharti ili tuweze kufanikiwa *AFCON* 2027. Kwa hiyo miundombinu ya viwanja ni maeneo ya vipaumbele lazima tuone

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nimeshawasiliana na Waziri mwenzangu wa TAMISEMI pamoja na Waziri wa Elimu. Waziri wa Elimu tumekubaliana kwamba suala la somo la michezo liwe ni miongoni mwa masomo ambayo yanaweza kufundishwa na kufanyiwa mitihani liwepo kwenye mitaala, kwa hiyo, kuna mafunzo ya amali. Suala la masomo ya sanaa, muziki iwe ni miongoni mwa masomo ambayo yako katika *curriculum* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kushirikiana na Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Elimu tumekubaliana kuwa, hakuna kusajili shule ya msingi au sekondari hadi watuthibitishie wana viwanja mahali hapo. Mtoto hawezi kwenda shuleni miaka saba bila kushiriki michezo*, O – level* miaka minne, *A – Level* miaka miwili bila kushiriki michezo, anakuja kukutana na michezo *University,* lazima tuwazoeshe wakiwa wadogo. Kwa hiyo, hiyo ni miongoni mwa mikakati ambayo tunayo kuhakikisha kwamba eneo hili la michezo linaendelea kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango mbalimbali, kuna hoja hapa kwamba kampuni ya *betting* ili ipate leseni kigezo iwe ni kudhamini timu ya mpira na sisi kama Wizara jambo hili tunaona ni muhimu tunalichukua tuone namna gani ya kulifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kushirkisha sekta binafsi pamoja na *CSR,* tuwe na *sports academy* za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilithibitishie Bunge lako mpaka sasa Wizara imesajili *sports academy* kutoka ngazi mbalimbali 180. Hivi sasa hata wadau binafsi wanatengeza viwanja kwa mfano *Azam Complex.* Pale Morogoro wamekuja kuomba vibali wanaweka uwanja pale, kuna Mmasai mmoja yeye amesema anataka eneo lake litumike kwa ajili ya uwanja wa michezo na ameingia makubaliano na Italy na analeta wataalam wa kufundisha michezo kwa vijana kutoka Italy. Kwa hiyo, hii ni sehemu ambayo pia ni miongoni mwa vipaumbele vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala limezungumzwa hapa la *Ndondo Cup.* Tunaamini kwamba *Ndondo Cup* ni eneo la kukuza vipaji, pia kwenye mchango wa Mwenyekiti wa Kamati amesema kwamba tuone namna gani ya kurasimisha eneo hili la *Ndondo Cup,* nasi tunasema kwa kuwa ni eneo ambalo linarasimisha vipaji, *Ndondo Cup* inaendelea kuwa muhimu kweli. Kwa hiyo, tutaweka utaratibu kwa kushirikiana na wenzetu wa *TFF* kuona namna gani vibali vinaweza vikatolewa taratibu na wadau wanaotaka kuendesha mashindano haya waweze kushirikishwa na kutambulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kushirikiana na sekta binafsi kama Mabenki kuweza kuuza haki za majina ya viwanja. Kuna baadhi ya viwanja ukienda nchi nyingine unakuta uwanja una jina la benki fulani labda CRDB. Kwa hiyo, hayo ni maeneo ya kimkakati ambayo tunataka tuhakikishe kwamba tunashirikisha sekta binafsi na tuweze kuendeleza eneo hili la michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa tumezungumza hapa imeonekana kama wasanii wengi, wachezaji wengi wanatokea Dar es Salaam, niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa kwamba katika kila Halmashauri tuna Afisa Michezo, katika kila Halmashauri kuna Afisa Utamaduni na Sanaa maeneo haya kuna Kamati maalumu za kichezo na Mwenyekiti wake kwa ngazi ya Wilaya ni *DAS* na kwa ngazi ya Mkoa ni *RAS*. Kwa hiyo, nitoe wito sasa kwamba Kamati hizi zinapaswa kukutana na kuweka mikakati ya kutosha na hivi sasa tunakwenda katika michezo mtaa kwa mtaa, tunakwenda katika suala la sanaa mtaa kwa mtaa, tumeingia makubaliano ya michezo mashuleni kwa kushirkiana na *FIFA* tutatoa mipira 2,000 kila Mkoa katika *spirit* ya kuendeleza michezo mtaa kwa mtaa. Kwa hiyo, tayari tumekwishaingia makubaliano *(MOU)* pamoja na *FIFA* kwa kushirikiana na *TFF* ili kuona ni namna gani tunaboresha na tunahamasisha suala zima la michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na swali pia inakuwaje kwamba labda watu wanataka kusajili masuala ya sanaa wasafiriki kutoka mikoani? Sasa hivi kupitia Wizara tunataka kuweka utaratibu wa ku–*digitalize*. Kwa hiyo, unaingia kwenye *www.sanaa.basata.go.tz* mahali hapo unaona taratibu zote za kusafiri hauhitaji kusafiri. Unaweza ukawasiliana na Maafisa wetu walioko katika ngazi za Serikali za Mitaa, kila halmasahauri tuna Maafisa Michezo, Maafisa Utamaduni, tunataka kuendeleza eneo hili kwa sababu tunajua linaajiri vijana wengi kabisa na baada ya sensa vijana wapo takribani zaidi ya milioni 30, kati ya idadi ya watu milioni 61 zaidi ya *51 percent* ni vijana, ni lazima tuweke mikakati ya kuhakikisha kwamba vijana hawa wanashirikishwa na wako imara kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, tunao Mfuko wa Utamamduni, na mfuko huu kazi yake ni ku-*support* kutoa

mikopo. Tumeshatoa mikopo takribani shilingi 1,077,000,000. Sasa tunaangalia namna gani ya kufika nchi nzima. Mikopo hii wanapewa watu wote; awe ni msanii maarufu, hata asiye maarufu, wote wana haki pale ambapo vigezo na masharti vimezingatiwa. Kwa hiyo, tunaendelea na mazungumzo na Mabenki yetu na taasisi za kifedha. Lengo ni kwamba hizi benki zina *branch* katika kila wilaya na kila mkoa. Tumeshaanza mazungumzo na benki mbalimbali ikiwa ni pamoja na *National Bank of Commerce* kuona ni namna gani tunaweza tukaingia makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na fedha ya kukopesha, tunaipeleka benki, tunasema sasa wewe benki utoe kwa niaba yetu. Huu ni mkakati ambao tumeujadili hapa Bungeni kwa pamoja, pia kuona ni namna gani tunawezesha vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, huo ni mkakati ambao tunao, tunataka kila mwenye uwezo wa kupata fursa, kupata mitaji ya kuendeleza masuala ya utamaduni, sanaa na michezo, waweze kupata mitaji. Kwa hiyo, Wizara imedhamiria kuleta mageuzi na tuko imara kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vazi la Taifa, niwahakikishie Kamati kwamba suala hili ni jambo ambalo tuko makini, tuko *serious.* Mchakato huu ulishafanyika hapo awali na ulienda hadi ngazi za Wizara, lakini Wizara tulitoa maelekezo mengine kwamba warudi kupata maoni mengine. Wameshamaliza kukusanya maoni Visiwani na Bara na hivi karibuni watakwenda kuwasilisha ripoti maalum kabisa. Tumeshawapa *deadline,* wahakikishe kwamba suala la vazi la Taifa linakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mdundo wa Taifa, tayari tuna *Producer's Kit* ili mtu anapotaka kuweka nyimbo, aweke nyimbo yenye Mdundo wa Taifa. Kwa hiyo, hili la vazi la Taifa tunaelekeza Kamati kwamba wahakikishe wanakamilisha suala hili mapema kabisa liweze kukamilika kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kama nilivyosema, maoni yote tunachukua, lakini tunaendelea na suala zima la kubidhaisha Kiswahili. Tunataka Kiswahili kiwe na manufaa, vijana

wetu waweze kufundisha Kiswahili, waweze kutoka nje ya nchi, na waweze kuwa Wakalimani. Tuna ushirikiano na nchi mbalimbali kama tulivyosema awali, Ujerumani na hata *Spain* tayari wameshatuomba tuwapeleke walimu wetu kujifunza *Spanish*. Kwa sababu ukijua Kiswahili lazima ujue na lugha ya pili ili kuweza kutafsiri; kama ni Kiarabu, kama ni Kifaransa, au lugha nyingine. Maana ukijua tu Kiswahili peke yake, bado, lazima tuwe na lugha ya pili. Kwa hiyo, tunaendelea na mkakati wa kubidhaisha lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye mara kwa mara amekuwa akitoa hotuba hata ngazi ya *AU* kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, Watanzania wenzangu, Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kutumia lugha yetu hii ya Taifa. Mataifa mengine wanathamini sana lugha zao, wanajali lugha zao. Tumeshatoa kamusi, tuendelee kutumia lugha yetu, tufurahie lugha yetu. Vilevile tunazo filamu kwa lugha ya Kiswahili. Tuwe tunapenda kuangalia sanaa zetu na utamaduni wetu, tuufurahie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja kwa upande wa filamu kuhusu vibali. Vibali vya Filamu tunaendelea kuvitoa kupitia Bodi ya Filamu na sasa hivi mambo mengi tunafanya *online,* haihitaji mtu kusafiri. Pia tunatoa *documentary,* siyo tu filamu za kawaida, *documentary* za kufundisha, Historia na *documentary* mbalimbali. Huo ni mkakati ambao tunao. Huko nyuma tulikuwa tunatoa filamu 200 kwa mwaka hivi sasa niwahakikishie Wabunge tunakwenda mpaka filamu 2,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo limechukua vijana wengi na vijana wengi wanakuwa maarufu ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, hii ni mikakati ambayo tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli yeye amekuwa ni chachu upande wa michezo, amekuwa ni kinara kabisa upande wa michezo. Taifa letu leo linajulikana ndani na nje ya nchi. Tumeendelea kupata maombi mbalimbali. Hivi sasa timu ya *cricket* Taifa wana mashindano yao ya kimataifa, wameshaleta maombi, tunaomba Tanzania mtu-*host.* Hii yote ni kutokana na uongozi bora wa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa

Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameonesha kabisa anapenda michezo, lakini siyo tu michezo, hata masuala ya utamaduni na sanaa. Watu wa utamamduni na sanaa tunamtambua kwa jina la Chifu Hangaya. Tuko naye, yuko vizuri. Mheshimiwa Rais ameacha alama maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imeungwa mkono, tunakushukuru na kukupongeza sana.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni mchana huu, ni wageni 32 wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mbunge na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Wajumbe wa *Adorable Wedding Trade Fair* wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Ndugu Anna Lema, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 28 wa Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge ambao ni wanachama wa *Giving Back to the Community Foundation* kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi, Mbunge ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Malinyi, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wapo wageni 28 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini ambao ni Watendaji wa Kata na Wachungaji kutoka Longido Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile wapo wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge ambao ni Kwaya ya Utatu Mtakatifu kutoka Kanisa la Andrea, *Parish* ya Miyuji, Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 180 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Canossa ya Jijini Dar es Salaam, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi wa Shahada ya Famasia kutoka Chuo Kikuu cha *St. Johns'* cha Jijini Dodoma ambao ni Ndugu Amos Nyanda na Ndugu Faith Godwin. *(Makofi)*

Wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge ambao ni wanafunzi kutoka Vyuo Vikuu Dodoma kutoka Wilaya ya Ngorongoro Mkoani Arusha, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 96 - Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………………Sh. 6,680,809,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………Sh. 478,027,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………………Sh. 565,448,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*….Sh. 341,516,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 312,378,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*………………………Sh. 184,394,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*.................................. Sh. 385,279,000
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*………………………Sh. 135,132,000
Kifungu 6001 – *Culture Development Division*……..Sh. 2,246,783,000
Kifungu 6004 – *Sports Development*…………………Sh. 4,406,353,000

Kifungu 6005 – *Arts Development Division*…………Sh. 7,877,762,000
Kifungu 7003 – *Information Services*………………………………...Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 - Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kifungu 6001 – *Culture Development Division*…..…Sh. 2,350,000,000
Kifungu 6004 – *Sports Development*…………………Sh. 8,611,160,000
Kifungu 6005 – *Arts Development Division*…...………Sh. 870,000,000
Kifungu 7003 – *Information Services*……………………...……...Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na tunawatakia kila la heri katika utendaji kazi kwa mwaka wa fedha unaokuja. Pia naipongeza Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa masuala ya Elimu, Utamaduni na Michezo kwa kazi nzuri waliofanya ya kuishauri Wizara hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.42 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 7 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*